# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

## Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 24 Mei, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa Azzan Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI**: Tukae, Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**:

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI**: Ahsante, Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 264

**Vituo vya Afya Nafa, Iramba na Kamgesi**

**MHE. MARWA R. CHACHA** aliuliza:-

Kumekuwa na mpango kabambe wa Mfuko wa Afya wa Bima *(CHF)* ambao ni "Papo kwa Papo na Tele kwa Tele"' na Watanzania waliopo Serengeti wamekuwa wakichangia huduma hiyo lakini kila waendapo kwenye matibabu hupewa cheti badala ya dawa.

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la ukosefu wa dawa kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma za afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mala Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa dawa unategemea upatikanaji wa fedha kupitia Mfuko wa Afya wa Pamoja ambapo Halmashauri hiyo imeshapokea fedha zote kiasi cha shilingi milioni 826.4 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri imepanga kutumia shilingi milioni 843 kwa ajili ya upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyopo. Kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii *(CHF)* Halmashauri zinakusanya mapato yatokanayo na uchangiaji kwa kuzingatia sheria ndogo za Halmashauri ambapo kipaumbele ni upatikanaji wa dawa. Natumia fursa hii kuzikumbusha Halmashauri kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuendelea kuhamasisha wananchi kuchangia mfuko.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Chacha.

**MHE. MARWA R. CHACHA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nirekebishe naitwa Marwa sio Malwa kuna “r”.

**MWENYEKITI:** Ngoja, ngoja kwa hiyo sio swali lako hili.

**MHE. MARWA R. CHACHA**: Katamka vibaya.

**MWENYEKITI**: Sio swali lako?

**MHE. MARWA R. CHACHA**: Ni swali langu.

**MWENYEKITI:** Basi endelea. *(Kicheko)*

**MHE. MARWA R. CHACHA**: Mheshimiwa Mwenyekiti nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kuna huu utaratibu wa *MSD* kwenda kwenda vituo vya Afya wamebeba, wanapeleka kondomu na mseto pakiti nane unaenda kwenye zahanati unakuta wamepeleka kondomu na mseto nane, huu utaratibu unasafirisha hivi vitu kutoka Mwanza mpaka kule Serengeti haukubaliki. Je, ninyi kama Wizara mnaona huu utaratibu uendelee?

Swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri umekuja pale Serengeti na Serengeti sasa ni Wilaya ya kitalii, tunapata watalii wengi lakini tulikupeleka kwenye ile Hospitali ya Wilaya ukaona umaliziaji wa ile *OPD.* Wizara mpo tayari kutoa fedha kwa ajili ya kumalizia ile *OPD?* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la upelekaji wa dawa *MSD* naomba nitoe ufafanuzi ifuatavyo:-

Ni kwamba dawa zinapofika kule kwanza kuna *request* ya kawaida inayopelekwa, lakini dawa zinapofika lazima Kamati ya Afya ya kituo husika lazima ihisike katika upokeaji wa dawa, lakini nitoe wito kwa Halmashauri ya Serengeti kwa sababu japo kuwa tumepeleka fedha nyingi pale kuna baadhi ya fedha zingine bado hazijatumika katika ununuzi wa dawa, kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Mbunge najua kwamba kwa sababu pale eneo lako lina changamoto kubwa tushirikiane vema kwamba kuhakikisha tunasukuma *MSD* dawa ambazo zimebakia karibuni za shilingi milioni 180 zifike pale *site,* lakini hali kadhalika mnao pesa nyingi zaidi za *basket fund* bado hazijanunua dawa, nitoe maelekezo hayo kwa Serengeti haraka iwezekanavyo dawa zipatikane kwa sababu tayari Serikali tumepeleka fedha.

Lakini katika suala la pili ni suala zima la hospitali tuliofika, ni kweli na mimi nimefika pale na tulivyoenda kuangalia tukasema ajenda ya Mheshimiwa Rais alipofika pale ni kuahidi kwamba atawahudumia wananchi na ndio maana katika kipindi cha sasa tumefanya *commitment* zile wodi mbili tutazifanya *two wards in one,* tutafanya zoezi kubwa pale la kupeleka takribani tutaweka nguvu karibu shilingi milioni 700 lengo kubwa ni kufanya ahadi ya Mheshimiwa Rais katika maeneo mbalimbali iweze kutekelezeka. Kwa hiyo hili ni jukumu la Serikali tunaenda kulitekeleza. *(Makofi)*

**MWEYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile halafu Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bima kwa Wote ni utaratibu ambao ungeweza kusaidia sana wananchi wanyonge kuweza kupata huduma nzuri za afya kwa gharama nafuu, lakini vilevile ingesaidia serikali kupata mapato ya kuendesha huduma za afya, sasa nataka kuuliza ni lini Serikali italeta

Muswada wa Sheria wa Bima ya Wote *(Universal Coverage)* kwa ajili ya kujadiliwa hapa Bungeni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lipo katika *negotiation* ambapo wadau mbalimbali wameenda kushiriki na Wizara ya Afya na Wizara yetu inaangalia utaratibu mzuri, naomba niseme kwamba Serikali imejipanga katika hili na si muda mrefu baada ya wataalam kupita katika ngazi mbalimbali basi Serikali itakavyoona kwamba huu muswada sasa umeiva, basi utakuja hapa Bungeni kwa ajili ya kufanya maamuzi hayo.

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Sokombi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa tatizo lililopo Serengeti linafanana kabisa na tatizo lililopo katika Tarafa ya Mtae, Shagayu, Sunga na Rangu, wananchi wamehamasika kuchangia huduma za *CHF* lakini wanapokwenda kwenye Kituo cha Afya cha Mtae huduma hakuna. Je, Serikali inawambiaje wananchi hawa wa Tarafa Mtae?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niweke rekodi sawa kwamba bahati nzuri tulikuwa na Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo lake kipindi kile wakati nilipokwenda kutembelea Wilaya ya Lushoto. Ni kweli kwa sababu tumegundua changamoto ya afya ipo kubwa zaidi ndio maana katika vipaumbele vyetu tumeamua kukiteua hiki Kituo cha Afya cha Mtae ni miongoni mwa vituo ambavyo ndani ya mwezi huu mmoja unaokuja tutaenda kufanya ujenzi wa *maternity ward* pale na kufanya ukarabati mkubwa lengo kubwa wananchi wa Mtae na maeneo ya jirani waweze kupata huduma nzuri katika eneo lile.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Sokombi.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Ahsante Mwenyekiti, nipende tu kuuliza swali kwamba Wilaya ya Bunda ina hospitali moja ambao ni Hospitali ya Manyamanyama, na ile hospitali ya Manyamanyama inaitwa Hopsitali ya Wilaya, lakini haina hadhi kama Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Waziri, je, ni lini itakuwa na kiwango kama Hospitali ya Wilaya na dawa zipelekwe kama Hospitali ya Wilaya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa majibu kwa kifupi

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na tulipofika pale Bunda tulitembelea yale maeneo yote tukaona kwamba kuna changamoto kubwa na hili tulitoa maelezo katika maeneo mbalimbali, hata hivyo kwa ajili ya *the backup strategy* ya kufanya kwa Bunda na kwa sababu ukiangalia kwa ndugu yangu Kangi Lugola wagonjwa wote wanakuja pale, kwa ndugu Boniphace wagonjwa wote wanakuja pale, ndio maana sasa hivi kwa muda unaokuja na si muda mrefu sana japo tunaweka mikakti ya ile sehemu ya Manyamanyama pale lakini katika eneo la Mgeta tunakwenda kutengeneza kituo cha afya tunakwenda kukiimarisha kwa kiwango kikubwa lengo kubwa ni kupunguza idadi ya wagonjwa wanaokuja pale kuweza kuhakikisha kwamba akina mama na watoto afya zao tunazilinda vizuri.

**MNWENYEKITI**: Mheshimiwa Frank ajiandae Mheshimiwa Keissy.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Sera ya nchi na ya Serikali ni kuhakikisha kwamba kila kijiji na kila kitongoji kuna kuwa na zahanati, na katika mji wa Tunduma katika mtaa wa Makambini eneo la Sogea

wananchi wameamua kujenga zahanati katika eneo ambalo lilikuwa limetengwa na Serikali, lakini kutokana na mgogoro uliokuwepo na ambao alikuja kuumaliza Naibu Waziri wa Ardhi, alitoa maelezo kwamba eneo hilo lisianze kujengwa mpaka atakavyotoa ruhusa ya wananchi kuendelea kujenga Zahanati pale. Je, ni lini atatoa ruhusa ili wananchi wa mji wa Tunduma eneo la Makambini waweze kuendelea na ujenzi wa zahanati kama ambavyo sera za nchi zinasema?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nadhani Mheshimiwa Waziri wa Afya alivyopita pale wananchi waliandamana katika suala zima katika kituo kile cha afya nadhani tutafanya utaratibu kupitia ofisi yetu ya TAMISEMI nini kifanyike, lakini kutokana na changamoto ya Tunduma kwa sababu ukipita pale siku niliyopita pale *population* ni kubwa sana na ndio maana tunaamua kwenda kukiimarisha kituo cha Chipaka na lengo kubwa ni kwamba angalau ile kituo cha afya cha Chipaka kiweze kuwa *accommodate* wagonjwa wengi na tunakwenda kufanya kazi hizyo muda si mrefu ndani ya mwezi mmoja ujao kwa ajili ya wananchi wa Tanzania lengo letu ni kuboresha maeneo yale.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:**Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi bima za afya baadhi ya maduka na hospitali zinatumika vibaya, kuzidisha *double allocation* mtu anaenda kutibiwa anaweza akaandikwa *double* akaiga saini ya mteja au na zingine zinazidisha bei mara mbili, je, nani anazikagua bima ya afya kabla ya malipo, kwa kuwa zinaendesha wizi wa hali ya juu,

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli kwa

kipindi kirefu sasa hata ukija kuangalia wakati mwingine kuna takwimu na kuna *fraud* inafanyika katika hizi *document* hasa za bima ya afya na ndio maana sasa hivi utaratibu wa bima ya afya imeweka sasa hivi *document* ambayo haijakaa vizuri hawawezi kuilipa, lakini hili sasa naomba niwa sisitize hasa katika wenzetu wa bima ya afya wahakikishe wanaweka *mechanisim* nzuri ya kuweza kuangalia tuna *monitor* hizi fomu zinajazwa vizuri, lakini sio kujazwa tu, iangalie ili mradi *compliance* kwamba fomu iliyojazwa ndio kweli iliyotoa matibabu.

Kwa hiyo Mheshimiwa Keissy naomba tuichukue hoja hii kwa sababu ni hoja ya msingi tunaenda kulinda fedha za wananchi, fedha za serikali tutaenda kulisimamia vizuri kwa kadri iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma.

Na. 265

**Kutofidiwa Wananchi wa Mji mwema na Tangira – Mtwara Mjini**

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA** aliuliza:-

Mwaka 2012/2013 Serikali ilichukua ardhi ya wananchi wa Mtwara Mjini eneo la Mji Mwema na Tangira. Aidha, Serikali imewazuia wananchi hao kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo hayo. Serikali iliahidi kuwalipa wananchi hao fidia lakini hadi sasa fidia hiyo haijalipwa.

Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi wao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Maaftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia stahiki itaanza kulipwa kwa wananchi 2,020 kuanzia mwezi Juni, 2017 hadi robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/2018. Taasisi ya UTT - PID kwa kushirikiana na Halmashauri inatarajia kutumia shilingi 7,523,000,000 kwa ajili ya malipo ya fidia kabla ya kuanza kwa kazi ya upimaji wa viwanja. Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilitoa kibali cha kuendelea na utekelezaji wa mradi kupitia barua yenye Kumb. Na. GB. 203/234/01/117 ya tarehe 02/09/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ulipaji wa fidia haukuanza mapema kutokana na kampuni husika ya UTT - PID kutokuwa na Bodi. Bodi imeshaundwa na makubaliano ya pamoja yamefanyika katika kikao cha tarehe 02/05/2017 baina ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, UTT – PID na Halmashauri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kwa namna ya kipekee nishukuru kwa sababu suala hili la ulipaji wa maeneo haya fidia hii ni suala la muda mrefu sana kwa kuwa Wizara hii ya TAMISEMI na Wizara ya Ardhi imekubali sasa kulimaliza suala hili tunashukuru kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini, lakini hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, nilikuwa naomba kujua sheria inatueleza kwamba kwa kuwa maeneo haya yamechukuliwa mwaka 2012/2013 ni muda mrefu hivi sasa wananchi wale wamekosa maeneo ya kulima na kufanya shughuli zao za kimaendeleo, je, Serikali ipo tayari kulipa pamoja na fidia ya nyongeza?

Swali la pili, kwa kuwa ahadi hii ya kuwalipa wananchi hawa Jimbo la Mtwara Mjini ni la muda mrefu, je Mheshimiwa Waziri yupo tayari kulithibitishia Bunge hili kwamba wananchi

wa Mtwara Mjini wa maeneo haya ya Mji mwema na Tangira kwamba tarehe hizo walizotaja ni kweli wataenda kulipa fidia? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kulifuatilia hili jambo kwa sababu ni haki za wananchi wako kwa hiyo *commitment* yako kwa wananchi wako imekuwa vizuri, lakini jambo la pili, utaratibu wa malipo ya fidia ni kwamba mara baada ya tathimini ikishafanyika ikipita miezi sita maana yake malipo yanatakiwa yalipwe ndani ya miezi sita; ikipita miezi sita lazima kuna malipo ya nyongeza yatafanyika. Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie kwamba Wananchi haki zao zitalindwa kulingana na muda uliocheleweshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la pili kwamba *commitment* ya Serikali sasa itaenda kulipa hili nimezungumza hapo awali kwamba kilicho chelewesha mwanzo kutokana na Bodi ilikuwa haijaundwa na bahati nzuri sasa bodi imeshaundwa na ndio maana sisi ofisi yetu ina jukumu la kutoa kibali tumeshatoa kibali. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba uondoe hofu kwamba wananchi wa Mtwara leo hii wananisikiliza *live* kupitia vyombo vya habari kwamba Serikali imejipanga katika hili na itaenda kutekeleza kwa kadri mipango yote ilivyowekwa vizuri kupitia Halmashauri yenyewe.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi, kwanza naipongeza Serikali kurudisha Ardhi ya Dodoma mikononi mwa wananchi yaani Baraza la Madiwani. *(Makofi)*

Kwa kuwa *CDA* imevunjwa na ndio mamlaka iliyokuwa na madaraka juu ya ardhi ya Dodoma na wakati inavunjwa wapo wananchi ambao walishapata barua za

kumiliki ardhi, lakini walikuwa hawajaonyeshwa maeneo yao na wapo wananchi ambao wanalipa kidogo kidogo pale *CDA,* je, Serikali imeweka utaratibu gani wa dharura wa kuhakikishwa kwamba wananchi wa Manispaa ya Dodoma wanahudumiwa wakati taratibu zingine zinaendelea? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunashukuru kwa Mheshimiwa Mbunge ku- *recognize* kwamba kilio cha wananchi wa Dodoma katika hilo, lakini jambo la pili *government works on papers,* hakuna haki mtu itayopotea. Kwa hiyo, Serikali itaandaa utaratibu wowote ambao unawezekana na kikosi kazi kwa mujibu Serikali itakavyokuwa imejipanga naomba muondoe hofu kwamba Ofisi ya Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo jambo hili inaisimamia vizuri tutakuja kutoa taarifa hapa iliyokuwa rasmi juu ya jinsi gani jambo hili linatekelezeka na wananchi wote wa Dodoma wasiwe na hofu kila jambo litakuwa limewekwa vizuri kwa utaratibu wa Kiserikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, subiri Mheshimiwa Halima, Naibu Waziri wa Ardhi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa majibu ya nyogeza kwa niaba Waziri wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhusiana na swali lililoulizwa na Mheshimiwa Bura kama ifuatavyo:-

Naomba niwahakikishie wananchi wa Dodoma kwamba mbali na kuvunjwa na *CDA* huduma zote za ardhi zinaendelea chini ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Dodoma na watumishi waliokuwa wakifanya kazi sekta ile wapo ambao wataendelea na kazi hiyo na wale ambao walikuwa wamelipia nusu ya maeneo yao wataendelea na utaratibu huo mpaka pale watakapokamilisha kulingana na makubaliano waliopeana awali.

Aidha, wale wote ambao wana zile hati ambao si hati miliki ambazo tunazitambua kutakuwa na utaratibu wa kubadilishiwa na kupewa zile hati ambazo watapewa muda wa miaka 99 kuanzia pale alipopewa awali. Kwa hiyo, wasiwe na hofu Wizara imejipanga vizuri na kila mmoja atapata haki yake kadri utaratibu wa ofisi ilivyopanga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante, Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA ALI MOHAMMED**: Ahsante, Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja.

Mheshimiwa Waziri kwa kuwa suala la Mtwara linafanana sana na suala la Halmashauri ya Kisarawe kata ya Kibongwa, wananchi wamechukuliwa ardhi yao, ikakatwa viwanja, lakini wao hawakupatiwa viwanja wala hawakupatiwa fidia yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Waziri ni lini wanmanchi wa jimbo lako hili watapatiwa haki yao ya fidia? *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli viwanja vilipimwa toka mwaka 2005 na ni kweli baadhi ya wananchi walichukuliwa eneo, lakini suala zima la mchakato wa fidia lilikuwa halijalipwa na ndio maana katika kulinda haki za wananchi tulisema hata vile viwanja vya mwanzo watu walitakiwa wapewe na wengine miongoni mwenu ni Wabunge humu ndani, tulivizuia kwamba watu wasipate vile viwanja mpaka wananchi wa pale wapate haki zao.

Kwa hiyo, jambo hili chini ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri linashughulikiwa vizuri na kila mtu atapata haki yake stahiki kwa sababu jambo hili viongozi tumelisimamaia kulinda haki za wananchi wetu.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MWENYEKITI:** Sijakuita Mheshimiwa, haya sasa nakuita. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 266

**Hitaji la Chombo Kinachojitegemea kwa Ajili ya Ukaguzi wa Elimu**

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA (K.n.y. MHE. MARGARET S. SITTA)** aliuliza:-

Kwa mujibu wa takwimu za Serikali kumekuwa na ongezeko kubwa la Taasisi za Elimu zikiwemo shule za Serikali na zisizo za Serikali za msingi na sekondari, shule maalum, vyuo vya ualimu na vituo vya elimu ya watu wazima; na kwa kuwa suala la ubora wa elimu ni kipaumbele kwa Watanzania walio wengi.

Je, kwa nini Serikali isiunde chombo kinachojitegemea cha ukaguzi wa elimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi wa Shule iliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Sura ya 353 ya sheria za nchi ikiwa na jukumu ka kufuatilia ubora wa elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa kuzingatia viwango vya utoaji wa elimu vilivyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Idara ya ukaguzi wa shule ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu, kwa

sasa wizara yangu inafanya mabadiliko ya sheria ya mfumo mzima wa elimu ili iende sambamba na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Suala la ukaguzi wa shule kuwa chombo kinachojitegemea litaangaliwa kwa mapana katika hatua za kufanya mabadiliko ya sheria hiyo, pamoja na nyingine ambazo zitaweza kuongeza ufanisi katika ukaguzi wa shule.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa ruhusa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto nyingi za ukaguzi kwenye shule zetu za sekondari, msingi na vyuo vya ualimu, je, Serikali haioni sasa imeshafika wakati wa kuunda mamlaka au taasisi itakayosimamia ubora wa elimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Idara zetu za Ukaguzi wa Elimu, shule za sekondari na msingi zimekuwa zikipata changamoto nyingi hasa za vyombo vya usafiri na watendaji. Je, Serikali ina mpango gani wa kuiwezesha Idara hiyo ya Ukaguzi ili iweze kufanya kazi yake katika ubora unaotakiwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema awali ni kweli Idara yetu ya Ukaguzi inakabiliwa na changamoto mbalimbali hususan katika ukuaji wa sekta ya elimu kama ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyemiti, mwanzo idara hii ilikuwa inakaguliwa kupitia kwenye kanda zetu, lakini kwa sasa ni kanda pamoja na Wilaya, hata hivyo tunaona kwamba kuna mapungufu kidogo katika mfumo mzima, na ndio maana kupitia mabadiliko haya ya sheria tutaangalia namna bora zaidi ya kuendesha shughuli ya ukaguzi katika shule zetu za *primary*, sekondari na vyuo. Hali kadhalika kwa upande wa uwezo wa Idara za Ukaguzi, ni kweli kuna mapungufu hasa yanayotokana na vifaa kama vitendea kazi kama magari,

ofisi na Wizara imeshaona hilo na tayari tumeshaanza kufanyia kazi, tayari kuna magari yamekuwa yakipelekwa kwenye Wilaya na mwaka huu tumeagiza magari mengine kwa ajili ya kupeleka kwenye Wilaya nyingine na wakati huo huo tunatarajia pia kwa mwaka huu kuanza kujenga angalau ofisi 100 kwa ajili ya wakaguzi katika Wilaya zetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa suala la udhibiti wa elimu huwezi kutofautisha na udhibiti wa vitabu vinavyoingia kwenye mfumo wa elimu na kwa kuwa imeonekana wazi kwamba taasisi ya elimu ambayo imepewa jukumu la kuthibiti ubora wa vitabu vinavyoingia kwenye mfumo wa elimu imeonekana kuna dosari kubwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha chombo cha ithibati kama ilivyokuwa *EMAC* huko nyuma ili kudhibiti vitabu vinavyoingia katika mifumo yetu ya elimu na kuacha madudu yanayoendelea sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kurudisha mamlaka zilizokuwa zinafanya juu ya utungaji wa vitabu za wakati huo ni suala ambalo linabidi kuangaliwa zaidi. Kimsingi mapungufu yaliyojitokeza kwa mwaka huu Wizara ya Elimu imeanza kutunga vitabu kwa mara ya kwanza. Kwa hiyo, chombo kama hicho inabidi lazima kijengewe uwezo na ndio maana katika kufanya tathmini ya matatizo yaliyojitokeza, moja ya mambo yatakayoangaliwa ni uwezo wa chombo chenyewe, vilevile hata ushirikishwaji mpana wa wadau mbalimbali ikiwemo watu binafsi na wataalam kutoka katika maeneo mbalimbali.

Kwa hiyo, mimi nadhani kiujasiriamali tunasema kwamba kujifunza ni pamoja na kufanya makosa, lakini yasiwe ya kudhamiria yawe ni ya bahati mbaya. Kwa hiyo, tutaendela kuboresha na kushirikisha wadau wengi zaidi ili kuona kwamba tunapata vitabu vilivyo sahihi.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata hii nafasi. Kwa kuwa Mheshimiwa waziri amesema kwamba wana mpango wa kupeleka vitendea kazi na magari katika Ofisi za Ukaguzi wa Elimu, lakini kwa muda mrefu kumekuwa na matatizo makubwa ya ukosefu wa fedha za uendeshaji, unaweza ukapeleka magari kama hakuna fedha za uendeshaji bado hawataweza kufanya kazi; na kwa kwa muda mrefu wakaguzi wamekuwa wakifanya ukaguzi katika shule ambazo ziko jirani tu kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea *OC* ofisi hizo zote za kanda ili ziweze kufanya kazi yao sawasawa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema awali ni kwamba kimsingi Wizara imedhamiria kuboresha eneo hili la ukaguzi. Suala la *OC* limekuwa likiimarishwa kila wakati na ndio maana tunataka kuangalia mfumo mzima, hata ikiwezekana mafungu yao ya upatikanaji wa *OC* yaende moja kwa moja bila kupitia katika ngazi nyingine.

Vilevile ukaguzi tunaotaka kuuzingatia si tu ule wa kuangalia masomo peke yake, mpaka miundombinu, shule iko wapi? Inafundisha vipi na imesajiliwa katika sura ipi? Kwa hiyo, tunataka kwenda kwenye ukaguzi kwa njia ambazo ni pana zaidi ili kuwezesha kuona kwamba mambo ambayo tunaagiza kupitia sera zetu na miongozo yanatekelezwa pia katika shule zetu za Serikali.

Na. 267

**Kurekebisha Mitaala ya Elimu**

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itarekebisha mitaala ya elimu ili elimu ya ujasiriamali na stadi za maisha ziweze kufundishwa kwa wanafunzi wanaohitimu darasa la saba na kidato cha nne ambao hawatabahatika kuendelea na masomo na

hatimaye waweze kuwa na uelewa wa kujiajiri na kujitegemea?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na utaratibu wa kuboresha mitaala ili kuendana na mahitaji ya jamii kwa wakati husika. Mwaka 2005 Serikali iliboresha mitaala ya elimu ya msingi na sekondari ambapo masuala ya ujasiriamali yaliingizwa ili kuwajengea wahitimu uwezo wa kujiajiri. Uboreshaji huu ulihusisha pia kuingiza maudhui ya stadi za maisha kama suala mtambuka. Kwa ujumla mitaala imezingatia kutoa elimu ya ujasiriamali kupitia maudhui na mbinu za kufundishia na kujifunzia ambazo zinawafanya wanafunzi kuwa watendaji wakuu au kitovu cha kujifunza.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali yetu ya awamu ya tano imedhamiria kuifanya Tanzania kuwa Taifa la viwanda je, Serikali haioni muda muafaka sasa wa kuandaa mitaala ya stadi za kazi na ufundi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa kuwa mahitaji ya dunia sasa yamebadilika, je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya marekebisho makubwa ya sera yetu ya elimu ya juu na elimu ya kati ili wahitimu waweze kushindana kimataifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sera zetu mpaka sasa zimekuwa zikizingatia masuala ya kuwezesha stadi za kazi. Suala linalojitokeza katika ugawaji wa rasilimali na kuboresha ili ziendane na uhalisia hiyo ndio inakuwa ni changamoto. Kwa mfano suala la kujifunza kwa vitendo ni jambo muhimu sana, lakini wakati mwingine unakuta kwamba bajeti inapokuwa finyu ule muda wa vitendo unapunguzwa.

Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuongeza jitihada katika maeneo hayo ikiwemo kuboresha vyuo vya ufundi kama vile vyuo vya wananchi ambavyo tumeshavichukua kwenye Wizara yetu pamoja na *VETA,* lakini pia kufungua vituo mbalimbali vya kujifunzia ukiacha katika mfumo rasmi hata mfumo usio rasmi ili baadaye hata wale wanaokuwa wanajifunza kupitia mifumo isiyo rasmi waweze kupata hizo stadi za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu ya juu hivyo hivyo, wanafunzi wamekuwa wakifundishwa, lakini pia tumekuwa tukiangalia nchi mbalimbali zinaenda vipi kupitia *workshops* ambazo tunabadilishana mawazo, vilevile hata kupitia mitaala yetu. Kwa mfano siku nyuma elimu ya ujasiriamali ilikuwa haipo vyuoni, ilikuwa haifundishwi lakini sasa hivi tunazo *degree, masters* mpaka *Ph.D* za ujasiriamali. Kwa hiyo, tumekuwa tukifanya hivi na naamini tutaendelea kuzingatia kadiri tunavyopata mawazo mbalimbali ikiwemo ya kwenu Waheshimiwa Wabunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiteto Koshuma ajiandae Mheshimiwa Sophia.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Kwa kuwa mitaala ya elimu Tanzania inazingatia misingi na mahitaji ya kijamii hususan masuala ya utandawazi. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka somo la *computer* katika shule za sekondari na msingi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi tayari Serikali ilishaanza kuweka masomo ya *computer* au TEHAMA kwa ujumla katika shule zetu, isipokuwasiyo shule zote ambazo tayari zimeshapata hizo fursa kutokana na miundombinu halisi. Lakini kupitia hii miradi ya *REA* ambayo sasa karibu kila kijiji kinakuwa na umeme, vilevile karibu taasisi zote za umma ikiwemo shule zitakuwa na umeme. Kwa hiyo, tunaamini kwamba eneo la TEHAMA litaweza kupata nguvu zaidi na tayari wizara inafanyia kazi kuhakikisha kwamba wanafunzi wengi wanapata fursa ya kupata mafunzo hayo.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa takribani miaka miwili iliyopita kumekuwa kuna uhitaji mkubwa sana wa mafunzo ya ujasiriamali, lakini kumekuwa kuna walimu wanaofundisha chini ya kiwango. Serikali inasema nini kuwadhibiti walimu hao kwa kupunguza bei lakini pia kufundisha katika viwango ambavyo vinaweza kusaidia walaji ambao wengi ni wanawake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, ajiandae Mheshimiwa Riziki na Mheshimiwa Almas.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, somo la ujasiriamali ni somo ambalo linaweza likafundishwa katika ngazi mbalimbali kama ambavyo wengi tunafahamu, ujasiriamali upo katika sura mbalimbali. Kuna ule ambao unakuwa *informal* ndio wajasiriamali hawa wadogo wadogo wanaanza, lakini kuna ule ambao unakuwa katika ngazi kubwa zaidi. Kwa hiyo kunaile kupata mafunzo ya awali na kupata mafunzo makubwa zaidi. Jambo kubwa ambalo ningependa leo Waheshimiwa Wabunge mlifahamu ni kwamba katika suala zima la ujasiriamali wengi tunafikiria ni ile kufanya biashara, kuuzauza labda vitu au maduka na vitu kama hivyo. Lakini ujasiriamali tunachotamani hasa watu wakifahamu, ni ile namna gani mtu anafanya shughuli zake kwa njia tofauti ili kuongeza thamani, kiasi kwamba hata Waheshimiwa

Wabunge kufanya Ubunge pia ni ujasiriamali wa aina yake. Kwa hiyo, naomba tulizingatie katika sura hiyo.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nishukuru kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri ameweka vizuri swali ambalo nilitaka kuuliza, ni hiyo hiyo kwamba kuja na misamiati ambayo mwisho wake tunaona kama tunakwama na pale mwanzo akazungumzia mpaka suala la bajeti. Lakini ni vipi Serikali sasa itarudisha katika shule za msingi na sekondari yale mafunzo au taratibu za elimu ya kujitegemea ambapo watoto walikuwa wanajifundisha kupika maandazi, kufuga kuku, kutengeneza mifuko na kazi kama hizo, hizo hazihitaji bajeti wala hazihitaji misamiati lakini watoto wakitoka pale wana ujuzi. Ni lini Serikali itafanya hivyo? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kupitia stadi za kazi wanafunzi wamekuwa wakipata muda wa kujifunza masomo kama hayo. Lakini kuna wakati sera zetu huwa zinakuwa kama zina mgongano kidogo. Kwa mfano kuna wakati tulisema kwamba wanafunzi wasipewe kazi, watoto wasipewe kazi, watu wakachukulia hiyo ni kufuta mpaka hizo stadi za kazi. Lakini kwa kuacha kufanya hivyo, tumejikuta tumerudi nyuma. Kwa mfano, katika shule tunazosema kwamba wazazi wachangie chakula, kwa kweli kupitia mashamba hasa kwa shule zile ambazo zina maeneo huko vijijini wangeweza kulima mashamba yao na wakapata chakula, watoto huku wakiwa wanajifunza na wakati huo wanapata chakula.

Kwa hiyo, mimi nitoe rai yangu kwa shule zote kuona kwamba stadi za kazi hasa kulingana na mazingira yetu ni ya muhimu sana nawapongeza sana shule kama sekondari ya Rugambwa, wao wanafanya vizuri sana.*(Makofi)*

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Ni lini Serikali itarudisha mitaala ya shule za upili ili iweze kuzalisha mafundi mchundo na mafundi sadifu kama

ilivyokuwa zamani watu hawa walizewa kujitegemea? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nikiwa ni mnufaika katika eneo hilo niliweza kutembelea katika shule nyingi ambazo zinatoa mafunzo ya ufundi, ikiwemo Ifunda, Mtwara, Bwiru na kadhalika. Lakini kitu nilichojifunza ni kwamba zile shule baada ya kuzichanganya na wanafunzi ambao wanasoma kidato cha tano na cha sita imejikutwa kwamba kwa upande wa ufundi ni kama vile ufundi haupo. Vilevile baada ya kuwa *VETA* ina uwezo wa kuingiza wanafunzi moja kwa moja katika masomo ya ufundi sanifu.

Kwa hiyo, ilionekana lile eneo kama linakuwa *reduntant,* sasa baada ya hapo tuliita timu kutafakari namna gani tunaweza tukaendelea na shule hizo. Jambo tuliloliona ni kwamba kwa hali ya sasa ambayo elimu imeongezeka na shule nyingi zinatoa wanafunzi wanaofaulu vizuri mpaka kidato cha nne, tunafikiria kwamba hizo shule zirejeshwe katika kutoa mafunzo ya ufundi sanifu, lakini baada ya kujenga shule ambazo zitawachukuwa wale waliokuwa wanasoma kidato cha tano na sita ili kusiwe na upungufu katika eneo hilo, kwa hiyo hali halisi ndio hiyo.*(Makofi)*

Na. 268

**Matibabu Bure kwa Waathirika wa Matumizi ya Dawa za Kulevya**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Vijana wengi walioathirika na dawa za kulevya wanaleta kero kubwa ndani ya jamii, kutengwa na wazazi wao na kukosa msaada wa kifedha pale wanapoamua kuacha na kujiunga na kituo cha tiba.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa matibabu bure kwa vijana hao ili warudi katika hali zao za kawaida na hatimaye kuendelea na ujenzi wa Taifa?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa nchi yetu imeendelea kuwa na wimbi kubwa la ongezeko la matumizi ya dawa za kulevya katika sehemu mbalimbali hapa Tanzania, na hii hupunguza nguvu kazi ya Taifa na kudidimiza uchumi wa nchi yetu. Matumizi ya dawa za kulevya hasa kwa vijana yanaongezeka hapa nchini hasa katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Tanga, Arusha, Mwanza na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto imeendelea kutoa huduma kwa waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya hapa nchini bila malipo katika vituo mbalimbali vya umma vinavyotoa huduma hizo. Hivi karibuni Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imefungua vituo katika Hospitali ya Muhimbili, Mwananyamala na Temeke kwa Mkoa wa Dar es Salaam ambavyo vimeshahudumia waathirika takribani 3,000 kwa kuwapa tiba ya *methadone*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya dawa za kulevya, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani ilianza Mradi wa Utafiti wa Matumizi ya Dawa ya Methadone Hospitali ya Taifa Muhimbili mwaka 2011, na kuonyesha mafanikio makubwa na kufuatia kufunguliwa kwa vituo vya kutolea huduma za methodone katika Hospitali za Rufaa za Temeke na Mwananyamala. Upanuzi wa huduma hizi unaendelea kwa mikoa ya Mwanza na Mbeya ambayo itaanza kutoa huduma hizo hivi karibuni na mikoa mingine itafuata. Arusha, Tanga na Pwani wako katika hatua za awali za kuanza kutoa huduma hizo.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali kwa kuunda Tume ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya na kuongeza vituo vya tiba. *(Makofi)*

Swali langu la kwanza, Serikali baada ya kupiga marufuku uingizaji wa biashara za viroba na kuteketeza mashamba ya bangi, je, adhabu gani iliyowekwa kwa wale watakaoingiza viroba na wale watakaopanda mbegu za bangi katika mashamba yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, je, ni Mkoa gani unaoongoza kwa idadi ya vijana walioathirika zaidi kwa dawa za kulevya? Na Serikali inawaangaliaje vijana hao baada ya kupona? Watawapa msaada gani ili waweze kujiendeleza na maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, adhabu gani watapata; adhabu zimeainishwa kwenye sheria zetu, tuna sheria inayozuia matumizi ya vilevi, hususan dawa za kulevya *(The Narcotic and Drug Abuse Act)* kwa hivyo, ndani mle imeainishwa adhabu ya mtu anayetumia na mtu anayeingiza na mtu anayesaidia kuwezesha mambo hayo. Kwa hiyo, adhabu itatolewa kwa mujibu wa sheria hizo, sikumbuki ni adhabu yenye ukubwa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali lake la pili, ni Mkoa gani ambao unaongoza; Mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi kuliko mikoa yote, ukifuatiwa na majiji mengine na sasa Serikali inachukua hatua gani kuwasaidia watu ambao wameathirika na dawa za kulevya. Mikakati tuliyonayo ni kama hii ya kuanzisha kliniki za kutoa dawa ya *methadone.* Hii dawa ya *methadone* inasaidia sana kwa wagonjwa kuacha kutumia hizi *opioids* kwa sababu *methadone* na yenyewe ni katika *group* hilo

hilo la *opioids,* lakini uzuri wa *methadone* haisababishi utegemezi kama zile dawa nyingine. Kwa sababu dawa hizo nyingine kama *heroin* na *cocaine* zinasababisha utegemezi ambapo utegemezi ule unaweza ukaondolewa na dawa nyingine ambayo inafanya *replacement* ya dawa zile, kwa hiyo, mtu anaweza akaacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ni la kwanza, lakini la pili, ni kuwasaidia kwenye shughuli mbalimbali za kurudi kwenye jamii, kama kushiriki kwenye ufundi na kuwapa mafunzo mbalimbali, ili waweze kuwa *intergrated* kwenye jamii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib, halafu Mheshimiwa Amina.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nichukue nafasi hii kuwapa pole wananchi wangu waliopotea na chombo baharini, leo ni wiki hawajaonekana, niwaombee Mwenyezi Mungu awajalie kama bado wako hai awafanyie wepesi na kama wamefariki awaweke pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiona azma nzuri ya Serikali katika kupambana na dawa za kulevya; na ninaisifu sana, naipongeza Wizara hii kwa usimamizi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kukinga ni bora kuliko kutibu, kwa muda mrefu imesemekana na ni ukweli usioshaka kwamba, Zanzibar imekuwa ni lango kuu la kupitisha dawa za kulevya. Tumeona juhudi ya Serikali pale inapowaonea huruma wananchi wake wa Zanzibar katika mambo tofauti mbalimbali yanapojitokeza. Je, ni lini Serikali itachukua kwa makusudi jitihada za kuiweka Zanzibar katika uangalizi maalum wa kukomesha kuwa *corridor* muhimu ya kupitisha dawa za kulevya ambazo uingiaji wake na matumizi yake makubwa inakuwa ni hapa Tanzania Bara? Ni lini Serikali itaonesha kujali na kuchukua hatua madhubuti kukomesha janga la Zanzibar kuendelea kuwa uchochoro wa dawa za kulevya? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niungane na yeye kumpa pole juu ya wananchi wake waliopotea na boti.

Lakini la pili, jibu lake kwenye swali lake ni kwamba nakubaliana na yeye Zanzibar kwa muda mrefu imekuwa ni *corridor* ya dawa za kulevya, lakini kwenye mikakati ya kupambana na dawa za kulevya kuna maeneo mawili; kuna *supply reduction* na kuna *demand reduction,* kwa hiyo, kwenye *supply reduction* wenzetu wa Tume ya Dawa za Kulevya ambayo inaongozwa na Kamishna Siang'a wanaongoza mapambano kweye eneo hilo na mikakati yao zaidi ni ya kiintelijensia na mambo mengi wanayoyafanya hayasemwi hovyo hovyo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nikuhakikishie tu Mheshimiwa Khatib, Tume kwa sasa kwa kweli imepunguza sana *supply* ya dawa za kulevya kwenye nchi yetu, ikiwemo kule Zanzibar. Na hilo wala halina shaka na huo mfereji unaousema kwa hakika kwa sasa umezibwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye *demand* ni kutoa tiba na kuwasaidia kwenye *impact reduction. (Makofi)*

**MWNEYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Amina halafu Mheshimiwa Kabati.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kupambana na dawa za kulevya.

**MWENYEKITI:** Subiri Mheshimiwa Amina.

Mheshimiwa Waziri, wewe ndio mhusika mkuu, ngoja waulize halafu wewe utamalizia. Endelea Mheshimiwa Amina.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa mara ya pili tena.

Ni kwamba naipongeza Serikali kwa jitihada zake. Na vijana hawa wanapoathirika na hizi dawa za kulevya moja kwa moja tayari wanaingia katika kundi letu, kwa maana ya kundi la watu wenye ulemavu. Na kwa sababu wimbi ni kubwa kwa hivi sasa, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inaongeza Madaktari Bingwa kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa hawa walioathirika na dawa za kulevya? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, kuna bado moja Mheshimiwa Ritta Kabati, maana ukijibu uyajibu yote. Mheshimiwa Ritta Kabati!

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu majibu yake alisema kwamba, kwenye miji mikubwa kuna hiyo huduma inatolewa, lakini ukija kwenye miji midogo kwa mfano Iringa kuna vijana wengi sana wameathirika. Lakini tumshukuru sana Dkt. Ngala pale Iringa, ameweza kuhamasisha wananchi wamefungua vituo kama hivi, lakini sasa wananchi wanashindwa gharama imekuwa kubwa sana kwenda kwenye vituo.

Sasa je, Serikali iko tayari kutoa ruzuku kwa watu ambao wamenzisha vituo hivi ili viweze kusaidia kwenye miji midogo kama Iringa?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nijibu maswali haya mawili, Mheshimiwa

Waziri wa Nchi atamalizia kwa ujumla yanayohusu *supply reduction.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la kwanza la Mheshimiwa Amina Mollel, kwanza nimpongeze siku ya jana aliniletea wageni kutoka Chama cha Wananchi ambao wanajihusisha na Afya ya Akili Nchini na katika mazungumzo tuliyoyafanya ni pamoja na hili suala la Madaktari Bingwa wa Afya ya Akili kwenye Mikoa nchini. Mkakati tulionao na ndio taarifa niliyowapa wale wananchi wenzetu ni kwamba Serikali ina-*scale up* huu mkakati wa kuwa na hizi kliniki kama iliyopo Muhimbili, Temeke na Mwananyamala kwa mwaka huu kwenye mikoa kumi ya Tanzania Bara na kwa mwaka ujao tutaongeza mikoa mingine kumi, tunakwenda kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, kila tutakapoanzisha hii kliniki ya *methadone* ni lazima awepo Daktari Bingwa anayehusika na ku-*administrate* hiyo dawa kwa sababu *methadone* inalindwa kwa taratibu maalum za kuitunza na kuitoa kwa wagonjwa. Kwa hiyo, ni lazima awepo Daktari Bingwa anayeweza kufanya hivyo kwa hivyo, kwa mwaka huu nimhakikishie Mheshimiwa Amina Mollel kwamba tutakuwa na Madaktari Bingwa kwenye mikoa kumi ncjini, pindi kliniki za *methadone* zitakapoanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni la Mheshimia Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kuhusu hizi kliniki na *rehabilitation centres* kwenye Mikoa; kwa sasa kweli, tuko Dar es Salaam peke yake, lakini kwenye mkakati wetu tunakwenda kwenye mikoa kumi kama nilivyosema. Na kwenye kila kanda tunakwenda kuanzisha *rehabilitation centre* ambapo tutakuwanazo nne sasa katika nchji nzima. Kwa hivyo, hii ni mikakati ambayo tunayo katika siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ruzuku, Serikali haina utaratibu wa kutoa ruzuku kwenye taasisi mbalimbali za binafsi, kwa sababu wao wanafanya kwa hiyari na tunawaomba na kuwatia moyo waendelee kufanya hivyohivyo kwa hiyari, lakini sisi kama Serikali tuna mikakati

yetu ya kuwasaidia wenzetu ambao wameathirika na dawa za kulevya.

**MWENYEKITI:** Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba nijibu maswali ya nyongeza yaliyoulizwa kwa umoja wake, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwanza nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, kwa majibu mazuri aliyokwishakuyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tena kwa kulipongeza Bunge letu Tukufu kwa sababu mwaka 2015, ndilo lililosababisha kufanyika kwa mageuzi makubwa ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini kwa kutungwa kwa sheria mpya ambayo imeunda hiyo mamlaka sasa ambayo tumemuona Kamishna Jenerali akifanya kazi kubwa sana kwa kushirikiana na makamishna wenzake kuhakikisha kwamba tunapambana na tatizo la dawa za kulevya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niliarifu Bunge lako Tukufu Kamishna Jenerali baada ya kuteuliwa na mamlaka kuanza kazi rasmi, ameshahakikisha ametengeneza Mpango Mkakati Maalum wa Taifa wa kuhakikisha kwamba tatizo hili la dawa za kulevya nchini linaondoka. Na mpango mkakati huo unashirikisha pande zote mbili za Muungano, upande wa Zanzibar na upande wa huku Bara. Kwa hiyo, Mheshimiwa Khatib wala usiwe na wasiwasi, tunafanya kazi hizi kwa pamoja, vyombo hivi vyote viwili vinafanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumegundua kwamba, wenzetu wa *private sector* wanafanya kazi nzuri sana kwenye mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini. Na hivyo nichukue nafasi hii kwanza niwapongeze wale wote ambao

wameamua kujitolea kusaidiana na Serikali katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika mwaka huu wa bajeti, Ofisi ya Waziri Mkuu imeamua kuweka bajeti kidogo ambayo itasaidia kushirikiana na hao wenzetu ambao wameonesha kwamba, wana nia ama ya kuanzisha *sobber houses* kwa ajili ya kuwasaidia hawa walioathirika na dawa za kulevya, lakini vilevile kufanya kampeni na kuleta uhamasishaji mkubwa wa kuwasaidia vijana wetu kuwaondoa kwenye tatizo hili.

Kwa hiyo, tuko pamoja tunafanya kazi hii kwa pamoja, mapambano yanaendelea na tunataka kuona kwamba tunaondoa tatizo hili katika nchi yetu. *(Makofi)*

Na. 269

**Tatizo la Mawasiliano ya Simu Jimbo la Lulindi**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** aliuliza:-

Serikali iliahidi kuweka minara katika Kata ya Sindano, Mchauru, Lipumbiru na Lupaso.

Je, ni lini minara hiyo itajengwa ili kuondoa tatizo la kutokuwa na mawasiliano katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote iliingia mkataba na Kampuni ya *TTCL* kufikisha huduma ya mawasiliano katika Kata za Lupaso na

Lipumbiru kwa ruzuku ya dola za Kimarekani 94,000. Ujenzi wa mnara huo ulikamilika tangu mwezi Machi, 2015 na kuanza kutoa huduma. Hata hivyo, baada ya mnara huo kuwaka Kampuni ya *TTCL* inaendelea na taratibu a kubadilisha masafa kutoka teknolojia ya *CDMA 800 Mhz* kwa lengo la kukabiliana na changamoto iliyopo katika teknolojia hiyo ya *CDMA* katika kutoa huduma za ziada kwa wateja, ikiwa ni pamoja na huduma za *mobile money, mobile banking,* na kadhalika. Kampuni ya *TTCL* inaendelea kuboresha upatikanaji wa mawasiliano kwenye eneo la Lipumbiru na Lupaso na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Simu za Mkononi ya *Viettel* itafikisha huduma ya mawasiliano katika kata za Sindano na Mchauru, kwa mujibu wa makubaliano baina ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Kampuni hiyo. Kwa upande wa kata ya Mchauru yenye vijiji vya Mchauru, Mhata, Mirewe na Namombwe iliingizwa katika zabubi ya mfuko ya kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo ya mipaka iliyofunguliwa tarehe 27 Aprili, 2017 ambapo kampuni itakayopewa jukumu la kufikisha mwasiliano kwenye kata hiyo ya Mchauru itajulikana mara tu baada ya taratibu za tathmini kukamilika.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninaomba sasa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba, *TTCL* walishalipwa fedha za sola za Kimarekani 94,000 na ilikuwa ni mwaka 2015. Je, Serikali kwa nini haijawasisitiza *TTCL* kukamilisha kazi hii ambayo imechukua muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, miongoni mwa kata ambazo Kampuni ya *Viettel* ilikuwa imeshinda zabuni mwaka 2015 ni pamoja na kata ya Sindano, lakini hadi sasa kazi hiyo haijafanyika. Je, Mheshimiwa Waziri atalithibitishia Bunge hili kwamba *Viettel* watakwenda kufanya hiyo kazi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeisisitiza sana *TTCL* ikamilishe kazi iliyoianza. Na kama utarudia tena sehemu ambayo nilijibu swali la msingi ni kwamba, kazi hii waliikamilisha, lakini waliikamilisha kwa kutumia teknolojia ya *CDMA* na sasa wanaondoka katika teknolojia hii ya *CDMA* kwa sababu teknolojia hii haiwawezeshi wao kuongeza hizi huduma za nyongeza za *mobile money* na *banking* kwa hiyo, wanabadilisha mtandao na mtakumbuka kuna wakati hapa Dodoma walizindua ile ya *4G LTE* kwa hiyo, sasa wapo katika mpango huo wa kuzindua huo mtandao mpya na hivyo kazi hiyo tutahakikisha inakamilika mapema kama ambavyo wao wameahidi *by June, 2017* watakuwa wamefika kule Lupaso na Lipumbiru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu *Viettel,* ninafahamu *Viettel* wamekuwa na matatizo kidogo kwa sababu ya mikataba na tunarekebisha kwa sababu, kuna baadhi ya kodi walikuwa wanatarajia wasilipe. Kwa hiyo, wameingiza vifaa vyao vya kuweza kutuletea mawasiliano, lakini vimekwama kidogo kwa sababu ya malipo ya kodi na tutahakikisha hilo linasuluhishwa haraka, wanalipa kodi inayotakiwa, ili hatimaye vifaa hivyo viende vikafanye kazi, vikasimikwe kule kulikokusudiwa.

**MWENYEKITI;** Ahsante, Mheshimiwa Aida Khenani, Dkt. Mponda na Mheshimiwa Oliver.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuwa, ni Wizara hiyohiyo ya Uchukuzi, ingawa niliomba swali namba 70.

Kwa kuwa mawasiliano ni haki ya kila Mtanzania, lakini toka nchi imepata uhuru kuna maeneoa ambayo hayajapata mawasiliano, ikiweko kata ya Kala na Ninde. Ni lini Serikali itatimiza wajibu wake wa kupeleka mawasiliano katika hizo kata, ikizingatia ziko pembezoni? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie

Serikali ina nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba vijiji vyote vinapata mawasiliano na ndio sababu kubwa ya kuanzisha huu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Kwa hiyo, mara tutakapopata fedha tutakuja huko ambako Mheshimiwa Aida umekueleza.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yanayowakumba wakazi wa Lulindi, Masasi, yanafanana kabisa na wakazi wa Wilaya ya Malinyi katika kata za Sufi, Kilosa Mpepo; swali langu, kata hizo ninazozitaja ni kwamba kama alivyosema jibu la msingi Mheshimiwa Waziri, kwamba, kupitia Mfuko wa Fursa ya Mawasiliano kwa Wote *(UCAF)*, wamejenga minara miwili katika Kata ya Ngoeranga na kata ya Sufi, lakini minara hiyo ambayo imejengwa chini ya Tigo haifanyi kazi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali nangu. Je, ni lini Serikali watarekebisha minara hiyo na vilevile kumalizia Kata zile mbili ambazo hazina mawasiliano kabisa, kata ya Sufi na kata nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwakikishie kwamba kata hizo mbili alizozieleza ambazo hazina mawasiliano kabisa ikiwa ni pamoja na kata ya Kilosa Mpepo, tutahakikisha kwamba tunazifikishia mawasiliano kwa kadri tutakapopata fedha na maadamu ulishawasilisha hilo mapema Mheshimiwa Mponda nadhani utakumbuka Mheshimiwa Waziri wangu alivyokujibu na nikuthibitishie lie jibu alilokupa Waziri wangu na mimi nitalifuatilia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mponda kuhusiana na kata mbili ambazo...

**MWENYEKITI** : Mheshimiwa jibu moja tu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Alitaja kata nne na nimeongelea kata mbili, kata hizo mbili ambazo Tigo wamejenga minara nitazifuatilia kuhakikisha kwamba minara hiyo inafanya kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimwia Deo.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa suala la Lulindi linafanana kabisa na tatizo lililoko katika jimbo la Makambako. Makambako kuelekea usawa wa kwenda Mbeya ni kilometa mbili eneo moja linaitwa Majengo hakuna mawasiliano. Kilometa tano kuelekea usawa wa kwenda Njombe kijiji chenye eneo la Kyankena Kiumba hakuna mawasiiano; Kitandililo Mawandea hakuna mawasiliano. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka minara hii ilimawasiliano yaweze kupatikana katika maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliongea na Mheshimiwa Deo Sanga kutokana na matatizo hayo na matatizo hayo yanatokanana maeneo yenye mteremko kwa hiyo mawasiliano yaliyopo katika eneo hili kuna maeneo ambayo hayana mawasiliano kwa sababu yako chini. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba kwanza kama nilivyokuambia nitapenda nipite hayo maeneo barabara hiyo nikajionee halafu baada ya hapo tuwatake watu wa Mawasiliano kwa Wote wajaribu kurekebisha hayo maeneo ambayo ni ya mteremko tunawezaje kuyapelekea mawasiliano.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali ya nyongeza.

Tatizo la mawasiliano lililopo Lulindi linafanana na tatizo lililopo katika jimbo la Lupembe Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Katika Halmashauri tuna kata nne ambazo hazina mawasiliano kata za Ninga, Ikondo, Ukalawa na Mfiriga hakuna minara na hakuna mawasiliano, je, ni lini Serikali itajenga minara katika kata hizi ili wananchi waweze kupata mawasiliano kwa kuwa inawaathiri kiuchumi kutokana na kutokuwepo mawasiliano? Naomba majibu ya Serikali. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kila kijiji Tanzania kinafikishiwa mawasiliano. Na ndio dhamira ya kuanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Kwa hiyo, nikuhakikishe Mheshimiwa Mbunge tutayafikisha mawasiliano katika maeneo hayo uliyoyataja mara tutakapopata fedha za kutuwezesha kufikisha mawasiliano maeneo haya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

Na. 270

### Hitaji la Mawasiliano

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Kuna maeneo ambayo hayana kabisa mitandao ya mawasiliano huko Mpanda Vijijini hususan kata ya Katuma, Sibwesa, Mwese na maeneo ya Bujumbo, Kapanda pamoja na Wilaya ya Mlele kata ya Ilunde.

Je, ni lini Serikali itawapelekea mawasiliano wananchi wa maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote uliviainisha vijiji vya Kata za Katuma na Sibwesa na kuviingiza katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya mawasiliano vijijini.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba utulivu ndani ya Bunge,

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Kata ya Katuma imekwishafikishiwa huduma ya mawasiliano na Kampuni ya Simu ya Vodacom ambapo shughuli za ujenzi wa mnara zilikamilika mwezi Septemba kwa ruzuku ya dola za Kimarekani 236,700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kijiji cha Sibwesa katika kata ya Sibwesa tayari kimefikishiwa huduma ya mawasiliano kupitia kampuni ya simu ya Vodacom kwa rukuzu ya dola za Kimarekani 90,411 ambapo utekelezaji wa mradi ulikamilika tarehe 23 Mei, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, vijiji vya Ligonesi, Lwesa katika kata ya Mwese vimeshafikishiwa huduma ya mawasiliano kupitia mtandao wa Viettel (Halotel). Ujenzi wa mnara kwa ajili ya vijiji vya Nkungwi na Kabage vilivyoko katika kata ya Sibwesa uko katika hatua za mwisho kukamilika. Kata ya Ilunde yenye vijiji vya Ilunde na Isengenezya pamojana vijiji vya Kasekese vitaingizwa katika orodha ya utekelezaji wa mradi ya siku za usoni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lupembe, ajiandae Mheshimiwa Ulega.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano sasa hivi kwa wananchi ni uchumi. Kwa sababu wananchi sasa hivi wanafanya mawasiliano kwa mambo mengi ya kibiashara ya mawasiliano ya magonjwa na kila kitu na vilevile mawasiliano ninafikiri kama hakuna sehemu hakuna mawasiliano hakuna maendeleo. Katika kata za Sibwesa na Kasekese wameweka minara tayari toka Mei na pesa zimashatumika sasa ni lini Serikali itawasha kwa sababu wananchi wanaona ile minara lakini haina faida katika muono wao?

Swali la pili, wananchi wa Ilunde wameahidiwa kwa muda mrefu sana kuhusu mawasiliano. Na ukiangalia kata ya Ilunde iko katikati ya pori ina maana wananchi wale maisha yao yako hatarishi na wengine wanakwenda kupanda kwenye miti, wengine wanadondoka wanavunjika mikono na miguu kwa ajili ya kutafuta mawasiliano. Ninaomba kauli ya Serikali, ni lini sasa Serikali itawajengea mnara kata ya Ilunde? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Mheshimwa Mbunge kwamba mawasiliano ni biashara na nakubaliana naye kwamba ni muhimu sana kuwe na mawasiliano maeneo yote na kama nilivyosema katika majibu yangu ya swali la msingi kwamba Serikali nia ya dhati ya kuhakikisha tunapeleka mawasiliano kila sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nikiri kwamba mikoa mitatu hii ya Songwe, Rukwa na Katavi sijaizungukia sawa sawa ili nijue hasa matatizo yake katika sekta zote tatu. Nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kikao hiki cha Bunge la Bajeti nitafika katika mikoa hii mitatu hususan katika kijini hiki cha Ilunde nione na nipate hali halisi. Na mimi nijisikie hali...na hatimaye tupange mipango ya kuondoa matatizo haya.

**MWENYITI:** Ahsante Mheshimiwa Ulega atafuatia Mheshimiwa Oliver.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa rufsa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo haya yaliyopo kwenye Mkoa wa Katavi yako pia katika imo jimbo langu la Mkururanga kilometa 60 tu kutoka katika Mkoa wa Dar-es salaam ambapo kata za Kwanzuo Kisegese, Mkamba na kwingineko ikiwa ni pamoja na kijiji ambacho wewe unalima kijiji cha Koragwa Tundani na pale Mkuranga maeneo ya Kiguza. Yote yana shida ya mawasiliano.

Je, Mheshimiwa Naibu yuko tayari yeye na hao viongozi wa huo Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kushirikiana name kuhakikisha maeneo haya yanapata mawasiliano? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa dhati kabisa niko tayari.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Oliver ajiandae Mheshimiwa Anna.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona niulize swali ndogo la nyongeza. Matatizo ya usikivu wa simu yaliyopo Mpanda vijijini ni sawa na yaliyopo Wilaya ya Ngara kata Muganza, Nyakisasa Keza, Kabanga na Rusumo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha usikivu wa simu katika kata hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, ajiandae Mheshimiwa Anna.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Serikali ina nia ya dhati kabisa yakufikisha mawasiliano kila

sehemu na hasa, eneo hili analoliongelea ni maeneo ya mpakani na maeneo ya mpakani tuna utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba mawasiliano yanafika haraka katika maeneo hayo. Kwa hiyo Serikali itahakikisha inafikisha mawasiliano mara fedha zitakapozipata.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Anna.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Matatizo yaliyoko Katavi yanafanana sana na matatizo yaliyoko katika Jimbo la Babati Vijijini kata ya Duru vijiji vya Endagwe, Hoshan, Ameyu, Eroton na Wikanzi maeneo haya hayana mawasiliano ya simu. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri ni lini maeneo haya yatapewa vipaumbele ukizingatia uwanja wa ndege wa Manyara unapelekwa Mwikanzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, anataka kujua ni lini tu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, mara tutakapopata fedha tutahakikisha tunapeleka mawasiliano katika maeneo haya ya Mkoa wa Manyara na hasa maeneo hayo ambayo tuna kusudia kujenga uwanja wa ndege kama ambavyo Mheshimiwa Anna umeyaeleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kakoso.

Na. 271

**Kupandishwa Hadhi Barabara ya Mishamo**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Barabara ya Mishamo imeombewa kibali ili ipandishwe hadhi na kuwa barabara ya Mkoa lakini hadi sasa hatujui kinachoendelea.

Je, ni lini barabara hiyo itapandishwa hadhi na kuwa chini ya *TANROADS?*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandishwaji hadhi wa barabara hufanywa kulingana na Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 pamoja na kanuni zake za mwaka 2009 ambapo maombi yanatakiwa kuwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana na Wizara ya Ujenzi kupitia kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano haijapokea maombi ya kupandishwa hadhi barabara ya Mishamo. Hata hivyo, Wizara yangu itaifanyia tathmini barabara hii iwapo inakidhi vigezo vya kupandishwa daraja na kuchukua hatua stahiki kulingana na matakwa ya sheria.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa taratibu zote za kuipandisha hadhi barabara hii zilishafanyika ikiwemo kupitia vikao halali vya Wilaya na Mkoa na kikao cha *Road Board* mimi mwenyewe nilishiriki tukaipitisha hii barabara. Nilikuwa nataka kuuliza ni sababu ipi inayokwamisha kutokupandishwa hadhi kwa barabara hii?

Pili, kwa kuwa Mheshimiwa Rais wakati anaanza safari ya ushindi ya kuomba ridhaa ya wananchi, ziara yake ya kwanza aliifanya Mkoa wa Katavi na kituo cha kwanza alianzia maeneo ya Mishamo aliwaahidi wananchi wa Mishamo kuwaboreshea barabara hiyo ya kutoka Mishamo mpaka Ziwa Tanganyika kwenye jimbo la Mheshimiwa Hasna Mwilima.

Je, hawaoni sasa ni wakati muafaka wa kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, ambayo aliwaahidi wananchi wa Mishamo ili kutekeleza ahadi iliyokuwa ameiahidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukurusana Mheshimiwa Moshi Kakoso kwa sababu itabidi nikapate ukweli ama mkoa haujawasilisha Wizarani ama pale Wizarani pana uzembe. Kwa hiyo, nitakwenda niangalie na nifuatilie hili suala kama kikao halali kilishakaa kwa nini Wizarani hatujapata hayo maombi.

Kwa hiyo, baada ya hapo nikishajua *wether* kuna tatizo Mkoani inawezekana walikaa lakini hawakuwasilisha au pengine pale Wizarani kuna tatizo.Nitakapopata jibu mtaona matokeo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Mishamo kwenda mpaka Baharini ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, wakati wa kampeni tumeipata tunayo katika orodha ya ahadi tulizonazo, nikuhakikishie kwamba tunakwenda awamu kwa awamu katika kutekeleza ahadi zote ambazo tuliziahidi katika kipindi hiki cha miaka mitano. Tutahakikisha ahadi hiyo nayo tutaitekeleza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlinga.

**MHE.GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Sasa hivi ninavyoongea barabara ya Ifakara - Mahenge haipitiki kabisa, wananchi wanakosa huduma za muhimu kama petroli, dizeli na dawa kwa ujumla. Je, wananchi wa Ulanga wanataka kusikia kauli ya Serikali nini kitafanyika sasa hivi ili watu hawa wa waweze kusafiri kwenda Mahenge? *(Makofi)*

**MWENYEKITI.** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuitaka *TANROADS* Taifa na *TANROADS* Mkoa wa Mogororo washughulikie ufunguzi wa barabara hii iliyokatika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bwagala, hayupo. Mheshimiwa Waitara, halafu Mheshimiwa Julius.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Barabara ya kutoka Kitunda - Kivule - Msongola ninapozungumza sasa hivi haipitiki kabisa nauli imepanda kutoka shilingi 500/= mpaka shilingi 1,000/=; walimu na wanafunzi ambao wanasoma shule ya Mvuti, Mbondole, Kitonga wanatembea kwa miguu kwa umbali wa zaidi ya kilometa 11.

Ningeomba kujua ni hatua gani kwasasa Mheshimiwa Waziri unaweza akachukua kuwasaidia wananchi wale na hasa watumishi wa umma ili waweze kuendelea kupata huduma muhimu katika eneo hilo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafurahi sana hawa Wabunge wawili wanafanyakazi pamoja ikiwa ni pamoja na Mbunge Bonnah Kaluwa, Mbunge wa Segerea. Alishalileta hilo na kwa taarifa yako *TANROADS* Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na *TANROADS* Taifa hivi tunavyoongea wanalishughulikia hilo kwa namna ambayo lililetwa kwetu na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kafumu

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize swali ya nyongeza kwamba barabara ya kutoka Igurubi mpaka Igunga kwenda Loya

tuliiombea na tulishapeleka maombi kwamba ipandishwe hadhi. Leo mwaka wa tano kuna shida gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya kupandisha hadhi barabara tunayoyashughulikia sasa ni ya muda mrefu ya kuanzia mwaka 2011/2012 mpaka sasa. Kwa hiyo, nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara yako nayo tutakuja kutoa majibu ipi imekubalika kupandishwa hadhi, ipi imekubalika kukasimiwa na ipi tutapendekeza ibakie kwenye Halmashauri, muda sio mrefu maadamu Waziri wangu tayari ameshaanza kulifanyia kazi kwa kasi inayotakiwa kwa sasa...

**MWENYEKITI:** Ahsante ameshakuelewa, Mheshimiwa Kigola, halafu Mheshimiwa Komu.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigola halafu Mheshimiwa Julius, subiri.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize kwali la nyongeza. Kuna barabara ya kutoka Nyororo – Igohole mpaka Mtwango ina kilometa 40 na upembuzi yakinifu ulishafanyika miaka miwili iliyopita. Je, Serikali ni lini itaanza ujenzi wa kiwango cha lami ile barabara? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane tupate takwimu sahihi ya barabara unayoongelea inaanzia wapi, inafikia wapi, ina kilometa kiasi gani na kama imeshajadiliwa kwenye *Road Board* ya Mkoa ili hatimaye tutende haki ya kile kinachotakiwa katika barabara hiyo.

**MWENYEKITI:** Subiri hapo hapo utapata taabu, Mheshimiwa Julius halafu Mheshimiwa Komu.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:**Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize swali kwamba kwa kuwa ahadi za Rais wakati anaomba kura zimekuwa nyingi na Serikali imekuwa ikitoa ahadi ya kuzitekeleza ikiwepo barabara ya Monduli Juu kule kwa Sokoine. Ni kwa nini Serikali sasa isilete programu maalum inayoonyesha ni lini ahadi hizo zitatekelezwa na fedha zake katika nchi nzima? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi zote ambazo Mheshimiwa Rais alizitoa wakati wa kampeni tunazitekeleza awamu kwa awamu, hatuwezi kuzitekeleza zote katika kipindi cha mwaka mmoja. Kuna kipindi cha miaka mitano na tutahakikisha...

**MWENYEKITI:** Ameshakuelewa, ahsante, Mheshimiwa Komu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** ... ahadi zote tunazitekeleza.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kwa hali ilivyo sasa hivi Moshi Vijijini barabara nyingi hazipitiki na hali ni mbaya sana katika kata ya Mabogini barabara inayoanzia Bogini kwenda Chekereri mpaka kule Kahe na kule Uru Mashariki kata ya Uru Madukani, Mamboleo, Kishumundu mpaka kule Materuri. Hizi barabara zote zimeshaombewa kupandishwa daraja lakini hakuna kinachoeleweka. Sasa ninataka kufahamu kutoka kwa Waziri atakuwa tayari kutoa agizo kwa ajili ya kufanyika tathmini maalum ili hizi barabara tujue tatizo liko wapi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaamini

Halmashauri iendelee kurekebisha hii barabara iweze kupitika muda wote, lakini wakati huo huo majibu ya barabara zipi tutapandisha hadhi yatakuja muda sio mrefu ujao.

Na. 272

**Hati za Hakimiliki ya Kimila Kutumika Kama Dhamana ya Kupata Mikopo Benki**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Lengo la Serikali ni kuwainua kiuchumi wananchi maskini vijijini hasa wanawake ambao hawana dhamana ya kuweka benki ili waweze kupata mikopo kwa sababu nyumba nyingi za vijijini hazina Hatimiliki ambazo zingeweza kutumika kama dhamana benki.

Je, Serikali inawasaidiaje wananchi na hasa wanawake kwa kuzungumza na benki ili zikubali kukpokea Hatimiliki za kimila kama dhamana ya mikopo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa Hatimiliki za kimila ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999 na kanuni zake. Utoaji wa hati za Hakimiliki ya kimila ulianza mwaka 2004 Wilayani Mbozi na baadae uliendelea katika Wilaya zingine ambapo hadi sasa takribani hati za Hakimiliki za kimila 400,761 zimekwishatolewa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 18(1) cha Sheria ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999, hati za Hakimiliki za kimila zina hadhi sawa kisheria na hati inayotolewa na Kamishna wa Ardhi. Hadi sasa hati za Hakimiliki za kimila zimewezesha wananchi kupata mikopo yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 59 kutoka taasisi mbalimbali za fedha ikiwemo *NMB, CRDB, TADB, Stanbic Bank, Meru Community Bank, Agricultural Trust Fund Bank, SIDO, NSSF* na Mfuko wa Pembejeo katika Wilaya ya Mbozi, Iringa, Babati, Bariadi, Arumeru, Mbarali, Manyoni, Kilombero, Bagamoyo, Mbinga na Tandahimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, baadhi ya taasisi za fedha zimekuwa hazikubali kupokea hati za Hakimiliki ya kimila kama dhamana kwa wananchi kupata mikopo. Sababu ambazo zimekua zikitolewa na taasisi hizo ni pamoja na baadhi ya maeneo kutokuwa na thamani au ardhi husika kutoendelezwa; vikwazo katika kuuza dhamana pale mkopaji anaposhindwa kurejesha mkopo kutokana na sharti la kutaka ardhi iuzwe kwa mkazi wa kijiji husika na baadhi ya wamiliki wa ardhi kutokuwa na sifa za kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizo, Wizara yangu kupitia marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 yanayoendelea inaangalia uwezekano wa kuondoa vikwazo vinavyozuia uuzaji wa dhamana pale mkopaji anaposhindwa kurejesha mkopo pamoja kuzungumza na taasisi za fedha kuwa hati ya Hakimiliki ya kimila ina hadhi sawakisheria na hati inayotolewa na Kamishna wa Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wananchi hawana budi kuyaendeleza maeneo yao hususani yale yaliyopatiwa hati za Hakimiliki za kimila ili kuyaongezea thamani na hivyo kuzishawishi taasisi za fedha kuyakubali maeneo hayo kama dhamana ya mikopo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe, ajiandae Mheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya shida inayowapata wanawake ni mitaji na Serikali imeweka pesa nyingi sana kwenye mabenki ili wakope, lakini wanapotaka kwenda kukopa kwenye mabenki wanaambiwa wapeleke hati, wanapokwenda kutafuta hati kwenye Ofisi za Ardhi wanahangaishwa sana; wanaambiwa wapeleke vitu vingi sana na wanaambiwa milolongo ya mambo mpaka wanaamua kuacha, zaidi ya mwaka mtu anafuatilia hati. Ni lini sasa Serikali itaweka gharama halisi za kupata hati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Benki ya Wanawake ipo Dar es Salaam tu, ni lini sasa Serikali itaamua kufungua matawi mengine katika mikoa mingine ili wanawake wapate huduma hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna usumbufu katika kupata hati na hasa hizi Hakimiliki za kimila ambazo tunazizungumzia kwasababu shughuli yote inafanyika katika maeneo husika na katika vijiji husika. Kwa hiyo, mimi niseme pale ambapo Halmashauri yoyote inaonekana kwamba ni kikwazo katika kuwapatia wananchi hati za Hakimiliki za kimila tuwasiliane kwa sababu lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba mwananchi wa Kijijini tunamuwezesha kuweza kupata hati yake ya Hakimiliki ya kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwasababu ndio sehemu pekee ambayo inaweza kumkomboa na mpaka sasa kama nilivyosema hati 400,761 zimeshatoka ni kwasababu tu ya ushirikiano wa karibu sana na wenyewe baada ya kuwa tumewaelimisha kwamba hati zile

zinakwenda kuwakomboa katika shughuli za kimaendeleo. Kwa hiyo, pale wanapokwama naomba tuwasiliane ili tushughulikie.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali la nyongeza. Serikali ina mpango...

**MWENYEKITI:** Subiri, Mheshimiwa Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; naomba kujibu swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata na ninaomba majibu yangu yaende kwa wanawake wote wa Tanzania kwamba Benki ya Wanawake ilianzishwa kwa malengo ya kuwahudumia, lakini kwa sasa ina changamoto kubwa za kimtaji na tutafungua matawi mikoani pindi ambapo uwezo wetu wa kimtaji wa Benki ya Wanawake utakavyoimarika. Ila kwa sasa tulichokifanya ni kuhakikisha tunafungua vituo vya kuwahudumia na kuwawezesha wanawake kwenye mikoa zaidi ya 18 nchini ili kuwapa elimu ya ujasiriamali lakini pia mikopo midogo midogo isiyo na dhamana ambapo wanawake wanadhaminiana wao kwa wao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, baada ya majibu haya bado mna hoja? Mheshimiwa Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Serikali ina mpango kabambe wa kupima na kurasimisha ardhi nchi nzima na imekuwa ikishirikisha sekta binafsi katika kufanya hivyo. Aidha, kumekuwa na gharama kubwa sana katika upimaji na urasimishaji huo wa ardhi. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mapitio ya gharama hizo ili kuweza kuwapunguzia wananchi mzigo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zainab

anazungumzia habari ya gharama kubwa katika suala zima la upimaji. Lakini naomba nimkumbushe tu bajeti ya mwaka jana ilivyosomwa gharama zile zilishuka kutoka shilingi 800,000 kwa heka mpaka shilingi 300,000 kitu ambacho ilipunguza sana gharama zinaongezeka kulingana na ukubwa wa eneo ambalo linaenda kupimwa. Kwa mwaka huu pia katika bajeti yetu nadhani kuna maeneo ambayo Serikali imeyafanyia kazi mtayasikia wakati tunatoa bajeti.

Kwa hiyo, niseme kwamba gharama tunaziangalia na namna bora ya kuweza kumuwezesha mwananchi wa kawaida aweze kupima ardhi yake na kuweza kumiliki ili kumletea maendeleo katika shughuli zake.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Shally, halafu Mheshimiwa Mdee.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa Serikali kwa kutambua wanawake inakuwa vigumu kupata mikopo kwenye mabenki, imekuwa ikitoa hela na wakati mwingine pia ikipeleka kwenye mabenki, lakini wanawake wanakopeshwa kupitia kwenye vikundi vyao zikiwemo mabilioni ya JK.

Swali langu nauliza, wanawake wa vijijini hawakunufaika na hizo hela, sasa Serikali inafanyaje kuhakikisha kwa kuwa zile hela ni za mzunguko na bado tuna amini zipo, zitawafikiaje wale wanawake wa vijijini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa majibu kwa kifupi, ajiandae Mheshimiwa Mdee na Mheshimiwa Vulu; Waheshimiwa muda wetu umekwisha nakwenda tu sababu najua linwagusa sana wajasiriamali hasa wa jinsia hiyo mliosimama.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba sisi wote ni wajumbe katika zile Halmashauri zetu na mikopo inapopitishwa inapitia katika vikao vya Baraza la Madiwani.

Kwa hiyo, mimi naomba pale ambapo tunapitisha vikundi vyetu viweze kupewa mikopo ni lazima tuzingatie pia tunao akina mama wanaotoka katika maeneo ya Vijiji ili na wao waweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala la mabenki, benki wana masharti yao ambayo yanatakiwa yatimizwe, kwa hiyo tujaribu kuwaelimisha wakina mama ili waweze kukidhi vigezo vinavyotakiwa na mabenki na sisi wenyewe tuwe mstari wa mbele katika kuangalia ni vikundi vipi ambavyo vimekidhi vigezo hivyo na tuawasidie katika hatua za kuweza kupata mikopo *either* kutoka katika benki au kutoka katika Halmashauri kupitia ule Mfuko wa Wanawake na Vijana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, subiri hapo hapo Waziri; Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya asilimia 70 ya nguvu kazi ya kilimo ni wanawake, lakini ni kwa bahati mbaya sana inapokuja suala la umiliki wa ardhi, wanawake wanaomiliki ardhi ni pungufu hata ya asilimia 20. Na hata ninavyozungumza hati za kawaida na hati za kimila haziwanufaishi wanawake kwasababu sheria za nchi yetu zinatambua Sheria za Kimila ambazo zina ubaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka Wizara inisaidie katika mpango wenu mpana wa kuweza kufanya maboresho kwenye sekta ya ardhi mna mikakati gani ya kuweza kuondokana na sheria kandamizi ili umiliki wa ardhi usiwe na ubaguzi hivyo shughuli za uchumi zinufaishe makundi yote? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimhakikishie Mheshimiwa kwamba sheria zetu tulizo nazo sasa pamoja na kanuni pamoja na kwamba Sera ya Ardhi pia inapitiwa upya, hazikandamizi wala hazibagui mwanamke kuweza kupata hati. Ndio maana zoezi linaloendelea sasa la kutoa hati miliki za kimila kuna mahali

ambapo unakuta mke na mume wote wanakabidhiwa hati kwa pamoja, aidha wanakubaliana iandikwe jina la mke au iandikwe majina yote mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo tumeshaanza kuangalia kwa sababu wengi walikuwa wakinyanyasika katika hilo. Kwa hiyo, tunajaribu kupitia upya pia sera tuweze kuona lakini haya yote yanawezekana katika kufanyika ili kuweza kuhakikisha kwamba akina mama nao pia hawako nyuma katika umiliki wa ardhi. Ni kweli lilikuwepo tatizo hilo lakini limeanza kuondoka kwa taratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vulu...

**MHE.ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lukuvi, samahani kidogo kaa kwa sababu wewe ndio muhusika utayajibu yote kwa pamoja, utamtoa raha yule labda na yeye anahusika, Mheshimiwa Vulu halafu Mheshimiwa Lukuvi.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:**Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana; sambamba na wenzangu ni lini Serikali itakwenda vijijini kukutana na akina mama ambao wanahodhi maeneo mengi na maeneo hayo wanaweza wakaanzisha viwanda vidogo vidogo lakini unakuta wanakwama kwa kuwa hawana hati za kimila au zile za kiserikali ambazo zinaweza zikawasaidia kuwapa mikopo na wao kuingia katika uchumi wa viwanda? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumalizia kazi la Mheshimiwa Mdee, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri kwamba ni kweli sheria hazibagui, lakini pia hata kama akipata mwanaume hati ya kimila au hati ya muda mrefu, wakati wowote ule mwanamke ajue ile hati ni salama. Hii ni kwa sababu kwa utaratibu wa sasa mwanaume akitaka kuuza au kubadilisha ile hati hatumkubalii mpaka tumuulize mkewe na vilevile mwanamke akitaka kuuza lazima

tumuulize mumewe ili kuonyesha kwamba mali haipotei *whether* imeandikwa mwanaume au mwanamke wakati wa kupoteza lazima yoyote aulizwe. Kwa hiyo, mwanamke amelindwa sana katika sheria za sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Vulu nataka kukushauri tu kwamba hayo mashamba na maeneo ambayo wanawake wanamiliki au yapo kwenye mtaa au vijiji, washauri hao wanawake wajihusishe na mamlaka zinazohusika ndani ya Halmashauri ili wawapimie waweze kupata. Kama wapo mijini hawapati hati za kimila wanapata *Title Deed* za muda mrefu, lakini kama wapo vijijini wapete hati za kimila. Ardhi inapimwa na inamilikishwa na Halmashauri za Wilaya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru maswali yetu yamekwisha, huwa saa nyingine tunatoa nafasi nyingi ili na nyie muweze kusema hoja zenu, lakini kawaida maswali kwa kipindi cha bajeti mwisho ni saa nne, mnaona tumetumia zaidi ya dakika 35 ujue ni huruma ya kiti kwa sababu najua wengi mnalalamika hampati nafasi. Sio rahisi kila mtu akasema, tunajaribu ku-*manage* angalau wale ambao hawajasema na wao wapate nafasi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge ambao wamekuja kutembelea Bunge, mnaweza mkasimama tu kama mpo. *(Makofi)*

Pia kuna wanafunzi 50 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari Dosidosdi iliyopo Kiteto, Mkoa wa Manyara, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakristo wakatoliki leo Jumatano tarehe 24 Mei kutakuwa na ibada ya misa mara baada ya kuahirishwa Bunge saa saba mchana katika kanisa dogo lilipo ghorofa ya pili Ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wengine wote mnakaribishwa kushiriki ibada hii takatifu. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mwongozo, Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Mtolea, Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Frank, Mheshimiwa Bilago. Mnajua tunachukua muda wa kuchangia sasa.

**MBUNGE FULANI:** Sawa.

**MWENYEKITI:** Upande huu hamna? Haya Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mwongoz kwa Kanuni ya 68(7), naomba nisiisome, kwamba...

**MWENYEKITI:** Kanuni ya ngapi?

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7). Kuna jambo ambalo limetokea mapema leo humu Bungeni. Kwanza nieleze kwamba Bunge ni chombo ambacho ni sehemu ya mihimili mitatu ya kitaifa inayotambulika na kwamba limeundwa kwa Ibara ya 62 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati Naibu Waziri wa Elimu anajibu swali namba 267 kwenye maswali ya nyongeza ya ujasiriamali ameeleza kwamba Bunge ni ujasiriamali.

Sasa nataka kupata Mwongozo wako, kama kweli Bunge, chombo kikubwa hiki kinaweza kikaitwa nacho ni ujasiriamali, na wewe baadaye ukawa Mwenyekiti wa ujasiriamali na akawepo Spika wa ujasiriamali na Wabunge wajasiriamali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu Mwongozo wako au kwa vile ni mtani wangu ulimi uliteleza, tupate Mwongozo wako. Naomba Mwongozo kuhusu suala hilo, je, Bunge ni ujasiriamali au ni mhimili?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Frank.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi natumia Kanuni ya 68(7) kuomba Mwongozo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Naibu Waziri wa TAMISEMI akijibu swali langu la nyongeza kuhusu zahanati au eneo la kujenga zahanati, eneo la Makambini, hakuweza kujibu swali hilo, na badala yake amejaribu kutoa maelezo na kuelezea maeneo ambayo tunajenga hospitali lakini pia na eneo lingine ambalo wanataka kuongeza kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nataka Mwongozo wako, aweze kunijibu, lile eneo ambalo tunataka kujenga zahanati lakini pia kutokana na sera ya nchi kusema kwamba kila kijiji ni lazima kuwe na zahanati na wananchi sasa hivi wameshachanga fedha, simenti zimeanza kuganda, tofali ziko pale zimeanza kuibiwa na shughuli nyingine haziendelei kabisa. Kwa hiyo, ninaomba swali langu ambalo lilikuwa limeulizwa aweze kulijibu. Ahsante sana.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Natumia Kanuni ya 68(7) ikisomwa sambamba na Kanuni ya 46(1).

**MWENYEKITI:** Kanuni ya arobaini na ngapi?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 46(1). Nakushukuru ulinipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza hapa na imekuwa ni kawaida ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Ngonyani, kila mtu akiuliza swali anaongeza mbwembwe zake ambazo kimsingi zinaharibu kabisa maana

ya swali zima na hasa unapokuwa upande huu tukiuliza swali lazima amtaje Mbunge wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza swali dogo, kwenye barabara ya Kitunda ambayo unaifahamu kutokea kituo cha polisi pale, lile ni Jimbo la Ukonga, hakuna Segerea, kwa hiyo ukitaja Kitunda, ukataja Kivule, ukataja Msongola unamaanisha Jimbo la Ukonga ambalo anaongoza Mheshimiwa Waitara. Sasa ni lazima amtaje Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, sina ugomvi na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, lakini imekuwa ni kawaida yake, kwa nini asiwe kama Waziri wake ambaye ni mstaarabu sana. Nadhani mtu huyu aonywe, sio sawasawa kabisa, kwa sababu kila Mbunge hapa ana hadhi sawa, kama anataka Mbunge wa CCM Ukonga mpaka nitoke mimi, hapa nimejaa kweli kweli pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba utoe Mwongozo kwamba hii ni tabia mbaya na hatukubaliani nayo na sio sawasawa na yule ni Naibu Waziri amepewa dhamana kubwa, lazima aheshimu nafasi aliyopewa. Na Spika alishamuonya hapa, sasa ataonywa na nani. Naomba hili jambo ulitolee Mwongozo na likome kuanzia leo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini ninasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47(1), na kutokana na umahiri wako wa Kanuni naomba nisiisome.

**MWENYEKITI:** Kanuni ya ngapi?

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 47(1).

Katika siku za hivi karibuni Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alitembelea eneo la Rufiji, Kibiti, Mkuranga kwa sababu ya hali ya usalama iliyopo na alitoa maagizo mazuri sana, kama yangefuatwa jinsi alivyoyatoa. Lakini maagizo ya Waziri yametafsiriwa vibaya, hivi sasa polisi

wanakamata watu hovyo, wanawapiga watu hovyo na katika siku za karibuni walimkamata kijana Sultani Mpigi ambaye alikuwa anafua nguo zake, akateswa sana, baba yake amekwenda kukuta maiti yake *mortuary* ya Muhimbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanalalamika, wanahama, hali ni mbaya sana. Ninakuomba sana, kazi ya Bunge hili ni pamoja na kujadili maisha na usalama wa watu wake, Wabunge wa eneo hili wamejitahidi sana na wananchi wao wanapaswa waone Wabunge wao wanavyojitahidi.

Sasa nakuomba uniruhusu nitoe hoja Bunge hili lijadili likisaidiana na Wabunge wa maeneo hayo ili kuishauri Serikali namna bora ya kushughulika na jambo hili lisije likaponyoka kwenye eneo ambalo lipo likaenea katika maeneo mengine Taifa hili likapata matatizo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninasimama kwa Kanuni ya 68(7) ambayo pia nataka isomwe pamoja na Kanuni ya 47(1) ili ikiwezekana kama itakupendeza wewe, Waheshimiwa Wabunge waweze kupata fursa ya kujadili jambo hili kwa mustakabali mzima wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukipiga kelele muda mwingi hapa kwa kudai hakimiliki kwa wasanii wetu ili kazi zao ziweze kuwanufaisha wao pamoja na familia zao. Kumekuwa na malalamiko na kilio kikubwa cha Bwana Francis Maige Ngosha ambaye ndiye aliyebuni hii Ngao ya Taifa, ambayo tunaitumia kwa kiasi kikubwa na tunajivunia ngao hii kwa uzuri wake na umaridadi wake. Hata hivyo, mtu huyu hajawahi kunufaika na kazi yake hii ya mikono yake, anaishi pale Buguruni maisha ya ajabu, maisha mabovu, afya yake ni mbaya, anashindwa hata kwenda kupata tiba wakati ngao yake inaheshimika na inatunzwa sehemu nzuri sana kama tunavyoona inavyopendeza katika jengo letu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako, hivi kweli na sisi kama Bunge ambao tunaitumia nembo hii tunathubutu kuingia kwenye dhambi hii ya kutumia jasho la mtu ambaye hajalipwa haki zake.

Ninaomba Mwongozo wako, tuone namna gani tunaweza kumsaidia mwananchi huyu ambaye pia ana imani kubwa sana na Mheshimiwa Zungu kama Mbunge wake kwamba utaendelea kumpigania na kulipigania jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba Mwongozo wako.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi nasimama kwa Kanuni ya 68(7). Kabla sijaomba Mwongozo wako, natambua na Watanzania wanafahamu kwamba hili ni Bunge la Tanzania, kwa hiyo Mbunge anaweza kuzungumza suala hata la Kibaha, hata la Ukonga, hata kama anatoka Geita, kwa sababu mimi ni Mtanzania. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bonnah Kaluwa kuzungumza suala la Ukonga alikuwa sahihi kwa sababu hii ni *National Assembly,* sio Bunge la Ukonga*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako kwa jambo lililotokea kwenye Jimbo la Geita Vijijini. Vyombo vya habari vimeripoti...

**MWENYEKITI:** Kanuni?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya habari wameripoti kwamba kuna maafa yametokea na utaratibu wa Bunge tumekuwa tukifanya hivyo wanafunzi wanapopata matatizo. Sasa ninaomba Mwongozo wako kwamba, je, Bunge linaweza kutoa michango kwa wahanga, wale wanafunzi waliofariki? Msigune kwa sababu sio upendeleo,

kwenye Arusha hatukupiga kelele, kwenye Arusha tulichanga, ndiyo. Naomba Mwongozo wako.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa nini yule?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ipo tabia moja ambayo sio nzuri sana, na tabia hii hasa inakuja upande huu...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** ...subirini jamani, mimi ndio *referee,* ndio ninaona pande zote hizi. Kadi ninazo na *uniform* ninayo, ninyi mmevaa kama mimi? *(Makofi/ Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, ipo tabia moja, upande huu mkijenga hoja za miongozo au jambo lolote upande huu wanasikiliza, na kila mmoja anajua, lakini upande huu wakija na hoja zao upande huu mnaanza kulalamika, na wanaolalamika wanafahamika kwa majina. Sasa mimi naomba kila mtu ana haki sawa kwenye Bunge hili na kila Mbunge ana haki ya kujenga hoja yake, Kiti ndicho kitakachoamua.

Sasa muacheni aseme, Kiti kitaamua na Kanuni tunazo, mkidharau mamlaka ya Kiti adhabu yake mnaijua, na waya huu uliopo huko nje nikikwambia ukae nje siku tatu si utalia wewe! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Musukuma, endelea.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunilinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu Mwongozo wako kwamba kwa kuwa kwenye Jimbo la Geita watoto wa shule walizama na wakafariki watatu na kukatokea shujaa, kijana wa miaka 12 ameokoa watoto tisa. Na wenzetu wa *Clouds* wameweka programu ya kumsaidia

mtoto huyu pengine kumsomesha ama kumfanyia chochote na kuzisaidia zile familia ambazo zimepoteza watoto wao. Na kwa kuwa utaratibu wetu Bunge kunapotokea maafa, hata yaliyotokea Arusha tulishirikiana kwa pamoja bila kubagua wala kuguna, Bunge lako halioni kwamba kuna sababu ya kuwasaidia familia zile zilizopata matatizo na kumsaidia kijana huyu, shujaa wa miaka 12 aliyeokoa watu wazima? Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Wabunge sita, tunaanza na Mheshimiwa Musukuma. Kwanza pole kwa majanga yaliyotokea kwenye eneo lako na ni kweli Bunge tuna utaratibu wa kuchangisha pale ambapo kuna maafa na kuchangisha huku ni kuonesha namna Wabunge wanavyoguswa lakini namna gani Wabunge wanaweza kuwa na *solidarity.* Na asubuhi ni kweli Mheshimiwa Musukuma nimekusikia kwenye *Clouds* umechangia shilingi milioni moja, nakupongeza sana. Hili acha nilifanyie kazi halafu nitakujibu kwa sababu ni jambo la *solidarity* katika Bunge na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mtolea umetumia Kanuni ya 47 ambayo ni nzito sana, ni suala la dharura, lakini hili la kwako halina udharura, lina umuhimu, kwa hiyo hili nalo nalichukua au nitampa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu alijibu kwa sababu ndiyo idara yake.

Kwa hiyo, sasa Mheshimiwa Waziri jiandae na hili jibu la msanii huyu ambaye wanaona kidogo ametoa mchango mkubwa kwenye ngao lakini hashughulikiwi. Sasa inawezekana Serikali majibu yake mnayo, labda mnamsaidia na yeye mwenyewe labda zile pesa mlizomsaidia zimekwenda zimepigwa na watu pembeni, kwa hiyo, mtatoa maelezo.

Mheshimiwa Waitara umetumia Kanuni ya 68 ambayo ni sahihi, jambo lililotokea leo Bungeni na umetoa hoja yako,

nipe muda niende kwenye *Hansard* nikatazame. Lakini vilevile swali la nyongeza mara nyingi Kikanuni huwa Waziri anakuwa na nafasi ya kujibu pale anapoona kuna jibu lake liko mbele yake. Kwa nini, swali la nyongeza ambalo wewe umeliomba Waziri hana majibu yake, takwimu zake anakuwa hana, sasa hilo nipe nafasi nikalitazame halafu nitakujibu.

Mheshimiwa Frank Mwakajoka umetumia Kanuni ya 67 ni kweli, lakini swali lako vilevile lilikuwa swali la nyongeza na swali la nyongeza kama unaliona halikujibiwa vizuri liandike lidai wewe hilo swali lako ili lije hapa kama swali la msingi.

Mheshimiwa Bilago ameomba mwongozo kuwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kusema Bunge ni ujasiriamali, ngoja mimi nikapitie *Hansard* kwanza nitazame kama maneno hayo unayoyasema ndiyo yaliyosemwa na Waziri halafu tutayatolea Mwongozo.

Mheshimiwa Selasini umetumia Kanuni ya 47 ambayo ni sahihi, sioni sababu ya kuahirisha Bunge au kuwa mjadala kwa sababu Serikali ipo na ninaamini Serikali inafanya kazi vizuri, juzi tumemuona Waziri kwenye pirikapirika hizi na ameonesha ujasiri mkubwa na hasa kuhakikisha vyombo hivi vinataka kusaidia eneo hili la Kibiti na maafa haya na majanga haya ya Kibiti yaishe *once and for all.*

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hebu tueleze kidogo taarifa rasmi za kwako unazoziona ili Wabunge wawe na *comfort* kuwa Serikali iko makini na inahakikisha kuwa suala hili mnalimaliza na wananchi wawe na amani.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nimshukuru Mbunge kwa kufuatilia jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu mazingira ya mambo yanayotokea Kibiti ni *complex* kidogo kwa maana ya uchunguzi wote unaonesha watu hawa wanaofanya

uhalifu hawatoki maeneo ya mbali na wanamudu kufanya hivyo kwa sababu wanapata ushirikiano wa kiwango fulani katika maeneo husika. Na mifano inayoonesha kwamba hawatoki mbali ni aina ya watu ambao wamekuwa *targeted,* mtu anayetoka Rombo kwa mfano, hawezi kwenda Kibiti kumuua Mwenyekiti Mstaafu wa CCM, huyu ni mtu ambaye lazima awe anajua Mwenyekiti Mstaafu wa CCM anakaa wapi, maisha yake yakoje. Na kama ametoka mbali basi lazima awe amekodiwa na yule aliyetokea katika eneo la hapo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine kitendo kilichotokea la mgambo wawili katika geti la Maliasili kuuawa wangali miili yao iko pale, wauaji wakawaita wananchi kwamba waende kuchukua mikaa yao na wale wananchi wakaenda wakaanza kuchukua mikaa huku wakivuka maiti huku na wauaji wangali bado wako maeneo yale, kinaonesha kwamba si mazoea ya Kitanzania kuona muuaji yuko pale na wewe ukaweza kumudu kwenda eneo la tukio, na mbaya zaidi, kuona mkaa una maana kuliko miili ya Watanzania ile iliyolala pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mazingira kama hayo, tumechukua hatua za kukabiliana na mazingira ya aina hiyo na hatua zenyewe hizo, moja ni kuhakikisha tumeweka vijana wetu wawe doria kila wakati.

Lakini la pili, tunawatafuta wahalifu na wahalaifu wale kwa sababu wanakaa palepale ina maana kuna wakati mwingine wanakwenda kuuza magenge, kuna wakati mwingine wanakwenda kupalilia mihogo, kuna wakati mwingine wanakwenda kwenye mikaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunachokisema sisi ni kwamba hawawezi wakafa watu wengi kwa kiwango kile katika eneo lile halafu maisha yakaendelea kama kawaida, hilo ni jambo ambalo hatuwezi tukakubaliana nalo. Lakini la pili, hatuwezi tukakubaliana nalo katika Tanzania yetu hii hii, kawepo kaeneo kamoja kaweze ku-*demonstrate*

kwamba wanaweza wakafanya mambo wanayoweza kuyafanya kwa namna yoyote ya aina ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, moja ambalo tunataka kutoka kwa wananchi, ni lazima watoe ushirikiano, hili sio ombi, ni lazima watoe ushirikiano. Na ushirikiano wenyewe watambue kwamba mazingira ya pale walipo ni tofauti na maeneo mengine. Kwa mfano, kama tunafanya msako na taarifa walizonazo wakaelezwa kwamba kuna ishara kwamba hapa tunaweza tutakawa na tatizo, kama mwananchi si mhalifu ni vema akatoa ushirikiano, kwa sababu akikataa tutafanya msako kwa nguvu. Kwa sababu tupo katika mazingira ambayo adui/ mhalifu anaishi pamoja na asiye mhalifu, ni tofauti na kupigana ukijua adui wako kule, walio wema wako huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, moja ambalo niwape *comfort* Waheshimiwa Wabunge ni kwamba Serikali iko kazini, vijana wako kazini lakini ni rai yetu tunatoa kwa wananchi waweze kutoa ushirikiano. Na ushirikiano mwingine wala sio wa kutaja nani ni mhalifu, ni pale ambapo tunataka kufanya misako na wenyewe watoe ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na maeneo mengine wananchi na wenyewe wanakuwa na ugumu wa kutoa ushirikiano na wakishakuwa na ugumu wa kutoa ushirikiano katika maeneo ambayo yana taswira za uhatarishi ni dhahiri kwamba wataamsha mapambano kwa sababu Serikali haiwezi ikarudi nyuma, vyombo haviwezi vikarudi nyuma vikashuhudia vitu vikifanyika ambavyo vinaondoa sifa yetu ya Tanzania ya suala la amani na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikuhakikishie tu kwamba kwa taarifa nilizonazo na kwa mikakati inayoendelea, jambo hili halitakuwa na muda mrefu linakwenda kuisha na Watanzania wa Wilaya hizo watakwenda kuishi maisha sawa sawa na watanznaia walioko maeneo megine...

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ....lakini waendelee kutoa ushirikiano kwa ajili ya kuwezesha zoezi hilo kufanikiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi suala hili la mtoa ngao, msanii.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaamini kabisa mimi binafsi lakini Serikali pamoja na Bunge lako linampongeza na kumshukuru sana Msanii huyu kwa kuweza kufanikisha Nchi yetu kuwa na nembo ambayo tunajivunia sisi wote kwa Tanzania kwa sasa.

Lakini kwa namna ya pekee ninaomba tu nimshukuru sana Mheshimiwa Mtolea kwa sababu ukiiangalia nembo yetu hii ya Taifa katikati ya nembo hiyo kuna mwenge wa uhuru. Kwa hiyo, Mtolea leo anapotambua nembo hii ya Taifa, ngao hii ya Taifa namshukuru sana ndani ya ngao hiyo pia kuna mwenye wetu wa uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Mtolea amesema hoja hapa ya msingi na hoja yake kwa kweli ninaamini kabisa kwamba kama Serikali tunapaswa kuichukua na nikuhakikishie Mheshimiwa Mtolea tutakwenda ndani ya Serikali kuitazama na kuona ni namna gani hoja hii itaweza kupewa uzito ule ambao wewe umeuweka hapa ndani, lakini kwa ujumla ninaomba niseme kwamba msanii huyu amefanya kazi nzuri sana kwa Taifa letu na Taifa letu limeendelea kutambulika katika mataifa na ulimwengu mzima kwa kutumia kazi hii nzuri aliyoifanya ndani ya nchi yetu ya Tanzania, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge mmesikia majibu ya Serikali na mimi ndiyo maana napenda saa nyingine wacha Serikali wajibu ili muwe na *comfort* na msianze kueneza mambo ambayo siyo ya ukweli. Nakushuru

sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwa namna ulivyoliweka na nina uhakika mtalishughulikia na mtapata ukweli wake, lakini nikushukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa namna na wewe ulivyolitolea kauli na kuonesha umahiri, uwezo wako na uwezo wa Serikali kudhibiti na kuhakikisha usalama wa Watanzania katika nchi yetu, nawapongeza sana, Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Mponda ajiandae Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mheshimiwa Musukuma Joseph na ajiandae Mheshimiwa James Mbatia.

**MHE.DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sisi wote kuwa wazima wa afya ili kukabiliana na majukumu yetu pamoja na kazi zetu za Ubunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kunipa nafasi angalau nitoe mchango wangu katika Wizara hii muhimu sana katika Wilaya zetu za Malinyi, Ulanga na Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nafasi hii niitumie kutoa shukrani kwa Wabunge, wakazi wa Malinyi, wakazi wa Morogoro na Watanzania nzima kwa ujumla, ndugu, marafiki na majirani kwa pole, salaam za rambimbi na dua kuhusu kifo cha mzazi wangu Mzee Hussein Mustafa Mponda lakini tunajua fika sisi wote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea. *Innalillahi Wainna Ilayhi Rajuun.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo utajikita kwenye eneo moja tu kubwa ambalo kutegemea hotuba ya Waziri imezungumzia Idara ya Wanyamapori na dhana ya ushirikishaji jamii katika uhifdhi wa wanyamapori na ardhi oevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo inajikuta na migogoro inayojitokeza baina ya Hifadhi, Mapori Tengefu na Mapori ya Akiba na Vijiji vinavyopakana ni hasa imetokana na mabadiliko ya Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009 ambapo kwa mabadiliko hayo yalivyofanyika, Serikali walipewa maelekezo wafanye mambo mawili:-

La kwanza, watafiti kama kuna ulazima wa uendelevu Mapori Tengefu kwa wakati huo ilikuwa 42; na la pili, ni kurejea mipaka ya Mapori Tengefu au Hifadhi kwa sababu sheria ya zamani ilikuwa inawaruhusu wakazi wa maeneo yale kutumia mapori yale lakini Sheria ilivyobadilika 2009 ikakataza. Niipongeze Serikali wameanza kutekeleza kwa ukanda wa kwetu kule Malinyi, Kilombero na Ulanga kwenye lile bonde la Kilombero, ardhi oevu yake na Pori Tengefu la Bonde la Kilombero. Walichofanya mwaka 2012 walirejea wakaangalia ile mipaka, wakaweka mpaka kati ya kiini cha Pori Tengefu la Kilombero na ardhi ya kijiji, ule mpaka wakauita *buffer zone.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lile ni panasana lina-*range* wakati mwingine kilometa mbili mpaka kilometa 25 ambayo imesababisha vijiji karibuni 23 na vitongoji vyake 18 wananchi wanaishi kihalali maeneo yale. Vijiji vile vimesajiliwa, sasa hii ni changamoto ambayo Serikali waliiona pale na baada ya kupigia kelele, kuishauri Serikali nishukuru tena wamekubali kurejea upya mipaka ile na nawashukuru uongozi wa Menejimenti ya Bonde la Kilombero walitushirikisha wadau ngazi ya Halmashauri walituita Mikumi nakumbuka ilikuwa tarehe 20.10.2016, tumewekwa semina ya siku mbili kuonyeshwa umuhimu wa lile bonde na kuonyesha namna gani bonde na namna linavyoathiriwa na nini hatima yake. Kulikuwa na *option* tatu:-

(i) Aidha, kisiwepo na *buffer zone;*

(ii) Iwepo na *buffer zone* lakini kuwe na masharti maalum; na

(iii) Imeridhiwa wadau wote wa mipaka ya *buffer zone* ile irejewe isiwe mipana kama kiasi kile ili kuokoa vijiji vile ambavyo viko kihalali na kuokoa maeneo ambayo wananchi tayari wameshaanza kutumia ambayo sasa itatusaidia kupunguza migogoro ya ardhi na pori tengefu lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi ulikuwepo; ukirejea matokeo ya utafiti wa wanyamapori *(TAWIRI 2009, 2010, 2011)* na mtafiti mmoja ambaye ni mtaalam wa wanyamapori katika Mkoa wa Morogoro ni Ndugu Joseph Joachim Chuwa alifanya utafiti kwa kushirikiana na *SUA* waliangalia changamoto, waliangalia masuala ya kijamii na uchumi yanayosukuma uhitaji wa ardhi na uendelevu wa lile bonde na baadae tafiti ile ilihitimisha kwamba ni vyema wadau, ni vyema wananchi wahusishwe ili kulilinda lile bonde na mimi nasema wananchi wa Malinyi, Ulanga na Kilombero ndiyo tunanufaika na lile bonde, tuko tayari na tunalipenda sana maisha yetu tunategemea lile bonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea, hao hao Serikali wenyewe hawasimamii ipasavyo bonde lile kwa sababu sisi hatuwezi kulima ndani ya bonde lile karibu na ule mto ambao unakuwa *protected,* ni watu wanatoka mbali na Serikali wanawatazama siku zote matokeo yake wanatuathiri sisi ambao wanasema hawa wakazi wa Wilaya hizi tatu wao ndiyo waharibifu wa lile bonde owevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali kipindi hiki wamerejea tena kuweka mipaka. Niwashukuru wamechukua dhana kweli shirikishi lakini ajabu yake na hii naomba heshimiwa Waziri unisikie kwa makini sana; kwamba wataalam wale kutoka Wizara ya Ardhi, TAMISEMI na Maliasili na Utalii wanakwenda kila kijiji, wanaongea na wananchi,

wanaongea na viongozi, tunafikia muafaka kwamba mpaka wa lile *buffer zone* uwe wapi. Tunaelewana kabisa, tunakubaliana lakini sasa kinachofanyika wanapokwenda kuweka mipaka ile kwenye *beacon* wanatofautiana makubaliano ya awali na wananchi wale.

Sasa mimi niwahoji; mnasema shirikishi mnawashirikisha wananchi, wananchi wamechukua muda wao, wameeleza matatizo yao, wataalam wenu mumewatuma kule lakini hamtaki kusikia mnakwenda kuweka *beacon* kama mnavyotaka, kwa kusema hapo hamtatatua tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri niwaombe, nimeongea na wataalam hawa wanawanyooshea vidole ninyi viongozi wa Wizara. Wansema tumeongea na wananchi na tumekubaliana lakini tunapokwenda kule wanatu-*monitor,* wanatufuatilia kwa njia ya TEHAMA, wanasema lazima mpaka uwe hapa. Kama ni hilo ni kweli hamtutendei haki kabisa wananchi wa Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe Mheshimiwa Maghembe najua bado utarudi mwaka 2020 na najua bado una sifa na utapenda kuwa Waziri, sasa hapa changamoto iliyopo 2020 Mheshimiwa Rais wakati tunamnadi kwenye Jimbo la Malinyi tarehe 05.09.2015 alisimama kwenye jukwaa baada ya kuelezwa changamoto hii, aliahidi ataongeza ardhi ya kutosha, ataongeza maeneo yale ambayo wananchi wapate kuendesha shughuli zao za kila siku. Labda mimi niseme tu, hapa changamoto kubwa siyo kwamba hatutaki bonde lile tusililinde, hapana, changamoto kubwa lile *buffer zone* ni pana mno; wewe umeona wapi *buffer zone* kilometa 25? Kawaida ya *buffer zone* ni kilometa angalau mita 500, angalau kilometa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe basi mtusikilize *buffer zone* ile muipunguze badala ya kuwa na kilometa 25, kilometa 8, kilometa 12 iweke ile *standard* yenu kama ilivyokuwa *buffer zone* kwenye maeneo mengine ya kilometa mbili ambayo itatuwezesha sasa kwanza, kutekeleza ahadi

ya Mheshimiwa Rais na hiyo itakuwa njia rahisi Mheshimiwa Rais atapita tu kama barabara imewezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo zoezi linaendelea tuna ombi maalum watu wa Malinyi; kwamba kwa kuwa wanaweka hiyo mipaka kwahiyo watu wanaoishi kule siyo kihalali kwenye ile kiini cha pori wataondolewa na wakiondolewa kule kuna mifugo itahamia kwenye milima.

Tunaomba mtusaidie Halmashauri hawana uwezo wa kulinda ile milima na ile milima ndiyo vyanzo vya maji yanayotiririka katika lile Bonde la Kilombero na hatimae unakuwa mto unaelekea mpaka unakuwa Mto Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mchengerwa, ajiandae Mheshimiwa Musukuma

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema, nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Rufiji kwa kuendelea kuniombea dua hususani katika kipindi hiki ambacho ni kipindi kigumu kabisa kupata kutokea kwa wananchi wa Mkoa wa Pwani hususani wakazi wa Kibiti, Rufiji na Mkuranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kufanya kazi nzuri kabisa katika Wizara hii ambayo ni moja ya Wizara ngumu kabisa katika nchi yetu hii. Mheshimiwa Waziri yeye pamoja na timu yake wamefanya kazi nzuri na mimi nawapongeza sana, sisi wananchi wa Rufiji wametusaidia kwa mambo kadhaa ambayo nitayazungumza hapo mbele lakini pia nimpongeze Mkurugenzi yule wa Misitu Ndugu Mohamed, nimpongeze Meneje wetu wa *TFS* kutoka kule Rufiji ambae marazote amekuwa akitatua kero za wananchi wangu na mimi namfananisha Profesa Maghembe na kanuni

ya kwanza ya uongozi iliyowahi kutolewa na Dkt. John Maxwell ambae aliwahi kuandika kitabu chake *The Laws of the Leadership* akisema kwamba; *"Personal and organizational effectiveness is proportional to the strength of a leadership"* na mimi namuona yeye kama ni kiongozi ambaye ameweza kuimiliki Wizara hii na ninaamini Rais Dkt. John Pombe Magufuli wakati anakuteua aliamini wewe ni muadilifu na umechapa kazi. Wizara hii ina madudu mengi sana na kama ungekuwa umeyumba kidogo basi Wizara hii kwa kweli ingekushinda mapema sana.

Lakini nikupongeze kwa kusimamia Ibara ya 26 ya Katiba na kumtaka kila Mtanzania kusimamia na kufuata sheria za nchi yetu na hii nimeiona kwasababu wakati wa mijadala ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii tumeona hoja nyingi zinazoibuka ni hoja zilizopo kwenye Wizara ya Kilimo na Mifugo na ni wewe sasa umekuwa kama Waziri wa Kilimo na Mifugo lakini pia umekuwa kama Waziri wa Ardhi na umeendelea kuchapa kazi na mimi naomba niwakukmbushe Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakumbuke kwamba Ibara ya 26(2) inatupa mamlaka sisi Wabunge iwapo tunaona sheria yoyote ambayo inasimamiwa na Profesa Maghembe sheria ile inakinzana na matakwa ya nchi yetu tuliyonayo sasa basi ni vyema Wabunge sasa tukaleta sheria ile ndani ya Bunge lako hili tukufu kupitia Ibara ya 64 ya Katiba ili tuweze kubadilidha sheria ile na tusimlaumu Profesa Maghembe kwa kuwa anasimamia Ibara ya 26 ya Katiba ya kusimamia na kufuata sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magazeti mengi ya wiki hii yameandika mambo mengi kuhusu Rufiji, Kibiti na Mkuranga. Gazeti la leo la *Citizen* limeandika taarifa kwamba; *"Why Rufiji residents are reluctant to cooperate over murders"* lakini gazeti la jana ninalo hapa limeandika taarifa kwamba; *"Rufiji families pain after losing their lovely ones."*

Jana mmoja wa wahanga aliyepigwa risasi siku tatu zilizopita amefariki jana alipigwa yeye na baba yake, yeye lipigwa risasi ya tumbo na jana amefariki na tunamshukuru

Mbunge wa Kibiti kwa kufanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba mwili ule unafika Kibiti na shughuli za maziko zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie katika Bunge lako hili tukufu, unao Wabunge watatu ambao wanaishi katika maisha magumu sana kupata kutokea katika nchi hii; Mbunge wa Mkuranga, Mbunge wa Kibiti pamoja na Mbunge wa Rufiji. Tunaishi katika maisha magumu sana na siyo sisi tu hata katika familia zetu, lakini pia hata wapiga kura wetu wanaishi katika maisha magumu sana. Wananchi wamekonda sana hawawezi hata kushiriki katika shughuli za maendeleo hali ni mbaya sana na tunaiomba Serikali jambo hili kulifanyia kazi haraka kwasababu jambo hili linaendelea kutanuka na jambo hili siyo dogo kama ambavyo Wabunge wengine wanaweza kufikiria hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wamekuwa wakihoji maswali ni kwa nini Wabunge hawazungumzi ndani ya Bunge? Tunafanya hivi kwa makusudi kabisa lakini tunataka wananchi wetu wajue tunafanya kazi kubwa kuhusiana na jambo hili lakini yapo mambo sisi hatuwezi kuyazungumza kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani wananchi wangu wa Ikwiriri wanakushukuru sana kwa kufika, kujionea familia ambazo ziliathirika ambazo waume zao wamepigwa risasi na kufariki, wananchi wangu wanakushukuru sana. Lakini nataka niseme Serikali isikie na Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli ajue kwamba mambo haya yanayotokea hayatokei kwa bahati mbaya, mambo haya yana *root cause,* mambo haya yamepangwa, tunataka Serikali ijue hilo. Yapo mambo mengi, zipo chuki nyingi ambazo zimejengwa kwa wananchi, zipo chuki nyingi, yako mambo mengi ambayo yalifanyika yanatoa kero kubwa kwa wananchi ndiyo maana hata gazeti la leo lilipoandika taarifa hizi mimi siashangaa sana kwasababu ninajua kwamba yako mambo ambayo Serikali sasa inapaswa kuyafanya na inatakiwa iyafanye sasa wala isisubiri kwa sababu jambo hili ni kubwa na linaendelea kutanuka kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi naomba katika miongoni mwa mambo ambayo sisi tunaendelea kumpongeza Rais wetu ni terehe 31.03.2017 Rais Dkt. John Pombe Magufuli baada ya kufanya kikao chake na Waziri Mkuu wa Ethiopia alikubali kuwasaidia Watanzania kwa kuonyesha dhamira ya kujenga *Stigler's gauge* iliyopo kule Rufiji ili wananchi wetu waweze kupata umeme wa uhakika kwani tunaamini kabisa miongoni mwa kero kubwa za wananchi wangu ni kutokuwa na umeme kwa takribani miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwaka wa pili sasa wananchi hawana umeme wa uhakika sasaa hizi ni miongoni mwa kero kubwa ambazo wananchi wangu wanazo na leo nazungumza kwa uchungu kabisa, kero hizi muunganiko wa umeme ni kilometa nane tu lakini Waziri wa Nishati na Madini ameshindwa kutuunganishia umeme kwenye Gridi ya Taifa kwa miaka mwili wananchi wa Kibiti, wananchi wa Rufiji na wananchi wa kutoka kule Kilwa hawapati umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuliona hili na tunaamini kabisa kwamba uzalishaji wa umeme upo kwenye *Stigler's gauge* utasaidia upatikanaji wa umeme katika maeneo mengine hiyo ni miongoni mwa kero kubwa tulizonazo kwasababu tatizo hili ni kero kama nilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo tatizo la barabara ambalo Mheshimiwa Rais amekubali kutujengea barabara yetu ya Nyamwage kwenda Utete na mimi naomba nimpongeze na ninaomba wananchi watambue kwamba kero hii ya barabara imepatiwa ufumbuzi nasema haya kwa sababu ya kiini cha tatizo tulilonalo, wananchi wanalalamika sana na hatuna sababu ya kwa kweli kwa nini tuendelee kukaa kimya.

Nikuombe sasa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii nirejee kwako, zipo kero katika maeneo yetu. Kwa mfano, katika Kata ya Kipugira watu wako wanaweka *GPS*

kwenye nyumba za wananchi wetu, lakini naomba niikumbusghe Wizara yako kwa kusimamia Katiba; Ibara ya 16 ya Katiba inatoa uhuru wa faragha, lakini swali hili nilimuuliza Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ni kwa nini Wizara yako inaweka *GPS* kwenye nyumba za wananchi wangu? Wanavunja ibara ya 16 ya Katiba ambayo inatoa haki ya faragha ambayo kila mwananchi anayo haki ya ku-*enjoy* haki ya faragha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimuombe Mheshimiwa Waziri ukisimama hapa unipe majibu kuhusiana na jambo hili ni kwa nini Wizara yako sasa inakiuka Ibara ya 16 ya Katiba lakini pia nimuombe Mheshimiwa Waziri akisimama hapa atuelezee tarehe 9 Septemba Waziri Mkuu alifika Rufiji na katika maeneo aliyokwenda ni pale Utete na alijionea wananchi walikuwa na malalamiko mengi sana. Upo msitu wa Kale ambao wananchi wa Utete pamoja na Chemchem wamekuwa wakiutumia kwa kilimo kwa miaka mingi sana.

Mheshimiwa Waziri naomba nikukumbushe nafahamu kuna tamko la Waziri Mkuu la upimaji upya wa maeneo yetu, lakini tukumbuke kwamba michoro ya awali ambayo Wizara yako inatumia ni michoro iliyochorwa na wakoloni mwaka 1936. Nikuombe Mheshimiwa Waziri utambue dhamira ya wakoloni ya kuchora michoro ile ni kwa sababu *population* ya Tanzania ilikuwa bado ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule wa mkoloni tulikuwa tunazungumzia *population* ya watu milioni nane mpaka milioni 10. Lakini leo hii Mheshimiwa Waziri tuna watu zaidi ya milioni 55 na Rufiji wakati ule tulikuwa kuna watu ambao walikuwa hawazidi hata 20,000; 30,000, lakini leo hii tunapozungumza tuna wananchi zaidi ya 200,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe ulisimamie hili, lakini hii ni pamoja na Kata yangu ya Mbwala katika vijiji vya Nambunju pamoja na Kitapi, maeneo haya yote Wizara yako imeanza kuyapima upya na Wizara sasa inachukua maeneo yote ambayo wananchi walikuwa wakiishi na kutaka

kuyafanya maeneo yale ya misitu. Nikuombe Mheshimiwa Waziri uzingatie hili kwani ukichukua maeneo haya wananchi hawatakuwa na pa kwenda kabisa. Nikuombe ulisimamie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine kuhusiana na *hotel levy;* kodi hii ya *hotel levy* ambayo imekuwa ikitolewa kwenye nyumba za kulala wageni, kodi hii ni kero kubwa sana. Tukuombe sasa Wizara yako iweze kulingalia kulipitia kwani wananchi wanaomiliki nyumba hizi za wageni wanalipa shilingi 100,000 ya leseni kwenye Halmashauri, lakini pia wanalipa hii *hotel levy*. Wakati huo huo wanalipa tena kodi ya mapato *TRA* shilingi 560,000, wakati huo huo wanalipa *hotel levy,* wanalipa tena leseni, wanalipa gharama kubwa sana. Wananchi wangu kuanzia Jaribu Mpakani kwenda moja kwa moja Kibiti mpaka kule Mkuranga na Rufiji wanalalamika sana kuhusiana na kodi hii. Na nikuombe Mheshimiwa Waziri basi muweze kuingalia na kuweza kuona namna gani mtaweza kuitatua suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija pia katika suala zima la mahusiano kati ya Wizara yako na wananchi wetu wanaozunguka vijiji, nikuomba Mheshimiwa Waziri sasa ukija kujibu hapa ueleze mkakati wako wa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma, jiandae Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuwapa pole wananchi wangu wa Jimbo la Geita Vijijini ambao watoto wao wamefariki kwa ajali ya kuzama kwenye Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya, lakini pia nimpongeze sana kwa kumteua Profesa Maghembe kwenda kushika Wizara ya Maliasili na Utalii. Lakini sitakaa nimpongeze Maghembe hata siku moja kama hajabadilika, aliyemteua nampongeza, lakini Profesa Maghembe sitakaa nimpongeze hata siku moja.

Waheshimiwa Wabunge, sisi tunaotoka kwenye majimbo ya vijijini kuna matatizo makubwa hata ya Ikwiriri nikwa sababu yanaandikwa kila siku kwenye magazeti. Lakini kwa sisi ambao tunaishi pembeni mwa mapori tuna matatizo makubwa na ndio maana nasema siwezi kumpongeza Profesa Maghembe kwa  yafuatayo; kwanza kwenye Halmashauri zetu tumepitisha sheria, mwananchi akiwa na nusu debe, gunia moja tu la mkaa  haruhusiwi kukamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hebu nenda Ofisi za Maliasili, kumejaa baskeli tunasubiri sijui hata hiyo minada mtamuuzia nani hizo *scrapers* za baiskeli, watu wameshikwa na gunia moja au madebe mawili anakamatwa na ananyang'anywa baskeli, ananyang'anywa pikipiki yake. Sasa hivi sisi kwetu Kijijini ukiona gari ya Maliasili bora ukajitundike hata kwenye mti kuliko kusubiri kile kipigo utakachokipata.

Mheshimwia Mwenyekiti, lakini mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maghembe ya Maliasili, napata shida sana kujiuliza labda sisi Kanda ya Ziwa tulikuja kwa bahati mbaya kwenye hii Tanzania. Mbona yanayofanyika Kanda ya Ziwa, kule Kanda ya Kaskazini mbona hayafanyiki wakati na wao wana mapori. Waziri ametoa siku tatu tukamatiwe ng'ombe kwa kisingizio ng'ombe ni za Wanyarwanda. Wakati huo huo watumishi wake wanaowaingiza Wanyarwanda wanawaambia toeni ng'ombe wale Wanyarwanda, mnaenda kukamata ng'ombe za Wasukuma, halafu mnazipiga mnada, na Wabunge mnada wenyewe unavyopigwa ni wa *deal.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe 600 unaambiwa lete shilingi milioni tatu wanatoa watu wao Ubungo, halafu nakupongeza kwa sababu gani. Na mimi nataka nikwambie Profesa Maghembe kama Mwenyekiti King, tunajua mipango inayofanyika kwenye Wizara yako na nimewapigia kabisa watumishi wako, mtumishi mmoja anaitwa Masaro mwingine anaitwa Kidika, ananiambia mliipenda wenyewe, kwa kauli yake kama Mwenyekiti wa Chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesho yake akapiga ng'ombe za watu mnada, ng'ombe 500 zinauzwa shilingi milioni tatu, kwa nini msituite sisi ambao wenye ng'ombe tunashindwa kutoa milioni tano. Halafu mnasimama humu mnaipongeza Wizara kwa sababu gani, nataka nikuambie Profesa inawezekana ninyi mmesoma na Mungu amewasaidia hamjui uchungu wa kufuga ng'ombe kuanzia moja mpaka kumi. Hamjui watu tumeshindwa kwenda shule kwa sababu ya kuchunga ng'ombe tukawasomesha ninyi mkawa Maprofesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi Wasukuma sasa tumeamua, na nimezungumza uelewe, tutaziroga hizo ng'ombe mtavimba matumbo mnaozila huko Dar es Salaam. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kwa nini wanunuzi watoke Dar es Salaam peke yake, yaani leo siku ya mnada watu wametoka na malori Pugu, wanajuaje kama wanakuja kushinda kwenye mnada! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnatukamatia ng'ombe hivi hii Serikali imekosa sehemu ya kukusanya hela mpaka mkanyang'anye ng'ombe za wafugaji, haiwezekani Mheshimiwa Maghembe hata kama utanielewa vibaya lakini huo ndio ukweli. Kuna manyanyaso makubwa, mwananchi wangu wa Bukombe amepigwa risasi ya jicho hakuna fidia, aliyempiga yupo, halafu mimi nakusifu kwa sababu gani! Haiwezekani na ninaomba sana haya maneno yaingie hivo hivo nilivyoyaongea.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Taarifa Mwenyekiti.

**T A A R I F A**

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba dhuluma anayoiongelea hata wafugaji walioenda kuweka *court injunction* wakashinda kesi mahakamani, ambao ni Bwana Erasto Theophil, kesi namba 125 ya mwaka 2017 - Ngara, ng'ombe wake zikauzwa 110, Bwana Bahati Ndemezo mkazi wa Ngara kabila Msukuma ng'ombe 80 kesi namba 126 ya mwaka 2017 ameshinda Mahakamani lakini wale wanaopiga mnada wameziuza. Jumla ya ng'ombe 1019 zimeuzwa zikiwa na hukumu ya mahakama ya kwamba watu hawa warudishiwe mifugo yao. Nilikuwa nataka kumpa tu taarifa kaka yangu Musukuma.

**MWENYEKITI;** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili, nasubiri na nyingine kama hiyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwambia tu Profesa kwamba ingekuwa ni mimi nateua yaani katika Mawaziri walio-*fail* wewe ni namba moja. Sijui ni wewe ama ni watu wanaokuzunguka ni mfumo wa hiyo Wizara sielewi. Inawezekana vipi Mheshimiwa Waziri mtumishi wako kabisa anayelipwa mshahara na Serikali unampigia simu mimi kama Mwenyekiti wa Chama namwambia kuna tatizo gani kwa nini msikae na hawa watu mkawapa ng'ombe hata wiki moja wauze watoke. Anasema hili ni agizo la Rais, hivi Rais kabisa huyu tunayemjua mwenye upendo na maskini anaewajengea watoto wa Dar es Salaam maghorofa, anayewapa watu hela, anaetoa misaada, anatuuzia ng'ombe sisi kwa sababu gani, kwa nini wasiseme watumishi wako kuwa wewe ndo umewaagiza. Na kwa nini yafanyike Kanda ya Ziwa tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda Loliondo na Kamati, unataka kuwatoa wafugaji kwenye Pori la Loliondo kwa kisingizio wanaharibu ili umpe Mwarabu tukakutalia mbona hujaenda kuwanyang'anya kule, haiwezekani na hiki kitu haitawezekana. Kwa mara ya kwanza nitatoa shilingi hata kama ziko nne zote nitaondoka nazo. Nitatoka shilingi lazima uje na majibu ya msingi ni kwa nini mnatudhulumu mali zetu. Hivi kwa nini msingetupa hata kipaumbele kwama mnataka kukusanya hela za kuuza ng'ombe za watu, kwa nini msitupe kipaumbele mkatuambie njoo tarehe fulani saa fulani wote tukapambana kwenye mnada, kwa nini wanunuzi watoke Dar es Salaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu vingine vinauzi potelea mbali hata kama tutatoka humu tumenuniana lakini *message* imeenda inauma sana. Kwa wale waliozaliwa kwenye ufugaji mmesomea ng'ombe, ng'ombe inalelewa kama binadamu, kwa nini ng'ombe wa Tanzania anageuka kuwa adui. Akiingia Serengeti mnakamata, hivi mlishawahi kuona ng'ombe amekula Simba, kwanza ng'ombe ni chakula cha wanyama hata digidigi ng'ombe hali. Ana madhara gani ananyanyasika ng'ombe wa Kisukuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua sheria pengine zinamlinda Mzee Maghembe lakini hivi vitu vinauma sana, wewe leo ukienda ku-*draw* hela kwenye akaunti yako ukakuta hakuna hela kuna *zero,* utachanganyikiwa utawekaje hata mafuta kwenye gari. Ukituuzia ng'ombe ndo benki yetu sisi ambao hatukusoma tuliishia darasa la saba, ukilima pombe una nunua ng'ombe halafu tena ng'ombe unakuja mna-*deal* na watu wa Dar es Salaam. Sisi tumefuga ng'ombe ili wakale watu wa Dar es Salaam, sitaunga mkono hoja yako kabisa Mheshimiwa Maghembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, mimi nina Hifadhi kwenye Jimbo langu la Geita inaitwa Rubondo, ina Sokwe Mtu wameletwa miaka ya 1962 wanafundishwa kukutana na binadamu. Na kuna watu wanakula posho kila siku na Wizara inatoa hela. Umri wa sokwe kuzeeka yaani maisha yake niliwahi kuuliza wataalamu wakasema miaka

45 mpaka 50. Leo sokwe hawa bado wanafundishwa yaani umri wao umezidi na bado wanaishi kwa huruma ya Mungu lakini sokwe bado hawajaanza kutizamwa. Lakini kingine Maghembe, hifadhi yetu na yenyewe ni ya miaka mingi, tunahamasisha watalii wanaenda kule, kuna gari moja tu juzi umepeleka mbili haitoshi, watalii wakienda 30 mpaka wasubiriane na wakati wamekuja timu moja. Kwa nini msiongeze gari kama zilivyo kule kwenye mbuga zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Ngorongoro huko Kilimanjaro zimejaa, kwa nini usipunguze ukaleta kwenye mbuga zetu hizo ambazo hazina usafiri na watalii wanataka kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine uwekaji wa mipaka wamezungumza na wenzangu, Mheshimiwa Waziri toka Dar es Salaam zunguka huko vijijini uje uone *beacon* za watu wako walivyoziweka. Sijui mna huruma ya *design* gani au mnataka kuipanga Tanzania kwa *style* nyingine. Haiwezekani vijiji vipo toka mwaka 1974 watu wamezeekea hapo wametoka maprofesa hapo na wengine ma-k*ing* kama mimi halafu unakuja kuniwekea kigingi katikati ya kijiji changu. Halafu na simama hapa nakuunga mkono, sitaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine Profesa kuna Tume ya Wizara sita, mbona majibu yake hayatoki? Sisi tunasubiri hiyo Tume ambayo imezunguka kisanii sanii wala haijatuhoji mmeulizana wenyewe na Wakuu wa Wilaya hatujapata majibu, umeleta kutuuzia ng'ombe. Tuelekeze wapi tuzipeleke ng'ombe zetu kama unataka tuziue tununueli kwa bei tuliyofuga nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nikiendelea hapa naweza kutoa machozi halafu huyu Mzee akapata laana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mbatia, ajiandae Mheshimiwa Alberto.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwenye *cover* la juu kabisa ukurasa ule wa kwanza, anaonyesha binadamu wa kale walioishi zaidi ya miaka milioni 3.6. Kulikuwa na hoja hapa ya nembo ya Taifa. Nembo ya Taifa (Uhuru na Umoja) ni alama za Taifa. Hatuhitaji mpaka watu wafe ndio tuanze kuwakumbuka kwenye mambo mazuri waliolifanyia Taifa. Huyu Mzee Francis Maige Ngosha, aliye-*design* hiyo nembo ya Taifa na anaishi bado na yuko kwenye hali hoi bin taabani maisha yake. Naipongeza sana kituo cha ITV Ndugu Godfrey Monyo jana alivyoonyesha tukio la mzee huyu. Tuitake Wizara ya Maliasili na Utalii ni nembo ambayo ni kielelezo cha Taifa, waagize mara moja Mzee huyu ajengewe makazi mazuri na apewe matibabu kwa ajili ya kuendeleza vigezo vya Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Wizara hii uwezo inayo ni sehemu ya mali kale na Mzee huyu amefanya kazi kubwa tuachane na Urasimu Serikalini, Wizara yake ina uwezo na Mzee huyu yupo Jimboni kwako wamjengee makazi ya kisasa, wampe matibabu mazuri ili mzee huyu aweze kufaidi akiwa hai asisubiri mpaka afe ndio tuanze kusema mazuri ya kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema ya kupongeza ITV kwa tukio la jana la Francis Maige Ngosha na kazi nzuri aliyoifanya, sasa niombe nizungumzie sekta ya utalii kwa ujumla wake. Ningeomba nianze na maswali, je, Tanzania tunashika nafasi ya ngapi sasa baada ya takribani miaka kumi mfululilizo kwa vivutio vya utalii duniani. Tunashika nafasi ya ngapi kwenye yale mataifa 133 ambayo tunajiwekea kwenye vigezo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, akishatujibu wakati wa kuhitimisha, atueleze kwamba kwenye miundombinu na ushindani kwenye sekta ya utalii, Tanzania tumewekeza kiasi gani ili kushindana na nchi wenzetu kwa sababu Tanzania tuliokuwa tunashika namba mbili baada ya Brazil tulikuwa tunashika nafasi ya 110 kati ya nchi 133 kwenye miundombinu na ushindani wa utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pato letu la Taifa sasa hivi asilimia 17.5 inatokana na utalii. Miaka zaidi ya mitano iliyopita tulikuwa ni asilimia 17 hiyo hiyo miaka minne/mitano iliyopita 17.5. Lakini Serikali walitamka Bungeni hapa mwaka 2014 kwamba ifikapo mwaka 2020 sekta ya utalii itaingizia Taifa hili Pato la Taifa kwa mwaka walikuwa wana malengo ya zaidi ya asilimia 30. Sasa mbona mfululizo tunabaki kwenye tarakimu hiyo hiyo asilimia 17.5 na mapato ya fedha za kigeni zaidi ya asilimia 25, lakini ili uweze kumkamua ng'ombe vizuri inabidi umlishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii ina kodi nyingi za kero, ina tozo nyingi za kero na sasa hivi kuna kodi na tozo zaidi ya 57. Mimi natoka kwenye eneo la utalii, ukiangalia wanaohudumia watalii, ukiangalia watu wa kati, Makampuni yanayofanya kazi ya utalii, kodi zilizopo ni kero kweli kweli na tozo. Yasiwe ni maneno yangu, kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 98 katika changamoto anazozungumza katika sekta ya utalii ni pamoja na huduma hafifu zinazotolewa kwenye sekta ya utalii. Gharama za juu za huduma ya utalii, anasema gharama za juu, anakiri kwamba *Tanzania is the most expensive destination* katika *region* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Tanzania tuko *expensive* kodi hizi, tozo hizi ndizo zinazosababisha nchi yetu tunazidi kuondoka kwenye asilimia 17.5 ya Pato la Taifa kwa sababu tunaendelea tu kukusanya kukusanya wakati ng'ombe huyu hatumlishi. Hatuna mazingira rafiki, hatuna mazingira mazuri tunayoweka kwenye sekta ya utalii. Wekeza kidogo usiangalie kuvuna leo hii, wekeza vizuri, wekeza vizuri tuwe na washindani. Leo hii Afrika ya Kusini, Zambia, Mozambique, Mauritius, Botswana, Namibia wanatushinda kwa kasi kubwa na Kenya walikuwa na mgogoro na hali yao ya ulinzi na usalama, lakini na wao wanakuja kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serengeti eneo lake ni zaidi ya kilometa za mraba 14,750; Masai Mara wana kilometa za mraba 1,510 lakini wanashindanaje na sisi, vivutio vyote

tulivyonavyo hivyo, ufukwe wa bahari ambao ni kilometa 1,424; sisi ni kwamba bado tunaendelea kupiga danadana hatufanyi maamuzi, na kama ukiondoa kodi hizi, tozo hizi kwa mfano, *concession fee*, mtalii akitaka kuja nchini anamkataba wa zaidi ya mwaka mmoja, miwili, mtiatu kabla. Lakini hapo hapo unataja kwamba kuanzia labda mwezi wa saba, *concessional fee* inatoka dola 25; dola 20 mpaka dola 50. mtalii wa namna gani atakuja kwenye nchi ambayo ni *expensive* kiasi hichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kujenga mazingira rafiki, mazingira mazuri, mazingira ambayo yanakubalika. Kwa mfano, Tarangire kule na Manyara, sasa hivi mnatoka kwenye dola 15 mnaenda mpaka dola 35, watalii wa namna gani watakuja namna hii. *Concession fee* kwa mtalii kwa siku tano ni dola 635 ukiweka na *VAT* ndani yake ni zaidi ya dola 700, utaenda sehemu ambayo ni rahisi na yenye mazingira mazuri ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili utalii wetu kweli uweze ukawa na maana hata suala la *single entry* kwenye sekta hii ya utalii, anaingia mbugani anataka kutoka, akae kwenye hoteli zilizoko karibu na maeneo ya mbugani, arudi tena wakati wa jioni angalau akaone wanyama wametulia, lakini una mdai tena. Hii inaingiaje akilini, jenga mazingira mazuri, *let us think globaly but act locally*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipojenga mazingira mazuri, hata Sera yenyewe ya Utalii wa Taifa ya mwaka 1999 na mazingira yake yote hayo, kwa mfano, Mlima Kilimanjaro, lango kuu la kuingia Mlima Kilimanjaro linapita Marangu katika Jimbo la Vunjo, vijiji vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro maeneo ambayo wanatakiwa kuwa rafiki, sekta hii inahudumia namna gani vijiji hivi viweze vikaonekana kweli mazao ya Mlima Kilimanjaro katika sera, kama ni asilimia 10; ni asilimia 20 ya mapato yale yanabaki pale kujenga mazingira rafiki na mazuri katika sekta hii ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiyazungumza haya kwa mfano suala la *park fees*, *VAT* kwenye *park fees*, kwa nini uweke *VAT* kwenye *park fees* kama umeshaweka *VAT* kwenye usafiri, umeshaweka *VAT* kwenye malazi ondoa *VAT* kwenye *park fees* ili mazingira haya yaweze kuwa rafiki kwa vivutio vya utalii, la sivyo tutakuwa tunapiga danadana hapa hapa asilimia 17.5. Tufanye maamuzi ya kuweza kuweka Tanzania kuwa ni sehemu rafiki Tanzania ni sehemu yenye kuvutia watalii, Tanzania ni sehemu yenye miundombinu mizuri ya utalii, Tanzania ni sehemu ambayo yanajenga mazingira rafiki na Bodi ya Utalii ipewe madaraka ya kutosha. Bodi ya Utali na vile vyama vinavyozunguka waweze kukaa pamoja washirikishwe vizuri. Suala hili liwe ni *inclusiveness,* washirikishwe vizuri kutoa mawazo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nimesoma hotuba hii yote *Tanzania Tour Operators (TATO)* ambapo kwenye hotuba wala hawakujulikani kana kwamba wanafanya kazi katika Taifa la Tanzania. Sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri maeneo yote ya Tanzania ambayo yanazungukwa na mbuga hizi yajengewe mazingira rafiki. Walikuwa wanazungumza Selous jana, mbuga ya Selous ambayo ni kubwa hata wanafunzi wetu kwenye vitabu vya shule hawafundishwi kwamba Tanzania tuna *national park* kama maeneo ya Selous, Tanzania wanafundishwa kuna Serengiti, Mikumi, Manyara na Ngorongoro, je, mbuga kama za Selous, Ruaha ziko nyingi tuu vivutio viko vingi tuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuvitangaze hivi tuwekeze kweli kweli, fedha hizi za maendeleo zilitengwa kwenye bajeti ya Wizara hii kwa ajili ya kutangaza na kuvutia utalii Tanzania ni kidogo mno. Wekeza vizuri na wewe umekili kwamba bajeti ya utalii ni kidogo kwenye hotuba yako ukurasa wa 98, sasa kama bajeti ya utalii na utalii huo huo unaleta mapato, mapato haya Serilkali ifikilie kwa mapana tuwekeze ipasavyo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Alberto dakika tano na Mheshimiwa Ngombale dakika tano.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nilitaka kuchangia maeneo manne, lakini matatu nimeyaleta kwa njia ya maandishi ambayo ni kuhusu *conference tourism, festival tourism* na *water sports tourism* ambayo bado nchi hii haijatilia mkazo na haijawekeza vya kutosha. Lakini eneo ambalo nitalizungumza kwa urefu kidogo na ambalo nina *interest* lakini ninauzoefu nalo ni *sports tourism* ambayo hivi sasa inaambiwa ni *the still sleeping giant,* hii inafaida kubwa duniani na ikitumika vizuri inaweza kusaidia Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa *globally sports tourism* inatengeneza karibu *90.9 trillion dollars* kwa mwaka mpaka 2017. Lakini kutoka 2015 ilikuwa *46.5 trillion dollars* kwa hivyo ni biashara kubwa duniani lakini Tanzania bado hatujaitumia vizuri. Lakini hata katika *individual sport* kwa mfano *golf, golf* ni biashara kubwa na Kenya wanazungusha *a lot of money* kwa sababu wamewekeza katika *golf.* Wana viwanja vyenye kutosha yale mashimo yanayotakiwa vitano ambavyo karibu *35 percent* ya watalii wanaokwenda Kenya ni wale ambao wanakwenda kwa ajili ya *golf.* Halikadhalika na Afrika Kusini nao wamewekeza katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa ujumla *golf* ni biashara kubwa duniani na wanaongoza duniani ni Ireland ambao wanatengeneza wageni kiasi 165,000 kila mwaka wanatembelea Ireland kwa ajili ya *issue* ya *golf* wakati sisi hatujaitumia *golf* kama mchezo ambao unatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye riadha mimi ningetarajia watu wa utalii wangehimiza sana *marathon* zote ambazo Tanzania wangejitokeza wakazidhamini na wakasimamia, lakini pia wakazikuza. Kuna mchezo kama *cycling* ambao tuna maeneo ambao unaweza ukatengeneza pengine *Dar es Salaam to Tanga* tunaona ile Paris mashindano ya baiskeli yanaisaidia sana na

yanaitangaza sana nchi ile, Arabuni wanafanya mashindano ya baiskeli lakini sisi bado hatujaanza kutumia michezo katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu ni kwenye *individual sports* ni rahisi kuwekeza. Kwa mfano Watanzania wote sasa hivi wanajivunia Simbu, Simbu lakini kumbe taasisi za kitaliii zingeweza kutengeneza Simbu wengine kumi kwa sababu kuwekeza katika *individual sports* ni rahisi kuliko kuwekeza katika *team sport.* Kwa hiyo, mimi ningewashauri watu wa utalii wawekeze kwa mtu mmoja/mmoja wamdhamini mtu mmoja/mmoja tunaweza tukatengeneza watu hasa watu ambao wanakimbia kwenye *marathon.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingini ni kwenye mpira wa miguu na hili tayari naelezea *interest* yangu nimeshawaandikia *TANAPA* ni *decleare interst* nimeshawandikia *TANAPA* programu ya namna ya kuweza kuileta timu kutoka Ulaya kuja kucheza Tanzania. Eneo la *pre-season* ambao ni kuelekea kwenye ligu kuu za nchi za Ulaya timu nyingi za Ulaya zinapenda kwenda nje ya nchi zikafanye mazoezi na sisi Tanzania hatujaitumia. Nimekuwa nikisikia kwamba Everton inaweza ikaja hapa lakini tunaweza tukaleta Everton na tukaleta na timu nyingine na nyingine. Kwa hiyo, pia ningetaka watu wa utalii wawekeze katika eneo hili kwa sababu inakuwa na fedha nyingi. Wenzetu Thailand, Singapore na wengine huwa wanafanya kila mwaka na tayari kama nilivyosema nimewapelekea *TANAPA* pengine wataona kama inafaa wataitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna timu za ndani hapa tumezoea kuwekeza kwenye Yanga na Simba. Lakini Yanga na Simba *at the end of day* sio kwa maana ya kuingia watu uwanjani, lakini kwa maana ya kuonekana wanaonekana timu zingine zinaonekana kama timu nyingine katika *television* hasa *Azam Tv* ambayo kusema kweli sasa hivi ni *globally brand,* inafika mbali.

Kwa hiyo, watu wa utalii silazima wawekeze kwenye Yanga na Simba ambao wanapata wafadhili mbalimbali

*NMB, Sport Pesa* na wengine lakini pia wanaweza wakajitokeza kwa mfano timu ambayo najaribu kui-*promote* timu ya Lipuli au timu nyingine zilizopanda daraja wakawavisha jezi zao wakazi-*brand* matangazo ya utalii *at the end of the day* kwa maana ya kuonekana wanaonekana *ninety minuties* sawasawa wanavyoonekana Yanga na Simba na kwa hiyo, wataonekana dunia nzima. Kwa hiyo, ningependa hiyo pia mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza tuliambiwa hapa kwamba tulikuwa tunatangaza kwenye klabu za timu za nje hasa ilikuwa *Sunderland* lakini suala hili liliulizwa mwaka jana halikupata majibu ya kutosha. Na kwa hiyo bado kuna haja ya kutumia matangazo ya nje lakini *very strategical,* mwaka jana nilishauri kuhusu Samatta siju limefikia wapi lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ngombale dakika tano.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu katika muda huu wa dakika tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi ya kuhamisha mifugo kutoka katika Mikoa ya wafugaji kupeleka Mikoa ya Kusini na hasa Mkoa wa Lindi yameleta athari kubwa za mazingira. Na kimsingi hakukufanyika upembuzi yakinifu wa namna gani mazingira yataathirika, maamuzi yale yamepelekea kuathiri sekta ya utalii, mazingira lakini pamoja na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kijiji cha Ngea kuna zaidi ya mifugo 10,000 iko pale, lakini kijiji hiko hakiko katika mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya mifugo. Lakini ndicho kijiji ambacho kina hifadhi ya misitu ya Likonde na Mitalule na mifugo ile ipo ndani mle mle. Kwa hiyo sasa hivi kuna uharibifu mkubwa wa mazingira katika hifadhi ile.

Lakini isitoshe katika kile kijiji kuna Bwawa la Maliwe, bwawa ambalo linatunza viboko wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifanya ziara kule kina cha maji katika Bwawa la Maliwe kinapungua kwa sababu lile bwawa liko jirani kabisa na Hifadhi za Misitu ile. Hivyo basi kutokana na uwepo wa mifugo maana yake mifugo inapelekea mmomonyoko wa ardhi na hivyo kina cha bwawa lile la Maliwe kinapungua. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuiomba Wizara ifuatilie katika maeneo hayo ninayoyaeleza kwa sababu vinginevyo mazingira ya uhifadhi wa misitu ni kama yanaenda kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la wakulima na shughuli zao za kilimo. Wakulima katika msimu wa mwaka huu katika kijiji cha Ngea na vijiji vya jirani ni kama hakuna watakachovuna kwa sababu mazao yote yameharibiwa na mifugo. Kwa hiyo, niiombe Serikali pia iangalie suala hilo ili basi wakulima wetu waweze kuepukana na baa la njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza katika jitihada za kuhakikisha kwamba ile mifugo inatolewa pale Serikali ya Wilaya ya Kilwa ilifungua kesi mahakamani ili basi kuwaondoa wale wafugaji. Lakini katika hali ya kushangaza kwenda mahakamani Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kilwa imeshindwa mahakamani na wananchi wanalalamika kwamba inaonekana kuna dalili ya rushwa. Wananchi wanalalamika iweje vyombo vya ulinzi na usalama vimeenda kuwakamata wafugaji katika maeneo ambayo hawakupasa wawepo, lakini wanapoenda mahakamani wanashindwa. Kwa hiyo niombe Wizara ifuatilie suala hilo wananchi wa maeneo hayo wanapatashida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuna suala la fidia kutokana na uharibifu unaofanywa na wanyama au kwa mazao au kwa binadamu. Katika jimbo langu la Kilwa Kaskazini tunapakana na Hifadhi ya Selous kuna wananchi wamejeruhiwa na wanyama, lakini taratibu zote zinazofanywa ili basi kupata fidia inachukua miaka mingi kupata fidia kutoka Wizarani. Kwa hiyo, niiombe Wizara

kwamba kama ambavyo ninyi mnachukua hatua za haraka pale mwananchi anapomjeruhi mnyama au anapoua mnyama, basi iwe hivyo hivyo pale mnyama anapomjeruhi mwananchi zile fidia zipatikane kwa haraka. *(Makofi)*

Lakini sio hivyo tuu kuna suala zima la mashamba, kuna ekari nyingi za wananchi zimeharibiwa na ndovu, lakini taratibu zimefuatwa kupitia Maafisa wenu wa Maliasili lakini hakuna chochote kinafanyika baada ya taarifa kufika kwenu. Naomba sana hayo myazingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la mipaka kati ya hifadhi hizi na wanavijiji. Kuna tatizo kubwa la mipaka katika kijiji cha Namatewa na kijiji cha Ngarambe. Wananchi wako pale toka siku nyingi lakini sasa hivi inaonekana wenzetu wa Selous wanaidai katika eneo ambalo wananchi wapo wanadai kuwa ni eneo la kwao, kwa hiyo, tayari kumekuwa na migogoro baina ya hifadhi ya Selous na wananchi. Kwa hiyo, niiombe Wizara na hilo lishughulikiwe ili mgogoro uweze kuisha. Ahsante sana, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nape, Mheshimiwa Kakunda Mheshimiwa Silafi Maufi.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie na nianze kwa kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano hasa katika eneo hili la maliasili na utalii, ziko juhudi kadhaa zimefanyika na kwa kweli zinaonekana kwamba zinaweza kuzaa matunda mazuri. Ninaamini kwamba yako mambo yakiboreshwa tutapata matokeo mazuri zaidi, na nimefurahi leo nimemsikia rafiki yangu Musukuma akichangia hapa kwa ukali kidogo na nadhani ukali ule alioutumia ndio ukali tulikuwa tukiutumia hapa kuchangia kwenye maji na maeneo mengine na bahati mbaya wakati mwingine ukichangia kwa kueleza hisia za wapigakura wako unaonekana kama unashambulia Serikali hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa tupo kuboresha, kinacholetwa hapa kinaletwa mapendekezo ya Serikali,

tunapochangia lengo ni kuboresha ili tutoke na kitu kizuri zaidi kwa faida ya Watanzania, bila kujali mitazamo mbalimbali iliyoko hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni suala hili la migogoro ya hifadhi na wananchi wanaozunguka maeneo hayo. Hili limekuwa tatizo la muda mrefu sana na limekuwa likizungumzwa sana na kunaonyeshwa nia ya Serikali ya kulimaliza, lakini likiendelea kutolea kwa ahadi kama ambavyo limekuwa likitolewa halitakwisha.

Ushauri wangu Mheshimiwa Waziri hebu njooni na *time frame* ya kushughulika na tatizo hili kwa sababu liko mahali kwingi na limeumiza watu sana. Na ukisoma kwenye hotuba humu wanazungumza habari ya kuweka zile *beacons*, mimi nadhani badala ya kuendelea na utaratibu huo na kwa sababu hifadhi nyingi hizi ziliwekwa miaka ya 1974 wakati *population* yetu ilikuwa ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda leo ene la Mkoa kama Tabora karibu eneo zima ni hifadhi, watu wameongezeka sana, sasa mkiendelea kuweka mipaka kwa kufuata uamuzi huo huo wa mwaka 1974 nadhani tutakuwa hatutendi haki kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ushauri wangu mimi nilidhani sitisheni utaratibu wa kuweka mipaka fanyeni tathimini kama kweli bado tunahitaji kutunza eneo kubwa kiasi hicho katika mazingira ambayo *population* imeongezeka sana, halafu tukishafikia uamuzi ndio tuweke mipaka ambayo itatupeleka kwa miaka mingine mingi zaidi mbele na katika hili pamoja na *time frame* mmekuwa mnaweka utaratibu wa *task forces* mbalimbali za kushughulikia matatizo kama haya. Mimi nilidhani katika hili kama nia ya dhati ya Serikali ni kulimaliza kwanza tuweke *time frame* lakini tutengeneze *task force* ipewe muda maalumu iende ikalimalize tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la biashara la kusafirisha viumbe hai. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri

ambaye nakiri anafanya kazi nzuri amesema wazi kwamba walisitisha biashara hii kwa miaka mitatu. Naanakiri kwamba baada ya kusitisha imefanyika tathimini kwenye mazizi ya wale ambao walishakusanya hawa viumbe hai na mwishoni anazungumza kwamba tathimini hiyo lengo lake ni kutoa kifuta jasho kwa wafanyabiashara walioathirika na katazo hilo. Sasa kwanza kitendo cha Serikali kukiri kwamba wamefanya tathimini na wana nia ya kutoa kifuta jasho maana yake ni kukiri kwamba yako makosa katika uamauzi huu, ambao mimi nadhani ni jambo la kiungwana kwamba kuna watu wameathirika hawakustahili kuathirika lakini wameathirika na uamuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu mimi nilidhani la kwanza hawa watu wasisubiri hiyo miaka mitatu iishe, Serikali iruhusu hawa watu wasafirishe viumbe hai hawa ambao walishawakamata na waliwakamata wakawaweka kwenye mazizi yao kwa kufuata utaratibu, wamepata lesini, wamelipia kodi na wengine wamechukua mikopo kwenye mabenki na wengine walishalipwa pesa za utangulizi kabla ya kupeleka hawa viumbe kule nje. Kwa hiyo, mimi nilidhani badala ya kuzungumza habari ya kivuta jasho hapa izungumzwe habari ya fidia. Kwa sababu hawa watu wamepata hasara kutokana na uamuzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili uamuzi huu utenguliwe na Mheshimiwa Waziri mimi niko tayari kukamata shilingi yako leo hapa utengue huu uamuzi, hawa watu ambao kwa kweli hawakustahili kuadhibiwa nilikuwa naangalia zinapokiukwa sheria, kulikuwa na matatizo hapa katika uwindaji, kuna baadhi ya makampuni yalikiuka sheria hatukuwaadhibu wote walioshughulika na uwindaji, tuliwaadhibu wale waliokiuka sheria. Kwa hiyo, hata katika hili mimi sikuona sababu ya kuwaadhibu wote waliokuwa wanafanya biashara hii. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba walioathirika wapate fidia, lakini uamuzi huu sasa ufutwe na waruhusiwe kupeleka wanyama wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Waziri kwanza tumepoteza masoko, tumepoteza imani ya

wale ambao walikuwa wanaamini kwamba biashara hii ingeendelea lakini kwa takwimu inaonekana hata wanyama wanaopelekwa ni kidogo sana, lakini mwisho wa yote Mheshimiwa Waziri nyuma ya jambo hili kuna harufu ya rushwa. Pengine inawezekana wasaidizi wako hawakwambii lakini kunahalufu ya rushwa na inazungumzwa wazi wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo la kwanza nilidhani uamuzi huu tusizungumze habari ya kifuta jasho, tuzungumze habari ya kufidia, la pili, tusiendelee na uamuzi huu hasa kwa wale ambao kwa kweli hatuna shida nao wale ambao tayari walishakamata wanyama, wamekopa mikopo, wanawafanyakazi wao, lakini walishachukua *advance payment* za kusafirisha hawa viumbe kuwapeleka nje. Tubadilishe kwenye hili na tukifanya hivi tutakuwa tumewaokoa na kwa sababu sheria ilishabadilishwa biashara hii ifanywa na wazawa. Kuna mikono ya wageni, lakini biashara hii inafanywa na wazawa, mimi nilidhani tuisimamie na tuwasaidie Watanzania hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nchi yetu ina utajiri mkubwa wa utamaduni tuna makabila karibu 126 mimi nadhani umefika wakati sasa kwa kushirikiana na Wizara ya Utamaduni tuende tukawekeze kwenye utalii wa utamaduni wetu. Na mimi nadhani tukiwekeza huko tutapata faida kubwa, huu utamaduni usipowekezwa kitalii ukaanza kutuingizia pesa utaanza kupotea taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kaangalie leo tamaduni kama za Wamasai, Wamakonde, Wasukuma, Waha ni tamaduni ambazo zinaweza kuvutia utalii na uwekezaji wake sio mkubwa sana, uwekezaji wake mdogo sana ni kuutengeneza tu utamaduni ule ukae katika mazingira ambayo mtu akija anaweza akajifunza, anaweza akafanya utalii wake na wapo ambao watafanya tafiti mbalimbali katika utamaduni wetu. *(Makofi)*

Sasa mimi nazani tukiwaachia Wizara ya Utamaduni peke yake hawataweza, lakini sisi Wizara ya Maliasili na Utalii

tunaweza tukawekeza katika utajiri huo wa utamaduni ambao tunao wenzetu wakaja wakajifunza. Mimi nimekwenda Bujora pale, pana mkusanyiko wa utamaduni mkubwa sana wa Wasukuma, lakini nenda Kusini Wayao, Wamakonde...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nape, Mheshimiwa Kakunda, jiandae Mheshimiwa Maufi.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ni vigumu sana mimi kuchangia vizuri sana kwenye hii Wizara kwa sababu kuna wakati Waziri Maghembe akiwa Waziri wa Maji nilikuwa mshauri wake, lakini kwa sababu mimi sasa hivi ni Mbunge wa Jimbo, inabidi nichangie vizuri kwa kutumia nukuu nyingi hasa za Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 8(1) ya Katiba inasema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya Kidemokrasia na haki ya kijamii na kwa hiyo (a) wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba; (b) Lengo kuu la Serikali litakuwa ustawi wa wananchi; (c) Serikali itawajibika kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 9 kuhusu mamlaka ya nchi na vyombo vyake vyote vinawajibika kuelekeza sera na shughuli zake zote katika lengo la kuhakikisha kuwa; (i) kwamba matumizi ya utajiri wa Taifa yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi na hasa zaidi yanaelekezwa kwenye jitihada za kuondosha umaskini, ujinga na maradhi.

Sasa kwenye wajibu wa kulinda maliasili, Ibara ya 27(1) kila mtu anawajibu wa kulinda Maliasilia ya Jamhuri ya

Muungano, mali ya Mamlaka ya Nchi, na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi na pia kuheshimu mali ya mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ndogo ya (2) watu wote watatakiwa na sheria kutunza vizuri mali za mamlaka ya nchi ya pamoja, kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Taifa kwa umakini, kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haki ya kufanya kazi, Ibara ya 24(1) bila kuathiri masharti ya sheria za nchi, zinazohusika kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi kwa mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria. Sasa hapa kidogo nita-*pause.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu ambao wananyang'nywa mali zao, mifugo, hasa ng'ombe bila fidia, hiyo inavunja Katiba, na wakati mwingine wanapigwa faini za mamilioni kwa risiti *fake,* hiyo ni kuvunja sheria za nchi na kuvunja Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wakati mwingine katika risiti zile ambazo zingine mimi ninazo Mheshimiwa Profesa akizitaka mimi nitampatia, risiti imeandikwa hii umepigwa faini kwa ajili ya posho za viongozi, sasa kama posho ile huwa inakuja mpaka kwa Waziri mimi sijui, lakini risiti ninayo na imeandikwa faini hii umepigwa kwa ajili ya posho za viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Ibara 24(2) bila kuathiri masharti ya Ibara ndogo ya (1) ni marufuku kwa mtu yeyote kunyang'anywa mali yake, kwa madhumuni ya kutaifisha au madhumuni mengineyo bila idhini ya sheria ambayo imeweka masharti ya fidia inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba, hii ambayo mimi ninainukuu hapa ambayo ndiyo Katiba yetu inakataza kutumia sheria ambazo zinanyang'anya mali ya wananchi

bila fidia. Kwa hiyo mimi naomba sana tujitathimini kama Taifa, kama hatua zile kama zinaelekezwa na sheria hizo, basi sheria hiyo ni mbovu, na inatakiwa iletwe hapa tuirekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie masuala yanayohusu Jimbo langu la Sikonge. Jimbo la Sikonge au Wilaya ya Sikonge kwa asili yake hiyo Wilaya siyo ya wafugaji, lakini leo wafugaji wamekuja wengi sana kwa sababu ya makosa ya Serikali. Kosa la kwanza la Serikali, mwaka 1959 baada ya kuonekana kwamba kuna uharibifu wa mazingira katika maeneo ya wafugaji yaliyo mengi, Gavana alitoa *order* kwamba mifugo ipunguzwe hadi chini ya 100 kwa kila mfugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *order* ile ilichelewa kutekelezwa mpaka tukapata uhuru, tulivyopata uhuru Mwalimu Nyerere akawatetea wafugaji kwamba hii mifugo sio mingi ukilinganisha na ukubwa wa nchi. Nchi bado tunayo kubwa sana, kwa hiyo, hawa wafugaji kama wanaharibu mazingira huko wanaweza wakasambazwa katika maeneo mengine ya nchi na wakapata huduma yao bila tatizo lolote la uharibifu wa mazingira. Na ndio maana Sikonge kukawa na wafugaji leo wengi na maeneo mengine wamekwenda mpaka Lindi kwa sababu ya *order* ya Mwalimu Nyerere ya mwaka 1961.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Mwalimu Nyerere aliwatetea, kwa nini sisi tumeweka sheria ambazo zinawanyanyasa? Kwa nini tumeweka Sheria ambazo zinakuja kuwabugudhi Watanzania hawa ambao walitetewa na Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kosa la pili la Serikali; mwaka 1968 – 1974 *operation* vijiji kule Sikonge vijiji vya zamani vilivyokuwepo wakati wanapima maeneo ya hifadhi, vilikuwa mbali na maeneo ya hifadhi, wakati wa vijiji vya ujamaa, vijiji vya ujamaa vikapelekwa mita 100 kutoka kwenye hifadhi, unategemea nini kama umemuweka mwananchi mita 100 kutoka kwenye hifadhi, lazima ataingia

kwenye hifadhi, kule kwenye hifadhi kuna miti, asali, nta, na mazao mengine ya misitu, ataingia tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kuwa na utaratibu ambao unalinda maslahi ya wananchi kwa sababu Serikali yenyewe ndiyo imechangia kufanya makosa mengi, nataja maeneo kama Ngoywa, Kipili, Kilumbi, Kiloleli, Usunga, Igigwa, Nyahwa, Mole, Ipole, Chabutwa, Kisanga, kata kumi kati ya kata 20 zote ziko karibu na hifadhi au ziko ndani ya hifadhi, viijiji 29 kati ya vijiji 71 vya Wilaya vyote viko karibu na hifadhi au ndani ya hifadhi. Sasa unategemea nini na Serikali yenyewe ndiyo imewapeleka karibu na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanafaya uchaguzi, wana shule, umeme, kila huduma imepelekwa kule, leo hii unakuja unaweka *beacon* unasema hili ni eneo la hifadhi mhame. Karibu nusu ya watu wa Sikonge utawapeleka wapi, na ndiyo maana hoja ya Mheshimiwa Nape ya kusema Serikali iteue Kamati Maalum na kwa Sikonge iwe *case study* ninawaomba mje Sikonge mkae na *DC*, sisi tuna *DC* mzuri sana, kwanza hata kama mtakaa naye tu mimi sipo, mimi naunga mkono kila mtakachofanya kwa sababu yule *DC* yuko makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nisisitize maeneo haya ya hifadhi yalipimwa mwaka 1954 na maeneo mengi upimaji ulikamilika mwaka 1956 wakati wanapima watu katika Wilaya ya Sikonge ya sasa watu walikuwa 16,000 leo hii kwa *projection* kwa kutumia *formula* ya *NBS* watu wanakaribia 300,000 katika Wilaya ya Sikonge. Sasa watu 16,000 wakati unapima, leo watu 300,000 eneo lako bado lilelile bado unadai kwamba watu waendelee kuishi kwenye eneo lile lile lenye ukubwa ule ule. Eneo la Wilaya ya Sikonge, kilometa za mraba 27,873 eneo ambalo watu wanaruhusiwa kuisha kisheria ni kilometa za mraba 1,049 asilimia 3.7; waende wapi hawa watu 300,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Kamati hiyo ije Sikonge tukae nayo na tuwaelekeze maeneo mengine ambayo yamekosa sifa za kuendelea kuwa hifadhi na mapori

ya akiba yaondolewe kwenye utaratibu ili wananchi wapate kujitanua. Ng'ombe wakati wanapima walikuwa 2,500 leo tuna ng'ombe karibu 200,000 sasa tufanye nini katika hilo na kwa nini wananchi wamekuwa wanadhalilishwa na wanaonewa kwa sababu ya makosa ya Serikali kama nilivyoainisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwisho kabisa naomba sana njooni Sikonge, tukae kwa pamoja, sisi wote lengo letu moja, tunataka tulinde maliasili zetu, tunataka tulinde mazingira yetu na wananchi wako tayari, isipokuwa tu ramani zile zipimwe upya na wananchi tutaelimishana namna ya kulinda mazingira namna ya kulinda hifadhi zetu, zile ambazo zitakuwa zimepunguzwa ili kusudi kila mtu aweze kupata...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Maufi, ajiandae Amina Mollel.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya na nguvu na vilevile nawashukuru kina mama wa Mkoa wa Rukwa kuendelea kuniamini na mimi ninawaambia ya kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa shukrani za dhati na pongezi nyingi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara hii ni pana na ni Wizara ambayo inahitaji nguvu zaidi kuiongezea ili iweze kufanya kazi yake vizuri. Napenda kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri Maghembe na Naibu wake ndugu Makani, wanafanya kazi ni nzuri na kazi ni nzito, na wamejitoa kwa kuweza kuisaidia Tanzania hii katika suala zima la maliasili na utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwapaka matope ya namna moja au nyingine ni kutokana tu na baadhi ya watumishi ndani ya Wizara hii wamekuwa si waaminifu na si waadilifu, ndiyo wanaopelekea Waziri huyu na Naibu wake kupewa matope hayo. Lakini matope hayo hayawastahili hata kidogo kwa sababu ya kwamba wanafanya kazi yao vizuri katika wakati huu mgumu. *(Makofi)*

Napenda kutoa shukrani na pongezi kwa Rais wetu kutokana na jinsi anavyoweza kuimudu nafasi yake na kuisaidia Wizara yetu ya Maliasili kutuletea ndege ili utalii uweze kukomaa ndani ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala la mkaa. Mkaa sisi sote Wabunge humu ndani tumetumia mkaa na bado tunaendelea kutumia mkaa, wananchi wa Tanzania wengi wao takribani asilimia 96 wanatumia mkaa na hata hiyo miji na majiji ambayo wanaotumia umeme na gesi lakini bado wanatumia mkaa, mathalani Dar es Salaam wanatumia mkaa wa takribani asilimia 91 pamoja na kuwepo na umeme na gesi, kwa sababu umeme na gesi ni gharama na umeme na gesi hauna uzoefu kwa wananchi wetu wa Tanzania kwa sababu ndani ya miaka yao yote hii wametumia mkaa na kuni. Kwa hiyo, ninaomba tuzungumzie suala la mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Maliasili, Utalii na Ardhi, nimetembelea Morogoro Wilaya ya Mvomero, Wilaya ya Kilosa na Morogoro Vijijini, upo mradi ambao unaendeshwa pale, mradi ambao unaitwa Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa Tanzania *(TTCS).* Huu mradi ni mradi mzuri ambao tunasaidiana na wenzetu wa Uswis nimeuona utakuwa ni jibu sahihi la kutunza misitu yetu na suala lile la Wizara ama suala lile la Serikali kuzuia kuchomwa mkaa halitaweza kuwepo tena, bali watu wataendelea kuwa na mkaa na kuutumia mkaa. Watautumiaje, hawa ndugu zetu wanaleta mkaa endelevu, ni kwamba wanaelezwa namna ya kukata miche ya mkaa ndani ya misitu wakiacha miche ambayo ina viota vya ndege, miche inayotumika kurina asali, na miche

ya mbao. Wanaitenga, wanachukua miti inayostahili kukatwa na kutengenezwa mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameoneshwa namna ya kuchoma, uko namna kuchoma, namna ya chupa na namna ya *box* kwa kweli utaalam huu unapelekea hawa wachomaji wa mkaa wanapata mkaa mwingi wa kutosha, takribani gunia 50 mpaka gunia 60, na hii sehemu ambayo wanakata baada ya miaka mitatu wanaacha sehemu ile na sehemu ile inakuwa inapata maoteo, na yale maoteo yanarudisha msitu mapema zaidi kulikoni ule utaratibu tunaosema wa kukata mti, panda mti. Kwa sababu tunapanda miti kwa sababu uoto wake na ukomavu wake haupo, unakuwa ni asilimia ni ndogo sana, lakini hii ya maotea inaonekana kana kwamba ule msitu unarudi kama ulivyokuwa zamani na hatimaye unaweza kuwasaidia wanachi kuendeleza mkaa endelevu katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ushauri wangu kwa Serikali, ninaomba mradi huu kwa sababu unachukua muda mrefu, ni vyema Serikali ikaongeza mkono katika mradi huu ili mradi huu ukatawanishwe katika kanda zetu za nchi yetu. Tuna kanda nane za nchi yetu, kwa hiyo katika kanda zile nane wakapeleka utaalum huu wa mkaa endelevu. Ili huu mkaa kwa kweli ni rafiki mzuri sana wa utunzaji wa misitu yetu na mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliomba kabisa kwamba hata mapato ya Serikali yatapatikana kwa sababu yanakuwa na hesabu kwa sababu tanuru moja ni gunia 50; kwa hiyo, watajua Wilaya inapataje, Taifa linapataje, kwa bei ambayo inakubalika. Lakini tukiacha uholela ndio maana tunapelekea kwamba, Wizara yetu inasitisha, lakini inasitisha kwa sababu ya nini, wananchi hawa wanatumia mkaa na mkaa unatumiwa sana na akina mama na hata hii biashara ya mkaa ni kina mama, tunasema kina mama tunawatua ndoo, sasa tukiziba ziba hii mikaa bila kutumia utaratibu huu ni dhahiri kusema kwamba Serikali inaleta mzigo mwingine kwa akina Mama, wa mama watabeba ndoo ya maji, na watabeba tena na mzigo wa kuni ambao kwamba sio sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tanaomba tuwasaidie kina mama kwa kuongeza nguvu katika mradi huu, ili mradi huu uwe ni endelevu na tupate mkaa endelevu kwa wananchi wa Tanzania, kwa sababu mbadala wa mkaa katika nchi hii bado haujapatikana. Kwa hiyo, ninawaomba ndugu zangu tukubaliane na wewe Waziri Maghembe najua ni makini na msikivu, ninaomba huu mradi uje utoe semina kwa Wabunge wote hapa Bungeni, kabla ya Bunge halijaisha ili tukitoka wote na uelewa tutakwenda kutoa maelekezo kwa watu wetu kule na hatimaye na wao watafuata huu mkaa endelevu na sisi tutaweza kuokoa misitu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo kupanda miti itakuja kwa hiyo milima ambayo tuliyoiacha sasa hivi imeshakuwa ni kipara, lakini kwa sasa hivi kwa ile misitu tuliyokuwa nayo ni lazima tuweze kuweka utaratibu huo. Lingine ndio kusema ya kwamba mkaa ujitegemee katika maeneo yao, hao watu wa mjini Dar es Salaam watapata mkaa kutoka wapi, wakati mkaa wa Dar es Salaam unatoka Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuweke utaratibu amabo unaweza kujibu hoja kwamba miti yote haina misitu kwa hiyo hawatakuwa na mkaa, lakini katika miji yote takribani asilimia 91 watu wa mijini wanatumia mkaa. Kwa hiyo nawaomba kwamba utaratibu uwepo, mkaa uingie mijini na iwezekane kuhakikisha kwamba akinamama hawa wanatokana na adha hiyo. Tunavyozuia tunapelekea bei ya mkaa kupanda, sasa hivi Dar es Salaam ni 73...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Amina Mollel, ajiandae Mheshimiwa Kapufi.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu kama wasemavyo wahenga kwamba kila kiongozi basi anakuwa na baraka za Mwenyezi Mungu. Kwa kusema hivyo, naomba nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye mimi nasema wazi kwamba ni chaguo la Mwenyezi Mungu na ni chaguo la Mwenyezi Mungu kutokana na uthubutu wake hasa kwa tukio kubwa leo hii ambalo amelithibitishia Taifa la Watanzania ni kwa jinsi gani kwa muda mrefu tumekuwa tukiibiwa madini yetu na sisi Watanzania tukiendelea kuwepo katika limbwi kubwa la umaskini. Kweli huyu ni chaguo la Mwenyezi Mungu, nampongeza sana kwa uthubutu wake, kwa kile ambacho amedhihirisha leo hii, basi yale aliyokuwa akiyafikiria, kwamba ni kweli, kwa hili tuzidi kumuombea Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu ili aweze kuyabaini mengi na hatimaye Watanzania wafurahie rasilimali zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nichukue pia nafasi hii kuipongeza Wizara, nampongeza Waziri, nampongeza pia na Naibu Waziri, niwapongeze pia na Wakurugenzi wa *TANAPA,* lakini pia Mhifadhi Mkuu wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, pamoja na changamoto zote hizo na lawama nyingi lakini kazi wanayofanya ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwa nini naipongeza Serikali na naipongeza pia Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kwanza kwa hatua yake ya mfumo mpya wa kielektroniki wa kukusanya maduhuli, ambao unaitwa *NCAA Safari Porto* ambao umeonyesha ni kwa jinsi gani wameweza kukusanya shilingi bilioni 81 hii ni faraja kwetu, kwa maana kwamba endapo katika maeneo mengi kuhakikisha kwamba mfumo huu unafanya kazi pesa zitakazo ingia katika sekta ya utalii zitakuwa ni nyingi na zitaweza kusaidia kutatua changamoto mbalimbali zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niishauri Serikali na niseme tu kwamba uzuri wa Bonde la Ngorongoro na sababu ya Ngorongoro kuingia katika maajabu saba ya dunia ni

kutokana na upekee kwamba wanyama pamoja na binadamu wanaishi pamoja na kwa maana hiyo basi pamoja na changamoto mbalimbali zilizopo mimi naishauri tu kwamba Wizara itekeleze maagizo ya Waziri Mkuu ya kuhakikisha kwamba katika Bonde la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro wanatenga maeneo ili mifugo isiingie katika bonde lile na badala yake waende kunywesha maji katika maeneo hayo ambayo yatakuwa yametengwa tofauti na hivi sasa kwamba ndio tunataka kuwaondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwaondoa pasipokuwa na mbadala, je, tumewasaidia kweli hawa wananchi? Kwa hiyo tutimize tu hili agizo la Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba tunatenga maeneo na hayo maeneo basi hao wafugaji watakwenda kunywesha mifugo yao na badala yake hakutakuwa na mifugo itakayoingia katika Bonde la Hifadhi ya Ngorongoro kwa sababu uzuri wa Ngorongoro ni ile *Crater* yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine pia ambalo napenda niishauri Wizara, kwa mfano siku ya Jumapili hapa kulikuwa na semina na tulielezwa ni kwa jinsi gani ambavyo baadhi ya wanyama wapo hatarini kupotea, na hii ni kutokana na muingiliano kati ya binadamu na hao wanyama. Ni kweli nakumbuka siku za nyuma ukiingia tu eneo la Monduli ulikuwa unakutana na wanyama wengi katika maeneo hayo, lakini hivi sasa hakuna na hii inaonyesha kwamba ni kweli ni kutokana na muingiliano baina ya binadamu na wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa pamoja na yote hayo kama kweli katika hifadhi zetu, kama kweli katika mfano Bonde la Ngorongoro tunataka kweli wale wanyama waendelee kuwepo kule tuhakikishe kwamba hata haya magari yenyewe mfano, msimu wa utalii kwa siku zinaingia mpaka gari 200. Sasa Serikali iangalie jinsi gani itaweza kupunguza hayo magari na hata ikiwezekana pamoja na kwamba tozo la kodi lipo basi tuone uwezekano wa kuweka tozo kubwa ili magari yasiingie kwa wingi kule na badala yake tuendelee kuhifadhi mazingira tofauti na hivi sasa ambapo magari ni mengi sana katika *Crater* ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine pia tunafahamu kwamba Serengeti, hifadhi zilizopo Kaskazini ndizo ambazo hasa kwa kiasi kikubwa zinasaidia hata kuendesha hizi hifadhi nyingine, lakini ni pengine ni kutokana na miundombinu ambayo ipo katika maeneo hayo. Katika hizi hifadhi nyingine ambazo zipo naishauri Serikali kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu ili basi hifadhi hizi ziweze kufikika kwa urahisi na watalii waweze kwenda kule, lakini pia kuhakikisha kwamba inatangaza vivutio vingi ili watalii waweze kufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ukienda Kigoma kuna hifadhi ya Gombe na Mahale na kwa bahati nzuri hifadhi hii ina *chimpanzee* ambao katika hifadhi nyingine ni vigumu sana kuwapata. Sasa watalii wengi wanashindwa kufika kule kutokana na miundombinu ambayo sio rafiki. Kwa maana hiyo endapo tutaboresha miundombinu na kuhakikisha kwamba wanafika kule kwa urahisi na kwa bahati nzuri hivi sasa tunayo *bombardier* ambayo inakwenda kule, lakini je, katika kwenda huko Gombe na Mahale miundombinu ikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawahamasishaje watalii ili waweze kufika huko hii ikiwa ni pamoja na kutangaza zaidi na hata kwa kutumia vyombo vyetu vya humu ndani lakini pia vyombo vya nje kama ambavyo kwenye ripoti yenu mmeonyesha. Kwa kufanya hivyo tutaweza katika hifadhi zetu kupata watalii wengi zaidi na kuingiza pato kubwa kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia utalii sio kwamba ni hifadhi tu, utalii hata majengo ndio maana Zanzibar wanakwenda kule kwa sababu ya Mji Mkongwe wa Zanzibar. Ukienda katika Jiji la Dar es Salaam mfano Posta ni eneo ambalo lingefaa sana ule mji badala ya kuubomoa yale majengo ya zamani, majengo yale tungeyaacha ili uwe ni mji ambao utakuwa ni kumbukumbu. Tofauti na hivi sasa tunabomoa majengo yale ya zamani na kujenga majengo mapya, tupanue kwa kwenda katika maeneo mengine ambayo yatatengwa ili basi tuweze kujenga zaidi na hata kuwekeza vivutio zaidi ambavyo vitawavutia wawekezaji

na sio kubomoa tu yale majengo ambayo ni majengo yamekuwepo kwa muda mrefu na majengo hayo tunayapoteza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar wangeweza kufanya hivyo leo hii kusingekuwa na watalii wengi ambao wanakwenda, umebaki kuwa ni mji wa kihistoria, Mji Mkongwe wa Zanzibar. Kwa hiyo, mimi naishauri sana Serikali kuhakikisha kwamba inazingatia haya lakini kubwa zaidi ni kuhakikisha kwamba miundombinu inawezesha watalii wengi kuweza kufika kule. Lakini pia katika huu mfumo unaotumika na Ngorongoro tuhakikishe kwamba tunaongeza mashine katika lile eneo la geti pale ili kuepuka ule mrundikano wa watalii wanapofika pale kwa wingi, kwa sababu wakati mwingine mtalii anapokuja yeyeanataka afike pale amalize zile taratibu mara moja aweze kuingia, lakini matokeo yake anafika pale anapanga foleni kwa kweli inakuwa ni usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuangalie ni jinsi gani mzee wetu Maghembe pale kwamba tunaboresha vipi kwa kuweka kama ni hiyo mifumo ya kielektroniki inakuwepo ya kutosha ili wanapofika pale kusiwepo na huu usumbufu, lakini kwa wale ambao wanasema kwamba tozo hizi za kodi kwamba zimesababisha watalii...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kapufi, ajiandae Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante awali ya yote naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nje ya uhifadhi haya yote tunayoyazungumzia hayatakuwepo, tunayaona haya kwa ajili ya uhifadhi na sisi tukiwa binadamu mzigo tunamtwisha Waziri wetu Maghembe na watendaji mbalimbali, lakini nafasi ya uhifadhi ni ya kila mmoja na ndio maana hata kwa

kupitia kitabu cha Mwenyezi Mungu kitabu cha Mwanzo binadamu alipewa wajibu wa kuja kuitawala dunia na viumbe vilivyopo hapo ikiwa ni misitu na vitu vingine vya namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kuna kauli ambayo huwa naiongea mara zote nikipata nafasi, mazingira yaliyoharibiwa hayana huruma, yatatuadhibu tu hata kama ni miaka 50 ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo nitajikita zaidi kwenye utalii na uhifadhi. Nafahamu kwanza tunapoangalia matatizo tusiangalie kana kwamba hatujawahi kuwa na wakati tulivu tuyaangalie matatizo kwa namna ya kuyatatua, nikilisema hilo kwa kitabu cha wenzetu wa wanyamapori tunaambiwa kuhusu umuhimu wa maeneo yaliyohifadhiwa. Wanasema hivi; "Maeneo yaliyohifadhiwa yana umuhimu mkubwa nchini kiikolojia, kiuchumi na kijamii, aidha maeneo haya huchangia ustawi wa sekta nyingine kama vile mifugo, kilimo, nishati na maji," hilo eneo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikilisema hilo nataka kumaanisha nini, leo hii tukihifadhi asili itatulinda na tunapewa nafasi ya kuamua ni lipi lifanyike na kwa wakati gani. Mfano, wapi tuchunge, wapi tulime, wapi tujenge na tusipohifadhi tutakimbizwa na matukio kwa mfano ukame wa kutisha, mafuriko, mimea vamizi na magonjwa pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna watu tunaweza tukaona ni kwa nini wataalamu wanatuambia ikiwezekana tusichanganye mifugo na wanyamapori, kuna magonjwa ya ajabu, magonjwa ambayo baadae binadamu huyu kumtibia ni kazi ya ziada kutokana na hiyo ya kuwachanganya hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wakati mwingine tuendelee kuheshimu maelekezo ya kitaalamu, na mimi naamini sisiwote lengo letu ni kuijenga nyumba moja, kwa

hiyo tusigombee fito kama tatizo ni la mifugo turudi kwenye ufumbuzi. Je, tunasemaje mimi nafarijika sana, majuzi nikienda Dar es Salaam nilipita Kongwa pale kwenye ile ranchi nikabahatika kupata nyama nzuri kupelekea familia. Kwa maana ya ranchi tunasemaje kuwasaidia watu hawa wakati fulani kulikuwa na ajenda hiyo kwamba wakulima tuendelee kuangalia namna ya kuwasaidia kuwa na ranchi ndogo ndogo ili kuepukana na tatizo hilo. Kwa hiyo twende kwenye kutatua matatizo tusiwe walalamikaji twende kwenye kutatua matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda Kilombero, nikafurahia uumbaji alioutenda Mwenyezi Mungu na katika hili niseme, bonde lile nilifurahi kusikia kwamba hata maji wanayokunywa Dar es Salaam kumbe ni kwa sababu kuna watu wengine wametunza mazingira yao, kwa hiyo, mmoja amefanya kazi kubwa ya kutunza lakini kwa msaada wa watu wengine kwa hiyo nilikuwa naendelea kuliomba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikiwa mjumbe wa Kamati hii majuzi nilikwenda Ngorongoro nikaenda Loliondo nilifurahishwa sana na ule usemi wa kiingereza unaosema *seeing is believing,* niliweza kuona na nikaamini maajabu ya uumbaji aliyoyafanya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,Ngorongoro na Loliondo ile tuamue tunataka nini kama kweli tunahitaji uhifadhi sheria na taratibu nyingine zizingatiwe, nje ya hapo kama hatulitaki hili tuamue jambo lingine. Sisi *politicians* kwa maana ya *political will* tuna nafasi kwamba sasa tunasema uhifadhi, utalii kwa ujumla wake ukae pembeni tutafanya mambo mengine, lakini ukirudi kwa maana ya vyanzo vya mapato fedha zinazoingizwa katika maeneo hayo ni habari isiyofichika kwa mfano ukiangalia ukurasa huu unasema kwamba katika mwaka wa fedha 2013/2014 utalii pekee ulichangia takribani17.2% ya Pato la taifa ikilinganishwa kwa mfano na michango kutoka *GDP* kwa mwaka huo ya mazao ya kilimo ilikuwa 17.8%, mifugo 8.4% na uvuvi 2.4% kwa miaka miwili mfululizo utaliona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mi naendelea kusema tukiacha hilo la pato la Taifa kwa kupitia utalii mimi nina ushauri ufuatao, tusiwe kwamba tunafanyia kazi msaada wa Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hapa tulipo. Tumechukua hatua gani sisi kama binadamu baada ya msaada wa Mwenyezi Mungu kwa maajabu haya ambayo ametupa kuwa na Ngorongoro nzuri, Mlima Kilimanjaro na mbuga nyingine, *initiative* sisi kama sisi tumefanyaje Mheshimiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna watu wanaenda kufanya utalii kwa sababu binadamu amehangaika kujenga jengo refu, mnaenda kushangaa jengo refu lakini vipi sisi ambao Mwenyezi Mungu pekee ametupa maajabu haya *why can't we work on it?* Kwa nini tusifanyie kazi?

Kwa hiyo, mimi naendelea kusisitiza ndugu zangu bila ya uhifadhi itabaki kuwa gumzo, na leo hii kuna mtu unatamani hata kwamba bora nimpeleke ng'ombe pale kwa sababu ni eneo limehifadhiwa ni eneo limetunzwa, turudi tu kama kuna tatizo ya usimamizi wa sheria tujikite hapo, tusimamie sheria, taratibu na kanuni, mimi ushauri wangu ni huo. Lakini eneo jingine tena nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri kwa maana...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Genzabuke, ajiandae Mheshimiwa James Millya. Mheshimiwa Genzabuke vipi?

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema hivi napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa

kazi nzuri wanayofanya, wakati anapanga kununua ndege watu hatukuweza kuelewa alikuwa ana maana gani, lakini sasa baada ya ndege zile kuwa zimefika na zimeanza kazi tayari tumeshaona alikuwa ana maana gani. Tunamshukuru Rais hasa sisi watu wa Kigoma, ndege zile zimeongeza utalii katika Mkoa wetu wa Kigoma, kwa sababu usafiri upo mara kwa mara watalii wanaenda Kigoma, kwa hiyo watalii wanaongeza pato kwa kupitia ndege zile wanazozitumia zisingekuwepo tusingeweza kunufaika kupata watalii wanaoweza kutalii katika Hifadhi za Gombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizugungumzie kuhusu matatizo ya mara kwa mara yanayohusiana na ongezeko la watu na ardhi kutokuongezeka. Asilimia kubwa ya Watanzania wengi ni wakulima na hasa akina mama sasa kutokana na jinsi watu wanavyoongezeka na ardhi ni ile ile kumekuwepo na matatizo mengi yanayotokea mara kwa mara. Serikali kwa kupitia watu wa *TFS* wanagombana na wananchi kwa sababu wananchi wanapokuwa wanaenda kulima kwenye maeneo wanafukuzwa wasilime kwenye maeneo yale kwa sababu mipaka haijaweza kuonyesha wananchi wanalima wapi na mipaka ya hifadhi ni ipi.

Kwa hiyo, nilikuwa ninamuomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu hiki ni kilio cha muda mrefu, Mheshimiwa Waziri mimi ni Mbunge zaidi ya miaka kumi niko ndani ya Bunge hili na mara kwa mara tumekuwa tukitoa kilio chetu kuhusu Misitu ya Hifadhi kubaki haijawekewa mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninaomba kwa sababu Waziri wa Ardhi alisimama humu ndani akasema kwamba itaundwa tume na tume tayari iliishaundwa ikaanza kupitapita maeneo mbalimbali, kwanza nilitaka kujua je,majibu ya tume hiyo baada ya kuwa imezunguka maeneo mbalimbali yamefikia wapi? Kwa sababu majibu yakiishapatikana hayo sasa yatatoa majawabu ya kuweza kutenganisha ardhi ambayo wakulima watalima na ardhi ambayo itakuwa ni hifadhi kwa ajili ya Mapori Tengefu na Mapori Mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kasulu, Kakonko na Kibondo wananchi wameendelea kupata taabu sana, kila wanapoenda kulima mashamba yao ambayo yamepakana na misitu ya Makele na Pori la Moyowosi wanapata shida sana wanafukuzwa, wanakimbizwa na hata katika maeneo mengine. Nilimsikia Mheshimiwa Sakaya akisemaa kule kwao Kaliua nyumba zimechomwa na hata wakati mwingine kule kwetu Kigoma nyumba zinachomwa, wanawake wanapata shida, watoto wanateseka, mazao yanachomwa, mavazi yanachomwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tulikuwa tunaomba Serikali iweze kutusaidia kufanya haraka na kutathmini maeneo hayo ili wananchi wapate maeneo ya kulima kwa sababu wananchi wanaongezeka, ardhi ni ile ile, lakini kwa sasa hivi wananchi wamekuwa na mwamko sana wa kuweza kutaka kulima na hata sisi Wabunge humu ndani. Wabunge walio wengi sasa hivi wameshika maeneo mengi wanataka kulima.

Kwa hiyo, tunaomba kabisa Serikali ifanye haraka iweze kupima maeneo hayo, iweze kuweka mipaka kusudi isogeze mipaka wananchi wapate maeneo ya kuweza kulima ili waweze kuinua kipato chao kwa kutumia maeneo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeshuhudia maeneo mengi wakulima na wafugaji wanapigana, wanauana, vifo vimekuwa vingi kwa sababu ya kugombania mipaka, tulikuwa tunaomba Serikali ifanye haraka kuweza kubaini maeneo ya wakulima na wafugaji; na itenganishe mapema kusudi matatizo haya yanayotokea mara kwa mara ya watu kuuwana, kupigana mapanga na mikuki yaweze kumalizika mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahamasisha wananchi waweze kujitegemea, watajitegemeaje kama hawana maeneo ya kulima; na ndio maana mimi eneo langu kubwa ntakalolisemea leo hii ni kilio kikubwa cha kuiomba Serikali, Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maliasili waweze kukaa pamoja

kumaliza zoezi lile ambalo tayari waliishalianza waweze kutoa majibu ili Serikali sasa iweze kubainisha maeneo haya ya wakulima yawe ni haya ya wafugaji yawe ni haya na maeneo tengefu ya Serikali na yale yanayopakana na vijiji yaweze kujulikana ili kuwaondolea usumbufu wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wanateseka sana hasa wanapokwenda kulima mashambani huko. Wanaondolewa kwa kupigwa, wananyang'anywa baiskeli, mazao yakiiva wanashindwa jinsi ya kwenda kuvuna. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninakuomba na ninakusihi sana, ninafahamu faida ya misitu lakini binadamu nao vilevile wanahitaji kunufaika kupitia misitu inayowazunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tulioupokea ushauri wako uliosema kwamba tuwafundishe watu jinsi ya kufuga nyuki na kutengeneza mabwawa ya samaki. Lakini hawataishi kwa kuvua samaki tu, watahitaji kupata mahindi kwa ajili ya ugali, watahitaj kupata maharage na mboga nyingine zinazotokana na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ya kwangu leo yalikuwa ni hayo. Naiomba Serikali kwa mara nyingine tena, iwasaidie wananchi wa Wilaya ya Kasulu, wanaopakana na Kagera Nkandu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Millya.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nimshukuru saana Mungu kwa kunipa nafasi hii leo lakini niendelee kuwashukuru watu wa Simanjiro kwa kuniamini kuwa Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwenye Wizara hii na kuanza na maneno haya tu, kwamba ni lazima Wizara hii itambue pamoja na maslahi mapana ya nchi ni muhimu kutambua pia kwamba wale waliosaidia sekta hii ya kiuchumi ya maliasili kutunzwa mazingira yake na wenyewe waheshimiwe; maana imekuwa na fikra kubwa sana kwamba wale ambao wanaishi pale, maslahi yao sio mapana sana na sio makubwa kwa Taifa ukilinganisha na Taifa kubwa. Kwa hiyo, hilo Mheshimiwa Waziri naomba uliangalie sana kwasababu mimi ni mfugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niungane na Wabunge wenzangu, mipaka hii kuanzia mwaka 1954 mpaka leo haijaangaliwa tena, jamii imeongezeka na mimi niko kwenye msimamo mmoja kwamba haiwezekani tufike mahali kwamba kesho tukiwa bilioni moja kama Wachina tuseme na mbuga zetu ziliwe, haiwezekani! Ni lazima tukubaliane.Lakini wakati mipaka hii ikiandaliwa watu wetu walikuwa hawajui kinachotokea, hawajui thamani ya ardhi, hawajui nini maana ya mipaka hii na wanyama hawa. Ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri na zile Wizara ambazo zimeungana Wizara tano, mifugo, kilimo tuje na wawakilishi (wote sisi wawakilishi) tukae pamoja tuweke mipaka ya kudumu na tuwafundishe wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Simanjiro vijiji vya Kimotoro, kijiji cha Lobosiret, Emboret na baadhi ya maeneo ambayo mbuga hizi zimezunguka nipo tayari kuwaongoza wananchi wangu tutakapokubaliana na Serikali kwamba mipaka hii sasa huu ndiyo uwe mwisho, kwa maisha ya sasa na maisha ya baadae ya watoto wetu. Ni muhimu sana tukae wadau wote tukubaliane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nitambue kimsingi kazi kubwa iliyofanyika Ngorongoro, Loliondo. Nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri lakini bahati mbaya nimeona pia kwenye Kambi yetu Rasmi ya Upinzani. Wananchi wamekaa na watumishi wa Serikali, wamekubaliana njia ya kwenda mbele ili kumaliza migogoro. Mheshimiwa Waziri ninaona hutaki kutambua nguvu hii. Mimi

nafikiri ni vyema sana wanyamapori na Wizara yako ikae na wananchi tukubaliane wote kwamba kuanzia sasa na maisha ya baadae tunakaaje ili kuhifadhi wanyama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtalii, nikuambie tu ukweli, mimi nazunguka sana lakini namshukuru Mheshimiwa Nape na yeye siku moja nimeenda mbuga moja nikasikia na yeye yupo kwenye hoteli mojawapo. Ni lazima sisi kama Bunge, hii Wizara tuibebe, kazi kubwa tuifanye. Viongozi hamtalii, hamuendi mahali, lakini ni vyema sana Wizara hii iwepo *Ngorongoro Conservation Area Authority,* iwepo *TANAPA* kwa ujumla wake, kina *KINAPA* wote, mfanye juhudi za kipekee za kusaidia Watanzania watalii na viongozi wa nchi hii muanze kutalii kwenye mbuga zetu ili tupate mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nitambue leo Simanjiro, kijiji cha Kimotoro pamoja na kupoteza maisha ya mfugaji mmoja, kuuawa na wanyama, anafidiwa kijana wetu mmoja leo kwa mara ya kwanza tangu dunia iumbwe. Mimi naendelea kusema fidia hii haitoshi, lakini leo anafidiwa mmoja. Naomba Wizara muangalie uhalali wa binadamu, heshima ya binadamu *vis a vis* mnyamapori. Haiwezekani anapouawa, shilingi milioni moja tu! Badilisheni sheria hizi, tubadilishe ili tuheshimu ubinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa kwenye Wizara hii, leo mimi sitaongea sana *against you,*kubwa na imeandikwa kwenye Biblia na Qurani amri kubwa kushinda yote ni upendo. Ninyi wahifadhi kaeni na sisi, nami nitambue kazi kubwa ya Tarangire iliyofanya pale Kimotoro wakati mnapitapita pale Kimotoro tumeweka mahusiano mazuri, Mhifadhi na Afisa Uhusiano wa Tarangire ninaomba nitambue kwamba tumeanza kukubaliana vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee Makumbusho ya Taifa. Bahati nzuri nimesoma mwaka 2006/2007 Misri, nimetembelea makumbusho yao. Watu hawa wanaingiza watalii wengi sana kwa Makumbusho ile ya Cairo. Lakini Ujerumani wanaongoza pia kwa ajili ya makumbusho.

Ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuanzia ukurasa wa 12 mpaka 51 inaongelea wanyamapori, ukiangalia ukurasa wa 53 mpaka 89 kurasa 36 na 39 inaongelea nyuki. Lakini Makumbusho yetu ya Taifa mnaongelea kwa kurasa saba tu, hamuipi uzito utamaduni wetu wa nchi yetu. Makumbusho ya Dar es Salaam hayana maana kubwa ukilinganisha na makumbusho mengine yanayotuzunguka kwenye nchi yetu. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, weka nguvu kubwa kwenye makumbusho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Misri pale bajeti ya 2017/2018 wanapitisha *almost one billion USD* wamepata msaada kutoka *JINCA* wanaboresha makumbusho yao. Mwalimu Nyerere na ninyi bahati nzuri wazee kama ninyi mmeishi na Mwalimu Nyerere sisi wengine tunamuona kwenye makumbusho tu. Kwa nini hampendi kuutunza utamaduni wetu, alianzisha Makumbusho ya Taifa letu. Ninaomba kwa nguvu zote, bajeti ya Makumbusho iongezwe. Ninaombeni tuwape Watanzania heshima hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili kuna suala la utozaji, lakini Mabalozi wetu nimeshuhudia nchini Canada, Balozi wa Kenya anaenda kwenye shule za sekondari na vyuo vikuu vya nchini Canada anawaita watalii wakati wa *low season* wanafunzi anatangaza utalii, imefika wakati sasa nchi yetu tunapomteua Balozi wetu pamoja na hadidu za rejea za kumpa moja ni kutangaza nchi na kutangaza nchi yetu kwenye mataifa ambayo wanaenda. Haiwezekani Mabalozi wakakaa kule maofisini na ofisi kubwa na wanapewa kila kitu, lakini hawatangazi nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu hatupati watalii wa kutosha *Zanzibar is just amazing,* ukiangalia Ngorongoro ni nzuri, ukiangalia Mlima Kilimanjaro, hamna mlima kama huo duniani. Lakini hatutangazi vizuri, mabalozi wetu ni vizuri Serikali iweke hadidu za rejea za kusaidia utangazaji wa utalii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, Ester... dakika zangu.. Ester...

**MWENYEKITI:** Endelea, bado muda.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu mbili naomba nimpe Mheshimiwa Ester.

**MWENYEKITI:** Aah! Sasa utaratibu unatakiwa uniambie mimi sio yeye. Kwa vile kwa miaka mingi huko humu ndani basi nakusamehe. Haya Ester Bulaya! *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mweyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina jambo dogo tu la kumkumbusha Mheshimiwa Maghembe, kwanza kabla ya yote najua moja ya mambo ambayo yanachangia kutoendelea kwenye sekta ya utalii ni pamoja na miundombinu. Mimi naomba nikuambie ni mtalii mzuri tu hata *Easter* yangu nilienda kula pale *Ruaha National Park.*

Mheshimiwa Waziri na Wizara ya Miundombinu hakikisheni hizi mbuga zetu zinapitika vizuri, barabara mpaka katika maeneo ya mbuga yapitike vizuri ili sasa tuweze kuvutia watalii wengi zaidi. Hilo ni jambo la msingi sana kama tunataka kupunguza kwanza gharama na kuhakikisha kunakuwa na watalii wa ndani zaidi; na wa nje kufika kirahisi katika mbuga zetu za wanyama, hilo ni jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende jimboni; Mheshimiwa Waziri nilichangia mwaka jana na mwaka huu narudia, mimi napenda sana uhifadhi, lakini haya mambo yanategemeana na nilisema hatuwezi tukalinda mbuga zetu kwa mtutu. Watu ambao wanaweza wakawa walinzi wazuri ni wananchi wanaozunguka hizi hifadhi. Kule kwetu Mara, jimboni kwangu tuna Mbuga ya Serengeti lakini kila siku tembo wamekuwa wakitoka wakila mazao ya wananchi, wakiharibu nyumba za wananchi na kuua wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hili nimekuwa nikilizungumzia sana. ukienda Kunzugu, Miale,

Nyamatoke na maeneo mengine, ukija kule kwa kaka yangu Boni pia jimboni kwake na kwenyewe kuna matatizo hayo hayo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bulaya, ahsante muandikie mengine. Mheshimiwa Lissu dakika tano, Mheshimiwa Shangazi dakika tano.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa fursa ya kuchangia. Naomba nianze kwa kushauri Wizara, Mheshimiwa Waziri na timu yake kwamba kuna haja kubwa sana sasa ya ku-*diversify* vyanzo vya utalii wetu na mapato ya utalii.

Waheshimiwa Wabunge wamezungumza mengi tangu Mheshimiwa Ally Saleh asubuhi na wengine wamegusia. Nchi nyingi duniani zinapata mapato makubwa kutokana na utalii wa historia tu, *museums!* Ukienda *Vietnam War Museum in Washington DC, Lincoln Memorial, Washington Memorial,* nenda kwenye *museum* za Ujerumani, nenda kwenye *museum* inaitwa *Robben Island, it is a national park in South Africa.* Mamia ya maelfu ya watalii wanakwenda sio kwa sababu kuna wanyamapori; wanakwenda kwa sababu kuna historia. Sasa sisi asilimia 90 ya mapato yetu ya utalii ni wanyamapori na tunajipongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria siku hawapo au mnafikiri wataendelea kuwepo milele. Fikiria hivi kuna siku hawapo, unafanya nini, fikiria! Kwa hiyo, hoja kubwa Mheshimiwa Waziri, *think of diversification,* weka mayai yako kwenye makapu mengi, kapu moja likianguka yatakayovunjika ni machache, hilo niliachie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, haya masuala ya uhifadhi na mahusiano ya wananchi wanaoishi katika maeneo ya karibu na hifadhi zetu. Leo hii zaidi ya asilimia 30

ya *total land mass* ya Tanzania imehifadhiwa na maana yake nikwamba, wananchi kwa mamilioni wameondolewa kwenye maeneo hayo, wafugaji na wakulima hawapo. Namna pekee ambayo tumeitumia kwa miaka zaidi ya 50 ya kulinda maeneo haya ni kuyafanya kuwa maeneo ya kijeshi. Ndiyo maana katika sehemu kubwa yenye uvunjifu mkubwa wa haki za binadamu kwenye Tanzania ya leo ukiachia vituo vya polisi ni kwenye maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi wa aina hii unaotegemea kutesa na kunyang'ana watu maeneo yao hauna *future.* Kuna siku hawa watu wataamka, watajibu halafu tutaenda wapi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba nisaidie tu, kuna sababu gani ya kisayansi leo ya kuwakataza wafugaji wa Kimasai ambao hawawindi kuchunga kwenye hifadhi walikofukuzwa mwaka 1959. Kama unataka kujua sayansi inasemaje soma Allan Rodgers na Kay Homewood 1995 – *The Maasailand Ecology,* wamesema maeneo haya ya uhifadhi yana wanyamapori kwasababu wafugaji wa Kimasai hawana shida na wanyamapori, sio wawindaji. Mmewafukuza mnawaharibia uchumi wao wa kiufugaji, siku wanyama wao wakiisha watakuwa wawindaji, wakipata bunduki kama Karamoja muone mtakwenda wapi na wanyamapori wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna ya kuokoa *long term,* maslahi ya uhifadhi, namna ya kuwaokoa wanyamapori hawa na maeneo haya ni kuhakikisha kwamba zile shughuli za matumizi ya ardhi ambazo kihistoria hazina athari kwenye uhifadhi *(pastoralism)* zinakuwa *integrated. Ngorongoro is a failure* kwa sababu imekuwa *undermined, the idea was good* lakini imetekelezwa vibaya. Wamasai wa Ngorongoro leo ni maskini kuliko Wamasai wengine wote, sio kwa sababu Mungu amesema wawe maskini, ni kwa sababu yahii *militarism* katika *conservation.* Tunahitaji *a new thinking,* Mheshimiwa Mbunge wa Ngorongoro yuko hapa na sijamuona akizungumza, Wamasai wake...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu ahsante, mengine yaandike. Mheshimiwa Shangazi dakika tano.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi naomba nitoe mchango wangu katika hoja iliyoko mezani kwenye Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanyika katika mbuga yetu ya Hifadhi ya Mkomazi. Kuna wataalam kule wameenda kutatua matatizo yale ya mgogoro, kwa hiyo tunaamini kwamba kwa upande wa Lushoto, Korogwe na Mkinga, sasa maeneo yale ambayo wananchi walikuwa wanasigana na hifadhi majawabu yatakwenda kupatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine nilizungumza juzi kwenye semina naomba nilirudie kwamba Msitu wa Shagayu ambao ndiyo unatiririsha maji yanayokwenda kwenye Hifadhi ya Mkomazi uliungua mwaka 2012 takribani hekta 49 na zilizopandwa miti ni hekta 11 tu. Kwa hiyo, ikolojia ya msitu ule imeharibika. Niombe sana kwamba tukapande miti katika eneo lile ili angalau maji yaendelee kutiririka na kufaidisha Mbuga hii ya Mkomazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nimezungumza katika Bunge lililopita kuhusu usawa katika rasilimali za Taifa. Katika Halmashauri ya Lushoto hatuna mlango wa kuingia hifadhi ya Mkomazi, lakini hali kadhalika kwa Korogwe na Mkinga. Eneo pekee ambalo mtalii anaweza akaingia Hifadhi ya Mkomazi ni kupitia Wilaya ya Same. Sasa naomba na sisi wa Mkoa wa Tanga tupate mlango katika eneo lile la Kamakota ambayo iko katika kata ya Lunguza. Tumeshazungumza mwaka jana lakini mpaka ssa hakuna utekelezaji.

Sasa naomba sana kwamba sisi Lushoto tuna utalii wa misitu, tuna utalii wa mazingira na utalii wa miamba. Kwa hiyo ili mtalii aweze kuacha pesa ni lazima awe na siku nyingi za kukaa katika eneo fulani. Lakini anapotumia siku moja na kuondoka ina maana wananchi wa maeneo yale hawafaidiki na kuwepo kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba sana kuwa tuongeze *itinery* ya matukio ambayo watalii watakuwa wanayaona katika maeneo yetu. Kwa hiyo naomba suala hili la kupata geti katika eneo la Kamakota lifanyiwe kazi ili na sisi tuweze kuchangia uchumi wa Taifa.

Lakini suala lingine ni suala hili la uhifadhi na ujirani kwamba kumekuwa na matatizo kati ya wafugaji, lakini pia na maeneo haya ya hifadhi. Sisi kule tunajitahidi angalau kujenga malambo nje ya hifadhi kwenye zile kata ambazo zinapakana na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba *TANAPA* watuunge mkono katika majaribio haya ya kujenga haya malambo na majosho ili tupunguze kasi ya mifugo kuingia katika hifadhi kwa sababu kama tunavyojua hizi hifadhi zimeanza kuhifadhiwa tangu wakati wa ukoloni. Ina maana wakoloni waliona thamani zaidi kuliko labda hata sisi Tanzania huru sasa hivi tunataka kwamba kila mahali tufanye kuwa ni sehemu ya kuchungia wanyama. Ni vizuri tukaweka mipango yetu mizuri. Sisi tumepewa maarifa ya kuweza kutatua na kupanga rasilimali ardhi vizuri, lakini bila kuathiri nia njema kabisa ya kuhifadhi na kutunza rasilimali hizi za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la *concession fees* kwenye mbuga zetu. Hili nalo lazima liangaliwe na kuleta pia hamasa sio tu kwa watalii wa nje lakini kwa watalii hawa wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ahsante sana kwa kunipa dakika hizi tano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru, awamu yetu ya kwanza mchana imepita.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo kadhaa; ninaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kuanzia sasa utaratibu wa kuleta wageni Bungeni umebadilishwa, Mbunge mwenye nia ya kufanya hivyo anatakiwa kuwasilisha majina ya wageni wake angalau siku moja kabla siku inayopendekezwa kutembelewa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mfano; endapo Mbunge atapenda wageni wake watembelee Bunge siku ya Alhamisi atapaswa awe amewasilisha ombi hilo kwa Katibu wa Bunge ifikapo siku ya Jumatano, hatua hiyo itawezesha taratibu mbalimbali za kiofisi kufanyika kabla ya wageni hao kufika Bungeni. Imetolewa na Mkurugenzi wa Idara ya shughuli za Bunge.

Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi mnaombwa kuhudhuria kikao cha Kamati ya Chama leo *White House* mara tu baada ya kuahirisha shughuli za Bunge asubuhi hii. Kwa maana hiyo ni sasa hivi.

Mheshimiwa Halima Mdee anaomba kuwatangazia wanawake wa CHADEMA kuwa kutakuwa na kikao kitafanyika kwenye ukumbi wa chumba namba 227 kwenye jengo la utawala mara baada ya Bunge kuahirishwa mchana huu. Kwa maana hiyo na hili tangazo ni sasa hivi.

Wachangiaji wetu jioni tutaanza na Mheshimiwa Nsanzugwanko dakika tano, tutafidia dakika tano ambazo umegawana na Mheshimiwa Shangazi. Kwa hiyo, utaanza wewe dakika tano atakuja Mheshimiwa Hasunga, Mheshimiwa Yussuf Salim na Mheshimiwa Paresso.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7:00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea mchana nilimtaja Mheshimiwa Nsanzugwanko, atafuatiwa na Mheshimiwa Hasunga na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein ajiandae.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa namna ya pekee kwa kweli niwape hongera sana Waziri wa Maliasili na Naibu wake, lakini pia na watendaji wote ambao kwa kweli wamefika mahali wamesaidia sana ujangili kushuka kwa kiwango kikubwa, hongereni sana kwa kupunguza ujangili katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo mawili tu na ningeomba niyaseme kama ifuatavyo; kwanza ningependa kuzungumzia suala la msitu wa Taifa wa Makere Kusuni maarufu kama Kagera Nkanda. Msitu huu una ukubwa wa hekta 97,000 na msitu huu Waziri unanisikia msitu huu ulikuwa *gazetted* mwaka 1954 wakati eneo lile lilikuwa halina watu kwa kweli, sasa maeneo haya watu wameongezeka vijiji vimeongezeka na sasa watu wanasumbuliwa kujua mipaka halisi ya eneo lile na maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri na timu yako hasa wenzako wa *TFS* na juzi nilipata bahati kuzungumza hata na Dkt. Silayo kuhusu jambo hili, kwamba ni wakati umefika mkaweke mipaka

upya, mka-*re-map* eneo lile kwa sababu watu wameongezeka na kama alivyosema jana Profesa Tibaijuka hapa jamani mazingira yamebadilika huwezi kuwa na mipaka ya 1954 leo ni miaka 60 ukasema mambo yatabaki yale yale, hawa wananchi wameongezeka na lazima utaingia kwenye maeneo kufanya shughuli zao za kujitafutia kipato na uchumi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hili jambo tumelisema na ilishakuja Tume yako kule Kasulu tukalizungumza sana jambo hili, ningeomba sana suala la Kagera Nkanda lifikie mwisho na kwa kweli wananchi waweze kupata maeneo kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Pia niseme kwamba popote itakavyokuwa juzi Mkurugenzi wa Wanyamapori alikuwa anatupa habari ya *genesis* ya biblia, lakini tukubaliane pia kwamba hakuna mahali popote kwenye biblia pamesemwa kwamba sasa viumbe hivi vya wanyamapori na misitu vitakuwa badala ya binadamu, la hasha! Lazima binadamu awe mbele kwa sababu wameumbwa na Mwenyezi Mungu kuweza kutumia rasilimali hizi.

Suala la Kagera Nkanda Mheshimiwa Waziri ninaomba na wenzako wa *TFS* lifike mwisho, mka-*re-map* mipaka ile, sisi hatuna shida na uhifadhi, lakini mka-*re-map* mipaka ile ili watu waweze sasa kupata maeneo ambayo wanaweza kuyatumia kwa kilimo na ninasema tena mwaka 1954 lile eneo lilikuwa halina watu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa niliseme ni suala la la eneo oevu la Malagarasi, maarufu kama *Malagarasi wetland.* Eneo hili liko kwenye uhifadhi wa dunia chini ya *UNESCO,* chini ya *Ramsar site*, eneo hili linaharibika.

Mheshimiwa Waziri wale ng'ombe mliowafukuza kule Geita, ng'ombe waliotoka Burigi wamehamia kwenye chepechepe ya Malagarasi, sasa unataka tupoteze Mto Malagarasi? Kwetu watu wa Kigoma na watu hata Geita wenyewe, Malagarasi ni ikolojia ambayo ni muhimu sana kwa maisha ya watu wetu naomba sana maadam hii *wetland*

ya Malagarasi, eneo oevu ama chepechepe la Malagarasi lipo chini ya *Ramsar site,* chini ya uhifadhi ya dunia, kwa nini lisilindwe kwa nguvu zote, kwa nguvu ya pamoja kati ya *UNESCO,* Serikali ya Tanzania kupitia Wizara yako, maeneo haya tunayaacha yanaharibika na baadaye athari zake ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupotea kwa *wetland* ya Malagarasi maana yake ni kupotea kwa Ziwa Tanganyika, kupotea kwa Ziwa Tanganyika unajua madhara yake itakuwa ni makubwa sana. Hivyo nilikuwa naomba sana maeneo ambayo yametengwa, maeneo ambayo yametangazwa kidunia nina hakika, Wizara na Serikali mnaweza ku-*join hands* na watu wa *UNESCO* maeneo haya yakalindwa ili yaweze kuendelea kuwepokwa sababu binadamu lazima pia waendelee kuwepo.

Mwenyekiti baada ya kusema hayo mawili muhimu niliyokuwa nayo naomba niseme jambo moja la mbuga la Mahale na *Gombe National Parks*, hizi ni mbuga mpya, hizi ni mbuga *virgin* kabisa, nafikiri kupitia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante unga mkono hoja, Mheshimiwa Hasunga, ajiandae Mheshimiwa Yussuf Salim.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kidogo kwenye Wizara hii ambayo ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi.

Kwanza napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa na mambo ambayo wanayafanya katika hii Wizara, kwa kweli nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mchango unaotolewa na sekta hii ni mchango ambao hautoshelezi, haulingani na vivutio tulivyonavyo katika nchi hii. Nchi yetu ni nchi pekee duniani na nchi ya pili kwa kuwa na vivutio vya utalii duniani baada ya Brazil, ni nchi ambayo ina mlima mrefu katika Afrika na mlima wa pili duniani hicho ni kivutio kizuri sana. Ni nchi ambayo kwa mujibu wa wanasayansi mwanadamu wa kwanza duniani inasadikika aliishi hapa, hicho kivutio peke yake ni kikubwa sana katika nchi hii, wanasayansi wamegundua hilo, wameliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni nchi yenye mbuga nyingi sana za wanyama, ni nchi ina maziwa marefu, tuna maziwa mengi, tuna bahari tuna ziwa lenye kina kirefu duniani Ziwa Tanganyika, ni nchi ambayo kule kwenye Jimbo langu la Mbozi kuna kimondo ambacho ni cha aina yake hakipo duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni nchi ambayo watalii wanakuja kuangalia nyayo za watu waliopita miaka mingi walipo kanyanga tunapata hela nyingi sana. Ni nchi ambayo tumebahatika ambayo Mwenyezi Mungu kweli ametupatia kila kitu, lakini ukiangalia mchango wake kwenye Pato la Taifa haulingani na haya yote tulionayo, mikakati tuliyonayo hailingani na hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali sasa hivi kweli tumeanza kuchukua hatua za kuimarisha utalii, kwa mfano kwa sababu tumenunua ndege sasa za kusaidia kuimarisha utalii, hiyo peke yake haitoshi, yapo mambo mengi yanayotakiwa kufanyika ili kufufua utalii wetu. Kwanza lazima tuangalie kodi mbalimbali, tozo mbalimbali zinazotozwa kwenye sekta ya utalii, *concession fees* lazima ziangaliwe, ukilinganisha na wenzetu, ukilinganisha na Kenya, ukilinganisha na nchi zingine lazima tuangalie ni namna gani hizi kodi zinakuwa ni vivutio kwa watalii badala ya kuwa *discourage,* bila kufanya hivyo nchi hatuwezi kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kitu cha muhimu

sana katika sekta ya utalii ni kuimarisha miundombinu ya utalii, miundombinu hiyo ni pamoja na kujenga viwanja vya ndege kwenye maeneo mengi ambayo hiyo nadhani Serikali imeanza kufanya, tumenunua ndege, lakini hiyo haitoshi, tunahitaji barabara nzuri zinazoelekea kwenye vivutio mbalimbali, barabara zinazopitika ili watalii waweze kupita, lazima hayo yote yafanyike kwenda kule kwenye Jimbo langu kule kwenye kimondo barabara ni mbaya, tunahitaji hoteli za maana kwenye maeneo yale. Kule kwenye kimondo hakuna hoteli, hakuna barabara, hakuna nini, ni mtalii gani atakwenda? Sasa haya yote lazima tuyafanye ili kuhakikisha kwamba tunaimarisha sekta hii ya utalii ili iweze kutoa mchango mzuri na unaokubalika katika nchi. *(Makofi)*

Jambo la pili, hatujafanya jitihada za kutosha za kutangaza utalii. Ukiangalia matangazo yetu mengi ambayo tunayafanya hayatoshelezi, ukiangalia bajeti yetu tunayotumia kuitangaza bado ni ndogo, vivutio viko vingi lakini hatujavitangaza kama inavyotakiwa, bila kufanya hivyo hatuwezi kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulikuwa tunachangia hapa tukawa tunasema angalia tulikuwa na *Serengeti Boys,* vijana wetu wameenda kule wanatutangaza, lakini hebu angalia mashindano mengi yamefanyika kwenye nchi hii, kuna *Olympic* huwa tunakwenda, kuna mashindano ya Jumuiya ya Madola huwa tunakwenda, kuna Kilimanjaro pale huwa tunakwenda yale mashindano yalikuwa na watu wengi sana, mwaka jana nafikiri walikuwa watu 11,000 walishiriki kwenye yale mashindano, *Mount Kilimanjaro Marathon* walishiriki, lakini angalia jezi ambazo wanavaa watu wetu, angalia jezi wanazokuwa wamevaa hazitangazi utalii, makampuni yetu yapo wapi kutangaza huo utalii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kuna wachezaji, kuna mmoja ameenda kule ameshiriki Uingereza ameshinda, lakini alikuwa na jezi anatangaza bia, jezi yake ile inatangaza *Multi Choice* ya South Africa na ametoka Tanzania, hiyo lazima tusikitike, lazima tuhakikishe tunakuwa *very strategic*

tufanye maamuzi ambayo kweli yataisaidia katika kuimarisha nchi hii *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna michezo mingi inafanyika sasa hivi, najua tunajiandaa kwenda Japan, wenzetu Wakenya wanapoenda kwenye michezo kama hiyo huwa wanaomba mpaka *space* wanakuwa na *space* kule ya kutangaza, Ethiopia wanakuwa na *space* ya kutangaza wanakuwa na banda wanatangaza vituo vyao vya utalii pamoja na michezo, Watanzania tunagawa *business card* kwenye mabanda yetu, hatuna hata maeneo ya kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuimarisha ili kuhakikisha kwamba kwa kweli mambo yaende vizuri, bila kufanya hivyo tutashindwa. Sekta hii ina mchango mkubwa sana ambao ninaamini kabisa unaweza kuchangia sana katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie Ngorongoro, Serengeti na makampuni mengine yajaribu kudhamini michezo mbalimbali, tuna michezo mingi sana Tanzania, ikidhaminiwa tukawapa vifaa vizuri vya michezo kwa ajili ya kutangaza utalii, ninaamini tutajitahidi sana na tutaweza kufufua na kuisukuma mbele sekta yetu hii ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika mbuga zetu huku watalii wanapokwenda, zile huduma za msingi zinakuwa bado ni kidogo sana. Nimeangalia juzi walikuwa wanalalamika wanapopanda Mlima wa Kilimanjaro, wanapopanda wanasema kuna watalii wengine wanashindwa, wakishindwa kule hakuna hata *helicopter* ya kuwapa msaada, hakuna nini, hiyo inatuaharibia. Vifaa vya dharura vya kuweza kuwasaidia watalii wetu wanapokuwa wamepata dharura tuviimarishe katika maeneo yetu ili tuweze kusaidia katika hii sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vyuo vya utalii nimeangalia hapa na mambo mengine mengi, ushiriki wa

sekta binafsi yote ni mambo ya msingi sana, suala la msingi zaidi ili kuweza kuvutia watalii ni ulinzi na usalama ndani ya nchi yetu, bila kuwepo na usalama wa kutosha watalii wanaogopa hawawezi kuja.

Naiomba Serikali iweke utaratibu mahsusi, iweke mikakati ya kutosha kuhakikisha kwamba tunaimarisha ulinzi na usalama katika maeneo ya vivutio vyetu vya utalii na hiyo itasaidia sana kuweza kuleta mchango mkubwa na kuimarisha sekta yetu hii ya utalii ili iweze kutoa mchango mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ya msingi sana katika hii Wizara na ni Wizara ambayo inaweza ikatubeba, tukichanganya hii na ya Madini kama leo tumesikia taarifa zingine za madini tukichanganya zinaweza kusukuma maendeleo kwa kiwango kikubwa sana katika nchi yetu. Kwa hiyo, lazima mikakati ya kutosha kabisa iwekwe hapo ili kuhakikisha hii sekta inaimarika.

Suala la pili ambalo ningependa kuchangia katika hii Wizara ni suala la misitu na utunzaji wa misifu. Hifadhi ya misitu iko maeneo mengi, kule Jimboni kwetu sasa hivi imekuwa ni kero kubwa sana katika utunzaji wa misitu, ile misitu miaka ya nyuma tulikuwa na machifu walikuwa wanalinda sana ile hifadhi, wananchi walikuwa hawakati kati ovyo, sasa hivi Serikali ikaja kuanza kushughulikia inawakamata watu ovyo hadi misitu ile imeanza kuharibika. Ninaamini kabisa kama tukiwatumia na tukiwashirikisha wananchi katika kulinda ile misitu inaweza ikalindwa vizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo limejitokeza sana kule Jimboni hii Wizara inatoa vibali kwa wakata mkaa, baadhi wanakata magogo, wanakata mkaa, wanauza lakini wananchi wakikutwa na mkaa wananyang'anywa na wanapigwa, wakati tayari hao wamepewa vibali, najua kuna wengine ambao wanakuwa hawana vibali lakini wapo wengine wana vibali, sasa inakuwaje wananchi wale wanaotumia mkaa wakati hawajaambiwa nishati mbadala

hasa wanatumia mkaa wanakamatwa na bahati mbaya wanapokamatwa, wanaponyang'anywa ule mkaa haupelekwi Serikali. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hasunga, Mheshimiwa Yussuf Salim, ajiandae Mheshimiwa Paresso.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** *Bismillah Rahman Rahim.* Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie jioni ya leo, Mheshimiwa Waziri naomba unisikilize vizuri, nataka kuendelea kukushauri kwa mwaka wa pili mfululizo.

Mheshimiwa Waziri, Wizara yako ni ngumu sana na unapaswa kuwa mvumilivu sana, tenda wema uende zako usingoje shukrani.

Naanza na utalii, Waheshimiwa Wabunge wengi humu walikuwa wanachangia kila mmoja katika Jimbo lake, katika Wilaya yake anataja vivutio vya utalii ambavyo vipo katika eneo lake, lakini bado havijaanza kufanya kazi. Wengine wamesifia kwamba Rais ameleta ndege na idadi ya watalii wameongezeka, lakini hatuwezi kuvaa koti bila kuvaa shati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushauri kwamba ili kupata watalii wengi ni lazima tuwe na hoteli za kutosha, tuwe na *facilities* za kutosha kwa hiyo tuongeze *number of rooms* katika nchi yetu ili idadi ya watalii iongezeke na hilo litafikiwa baada ya kuwa na mahoteli mengi lakini pia baada ya kuweka miundombinu ya kutosha ambayo itawafanya wawekezaji wavutike kuja kuwekeza katika sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwa nchi yetu ya

Tanzania ukiangalia vivutio vya utalii tulivyonavyo ni *natural* siyo *artificial,* lakini unaambiwa nchi yetu inaingiza watalii milioni 1,200,000 ni aibu kubwa sana. Ukiwagawa hawa kwa vivutio tulivyonavyo labda kila mtalii anaweza kwenda katika kivutio kimoja tu. Kwa hiyo, nakushauri tuwe na lengo katika kipindi cha miaka kumi ya Serikali ya hapa kazi tu, basi angalau tuwe tunaongeza milioni moja baada ya miaka 10 tuwe na watalii milioni kumi na hili linawezekana kama tutakuwa na mipango madhubuti ya kuongeza mahoteli na kuboresha miundombinu katika sekta ya utalii kule chini, hizi ndege zitakuwa hazina maana yoyote kama mgeni akifika hapa hapati huduma za kutosha kule chini, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Pili, Mheshimiwa umezungumzia tu suala la utalii wa fukwe, lakini limezungumzwa sana hapa utalii wa baharini, sijaona hasa mkakati madhubuti ambao unatupeleka kwamba katika kipindi kijacho tutakuwa na hoteli ngapi za kitalii au tutakuwa na utalii wa fukwe wa aina gani. Naomba tuweke mikakati, tuweke mpango hasa madhubuti, haya maneno yasikutishe tuweke mpango madhubuti ili ukiondoka tuseme Mheshimiwa Maghembe na Naibu wake mlifanya nini, kwa hiyo maneno yasikutishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toba sikio, narudia toba sikio, nasikia kuna *fees* zinataka kuongezwa baada ya Bunge hili, hizo *fees* kama mtakubali na wataalam wako sijui kama mmeshauriana ziingie zitaua sekta ya utalii. Sidhani kama *TRA* ni wataalam wa sekta ya utalii, siwakatazi kupandisha kodi lakini wakae na wataalam wa sekta ya utalii waone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia kuna *fees* za *hunting block fees,* wanataka kuweka *fees* asilimia 18. Kuna *hunting block application fees,* kuna *application for hunting block transfer fees,* kuna *hunting permit fees,* kuna *conservation fees for hunters,* kuna *conservation for hunting observer's fees,* kuna *intercompany permit fees,* kuna *travel handling fees,* kuna *professional hunting licence fees,* kuna *examination fees, game fees, fees for non consumptive wildlife utilization photographic tourism.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakubali asilimia 18 katika haya unaenda kuua utalii. Naomba watalaam wa utalii wakae pamoja na watu wa *TRA* mkubaliane kwenye *fee* hizi, zikiingia zitaenda kuua utalii. Nakushauri hilo kama mtaalam ambaye nimefanya kazi katika sekta hii. Nafahamu kama mwekezaji, nafahamu kama mzalendo, nakushauri kitaalam kabisa. Serikali mkae mliangalie upya, *fees* hizi zikiingia zitaua sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwenye hoja ya utalii, suala la makumbusho, suala la Makumbusho ya Taifa limetajwa sana hapa, watu wamezungumza sana, bado halijafanyiwa kazi. Nakuomba uwaangalie wafanyakazi, stahiki zao, mazingira wanayofanyia kazi, tumetembelea makumbusho, tumezungumza na wafanyakazi, mfanyakazi anafanya kazi pale miaka mitano hajapanda cheo, hajaongezwa mshahara, hajaenda kusoma. Wakati mwingine anafanya kazi, masaa ya kazi yanamalizika bado kuna wageni hawezi kuondoka, hana hata malipo ya *over time,* hili nalo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu suala la misitu na nyuki. Watu wengi hapa wameshauri kwamba tuangalie suala la mkaa, wametoa mfano wa Kilosa. Kilosa imefanikiwa lile kwa sababu wana wataalam. Ule mradi kuna wataalam wa misitu pale ndani, kwenye Halmashauri wana wataalam wa misitu pale ndani, kwa hiyo, ule mradi wa kuchoma ule mkaa endelevu ni kwa sababu wana wataalam wa misitu. Nakushauri Mheshimiwa Waziri ufanye linalowezekana Chuo cha Misitu Olmotonyi kifufuliwe ili kuweza kuzalisha wanamisitu ambao wataweza kuendeleza misitu yetu. Bila kuwa na wataalam wa misitu ambao watakuonyesha hasa mti huu unakua mahali gani, una faida gani na kwa maslahi gani? Hatuwezi kufikia hayo malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko Kilosa mlikofanikiwa, mlifanikiwa kwa sababu wale Maafisa Misitu wanawaeleza wale wanakijiji kwamba mti huu ukiukata unatoa *coppice,* mti huu usiukate kwa sababu ndege ni mazalia yake. Mti huu ni mti wa asili ubakie, lakini mtu ambaye hajui yeye

atakata tu kila akiuona mti mnene ndiyo anauona huu nitapata mkaa zadi. Kwa hiyo, Chuo cha Olmotonyi kifufuliwe kitoe wataalam zaidi na siyo wanafunzi wajisomeshe wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wanyamapori. Mgogoro huu wa Loliondo, Ngorongoro naiomba Serikali kwa dhati kabisa ikae chini iamue inataka nini. Kama Serikali wanataka uhifadhi na maliasili zetu za Taifa zibaki kwa ajili yetu na kizazi kijacho basi iamue kutaka hivyo, kama Serikali inataka siasa iendelee na mchezo huu wanaoendelea nao. Suala la Ngorongoro, Loliondo linasababishwa na wanasiasa, tuwe wazi tuseme pale watu wana *interest* zao binafsi na hawaangalii, wakati hiyo mifugo ipo pale ilikuwa ni mifugo mingapi? Walikuwa ni watu wangapi wanaishi pale na leo ni wangapi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Nianze mchango wangu kwa sekta nzima ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii imekuwa ikichangia asilimia 17 ya Pato la Taifa ukilinganisha na sekta zingine. Kwa tafsiri nyingine unaweza ukasema Pato la Taifa chanzo chake kikuu ni sekta ya utalii. Sekta hii ya utalii imekuwa na changamoto nyingi ambazo zinazidi kuongezeka. Kama changamoto ni nyingi na zinazidi kuongezeka maana yake sekta hii haiwezi kukua na kuendelea kuongeza Pato la Taifa kwa maana ya kutoka kwenye hiyo asimilia 17 kwenda hata angalau asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto zilizopo kwenye sekta hii, imekuwa haitiliwi mkazo kutangazwa ipasavyo. Mikakati ipo lakini

inawezekana fedha zinakosekana ya kutangaza kwa upana sekta ya utalii ndani na nje ya nchi, imekuwa ni changamoto ya muda mrefu ndio maana tunabaki palepale hatuwezi kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine Serikali haina ubunifu wa kuongeza vivutio vingine vipya. Tumekuwa na vivutio vya zamani na hivyo vingine vimetelekezwa, lakini hakuna ubunifu wa kuwa na vivutio vipya ambavyo vitawashawishi watalii waweze kuja kuangalia kwa wingi hapa nchini. Kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali kuangalia namna gani vivutio vilivyopo mnaviendeleza, lakini mnabuni vivutio vingine ambavyo vitaweza kuhahakisha kwamba watalii wanakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linaifanya sekta hii ya utalii iwe na changamoto kubwa ni masharti magumu kwa wawekezaji ikiwemo suala la kodi. Katika Awamu ya Nne kodi ambazo zilikuwa zinalipwa na wawekezaji katika sekta ya utalii ilikuwa ni kodi kati ya 14 mpaka 16. Leo Serikali ya Awamu ya Tano mmeingia madarakani mmepandisha kodi ambazo wanalipa wawekezaji katika sekta ya utalii zimetoka 14 mpaka 36 na sasa hivi ninasikia tena mnataka kupandisha nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizi au namna gani kama mnaongeza kodi hakuna mwekezaji ambaye atakuja ku-*invest* kwenye sekta ya utalii na tukaona inakuwa atakuwa anazikimbia hizi kodi. Kwa hiyo, tunatarajia kwamba muende mkae, mpunguze kodi muweze ku-*encourage* wawekezaji wengi ili sekta ya utalii iweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika haya haya masharti magumu, leo mtu akitaka kupata *TALA licence* unalipa dola 2000 kwa magari kuanzia matatu. Tunajua huko huko nyuma ilikuwa ni magari matano unalipa dola 2000, mkapunguza mkafanya magari matatu kwa dola 2000, lakini kwa wale vijana wa Arusha ambao maeneo yenye utalii atapambana atapata magari matatu atalipa dola 2000, huyu anashindana na mwekezaji mkubwa mwenye magari

100 naye analipa dola 2000. Kwa mfano, *Leopard Tours* wana magari kibao, naye analipa *TALA licence* ya dola 2000. Halafu kijana wa Arusha anajitahidi amepata magari matatu naye analipa dola 2000. Kwa nini Wizara msifikirie kupunguza hii *TALA licence* mkalipa *TALA licence* kwa gari ambayo itaiingizia Serikali mapato zaidi; yule mwenye magari 100 atalipa kulingana na idadi yake ya magari na yule mwenye magari matatu naye atalipa kulingana na idadi yake.

Mheshimiwa Waziri hii limekuwa ni kelele ya muda mrefu lakini hatupati majibu ya kuwasaidia hawa. Pia itawasaidia na ninyi kuongeza mapato, kwa hiyo, ni vizuri mkalifikiria hilo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine katika sekta ya utalii ni ushiriki mdogo wa maonesho ya utalii na kutokupewa kipaumbele. Masuala mazima ya maonyesho ya utalii na vivutio vya utalii inaoneka imeachiwa sekta binafsi na Serikali imekaa pembeni, imekuwa ni changamoto ya muda mrefu. Sasa kama ninyi mkaa pembeni mnaziachia sekta binafsi ziende zenyewe zijitangaze, zijipambanue na kuonesha wana vitu gani, ni kwa namna gani sekta hii itaweza kukua. Haiwezi kukua *obviously* kutakuwa kunaendelea kuwa na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni vyuo vichache vya utalii vinavyotoa mafunzo ya utalii na imekuwa ikitoa mafunzo duni haiendani na kasi ya ukuaji wa utalii. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali mkafikiria namna gani kushirikiana na sekta binafsi kuhakikisha kwamba vyuo vya utalii vinakuwa na ubunifu zaidi, lakini inaendana na kasi ya ukuaji wa utalii duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la migogoro ya vijiji na hifadhi za wanyamapori. Migogoro hii imekuwa ni migogoro ya muda mrefu, ni migogoro ambayo ndani ya Bunge tumekuwa tukisema lakini unachokiona tukipiga kelele kuhusu migogoro, Serikali mnakimbilia kuunda Tume. Mnakimbilia kuunda Tume, mnatuahidi kwamba Tume zikifika maeneo hayo mtashirikisha wadau mbalimbali,

wanafanya kazi hizo wanamaliza hatujawahi kusikia ripoti ya Tume hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009 Bodi ya *TANAPA* iliunda Tume ya kuchunguza migogoro ikatoa mapendekezo, sijui yamefanyiwa kazi kwa kiasi gani. Mheshimiwa Waziri Mkuu wa zamani Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda aliunda Tume, Mheshimiwa Kagasheki akiwa Waziri aliunda Tume, Mheshimiwa Lukuvi aliunda Tume na sasa hivi nasikia mmeunda tena Tume inayohusisha sekta zote lakini hakuna majibu. Serikali mkisikia migogoro ya wananchi na hifadhi badala ya kutuletea majibu mnakimbilia kuunda Tume zinazotumia fedha nyingi za walipakodi, taarifa ya Tume mnaweka kapuni hamtuambii. Leo hapa msimame mtuambie angalau ni mgogoro gani ambao mmeumaliza? Hamna na migogoro inaendelea! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kila siku kuona wananchi wanashughulikia tu migogoro wanaacha shughuli zingine, Serikali mnakimbilia kuunda tume ambazo hatupati majibu yake. Kwa hiyo, nafikiri ni wakati muafaka sasa Serikali mtuambie kwanza hizi Tume zote ambazo mmeziunda majibu yake yako wapi? Ripoti yake iko wapi? Utekelezaji wa matokeo ya Tume hizo umefanyika kwa kiwango gani? Kwa nini kama ambazo hazijafanyika ni kwa nini imeshindikana kufanyika mpaka sasa hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mgogoro wa Loliondo. Mgogoro wa Loliondo pia ni kati ya migogoro ambayo imekuwa ni ya muda mrefu. Leo Serikali inataka kuondoa wananchi takribani 54,000 katika vijiji 14 waondoke kwenye eneo la kilometa za mraba 1,500, hivi unawaondoa watu 54,000 unawapeleka wapi? Huko unakowapeleka si ndiyo unaenda kuendeleza mgogoro mwingine wa ardhi? Serikali mtuambie mna maslahi gani na suala la Loliondo, kwa nini mmeshindwa kulipatia ufumbuzi wa muda mrefu? Kwa sababu umekuwa ni mgogoro wa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala mtuletee ufumbuzi

wa tatizo la Loliondo, mnakimbilia mnasema *NGO's* zilizoko Ngorongoro zinachochea wananchi kuendeleza migogoro hii. Kwanza hizi *NGO's* zilizo nyingi zimesaidia kujenga uelewa wa wananchi wa kule, lakini kama kweli kuna *NGO's* ambazo zinafanya ushawishi na uchochezi *it is okay* zichukuliwe hatua lakini siyo kuzihukumu *NGO's* zote labda kwa sababu ya baadhi ya *NGO's* ambazo zinafanya ndivyo sivyo.

Kwa hiyo, Serikali mtuambie hivi mna maslahi gani na huyu Mwekezaji wa Loliondo huyo *OBC* huyu Mwarabu mtuambie? Huu mgogoro umekuwa wa muda mrefu, mnaenda mnaunda Tume, sijui Waziri Mkuu ameunda Tume, sijui Waziri umeenda, Mkuu wa Mkoa Gambo ameenda, sijui ataenda na nani labda aje na malaika naye aende, lakini hamtupatii ufumbuzi, kwa nini wananchi wa Loliondo wanateseka kwa muda mrefu? Mtuambie Mheshimiwa Waziri kwanza mna maslahi gani na huyu Mwarabu na kwa nini mgogoro huu haumaliziki?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,......

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kanyasu, ajiandae Mheshimiwa Bulembo, dakika tano, tano.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na kwa sababu ya muda naomba nizungumze mambo machache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba Geita Mjini tulipopata bahati ya kuwa Makao Makuu ya Mkoa wa Geita karibu nusu ya eneo la upande wa Mashariki miaka ya 1954 lilikuwa *declared* kwamba ni hifadhi, hakuna msitu wowote kuna *bushes.* Nilimwandikia barua na kumuomba kwamba wananchi wa Geita ule mkoa hauwezi kutanuka kuelekea Kaskazini wala kuelekea Magharibi kwa sababu ni eneo

ambalo limepewa mgodi, eneo pekee la kutanuka ni kuelekea Kusini, na Mkoa kupitia *RCC* wameomba katika vikao tangu mwaka 2012 kuomba eneo la Msitu wa Usindakwe na eneo ambalo lilikuwa Msitu wa Geita (Usindakwe) liwe eneo ambalo Mkoa uruhusiwe kutoa maeneo ya makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza karibu nusu ya Mji wa Geita ni eneo ambalo zamani lilikuwa *declared* kwamba ni hifadhi, sasa nilikuomba Mheshimiwa Waziri kwa maandishi lakini sasa ni karibu miezi sita naomba leo uniambie ni hatua gani zimefikiwa? Sababu moja ni kwamba mpaka leo watu wa *TFS* wanazunguka, wanaweka alama kwenye nyumba, wana-*disturb* watu, lakini hakuna mti, hakuna chochote. Katika maeneo ya Nyakabale na Mgusu wananchi katikati ya kijiji kuna vigingi na katikati ya eneo la vijiji hivyo tayari mgodi umepewa eneo hilo, hivyo, wanashindwa kufanya chochote kwa sababu eneo hilo linaonekana kama ni hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni *TFS* katika Mkoa wa Geita, limetoka tangazo kupitia kwa Waziri kwamba ni marufuku kutumia pikipiki, baiskeli kubeba mkaa wala kubeba chochote. Vijiji vyetu vyote ambako wananchi wanakaa hakuna magari, hakuna chochote, kwa hiyo matokeo yake watu wa *TFS* wamerundika pikipiki na baiskeli Makao Makuu ya Ofisi zao na wanategemea kuzipiga mnada. Baiskeli ambayo imenunuliwa shilingi 150,000 inauzwa shilingi 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri jambo hili ni uonevu mkubwa kwa sababu wananchi katika maeneo hayo ya vijiji hawana usafiri mwingine wowote mbadala zaidi ya baiskeli. Sasa sheria inaposema kwamba ni lazima tutumie magari, kusafirisha mkaa, hivi wananchi kwenye vijiji wanapata wapi magari? Kwa sababu inavyonekana ni kama mkakati wa kuwadhulumu wananchi baiskeli zao, ananunua mtu baiskeli, anakamatwa anakimbizwa porini ananyanganywa na sasa hivi watu wa *TFS* wanakwenda kwenye masoko kusubiria watu. *(Makofi)*

Mimi nafikiri *TFS* wamesahau *core function* yao. *Core function* yao ni kulinda misitu, wanachokifanya sasa siyo kulinda misitu tena, ni kusubiri barabarani waendasha baiskeli na pikipiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuambie na tangaza leo hawa wananchi wanatumia nishati gani? Tuambie tu mimi niko tayari kuwaambia wananchi sasa acheni, ni nishati gani mbadala ambayo Wizara yako imeandaa kwamba sasa hii ndiyo itakuwa nishati mbadala? Kinachoendelea sasa hivi na kwa wananchi ni kwamba wananchi wanalazimishwa sasa waanze kulala njaa kwa sababu mkaa unakamatwa sokoni, unakamatwa barabarani, anakamatwa mwenye baiskeli, pikipiki, gari haijulikani utaratibu huu sasa unatupeleka wapi.

Mheshimiwa Waziri inawezekana wewe huna taarifa, nguvu inayotumika kwenye suala hili kule kwenye maeneo ya wananchi ni kubwa kuliko hata thamani ya kitu kinachoenda kuzuiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikushauri Mheshimiwa Waziri, kwa nini unapata tatizo kubwa sana la kulinda misitu yako, unapata shida ya kulinda hifadhi? Kwa sababu ya mahusiano mabaya sana ya *TFS* na vijiji. Watu wa samaki walibuni kitu kinaitwa *Beach Management Unit (BMU)* kwa sababu wananchi wanatakiwa wajisimamie wenyewe. Ninyi mnatumia nguvu kubwa, amesema Mheshimiwa Mbunge asubuhi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bulembo, ajiandae Mheshimiwa Nditiye kwa dakika tano.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi wanazozifanya, kazi ni kubwa, Wizara ni kubwa na ina mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu umenipa dakika tano nitaongelea maeneo mawili.

Suala la kwanza nitaongelea eneo la wawindaji na kwenye eneo la uwindaji kwenye vitalu miaka minne iliyopita tulikuwa tunaweza kukusanya kama dola milioni 20, jana wakati tunaangalia tuko kwenye dola 4,000,000 hapa kuna tatizo. Suala langu naliomba Wizara ya Mheshimiwa Profesa Maghembe hebu kaa na watendaji wako wakuambie ukweli, maana yake wewe ni Waziri, wao ndiyo wanatenda, bahati mbaya hawa watendaji siku zote huwa wapo tu, mambo yakichachamaa ninyi wakubwa ndiyo mnaangaliwa, hebu ingia mwenyewe ndani huku ujue tatizo liko wapi ili uweze kupata ufumbuzi angalau vitalu hivi visiwe tena kama mapambo. Vitalu vipo vinatakiwa vilipiwe viingize hela kwenye nchi, watu wakiingia leo, kesho wanarudisha wanaondoka lazima kuna tatizo hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi tatizo ni ninyi Mawaziri au Katibu Mkuu, lakini kuna watendaji wa chini wanaoshughulika na eneo hili wakae na ninyi chini wawape maelezo ya kutosha ili Bunge lijalo angalau tuweze kuwa na kitu kizuri cha kuongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu yangu ya pili ni utalii. Utalii katika nchi yetu ni shida, tunapata watalii milioni 1.2 nchi kama Tanzania yenye vivutio kila eneo, kwa nini Wizara hii haiwezi kuwekeza moja kwa moja kwenye Balozi zetu zilizoko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda nje ukaangalia Balozi za Kenya utakuta kuna dawati la utalii na kwa sababu hawa wana ndege wanatafuta watalii unalipia risiti hata miezi sita, watu wanajaa kwenda kule. Kwa nini sisi kwenye eneo la utalii tunaweka pesa kidogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu cha Waziri bajeti kwenye utalii tumeweka bilioni mbili, wenzetu wa Kenya wameweka bilioni nane kwa nini? Ukienda pale *TANAPA*, Ngorongoro yale maeneo ni kwa ajili ya watalii.

Kama tunaweza kukusanya bilioni 200, tunashindwaje kutoa hata asilimia kumi ya makusanyo yetu kwa ajili ya utalii? Kwa ajili ya matangazo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo Balozi nyingi, kwa nini Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje isione suala la utalii ni eneo lake? Kila Balozi ikapewa amri na masharti kwamba utaitangaza Serengeti, utatangaza Ruaha, utatangaza Ngorongoro, tukienda kwenye Balozi zetu watu hawana habari. Mwingine amepelekwa kwenye Ubalozi kama mchumi, lakini hawezi kuongelea utalii anaona siyo eneo lake, lakini ni Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini Wizara hii, Mheshimiwa Waziri, usiombe kwa wenzenu kwenye *Cabinet,* kama makusanyo ya *TANAPA* ni shilingi bilioni 200 chukua asilimia 10, kama Ngorongoro 150 chukua asilimia 10, yale maeneo yote. Tukipata *50 billion shillings* kwa ajili ya kwenda kutangaza watu watajaa, maana mtaji wetu ni watalii. Utakuta kwenye utalii tunaweka gharama nyingi, mambo mengi. Je, huyu ng'ombe anakamuliwaje kama hawezi kupewa chakula? Chakula nenda China kuna watu wangapi? Nani anatangaza utalii? Nenda Urusi, nenda Amerika, lakini Balozi zetu ajenda hii siyo yao! Wizarani watu wa utalii au *TANAPA* au Ngorongoro ukiwauliza nini wanafanya, hata matangazo, tukipita njiani pale tunaona Tigo, tunaona Vodacom, tunaona nani, ninyi mnatangaza wapi, utalii wa ndani? Vipindi mnatoa wapi? Watu hawajui! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Serikali iwape hela mkafanye matangazo. Kuna *CNN,* kuna *BBC,* kuna maeneo mengi hujawahi kuiona Serengeti. Mheshimiwa Hasunga amesema pale, mnaitangaza timu ya Serengeti, hata kuwapa jezi ambazo zimechorwa maana ya Serengeti ni nini, hamuwezi! Sasa huko mnakotangaza ni wapi au Mawaziri muingine ndani muangalie hizi hela zinazotangazwa zinatangaza kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu ya Taifa ya Wanawake

imekwenda Uganda pale, hata ku-*brand* tu kuiweka Serengeti ile gari peke yake moja, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatuwezi kuwekeza kwenye utalii tutalaumiana kila siku kwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nditiye, ajiandae Mheshimiwa Suzan Mgonokulima.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya bosi wangu.*(Makofi)*

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii adhimu kabisa. Mimi nitaongelea masuala matatu, suala la kwanza nitaanza na suala la Hifadhi yetu ya Taifa ya Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba tunawashukuru sana wananchi ambao wanaishi maeneo ya Ngorongoro kwa kutulindia Hifadhi yetu ya Ngorongoro ambayo ni alama ya Kimataifa, kwa maana ya urithi wa Kimataifa. Ni wazi kwamba sasa Sheria Namba 284 iliyoanzisha Ngorongoro imepitwa na wakati. Sheria ile wakati inaanzishwa mwaka 1959 ilihusu kuwahudumia wakazi 8,000 waliokuwa wanaishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, lakini kwa sasa hivi tunavyozungumza watu wanaoishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro wamezidi 87,000. Ni wazi kwamba *Ngorongoro Conservation Area* hawawezi tena kuwahudumia wananchi wanaoishi mle na matokeo yake tunashuhudia migogoro ya kila siku kati ya wananchi wanaoishi eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba sana Serikali, Mheshimiwa Waziri ulete Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro tuihuishe, ili iende na wakati. Ngorongoro hawana uwezo tena wa kuwanunulia chakula wananchi wanaoishi mle, hawana uwezo tena wa kuendelea kuwahudumia huduma

za afya, zaidi ni migogoro ya kila siku tunayoishuhudia na kuiona kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Ngorongoro licha ya kwamba inahudumiwa kwa maana ya wananchi kwa sheria iliyopo, lakini kuna Baraza la Wafugaji. Juzi wakati tunatembelea Ngorongoro na Loliondo, Baraza lilikuja na ajenda kwamba, hela wanayopewa haitoshi. Kusema ule ukweli Wajumbe wa Kamati wengi walishangaa kwamba kuna Baraza tu la Wafugaji ambalo linapewa *2.7 billion shillings* kuhudumia wananchi wa Ngorongoro ambao ni Wilaya inayojitegemea ambayo Serikali inapeleka pesa kwa ajili ya kuwahudumia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndiyo umuhimu wa kuitaka Wizara ilete Sheria ya Ngorongoro tuiangalie upya, tuifanyie marekebisho kwa kuwa mmeshindwa kuwahudumia wananchi wanaoishi mle ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la hifadhi zetu, *TANAPA.* Kwa upande wangu naona kwamba, kazi zinazofanywa na *TANAPA* na kazi zinazofanywa na Ngorongoro, ukiondoa lile suala la uhifadhi mseto, zinafanana. Vilevile kuna ile Mamlaka ya Wanyamapori *(TAWA).* Kazi zinazofanywa na *TAWA, TANAPA* na Ngorongoro zote zinafanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara iangalie namna ya kuzijumlisha hizi taasisi zote tatu kiwe kitu kimoja kikubwa kiweze kuwa *manageable* kirahisi kuliko migogoro ambayo tunaishuhudia kila siku katika taasisi hizo. Wakati fulani nimewahi kwenda kule Pori la Moyowosi, katika hali ya kawaida wale watu walikuwa hawajui majukumu yao na majukumu ya *TANAPA* ni yapi na majukumu ya *TFS* ni yapi. Ukimuuliza suala hili huyu, anakwambia hili ni suala la *TFS,* ukimuuliza huyu anakwambia hili la *TAWA,* ukiwauliza hawa wanasema kama *TANAPA* wangekuwepo hapa, hili lingekuwa limepatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu ni kwamba

Mheshimiwa Waziri, angalia namna ya kuunganisha hizi taasisi tatu ambazo zote zinafanya kazi ya aina moja kwa lengo moja, ziwe kitu kimoja ambacho kitakuwa na bodi moja na tutakuwa tumemsaidia Rais katika kupunguza hata baadhi ya matumizi yasiyokuwa ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nitaongelea kidogo hii migogoro ya mifugo na hifadhi zetu. Hakuna asiyekubaliana kati ya Wabunge kwamba, umuhimu wa kuhifadhi hifadhi zetu ni mkubwa sana. Kila Mbunge ninaamini anakubaliana kwamba lazima hifadhi zetu zihifadhiwe, tumezikuta kutoka kwa babu zetu ni vizuri tukubaliane kwamba tunaziacha kwa wajukuu zetu wazione na waziendeleze, nina mashaka na *seriousness* ya Wizara. Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Suzan Mgonokulima, ajiandane Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, hampo? Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya. Huwasiliani na Kiti kama uko mpirani hapa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hotuba iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara kufanya kazi kubwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wake, kwa sababu ya muda nijielekeze tu kwenye eneo la Wilaya ya Kaliua na changamoto zinazotokana na hifadhi kwa sababu Kaliua imezungukwa na hifadhi maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napata mashaka, naendelezea alipomalizia Mwenyekiti wa Kamati yetu. Napata mashaka kama Serikali ina dhamira ya dhati kuondoa migogoro ya wananchi ndani ya Tanzania, napata mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata mashaka kwa sababu huu ni mwaka wangu wa 12 kuwepo ndani ya Bunge hili, tumeunda Kamati nyingi sana na Kamati ya mwisho ambayo nilijua itaondoa migogoro ya wafugaji na wakulima; ya hifadhi na wananchi ni Tume Teule ya Bunge ambayo mimi nilikuwa Mjumbe wake, ilikuwa ina Maazimio tisa muhimu sana, nilijua kuanzia pale tunaondoa kabisa migogoro ya wananchi Tanzania. Bahati mbaya hakuna kinachofanywa, ukiangalia yale Maazimio tisa ya Tume Teule ya Bunge hakuna hata moja ambalo limefanyiwa kazi mpaka sasa hivi.

Leo tumeunda tena Kamati nyingine. Tume ambayo inahusisha Wizara nne na wataalam, jambo la kusikitisha wakati Wabunge tunasubiri tupate majibu namna gani ya kuondoa migogoro hii, tupate ushauri wa ile Kamati, huku wananchi wetu wanateswa, wanapigwa, wananyanyaswa, wananyang'anywa mifugo yao. Nataka Mheshimiwa Waziri atwambie leo, kulikuwa na umuhimu gani wa kutengeneza ile Kamati ambayo ilitumia fedha za walipa kodi wakati majibu hatutajapata ya uhakika? Naomba nipewe majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili; Serikali hii ndiyo imesajili vijiji ndani ya hifadhi, Wilaya ya Kaliuwa ina vijiji 21 ndani ya hifadhi. Wamekwenda kwenye vile vijiji watu wa maliasili wamekwenda kunyang'anya *certificate* za usajili wa vijiji. Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie vile vyeti vya vijiji walivyong'anywa, watu wake wamekuja kuchukua ndani ya vijiji vyetu, viko wapi? Kwa nini hawarudishiwi? Kwa sababu Serikali ni moja, *unless* niambiwe leo kwamba ndani ya Tanzania kuna Serikali mbili. Serikali inayosajili vijiji na inayokuja kunyang'anya *certificate! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo Mheshimiwa Waziri unipe majibu vile vyeti virudi kwenye vijiji, vimesajiliwa viko kwenye *GN* ya Serikali na vitongoji vyake. Naomba vyeti vyao virudi, msijidanganye kuwanyang'anya ili muendelee kuwaadhibu, hatukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza hapa Bungeni wiki iliyopita, bahati mbaya sana hata Mheshimiwa Waziri nimezungumza naye siyo mara moja siyo mara mbili, jamani mimi kwanza ni Mhifadhi *by professional,* lakini uhifadhi wa kutesa watu, kuumiza watoto, kulala kwenye mvua, kuchomewa vyakula, kuchomewa nyumba, hii siyo Tanzania tunayoiamini Tanzania ya amani, siyo kabisa. Wale siyo wakimbizi, kwa nini wakimbizi ndani ya Taifa hili wanaishi vizuri? Kama mlikosea Serikali ikaenda likizo, wakakaa ndani ya hifadhi mkawasajili, watoeni kwa utaratibu, kwa nini mnawatesa watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nimeongea na wewe mara nyingi suala hili, bahati mbaya sana huchukui hatua zinazotakiwa. Leo Mkuu wa Wilaya anakuwa na *power* ya kuruhusu watu wakanyanyaswe, nimeongea na wewe hufanyi kazi. Hujafuatilia suala hili hata kidogo! Naongea na watu wa Kanda wanasema hatujui, ukiongea na mtu wa Kaliua anasema hatujui, naongea na Waziri anasema napiga simu kule. Mheshimiwa Waziri wale watu mtuambie mliowasajili ndani ya hifadhi kule Kaliua ni Watanzania au? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtuambie leo, nataka majibu hapa leo, Mheshimiwa Waziri tutagawana mshahara wako leo hapa, hatuwezi kukubali watu waendelee kuteseka kila siku. Bahati mbaya sana ukiuangalia mjadala wa maliasili kila mwaka, *almost* nusu unajadili migogoro. Nafikiri mngejidhatiti mkaiondoa migogoro wakati wa bajeti tukawa tunajadili namna gani ya kukusaidia Mheshimiwa Waziri kuendeleza utalii, kuendeleza uhifadhi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kalanga, ujiandae Mheshimiwa Hawa.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru kwa kunipa nafasi, naomba Waziri atakapokuja kuhitimisha hapa aniambie ni lini wananchi wa Lokisale, Mswakini na Lemoti, ambao mazao yao yaliharibiwa na tembo takribani kwa mfululizo miaka kumi sasa mpaka siku ya leo Serikali haijawalipa, ni lini Serikali watalipwa fidia zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kuwa wahifadhi wazuri na ndiyo maana sisi hatuli nyamapori, lakini kama wanyama wenyewe wanakuja kula mazao yetu na Serikali haioneshi kujali tutapata ukakasi katika kuwalinda wanyama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimesikia mtu mmoja akichangia akisema watu wa Ngorongoro wametoka 8,000 wamekuwa 90,000. Kabla hatujahoji idadi ya Watanzania walioko Ngorongoro ambao ni haki yao na wala siyo hisani kwa sababu ni Watanzania wenzetu, ni muhimu pia tuhoji miaka hiyo na leo wanyama walioko Ngorongoro ni wangapi na wameongezeka kwa kiasi gani na ni lini jamii yetu imehusika? Tuambiwe hata Mmasai mmoja aliyehusika kufanya ujangili katika Hifadhi ya Ngorongoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hamuwezi kutuhukumu kwa kuwaangalia majangili ambao ninyi mnawafahamu na Serikali imeshindwa kuwashughulikia. Tunataka mtuambie ni lini jamii hiyo imehusika katika kufanya ujangili kwa wale wanyama, kama kweli hoja yenu ni ya ujangili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nashukuru kwamba leo watu wa Kaliua wameguswa, kwa sababu mara zote tunasema wananchi wa Ngorongoro wanaokaa kule wana haki kwa sababu ni ardhi ya vijiji. Leo wananchi wa Kaliua nao wameguswa, nashukuru sana Mheshimiwa Mbunge mwenzangu nae anakubaliana kwamba vijiji vilivyosajiliwa wapate haki kwa sababu vimesajiliwa na viko

kihalali. Ni vizuri kwa sababu wameguswa, tutaendelea kuwa wengi tunaotetea maslahi ya Watanzania wenzetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niihoji Wizara, hivi lengo la Wizara ni uhifadhi peke yake au lengo la Wizara ni kuhakikisha kwamba uhifadhi na maisha ya Watanzania yanaendelea kuongezeka? Maana leo ardhi haiongezeki, lakini hatuwezi pia, kubadilisha nchi hii ikawa ni nchi ya uhifadhi peke yake. Haiwezekani tukawa na uhifadhi bila watu, hata haya mapato tunayopata kutokana na wanyama, kama hakuna Watanzania watakaohudumiwa na fedha hizo, hakuna sababu ya kuwa na uhifadhi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani ili jambo hili liende vizuri ni lazima tujue kwamba, katika maeneo ya uhifadhi kuna watu pia na kuna wanyama. Tujenge mazingira mazuri ya kupanga matumizi bora ya ardhi ili wote tuweze kunufaika na ardhi hiyo. Tatizo hapa ambalo ninaliona Wizara haipo tayari kushirikiana na wananchi kutatua migogoro iliyoko katika maeneo ya uhifadhi. Inaonekana Wizara inatumia nguvu kubwa, inatumia Jeshi, inatumia Polisi, katika kuumiza na kuua wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali leo ituambie, hivi ni Serikali imebariki maumivu na mateso ya wananchi katika maeneo ya uhifadhi? Kama Serikali haikubaliani na uonevu na maumivu wanayopata wananchi wetu, hao askari wanaotesa watu na kuua watu, wanapata wapi mamlaka ya kufanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali haikemei, na mimi nadiriki kusema kama Serikali haikemei uonevu na mauaji yanayofanyika kwa raia, maana yake Serikali imebariki uonevu na mauaji ya raia walioko katika maeneo ya hifadhi. Haiwezekani watu wauawe tu halafu Wizara imekaa kimya, Serikali imekaa kimya! Wabunge tunapiga kelele hapa, halafu tuseme Serikali haijabariki! Mimi naamini kama Serikali haitoi kauli maana yake Serikali imeagiza polisi na Askari wa Wanyamapori waue raia katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie katika suala la uporaji wa mifugo katika maeneo ya uhifadhi. Kama walivyosema Wabunge wenzangu, hivi nani anayeharibu misitu kati ya ng'ombe na wakata mikaa? Hivi nani anayeharibu misitu kati ya wafugaji wanaofuga ng'ombe tu na wale wanaochoma mikaa na mikaa mmetoa kibali inauzwa kila mahali kwenye nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Serikali i-*admit* leo, kama Serikali ina chuki na uadui na wafugaji, tujue kwamba Serikali haitaki ng'ombe kwenye nchi hii. Jana tulikuwa tunajadili bajeti ya Wizara ya Mifugo, tunaambiwa thamani ya bidhaa inayotokana na mifugo ni zaidi ya trilioni 17 ya nchi hii, leo tunadiriki kuona kwamba wafugaji hawana haki katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai uhifadhi, lakini uhifadhi leo hii umefika hapa kwa sababu ya ukarimu wa wafugaji katika nchi hii. Kama ingekuwa ni watu wengine wameishi katika hifadhi wale wanyama wasingekuwepo leo, wafugaji tumekuwa tukiishi na wanyama bila madhara yoyote. Kwa nini leo ninyi, kwa sababu, mna nguvu, mna dola, mna jeshi, mna polisi, mnaona hatuna haki kuishi katika maeneo hayo ambayo ninyi mlitukuta katika maeneo hayo? Mimi naomba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa, ni dakika tano. Waheshimiwa Wabunge nimemtaja Mheshimiwa Hawa na Kalanga, dakika tano, kaa chini Mheshimiwa Kalanga. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, dakika tano.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Na mimi ningependa kuchangia katika Wizara hii na ninaomba nitoe masikitiko yangu makubwa sana kwa Wizara ya Maliasili kutokana na mambo yanayoendelea katika Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongea na Mheshimiwa Waziri Maghembe kuhusu matatizo ambayo yamewapata wananchi wa Sikonge kutokana na Maafisa wa Idara ya Misitu na Wanyamapori walioko katika Wilaya ile. Watu hawa wanachukua ng'ombe wao, wanasukumiziwa hifadhini, wanasema kwamba, ng'ombe hawa wamefika hifadhini, wanachukua ng'ombe wanatozwa faini ya shilingi milioni mbili mpaka milioni tano kwa ng'ombe mmoja, kuna mwanakijiji mmoja ambaye ametozwa faini ya shilingi milioni 22 kwa ng'ombe wake 22 kuingia katika hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa nilimueleza Mheshimiwa Waziri nikiwa hapo na hao wananchi na aliniambia niandike, nilimuandikia, mpaka sasa ninavyozungumza Mheshimiwa Waziri hakuna suala lolote ulilolifanya. Askari hao wamefikia hatua mbaya ya kuwafanyia vibaya wananchi hawa, wanawavua nguo, wanawatandika bakora na wanawalazimisha kufanya mapenzi na miti. Mheshimiwa Waziri nilikueleza na *messsage* niliyokuandikia ninayo. Haya mambo hatuelewi hii nchi ni Tanzania ama hii ni nchi gani? Hawa wafugaji ni Watanzania ama hawa wafugaji ni wafugaji wanatoka nchi gani? Tunaomba sana Waziri anapokuja ku-*wind up* atuambie hawa wafugaji wanatakiwa waende wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kwamba nina dakika tano, naomba nimuambie Mheshimiwa Waziri, suala linaloendelea sasa hivi Kaliua, kesho kutwa wanaelekea Ulyankulu. Jambo la ajabu ni kwamba wananchi hawa walipewa hati na *GN* Serikali ikatangaza, matokeo yake wananchi hawa wamenyang'anywa hati zao na wanaambiwa waondoke katika maeneo ya hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa vijiji saba hawa hawaelewi kwamba watakwenda wapi, wameshakaa pale zaidi ya miaka 30 wanaambiwa waondoke, hawaelewi wataondoka waende wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niweze kumsaidia Mheshimiwa Waziri, vijiji saba hivyo ni Kijiji cha Seleli,

Mwendakulima, Sasu, Kashishi, Nyasa, Iyombo na Ilega. Hawa wananchi mpaka sasa hawaelewi hatima yao, pamoja na Mkurugenzi kuwahakikishia usalama wao kwamba mpaka ripoti ya Waziri Mkuu itakapotoka ndiyo watajua kitu cha kuambiwa, lakini cha ajabu Wizara ya Maliasili inachukua hatua kabla hata hiyo ripoti ya Waziri Mkuu haijasema nini kinachofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini ripoti ya Waziri Mkuu ndiyo ingekuja kutueleza kwamba, nini kifanyike, hawa watu waende wapi na ndipo wale watu wangeanza kuondolewa. Lakini leo watu wanaondolewa, wameishi zaidi ya miaka 30, wanaambiwa ni eneo la hifadhi, hawaambiwi hawa watu wanakwenda wapi? Hatuelewi huko watu wanaenda wapi, tunawatia watu hasira zisizo hata na sababu, ajabu ni kwamba Mkuu wa Wilaya ya Kaliua anasema maagizo haya amepewa na Mheshimiwa Rais, huyu Mheshimiwa Rais anayejinasibu kwa kutetea wanyonge yuko wapi aende akawatetee wanyonge wale?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mama mjamzito amejifungua ana mtoto wa siku tatu analala nje na mtoto wake, lakini cha ajabu wanatoka wanakwenda kuchoma mpaka vyakula ambavyo wale watu wamejiwekea, wanavunja nyumba wanakata mabati, wanakata miti, sasa mnawatoa watu, kama mnataka waende wakajenge kwingine haya mabati mnayakata kwa nini? Vyakula vyao mnachoma kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aje atuambie kama ni maelekezo yeye ametoa na Wizara yake ama Mheshimiwa Rais ametoa haya maelekezo. Chonde chonde, wananchi wa Wilaya ya Kaliua wanateseka na njaa, wanalala nje bila msaada wowote na bado wanapigwa, wanawake wanabakwa na watoto hawaelewi watakwenda wapi. Haya ni mambo ya... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mtuka, ajiandae Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** nakushukuru kwa nafasi hii ya dakika tano, nitajitahidi kwenda kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sipingi kabisa kwamba ni lazima tuhifadhi misitu; huo ni utangulizi wangu, lakini haya yafuatayo naomba niyaseme kwa masikitiko. Tunayo migogoro ya mipaka baina ya hifadhi pamoja na wananchi kule Manyoni Mashariki. Nakumbuka tarehe 27 Mei, 2016 walikuja wawakilishi 18 walikutana na Mawaziri; Naibu Waziri Maliasili na Utalii na Naibu wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi na walitoa malalamiko yao kuna tatizo la kusongeza mipaka. Kuna hifadhi inaitwa *Muhesi Game Reserve* hii ni hifadhi mpya, ilianzishwa mwaka 1991.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hapo wananchi hawa walikuwa wanaishi kwenye vitongoji salama lakini baada ya kuanzishwa hii Muhesi ambayo ilianzishwa na *GN* Namba 531 tarehe 4 Novemba, 1991 ndipo ikawahamisha wananchi karibu vingoji vinane.Vitongoji hivyo ni Chisola, Msisi, Itovelo, Machochoroni, Mkindiria, Chigugu, Ngongolelo pamoja na Chibwee. Haya maeneo yalikuwa ni *potential* kwa ajili ya kilimo; kwa mfano kulikuwa na eneo linaitwa Chiumbo ni eneo ambalo ni *productive* kwa kilimo cha mahindi, lakini pia kuna eneo linaitwa Iluma, eneo hili likuwa ni machimbo ya madini likiwa linatoa dhahabu ambayo haijawahi kushuhudiwa katika nchi hii, *alluvial*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia taarifa za Benki Kuu za mwaka 1991 zinaeleza kwamba dhahabu inayotoka kwenye eneo hili hakuna katika nchi hii katika machimbo yote ambayo tumewahi kuyashuhudia, inaitwa *alluvial.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya kutangazwa eneo hili pia likachukuliwa, ambapo ilikuwa ni kitegauchumi kizuri sana kwa wananchi wa Manyoni. Vilevile kwenye mito hii ya Muhesi na Kizigo ilikuwa ni *source* ya maji kwa ajili ya

mifugo pamoja na wananchi. Baada ya hapo hatuna maji tena wala mifugo haiwezi kunywa maji pale. Pia tulikuwa tunafuga nyuki kwenye msitu ule wa Muhesi, sasa hivi hatufugi tena nyuki. Sasa ombi letu lilikuwa ni nini; ombi letu ni kwamba irudishwe ile mipaka ya zamani kwa sababu idadi ya watu imeongezeka, idadi ya mifugo imeongezeka pamoja na shughuli za kiuchumi zimeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Wizara ya Ardhi tulijadili sana mpango wa matumizi bora ya ardhi. Tunashindwa nini kugawa maeneo haya kwa kushirikisha wananchi kwamba wakulima kaeni huku na wafugaji kaeni huku, kitu gani kinashindikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi ilipewa jukumu hilo, lakini nadhani sijui ndiyo ile Tume imeundwa lakini Manyoni kule hawajafika. Cha kusikitisha zaidi hawa wananchi walipozungumza na Waheshimiwa Mawaziri wetu hawajawahi kutoa taarifa juu ya maombi haya mpaka hivi ninavyozungumza, ili niwapelekee wananchi wa Manyoni. Hawajawahi kuniita hata mimi Mbunge wao kueleza hata kwamba tumejadili kitu gani hebu wapelekewe majibu haya wananchi wa Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie jambo la Utalii. Tuna kivutio kipya kinaitwa Kisingisa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlinga

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba nitoe pole kwa Wana-Ulanga wakatoliki kwa msiba wa *Father* Mdai ambaye amefariki Ijumaa. Suala langu la pili, naomba nitoe pole kwa wananchi hawa wa Ulanga kwa barabara mbovu zilizotukuka lakini

naomba niwahakikishie kuwa Mbunge wao nipo na nitapambana mpaka kieleweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*declare interest,* mimi nitakuwa upande wa binadamu maana maliasili wao wamejisahau kama siyo Watanzania na kama si binadamu, wanawachukia binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu la Ulanga kuna tatizo kubwa la wanyama waharibifu hasa aina ya boko katika kata za Ketaketa, Ilonga, Mwaya, Iyuga na Chilombola. Boko hawa wamekuwa wakiharibu kwa kiasi kikubwa mazao ya wananchi mazao ya wananchi na kupelekea njaa, lakini wananchi wanapowagusa wale boko Maafisa Wanyamapori wanawakamata wanawafungulia mashtaka wanawapa kesi za kuhujumu uchumi. Wanyama wanapovamia tukiwaambia Maafisa Maliasili hawa–*responds* katika muda ambao unatakiwa. Tumeomba watuongezee ma–*game* kwa ajili ya kupiga hawa wanyama hawataki, tukitaka tuwavune hawa boko ili wananchi nao wapate kitoweo hawataki.

Sasa mimi naomba niiombe Wizara ya Maliasili mimi kama Mbunge nita–*recruit* ma–*game* wa kienyeji katika kila kata kama wao hawatafanya; katika kila kata ambao kazi yao kubwa itakuwa kufukuza hao boko ambao wanaharibu mazao ya wananchi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika Jimbo la Ulanga mazingira yake eneo kubwa ni milima na maeneo machache yaliyoko tambarare yote ni maeneo ya maliasili. Upande mmoja lipo eneo tepe tepe wanaliita eneo oevu ambalo kwa kiingereza analiita *buffer zone,* upande mwingine liko Ilumo na upande mwingine iko *Selous Game Reserve.*

Kwa hiyo, sasa mshangao wangu mkubwa wakati Wizara inafanya utafiti mwanzo inaweka hiyo mipaka walisahau kama wananchi wanazaliana. Kwa hiyo sasa hivi wananchi ni wengi na eneo ni dogo na hivyo wananchi wanakosa eneo la kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaposogea katika maeneo ya hifadhi kidogo watu wa maliasili wanakuwa wakali. Waziri Mkuu aliyepita Mheshimiwa Mizengo Pinda alipendekeza na aliunda Tume ifanye mchakato ili kuwaongezea wananchi maeneo ya kulima, lakini mpaka leo hakuna majibu. Mwaka jana baada ya mimi kuwakomalia Wizara wakaja wakatuchukua Wabunge wakatuzungusha na ndege kipindi cha kiangazi, wakasema mnaona wananchi wanavyoharibu maeneo? Mimi nikawakatalia niawaambia kwa nini mnatuzungusha kipindi cha kiangazi? Kwa nini msituzungushe kipindi cha masika. Kwa hiyo, sasa naomba Wizara kupitia hiyo tume yake itoe majibu haraka ili wananchi wapate maeneo ya kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nilikuta suala la *Operation Tokomeza.* Nimeenda nimekuta wananchi wana majonzi makubwa, wananchi wengi wa Ulanga wamekamatwa na mpaka sasa hivi wako ndani na hawajafunguliwa mashitaka yoyote. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara kupitia ofisi ya *DPP* waharakishe ili watu wenye hatia wahukumiwe na watu ambao hawana hatia waachiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo mambo yangu yalikuwa ni machache, hayo yanatosha.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mlinga.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu utalii katika Jimbo la Rungwe. Tuna utalii katika Wilaya ya Rungwe ambao Serikali haijaweka mkazo katika uendeshaji wake na kuisaidia Serikali kuongeza mapato. Vivutio hivyo ni Daraja la Mungu na *Lake Ngozi,* vivutio hivi havina miundombinu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutangaza utalii nje ya nchi. Serikali iongeze pesa katika Wizara hii ili tuweze kujitangaza na kupata wageni wengi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Kitulo haitatunzwa na Serikali kwa kupeleka pesa kidogo hivyo nashauri pesa zitengwe za kutosha kuweza kuitunza hifadhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu yetu, tunaomba Serikali itoe vibali kwa wazawa ili kuweza kuuza nje ya nchi miti na mazao yake na hivyo kuweza kuongeza kipato cha mwananchi mmoja mmoja na hatimaye wa Taifa.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla katika utekelezaji wa kazi za kuendeleza utalii hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni/ushauri; Wizara iendelee na kazi ya kuibua vyanzo vipya vya utalii na kuvitangaza duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Tanzania Forest Fund (TFF),* Kamati iliyoundwa kuangalia jinsi ya kutoa fedha za utafiti wa kuendeleza misitu Tanzania, uhifadhi wa misitu na viumbe wadogo wadogo kuna malalamiko kwamba wanaopewa fedha hizo baadhi yao hawakidhi vigezo na baadhi hawajishughulishi na shughuli hizo kabisa. Nashauri ufuatiliaji wa karibu juu ya fedha hizo za Serikali zilizotolewa kama zimetumika zilivyokusudiwa. Kabla ya kutolewa fedha hizo ukaguzi ufanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nawatakia utekelezaji mwema wa majukumu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwalipe wananchi fidia ambao mazao yao yaliharibiwa na tembo katika maeneo ya Mswakini, Makuyuni, Lokisala, Lemooti na Monduli Juu. Pia ni lini Serikali italipa fedha za *WMA* zinazodaiwa na *WMA* ya Randilen? Ni muhimu Wizara hii ikarejesha fedha hizo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Monduli imezungukwa na Mbuga za Ngorongoro na Tarangire tunaomba Wizara ione namna ya kutupatia gari la doria ili kunusuru mazao na maisha ya watu wetu.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na watendaji wote wanaohusika katika Wizara hii na sekta zote husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri/Naibu Waziri watakapokuja kutoa ufafanuzi, wanijulishe:-

(i) Wananchi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro wanafaidikaje na mlima huo?

(ii) Ni lini elimu ya utunzaji wa mazingira itatolewa kwa wananchi hao, hususani wanawake na vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tembo wanaogopa sana nyuki, je, Serikali iko tayari kuwagawia mizinga ya nyuki wananchi wanaoishi maeneo yanayovamiwa na tembo ili kuwazuia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza zijengwe hosteli za bei nafuu kwenye mbuga za wanyama ili wananchi wa kawaida na wanafunzi wapate fursa ya kutembelea vivutio hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono asilimia mia moja.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika hotuba ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uaminifu wa kibiashara; kutokana na kukiuka miiko ya kibiashara kwa kupandisha au kubadili kodi bila utaratibu wa kibiashara

Tanzania sasa haiaminiki kwa mawakala wa kimataifa ambao ndio wauzaji wakubwa. Imefikia wakati sasa ma-*agents* wa kimataifa wanauza nchi zilizo nafuu kwa bei na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Tanzania imeongeza idadi ya kodi na tozo hadi kufikia 36 kutoka 14 – 16 zilizokuwepo awali. Bado kuna malipo ya *TALA* ya kila mwaka kutokana na mahali kampuni inapofanyia kazi zake za kitalii au kutoa huduma za kitalii kama ni kupandisha watalii milimani au kuwapeleka mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mahoteli, kuanzia Novemba, 2016 mahoteli mengi wageni wamepungua ukilinganisha na kipindi kabla ya *VAT* haijaingizwa. Kwa kweli idadi ya wageni imeshuka sana kwa sababu zilizo nje ya uwezo wetu, hatuwezi kupata takwimu sahihi. Biashara ya utalii ni *delicate* sana na utachukua muda mrefu sana kurejesha imani ya mawakala na watalii wa dunia kwa ujumla kuiamini Tanzania katika sekta ya utalii. Athari ya maamuzi haya yataonekana kuwa makali zaidi katika kipindi cha mwaka 2018/2019/2020. Makampuni mengi hayana *bookings* za kuridhisha kwa miaka ya mbele kama ilivyo desturi ma-*agents* wengi wamebadili mwelekeo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni/ushauri; Bunge liunde tume huru kupitia wadau pamoja na watalii wanaoingia na kutoka juu ya maoni yao kwa kivutio Tanzania. Ofisi za Kibalozi nje zitumike pia kupata taarifa za umaarufu wa kivutio Tanzania. Serikali kupitia Wizara husika zote zikae chini na kuangalia hali ya ushindani iliyopo duniani, Afrika, Afrika Mashariki na nafasi yetu katika ushindani huu kwa miaka kumi ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi zinazokusanywa sasa si za biashara mpya bali ni biashra ya nyuma. Tujiulize kuanzia mwaka 2018 na kuendelea tutakusanya nini? Makampuni mengi ya Kitanzania yatakosa uwezo wa kushindana na makampuni yenye mitaji mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isipuuze taarifa za makampuni mengi ya kigeni za kufunga biashara zao na kwenda nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye hotuba hii muhimu. Ninamshukuru Mungu kwa fursa ya kuwa katika Bunge hili Tukufu. Ninawapongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Jumanne Maghembe na Naibu Waziri wake *Engineer* Ramo Makani na watendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchangia kwenye maeneo machache nikianza na hati za kumiliki misitu. Ninaomba kwa Wilaya na Mikoa yenye misitu mingi ya asili na ya kibiashara watu wakatiwe vitalu vya misitu kama watu wanavyopata hati za ardhi ili wawekeze kwenye upandaji miti na watumie hati hizo za vitalu vya miti kukopa kwa ajili ya kuendeleza misitu, ufugaji nyuki na viwanda vidogo vya mbao na samani za ujenzi na za taasisi na za majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali kuzidisha juhudi na mikakati ya kulinda *antiques* za nchi hii hususani za kitamaduni zilizopo vijijini ambazo huondolewa kwa sababu ya umaskini na kutokuwa na uelewa. Wanachi wengi wamekuwa wakirubuniwa na wageni wanosaidiwa na wajanja wachache kuwashawishi kuuza *antiques* hizo za kihistoria za makabila na jamii mbalimbali. Kwa mfano kulinda *antiques* za fimbo, vigoda, mavazi ya machifu na viongozi mbalimbali wa kimila, samani, vyombo vilivyotumika kulima, kusaga nafaka, kuhifadhi chakula, kuwinda na uhunzi. Mavazi ya sherehe mbalimbali vyote vinapotea na kupoteza historia muhimu ya Taifa letu na jamii mbalimbali. Serikali ilitupie macho na kuweka mikakati ya kuzilinda na kuzihifadhi na kuziwekea kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji wa miti kwa matumizi ya mkaa umeongezeka sana hasa maeneo yenye

ukame ambako misitu ni michache, na wakati huo huo matumizi ya gesi na umeme pamoja na majiko sanifu vimeongezeka. Ninaitaka Serikali kutoa takwimu za gharama ya kukata miti kwa kila gunia la mkaa na uharibifu wa mazingira. Tulinganishe uharibifu huu na gharama ya mbadala kama matumizi ya gesi, majiko sanifu na umeme tutaona jinsi gani matumizi mbadala ya nishati ni nafuu huko tunakoelekea. Gharama ya gesi ukishanunua mtungi ni rahisi kuliko mkaa. Kwa wastani mkaa unauzwa kwa familia ya kawaida ni gunia nne kwa mwezi 70,000 x 4 = 280,000/=; lakini gesi kwa mwezi ni mitungi miwili ya shilingi 90,000/= ukiongeza gharama ya mtungi 100,000 ni 190,000/=; ni dhahiri gesi ni nafuu. Kuhusu mkaa tutoe ulinganisho mkaa na gesi na tuwaelimishe wananchi gesi ni bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali itafute njia ya kutoa elimu kwa mapana yake ili matumizi ya mkaa yaachwe kidogo kidogo. Serikali ianze kuwatoza wote wanaokata miti kwa mkaa wa kuuzwa ili walipie gharama ya kupanda miti hii, tusilionee haya hili, tutajuta baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kutoa ushauri kwa Serikali juu ya utalii wa fukwe. Utalii huu ni mojawapo ya eneo linalovutia sana watalii nchini na kwa hali hiyo kuna haja ya kuwekeza kwa kiwango kikubwa kwenye vivutio vya utalii wa fukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kubwa ya upungufu wa mahoteli ya kutosha kwa ajili ya watalii wanotaka kuja Tanzania. Nataka kupendekeza kuwa Serikali iboreshe mazingira ya uwekezaji kwenye ujenzi wa hoteli nyingi kwenye fukwe zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe msamaha wa ushuru wa vifaa vyote vya ujenzi wakati wa ujenzi wa hoteli hizi ili kwa miaka miwii au mitatu wawekezaji wajenge hoteli za viwango vya kimataifa na baada ya hapo tozo na kodi zote zihusike. Hii imefanyika Zambia na Mozambique na imewezesha utalii kukua sana. Wizara hii itumie wataalam kufanya *benefit cost analysis* ya wazo hili na nina hakika

wataona kuwa kodi na ushuru tunaokosa sasa kutafidiwa kwenye mapato mengi ya utalii baadae. Wawekezaji wa ndani watahitaji kuwekeza. Serikali ipime maeneo kwenye ufukwe wa Bahari ya Hindi kuanzia Tanga hadi Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo dhana kuwa makaa ya mawe yanaweza kuwa mbadala wa mkaa wa miti, naomba Serikali ifahamishe wanachi juu ya hili. Makaa ya mawe yanahitaji majiko na tanuru maalum kabla ya kutumia kwa hiyo haitakuwa *automatic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yetu mengi hasa ya pembezoni kama Songwe na Ileje yana misitu, mabonde, mito mingi inayofaa kwa utalii wa utamaduni, wa kupiga picha na wa *camp sites* na kupanda milima. Lakini hatuna wataalam kabisa wa kuendeleza hayo. Tunaiomba Serikali itufikirie. Naunga mkono hoja.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ijikite katika kufanya tafiti mbalimbali kwa kushirikiana na Taasisi za Utafiti za Idara za Vyuo Vikuu na taasisi zingine zinazojihusisha na utafiti wa malikale au maliasili. Mpaka sasa bado Wizara haijajikita kiundani kuweza kuzigundua maliasili zetu nyingi tulizonazo hapa nchini hali inayopelekea Watanzania wengi kutokuwa na uelevu juu ya vivutio vya kale tulivyonavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe inayatambua maeneo yote ya urithi wa kihistoria tuliyonayo hapa nchini na maeneo mengine yote yenye maliasili kwa kushirikiana na watendaji wa vijiji na vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara kwa kushirikiana na Serikali kwa ujumla wahakikishe wanajenga miundombinu ya kufikia kirahisi maeneo yenye malikale na vivutio vingine vya asili ili paweze kufikika kirahisi na kujenga au kuweka karibu nyumba za kulala wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ikishirikiana na Serikali katika kuanzisha utaratibu maalum wa kuwa na somo la ziada mashuleni ambalo litawafunza wanafunzi wote wa shule za msingi na sekondari pamoja na vyuo vikuu juu ya umuhimu na faida za malikale zetu na utalii tulionao hapa nchini.

Pia naiomba Wizara kuanzisha utaratibu maalum wa kuwapatia elimu wanavijiji na wananchi kupitia mikutano ya hadhara na mikutano mingine ya maendeleo ya vitongoji, vijiji na mitaa mijini. Ifikie mahali wananchi na wasomi wengi waone umuhimu wa kutembelea mali kale zetu mbalimbali walau kwa mwaka mara mbili, hii itapelekea kuongezeka kwa pato la ndani kupitia utalii wetu wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe inayatambua maeneo yote ya urithi wa kihistoria tuliyonayo hapa nchini na maeneo yote yenye maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali/Wizara ihakikishe kila panapofanyika ujenzi wa barabara itakayopita sehemu ndefu kuna mtaalam wa malikale na vivutio vingine vya asili ambavyo atavigundua na kushauri mradi huo usipite maeneo hayo upitie njia nyingine ili kuvilinda vivutio hivyo na kuvifanya kuwa hifadhi kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwneyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na utalii. Tanzania kama nchi ina vivutio vingi sana vya utalii kwenye maeneo mengi mbalimbali lakini tatizo lililopo ni vivutio vingi kutojulikana, hivyo nashauri:-

(a) Kuwa na chombo mahsusi kwa ajili ya kutangaza vivutio hivi, chombo hiki kiwe na jukumu la kubaini vivutio hivi maeneo viliko na kuvitangaza kwenye maeneo mbalimbali duniani kupitia Balozi zetu na namna nyingine zinazowezekana. *TTB* ibaki na usimamizi na uratibu na kuacha chombo hicho maalum kibaki na kazi ya kutangaza utalii.

(b) Wizara iwekeze pesa za kutosha katika utangazaji wa utalii badala ya kufikiria kupata mapato ya kutosha kupitia utalii bila kuwekeza katika utangazaji. Mfano, vivutio vilivyoko Wilayani Ukerewe kama vile:-

(i) Jiwe linalocheza la Nyabureke;
(ii) Makazi ya Chifu Lukumbuzya;
(iii) Mapango ya Handebezyo;
(iv) Kaburi la mtunzi wa kwanza wa vitabu Hamis Kitelezya; na
(v) Pwani ya Rubya yenye mchanga mweupe na adimu sana na kadhalika.

(c) Mapato yanayotokana na maliasili yawafaidishe wananchi wanaoishi jirani na hifadhi hizi. Jambo hili litafanya watu hawa wajione ni sehemu ya hifadhi hizi na hivyo kushiriki kuzitunza bila kinyongo.

(d) Miundombinu kama barabara zinazoekea kwenye vivutio hivi vya utalii iboreshwe ili watu wenye nia ya kuvitembelea waweze kuvifikia bila matatizo jambo litakalowahamasisha kuendelea kutembelea vivuto hivi.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kuhusu fidia kwa wananchi. Katika maeneo mbalimbali ya nchi ambapo Hifadhi za Taifa zimepakana na vijiji ambavyo wananchi wanaendesha shughuli za kilimo kumekuwa na changamoto za wanayama kuharibu mazao ya wananchi na wananchi hawapewi fidia kutokana na uharibifu huo. Kilio hiki cha wananchi kimekuwa cha muda mrefu na wakati mwingine hata kama fidia inatolewa kwa kuchelewa sana na kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi. Hivyo basi naishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

(a) Kulipa fidia kwa wakati; na

(b) Malipo ya fidia yalipwe na mamlaka husika ambapo uharibifu umetokea kwani kwa kufanya malipo ya fidia kuwa *central* kwa maana ya kulipwa na Wizara imekuwa na usumbufu mkubwa na kuchelewesha malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya vijiji na hifadhi za wanyamapori; migogoro ya wananchi na mipaka au hifadhi za wanyamapori imekuwa ya muda mrefu bila kupatiwa ufumbuzi, matokeo yake Serikali imekuwa ikikimbilia kuunda tume ya kufuatilia migogoro bila mafanikio. Nashauri ije na mkakati wa namna gani inamaliza migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya misitu, natambua umuhimu wa misitu na tunaunga mkono juhudi na jitihada za kulinda misitu. Miongoni mwa mazao ya misitu ni mkaa ambayo ni nishati muhimu sana kwa wananchi kwa ajili ya matumizi ya kupikia. Wizara imetoa katazo kuwa mkaa usitoke nje ya Wilaya. Katazo hili limekuja bila kuwepo na nishati mbadala kwa wananchi hao. Miji ambayo haina sasa watakosa nishati ya mkaa na wananchi hawawezi kumudu gharama za gesi. Nashauri Serikali ifute katazo hili huku tukiwandaa wananchi kutumia nishati mbadala ambayo wataiweza na kuimudu.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na utalii wa ndani. Suala la utalii wa ndani halijawekewa umuhimu na Wizara. Ni vyema suala hili likapewa kipaumbele ili Watanzania wajenge tabia ya kutembelea vivutio vya maliasili ya nchi yetu. Na kwa kuanzia taasisi za Serikali, mashirika ya umma na shule zijenge mazingira ya kutembelea mbuga za wanyama, maporomoko, milima na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii wa Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Magharibi; kumekuwa na tabia ya kutangaza utalii wa Kaskazini tu ikiwa yapo maeneo mengine ambayo kama yakitangazwa yatakuwa kivutio kikubwa kwa watalii. Kwa mfano Mbuga za Ruaha, Selous, Katavi, Mahare, Maporomoko ya Kalambo na fukwe nzuri ya Ziwa Tanganyika hazijatangazwa, ni vyema na maeneo hayo yakatangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la migogoro ya *WMA;* Jimboni kwangu kuna migogoro ya *WMA* wa vijiji vya Kaseganyama, Kapalamsenga, Simbwesa na Kabage. Naomba migogoro ya vijiji hivi imalizwe kwani ni muda mrefu

suala hili halijapatiwa ufumbuzi. Naomba Waziri njoo jimboni kwangu umalize tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la misitu; Jimboni kwangu kuna misitu mikubwa ya Tongwe Mashariki na Tongwe Magharibi, maeneo haya ni makubwa sana na kuna wanyama vivutio kama sokwe na misitu minene ambayo inavunwa kwa wizi. Tunaomba Wizara yako itupatie magari ya doria ili tuweze kudhibiti uwindaji haramu na uvunaji haramu wa misitu. Ombi hili ni muhimu sana kwa Wilaya yangu ya Tanganyika kupatiwa magari kwa ajili ya uhifadhi.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Moshi Vijijini linapakana na Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro katika kata za Kibosho Magharibi, Kibosho Kati, Okaoni, Kibosho Mashariki, Uru Kaskazini, Uru Shimbwe na Uru Mashariki ambako kwa muda mrefu mahusiano kati ya wahifadhi na wananchi yamekuwa mazuri sana. Kumekuwepo na eneo linalojulikana kama *half mile* ambalo ni eneo la hifadhi, lakini wananchi toka enzi za wakoloni waliruhusiwa kufanya shughuli za kibinadamu kama kuokota kuni, kupata majani ya mifugo na ndipo vilipo vyanzo vya maji vingi vinavyolisha jimbo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kufuatia agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu la kuweka mipaka ya hifadhi upya mbali na kukataza kabisa eneo la *half mile* kutumika kwa shughuli za binadamu kwa masharti yaliyokuwepo mipaka mipya imechukua sehemu ya maeneo ya wananchi ambayo wamekuwa wakiyamiliki toka miaka ya 1940. Jambo hili limeleta mtafaruku mkubwa katika vijiji vya Sisimaro na Omarini huko Okaoni pamoja na Kibosho Kati, Singa Juu na Kibosho Mashariki. Ninaiomba Wizara kufuatilia jambo hili na kuona namna ya kuwapa wananchi husika maisha mbadala.

**MHE. HAROON M. PIRMOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa mpaka wa Hifadhi ya Taifa Ruaha na vijiji vinavyopatikana na vilivyomo ndani ya Hifadhi ya Ruaha umedumu takribani miaka tisa sasa tangu mwaka

2008. Hivi karibuni Serikali ilitoa maelekezo ya kushughulikia mgogoro wa mpaka huo ili uweze kuisha na wananchi waendelee na shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha hatua ya kupokea maoni ya mapendekezo ya wananchi katika vijiji 333 na Shamba la Mifugo Usangu linalosimamiwa na *NARCO* ili kufanya marekebisho ya Tangazo la Serikali Na. 28 *(GN 28 of 2008),* ni lini Serikali itapitia maombi hayo na kufanya marekebisho ya mpaka huo ili kuachia maeneo ya makazi, ufugaji na kilimo na kutoa tangazo jipya la Serikali litakalomaliza mgogoro wa muda mrefu?

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanazozifanya licha ya changamoto kubwa na nyingi zilizopo kwenye Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa heshima na taadhima Mheshimiwa Waziri apokee ushauri wangu kuhusu suala la kuwapa *offer* madaktari na timu yote ya madaktari hao kutoka Marekani ambao walifanya kazi kubwa kuwasaidia watoto wetu wa Kitanzania katika ajali iliyohusisha wanafunzi, walimu na dereva wa shule ya Lucky Vincent. Mheshimiwa Waziri, madaktari hawa walikuwa wamekuja Tanzania kwenye programu tofauti lakini wakiwa nchini waliona nia ya kwenda kutembelea vivutio vyetu ambapo walikutana na ajali hiyo eneo la Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu hii ilifanya kazi kubwa ya kuwasitiri watoto wetu ambao walifariki lakini waliendelea pia kuwasaidia waliojeruhiwa kwa kuwapeleka nchini Marekani kwa ajili ya matibabu. Huu ni moyo wa kipekee, kwani ilibidi wakatishe safari yao kutokana na tukio hilo. Naiomba Wizara licha ya ukweli kwamba madaktari hawa wana uwezo, lakini sisi kama Watanzania tuna njia nyingi za kuwashukuru kutokana na kitendo hicho, na kwa kuwa walionesha nia ya kutaka kwenda kwenye vivutio vyetu naona itakuwa ni jambo jema kama tukitambua mchango wao kwa kuwapa *offer* hiyo ya kuja bure kwenye vivutio vyetu

popote watakapotaka kutembelea. Kama ikikupendeza basi tuwape *offer* ya muda mrefu ili waweze kujipanga na kuamua siku watakazotaka wao wenyewe.

Mheshimiwa Waziri, hiyo itasaidia kuonesha shukrani yetu lakini pia itasaidia kuendelea kutangaza utalii wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza na kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii kutoa mchango wangu katika Wizara hii. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake wote kwa utayari wa kuiwasilisha hotuba hii kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni Idara ya Utalii. Sekta ya utalii ni sekta muhimu sana ulimwenguni. Azma ya kuendeleza utalii ni jambo jema angalau litatoa ajira za moja kwa moja na zile zisizo za moja kwa moja. Naiomba Serikali ichukue juhudi rasmi za kusimamia idara hii badala ya kuziachia sekta za wananchi jambo ambalo si zuri. Serikali iendelee kuwaelimisha wananchi na kuwahamasisha wajione kuwa ni sekta yenye manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali iweke ushawishi maalum kuwashauri watalii kutembelea sehemu zote za Muungano. Hivi sasa kumekuwa na mtindo ambao sio mzuri wa watalii ambao wanatembelea maeneo ya Bara kuishia huku tu, jambo ambalo linawanyima fursa Wazanzibar kuonesha vivutio vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni mafunzo kwa Idara za Wizara hii. Wizara hii ina idara nyingi ambazo ni muhimu katika kuiendeleza Wizara. Kumekuwa na mtindo ambao si wa kuridhisha sana juu ya kuwapatia mafunzo wafanyakazi

wa idara hizo. Mara nyingi nafasi za kujifunza zinapotoka huwa zinachukuliwa na viongozi na kuwaacha wafanyakazi wa chini ambao wao ndio wazalishaji wakubwa.

Naiomba Wizara kurekebisha mwenendo huu na kuweka mpango maalum *(training program)* ili wafanyakazi wa ngazi za chini nao wapate mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa hotuba yao nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukanda wa Kusini *(Southern Circuit)* upo nyuma sana kiutalii pamoja na ukweli kwamba kuna vivutio vingi vya kitalii. Kwa mfano, Kisiwa cha Mafia katika Mkoa wa Pwani kimejaaliwa kuwa na vivutio vifuatavyo:-

Kwanza kuna *whale shark,* samaki huyu aina ya papa (potwe) wamebaki wachache sana na katika nchi chache duniani. Moja ya sifa nyingi za samaki huyu ni rafiki kwa mwanadamu kama livyo pomboke *(dolphin)* na watalii wanapenda sana kucheza na kuogelea naye. Kwa sasa samaki huyu anapatikana Australia, Philippines na nchi chache za Bara la Amerika ya Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na umuhimu wake na mvuto wake kwa watalii hakuna juhudi zozote kutoka upande wa Serikali katika kumtangaza samaki huyu. Juhudi pekee ni zile zinazofanywa na mmiliki wa hoteli na mtalii mwenyewe. Tunaiomba Serikali sasa itangaze kivutio hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuna *scuba diving,* hiki ni kivutio kingine kinachopatikana kisiwani Mafia. Mandhari ya chini ya bahari ya Mafia imesheheni samaki wa aina mbalimbali ambazo zinawavutia watalii kuja na kufanya

uzamiaji wa bahari. Tunaiomba Serikali sasa itangaze kivutio hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni *sports fishing* ambapo ni uvuvi wa mchezo maarufu kama *catch and release* ambapo watalii wanavua samaki na kupiga nao picha halafu huwarejesha baharini akiwa hai. Ni kutokana na vivutio hivi pamoja na vivutio vingine vya Kusini vya Mji wa Kilwa na magofu yake, mbuga ya Selous na *hot spring* Utete Rufiji; Serikali sasa ije na mpango mkakati wa kutangaza vivutio hivi vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni idadi ya watalii wanaotembelea nchi yetu. Ni ukweli usio na shaka kumekuwa na ongezeko la utalii nchini. Lakini kuna utata mkubwa namna ambavyo takwimu hizi zinakokotolewa. Nimeomba Mheshimiwa Waziri wakati anakuja kujibu atupe ufafanuzi juu ya kadhia hii. Je, watalii hesabu inachukuliwa kwenye mipaka yetu au viwanja vya ndege na mipaka ya bandari na bandari zetu au wakati wanaingia kwenye vivutio vyetu? Je, watalii wanaoingia Zanzibar moja kwa moja na kuondokea huko huko hawa wamo katika idadi ya watalii milioni 1.2 walioingia Tanzania mwaka wa jana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. OMARY T. MGUMBA** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa uamuzi wake wa kununua ndege na kuimarisha Shirika letu la Ndege ili kuinua utalii wa ndani na nje kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya wataalam kwa wasilisho zuri la hotuba yao ya uchapaji kazi wao katika

Wizara hii. Baada ya utangulizi huo, naomba kutoa mchango na ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zuio la mkaa; zaidi ya asilimia 90 ya Watanzania wanategemea matumizi ya mkaa na kuni katika maisha yao ya kila siku, kwa mfano vijijini. Kwa kuwa nishati mbadala mpaka sasa haijasambaa nchi nzima hasa kwa maeneo ya vijijini katika Jimbo langu la Morogoro Kusini Mashariki ambako zaidi ya asilimia 70 ya vijiji umeme haujafika na hata gesi hakuna na wananchi hutegemea kuni na mkaa kama nishati ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni kwa kuwa wananchi wengi vipato vyao ni vidogo kumudu gharama ya umeme ukizingatia umeme wenyewe ni mdogo ambao haukidhi mahitaji ya nchi na kwamba anayetumia zaidi analipa zaidi na gharama kubwa sana ambazo wananchi hawawezi kumudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri Serikali kusitisha zoezi la katazo la matumizi ya mkaa kusafirisha sehemu moja kwenda nyingine mpaka pale Serikali itakapokuwa na uwezo wa kuzalisha na kusambaza nishati mbadala nchi nzima kwa wananchi na pia kupata maandalizi ya kutosha katika kutoa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu ahadi ya Serikali ya kutupatia ardhi ya kulima kutoka katika msitu wa Mkulazi ulio karibu na Kijiji kipya Bwila Juu walikohamia watu waliopisha ujenzi wa bwawa la Kidunda. Watu waliopisha ujenzi wa bwawa kutoka Kidunda Kitongoji cha Manyanyu na vingine walikuwa na nyumba zao pamoja na mashamba katika maeneo hayo kama ilivyo kawaida sehemu za vijijini. Lakini Serikali aliwapa wananchi hawa katika eneo jipya viwanja tu vya kujenga nyumba bila ardhi ya kilimo ili kujitegemea kiuchumi kama eneo la awali lilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia changamoto hiyo na umuhimu wa kilimo na uchumi wa wananchi hao, Serikali kupitia Mkuu wa Mkoa wa Morogoro

Dkt. Rajabu Lutengwe ilisema itawapa wananchi hawa ardhi yenye ukubwa wa ekari 50,000 iliyo karibu na vijiji vipya ili wananchi waweze kuhamia pale na kuendeleza shughuli zao za kilimo na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kutimiza ahadi hii haraka ili wananchi waweze kuendeleza shughuli za kiuchumi na kuepuka mambo kama yale yaliyotokea mwaka 1973 katika *operation* vijiji. Ni lini Serikali itatoa ardhi hii kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni mamba katika Mto Ruvu. Wakati wa kiangazi tunapata maafa mengi hasa katika Kata ya Tunanguo kutokana na mauaji yanayosababishwa na mamba wanaotoka katika Mto Ruvu. Ombi langu kwa Serikali, kwanza kuvuna mamba hawa kutoka Mto Ruvu kwa sababu wamekuwa wengi na pili kulipa fidia na matibabu kwa wananchi walioathirika na mamba. Pia Serikali kulipa wananchi wangu walioathirika na tembo miaka saba iliyopita katika kata ya Kidugala, Ngerengere, Mkulazi na Matuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ni kuhusu fidia ya watu wanaouawa na kujeruhiwa na wanyama wakali kama mamba katika kijiji cha Makaule na Kazamoyo Tunduru. Watu waliouawa na fisi katika kijiji cha Jiungeni na Mchesi Wilaya ya Tunduru bado hawajalipwa fidia hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia kwa watu waliohariбiwa mazao yao na wanyama wakali hasa tembo katika kijiji vya Mchoteka, Wenje, Likweso, Walasi, Nasomba, Kazamoyo, Lukumbule, Makande, Mtina, Angalia, Malumba, Misyaji na maeneo mengine ya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru hadi leo hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro wa mipaka na hifadhi katika kijiji cha Misyale na Ukala, ambapo askari walizoa vyakula vya wananchi wanaolima katika maeneo ya hifadhi na kuuza bila kuwachukulia hatua za kisheria. Maeneo mengine yenye migogoro ni Hifadhi ya Misitu Misedula na kijiji cha Msinji katika kata ya Ligoma. Ni vyema baadhi ya maeneo yakagawiwa kwa ajili ya kilimo na huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kuna vivutio vingi sana ambavyo vinaweza vikatangazwa na kutembelewa na watalii na kuliingizia Taifa pato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TFS* wanamaliza misitu kwa kutoa vibali ovyo vya mbao na uvunaji wa magogo bila kujali athari za mazingira. *TFS* wana mahusiano mabaya na wananchi waliopo karibu na hifadhi za misitu. *TFS* wameshiriki kuhujumu misitu karibu maeneo yote yenye hifadhi za misitu. Misitu ya asili inaisha kama *TFS* hawataacha kulinda vizuri misitu yetu.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, hongereni sana kwa kutekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu. Niwaombe mnisaidie kutatua migogoro ya maeneo yaliyohifadhiwa na jamii *(WMA)* ya Kimbanda, Kisungura na Mbarangandu dhidi ya wananchi walioyatoa maeneo hayo. Wananchi hao walitegemea mipaka ya *WMA* hizo ingepitiwa upya baada ya miaka kumi, kama walivyoahidiwa lakini inaonekana hakuna mpango wowote wa kupitia upya mipaka hiyo. Wananchi wameongezeka na wanahitaji maeneo zaidi kwa shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba mridhie kuachia eneo linalogombaniwa kati ya Chuo chenu cha Likuyu Sekamaganga (Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi), hususan eneo ambalo halitumiwi na chuo hicho na limevamiwa na wakulima wakazi wa kijiji cha Kikuyu Sekamaganga. Eneo

husika lilikuwa ni sehemu ya eneo la kijiji hicho na lilichukuliwa bila ya kulipiwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri aliyetembelea kijiji cha Likuyu Mandela kilichokumbwa na uharibifu wa mashamba uliofanywa na tembo ambapo baadhi ya wanakijiji hao kupoteza maisha kwa kuvamiwa na tembo hao. Naomba ahadi ya kulipa kifuta machozi na kipangusa jasho kwa waliouawa na tembo na walioliwa mazao yao na tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja na nawataka utekelezaji mwema.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba nzuri. Hongera Mheshimiwa Waziri kwa hotuba madhubuti. Wizara hii ni miongoni mwa sekta kiongozi katika ukuaji wa uchumi wa Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa namna ya pekee na kwa namna anavyofanya kazi na kuonesha ushirikiano mkubwa kwetu sisi watu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, hasa kuhusiana na hatua mbalimbali za uendelezaji wa Mapori ya Akiba ya Kigosi Moyowosi. Pori la Akiba la Kigosi Moyowosi ni pori zuri sana, hata hivyo liliachwa bila uangalizi madhubuti, matokeo yake pori hili likavamiwa na makundi makubwa ya ng'ombe wa ndani na wengine kutoka nchi jirani, hasa nchi ya Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Spika, kutelekezwa kwa Pori hili la Akiba la Kigosi Moyowosi kulisababisha miundombinu yake kukosekana, barabara katika pori hili ndio uti wa mgongo wa ulinzi na usalama kwa pori lenyewe na wanyama wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo kwa barabara za kudumu ndani ya pori hili kumedumaza maendeleo ndani ya pori hili, matokeo yake mwanya unapatikana kwa

majangili kuua wanyama, uvamizi wa wakulima na wafugaji na wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wa ndege ndani ya Pori la Akiba la Kigosi Moyowosi ni chachu ya ukuzaji wa utalii ndani ya pori hili. Kiwanja cha ndege kifufuliwe, ili kiwe kiungo muhimu na Hifadhi za Taifa za Mahale na Gombe, pia *Rubondo National Park*. Hongera Mheshimiwa Waziri kwa uamuzi wako wa busara wa kuonesha nia ya kulipatia Pori la Akiba la Kigosi Moyowosi magari mawili kwa ajili ya uendelezaji wa shughuli za utawala na ulinzi wa pori lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameonesha nia ya kulikarabati *grader* lililopo Kifura ili lifufuliwe na kuanza kutumika kufungua barabara ndani ya pori hili. Nakuunga mkono Mheshimiwa Waziri, songa mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa Mamlaka ya Wanyamapori *(Tanzania Wildlife Authority – TAWA),* ni hatua muhimu sana katika kuyaunganisha na kuyasimamia mapori yote ya akiba nchini. Ninaamini hatua hii itaongeza ufanisi kiutendaji kama ilivyo kwa *TANAPA* na *Ngorongoro Conservation Area Authority* na kwa mantiki hiyo, mchango wa mapori ya akiba nchini, chini ya *TAWA* kuongezeka katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa mwisho ni kuhusu uanzishwaji wa *Game Rangers* ndani ya Pori la Akiba la Kigosi Moyowosi na kufungua barabara ndani ya pori hili. Mungu ibariki sana Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na timu nzima ya Wizara kwa hotuba yao ambayo imeonesha matumaini ya dhati kabisa ya kuinua sekta ya utalii, wanyamapori pamoja na misitu. Nichukue fursa hii kuchangia maeneo machache katika hotuba hii, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 59 unazungumzia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Kwa mujibu wa Sheria ya Misitu ambayo ilianzisha Wakala wa Misitu, lengo kubwa la uanzishaji wa *TFS* lilikuwa ni kusimamia na kuhifadhi rasilimali za misitu na ufugaji wa nyuki. Wakala wanatekeleza wajibu wao vema, ila yapo baadhi ya meneo nchini utendaji wa wakala unagubikwa na baadhi ya watumishi wachache kuwa sehemu ya uharibifu wa misitu na kutosimamia uharibifu wa misitu, hili ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika Wilaya ya Kilindi ambako ndiko liliko jimbo langu kuna uharibifu mkubwa wa uvunaji wa misitu ambao haufuati utaratibu. Katika Kata za Kilwa, Kilindi Asilia, Kata za Msanja na Kata za Mswaki, maeneo haya kuna uvunaji wa mbao ambao si rasmi. Wakala yupo Wilaya ya Handeni, lakini cha kushangaza mbao zinasafirishwa usiku. Hivi Wizara na Mkurugenzi wa Wakala taarifa hizi mnazo? Nimuombe Mheshimiwa Waziri na timu yake wafuatilie suala hili kwa karibu sana na ningependa kupata maelezo ya kutosha kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Mbuga Tengefu ya Wanyama ya Saunyi. Serikali ina dhamira ya kuongeza Pato la Taifa kupitia utalii wa wanyama na kadhalika, lakini bado kuna maeneo ambayo Wizara haijayapa kipaumbele, mfano katika eneo la kitalii la Mbuga Tengefu ya Saunyi iliyopo Kata ya Saunyi, Wilaya ya Kilindi, eneo hili kuna wanyama mbalimbali, lakini sijaona jitihada za Wizara. Hivi Wizara haijui kama eneo hili lingesaidia kuinua Pato la Taifa? Wapo wawindaji wengi wanawinda isivyo rasmi, naomba Wizara itupie jicho eneo hili kwani Wizara isipofanya haya ni kuvunja moyo wananchi wa Saunyi ambao kwa muda mrefu ni wafugaji na ambao wamekuwa sehemu ya kulinda hifadhi ya mbuga hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie eneo lingine katika ukurasa wa 79 kuhusu Wakala wa Mbegu. Wakala huyu ni muhimu sana katika kuhakikisha mbegu zinapatikana za kutosha. Mbegu hizi ndizo ambazo zinatumika katika kuhakikisha maeneo ambako kuna ukataji wa miti kwa wingi

ambayo husababisha kuleta jangwa. Mbegu hizi zinasaidia kupunguza athari, lakini naona jitihada za Wakala katika eneo hili ni ndogo sana. Niombe sana jitihada ziongezwe kuhakikisha mbegu zinapatikana kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la mara kwa mara la wafugaji kuvamia misitu. Hivi kweli dhamira ya Wizara na Serikali kulinda misitu itafanikiwa kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Kata ya Msanja, Kijiji cha Mswaki, kuna msitu wa Bondo. Msitu huu ni wa Serikali, lakini viongozi wa Serikali katika kata hii wameruhusu wafugaji kufanya shughuli za ufugaji katika eneo hili, hivi hili ni sahihi kweli? Naomba Wizara ichukue hatua haraka ili kuhakikisha kuwa misitu hii inalindwa kwa gharama kubwa. Aidha, Wizara iweke utaratibu wa kuwa na timu katika Wizara ya kufuatilia watendaji wao ambao wana dhamana ya kusimamia misitu ya nchi yetu. Vilevile kwa wale wanaovamia misitu watozwe faini kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvunaji wa Asali na Ufugaji wa Nyuki. Tanzania ina misitu mingi na maeneo ambayo kama ufugaji wa nyuki utasimamiwa kwa dhati tunaweza kuzalisha kiasi kikubwa cha asali. Miongoni mwa mikoa ambayo ni wafugaji wa nyuki na kurina asali ni Mkoa wa Tanga na sisi wa Wilaya ya Kilindi. Tunafuga nyuki na kurina asali pia, ila kuna tatizo moja ambalo ningependa Wizara ilifanyie kazi, nalo ni kutuletea Wataalam wa kutosha ambao watatoa elimu ya utengenezaji wa mizinga pamoja na njia za kisasa za kufuga nyuki kwa sababu, Kilindi kuna nyuki na misitu mingi sana ambayo kama jitihada za kuwekeza zitafanywa basi, tutawapa wananchi wetu fursa ya kupata mapato katika eneo la ufugaji wa nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wa Wizara hii. Naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina nia ya kupanua eneo la Hifadhi ya Taifa ya Selous hadi Wilaya ya Mbinga katika Kata za Litumbandyosi na Ruanda. Fukuto la migogoro ya mipaka katika eneo hili limekwishaanza kujitokeza. Hivyo naishauri Wizara ichukue hatua za haraka kwenda kuweka vizuri mipaka katika kata hizo za Litumbandyosi na Ruanda ili kuepusha migogoro hiyo inayofukuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa katika upanuzi wa hifadhi kwa niaba ya wananchi wa kata hizo naomba mipaka ikarekebishwe ili yale maeneo yanayolimwa waweze kuachiwa waendelee na shughuli zao za kiuchumi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke wazi fursa zilizopo katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Misitu *(Tanzania Forest Fund)* ili wananchi wapate kunufaika nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Mbinga katika kijiji cha Mbuji, Kata ya Mbuji yapo mawe makubwa mawili ambayo inasadikika kuwa mawe hayo ni Bibi na Bwana, kwa maana kwamba kuna jiwe la kiume na jiwe la kike. Katika mawe hayo unafanyika utalii ambao si rasmi na miaka ya hivi karibuni kuna mzungu alidondoka kwenye jiwe mojawapo hadi kupoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mawe hayo kuna viumbe hai wanaoishi ambao wanafanana na binadamu isipokuwa wao ni wafupi sana. Viumbe hao wanafahamika kama “VIBUTA” kwa lugha ya Kimatengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ikafanye utafiti katika mawe hayo ili kubaini viumbe hivyo na kubaini fursa nyingine za kitalii. Inasadikika kuwa viumbe hao wanapatikana pia katika nchi ya Australia. Naomba kuwasilisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwanza kwa kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuniwezesha kushika kalamu na kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi.

Kwanza kabisa naomba kuchangia juu ya Wakala wa Uhifadhi na Uvunaji wa Mazao ya Misitu *(TFS).* Taasisi hii imekuwa ni mzigo kwenye Halmashauri zetu, badala ya kuwa taasisi ya uhifadhi yenyewe inaongoza kwa kuharibu misitu vilevile mahusiano ya taasisi hii na jamii au Halmashauri zetu siyo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hii imekuwa haitoi elimu ya kutosha kwa jamii juu ya uvunaji endelevu wa misitu badala yake imekuwa ikiwalinda wavunaji haramu kwa faida ya watendaji wa taasisi. Mfano mzuri ni katika Halmashauri yangu ya Liwale katika Wilaya ya Liwale kuna hifadhi mbili za misitu, kuna msitu wa Angai ambao unahifadhiwa na vijiji 24, na msitu wa Nyera-Kipelele, huu ni msitu wa kitaifa lakini hadi leo msitu wa Nyera - Kipelele bado uvunaji haujafanyika. *TFS* wanasema mwongozo wa uvunaji haujakamilika lakini wavunaji haramu wanavuna kila kukicha bila ya wahusika kuchukua hatua za kuzuia ujangili huu. Kwa ule msitu wa vijiji bado vijiji havina elimu ya kutosha juu ya uvunaji endelevu jambo linalochangia kwa kiasi kikubwa upotevu wa mapato katika vijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa uwakilishi wa Mbunge na Madiwani katika Kamati ya Uvunaji wa Rasilimali za Misitu kunaongeza mwanya wa wizi wa mali za misitu. Kamati hii huongozwa na Wakuu wa Mikoa. Je, kuna siri gani inayofanya Meya na Wabunge washindwe kualikwa kwenye Kamati hizi ikiwa wao ni wawakilisi wa wananchi? Vilevile makato ya asilimia tano yanayotengwa kwenye Halmashauri zetu ni kidogo mno kulinganisha na uharibifu wa misitu hiyo, Halmashauri zetu hutegemea misitu katika kukuza uchumi wake, hivyo naishauri Serikali kuangalia upya viwango hivyo ili kuviboresha na kuziongezea uwezo Halmshauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee Pori la Akiba la Selous. Hifadhi hii ni kubwa sana hapa Barani Afrika na duniani kwa ujumla na sehemu kubwa ya hifadhi hii iko Wilayani Liwale, cha kusikitisha hakuna miundombinu yoyote iliyojengwa Liwale katika kuhudumia hifadhi hii. Hata

barabara ya kuingia katika hifadhi hakuna, lango la kuingia kwenye hifadhi hii kwa watalii liko Mikumi Mkoani Morogoro jambo linalowanyima fursa za ajira kwa wakazi wa Wilaya ya Liwale na Mkoa wa Lindi kwa ujumla. Hivyo, naiomba Serikali kufikiri kufanya uwekezaji wa kutosha ili wale wanaozungukwa na hifadhi hii waone faida ya kuwa na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mamlaka ya Wanyamapori, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuanzisha mamlaka hii, utendaji wake bado siyo wa kuridhisha, bado kuna usiri mkubwa na ushirikiano na jamii zinazozungukwa na hifadhi siyo nzuri. Mfano katika Halmshauri yangu ya Liwale hadi leo hatujui hatma ya mgao wetu wa asilimia 25 ya mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii. Hatujui tunayapataje, ukiwauliza wahusika hawana majibu ya kuridhisha zaidi ya kukatisha tamaa. Kitendo cha kuficha taarifa za mapato na kuacha kuweka wazi stahiki za Halmashauri zetu hakioneshi au kinapingana na malengo ya kuundwa kwa taasisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya utalii kwa Kanda ya Kusini bado vivutio vingi havijatangazwa vema au vimesahaulika kabisa. Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi katika Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara kuna vivutio vingi havijatangazwa. Mfano, Boma la Mjerumani lililoko Liwale, Kaburi ya Mzungu (Mfaransa) lililoko Mikukuyumbu-Liwale. Kaburi la Bibi aliyesadikiwa kuwa ni Sharifu katika uhai wake lililopo katika kijiji cha Ndapata - Liwale. Vilevile kuna viboko wanaowasiliana na wazee wa kimila walioko Kilwa, pamoja na maji moto yaliyopo katika Mto Rufiji. Hivi vyote ni vivutio vya utalii vilivyosahaulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya mipaka, kuna mgogoro wa muda mrefu wa mpaka wa kijiji cha Kikulyungu na Hifadhi ya Selous, mgogoro huu umeshachukua roho za watu wanne, ni bora sasa mgogoro huu ukapatiwa ufumbuzi ili amani na usalama vikarejea baina ya jamii na wahifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia kwa ndugu Abilahi Njonjo, huyu ni mwananchi aliyejeruhiwa na Askari wa wanyamapori kwa kupigwa risasi kusababisha akatwe mkono. Taarifa zake ziko Ofisi ya Katibu Mkuu wa Wizara akilalamikia namna ya kupata hicho kinachoitwa kifuta machozi ni miaka miwili sasa tangu amekatwa mkono.

**MHE. ANGELINE S. L. MABULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja na kuwapongeza kwa kazi nzuri katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni Mkoa wa Mwanza pamoja na kuwa makazi ya makabila zaidi ya manne, lakini Wasukuma ni wengi zaidi. Kuna utamaduni wa Kisukuma ambao umejengeka na kuhifadhiwa kwa njia ya ngoma na vitendea kazi vilivyokuwa vinatumika enzi za mababu zaidi sana historia ya uchifu kwa koo tofauti za Wasukuma umehifadhiwa vizuri.

Aidha, namna ya maisha waliyoishi na kuweza kudumisha amani ya maeneo yao lakini pia Kituo cha Bujora kimetunza kumbukumbu zote vema ambapo watalii wanaweza kutembea na kujifunza mengi. Rai yangu naomba Kituo cha Bujora kiingizwe katika maeneo ya vivutio vya utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Victoria mbali na kuwa ziwa la pili kwa ukubwa duniani bado halijatangazwa vema, tunaweza kutangaza kivutio hiki kwa kuwekeza katika michezo ya ziwani kwa kuweka *sports boats (speed boats)* ambapo watalii wanaweza kushiriki kikamilifu. Aidha, wanaweza kufanya uvuvi *(sport fishing)* ambapo Ziwa Victoria ni tulivu, uvuvi wa aina hiyo ya utalii unaweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uwanja wa ndege wa Mwanza upo katika upanuzi, bado watalii wanaweza kutumia uwanja huo kwenda Serengeti ambapo ni karibu zaidi tofauti na *KIA* ambako ndiko watalii wengi wanapitia.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wengine wote wa Wizara hii muhimu kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao na kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi kwa sekta ya utalii kutoa ajira ya watu 500,000 za moja kwa moja. Ni vema hata hivyo Wizara ikaongeza nguvu katika ukuzaji wa utalii na matangazo katika nchi ambazo zina watalii wengi tena wenye uwezo wa kuja Tanzania kutalii kama China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ni muhimu tukaendelea kuhamasisha uwekezaji zaidi katika ujenzi wa hoteli ya kisasa ya nyota kuanzia nne, tano, sita ili kuongeza idadi ya vyumba kwa ajili ya malazi yenye viwango na ubora wa wageni, watalii wa nje na wa ndani. Hii inapaswa kwenda sambamba na kuwa na wafanyakazi wenye uwezo na viwango bora katika kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuchangia kwa kusema, naomba kuendelea kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuzuia kukata miti kwenye Hifadhi ya Msitu wa Amani naomba lipewe kipaumbele. Miti inakatwa na baadhi ya viongozi wa vijiji maeneo hayo wanasimamia, wanatumia misumeno ya *chainsaw*. Tumepeleka *FFU* mara mbili lakini wakiondoka tu kazi inaendelea wanaharibu vyanzo vya Mto Zigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri *humbly* mhamishe kikosi cha wanyamapori kihamie moja kwa moja kupunguza gharama. Nakuhakikishia Mheshimiwa Waziri ukidharau usishangae msitu huu wa Amani ukaisha, hamishia kikosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uangalie uwezekano wa kusaidia Ofisi za Ubalozi wetu zenye uwezo

wa kuleta watalii. Kuna wakati Wizara yako ilisaidia sana Ofisi zetu za Kibalozi na walisaidia sana kuwakilisha nchi mbalimbali ambazo mlishindwa kuhudhuria. Fikirieni kuweka fungu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika kama njia na sehemu za kupumzika wakati wa kupanda Mlima Kilimanjaro, nilipopanda Mlima huo mwaka juzi hali ilikuwa mbaya. Naomba viboreshwe tafadhali.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi anavyoisimamia Wizara hii na uchapakazi wake akitumia uzoefu na umahiri mkubwa alionao. Naomba nimpongeze Naibu wake na watendaji wa Wizara hii kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao.

Kipekee kabisa naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano mkubwa alionipa kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja ambao uliniwezesha kutekeleza vema majukumu yangu katika eneo langu la uwakilishi (kundi la watu wenye ulemavu). Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali dogo kuhusu kifuta machozi kwa waathirika wa katazo la usafirishaji wanyamapori hai nje ya nchi, kitatolewa lini? Na je, kitatolewa kwa uhalisia wa gharama walizotumia waathirika hawa? Naomba ufafanuzi wa kina kwa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa sababu imeonyesha mwelekeo wa wapi Serikali inatakiwa itekeleze katika vipaumbele vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji wa nyuki, pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali kukuza ufugaji

wa nyuki lakini bado Watanzania hawana elimu ya kutosha ili wayatumie mapori yetu kupata asali kwa ajili ya biashara. Serikali itoe elimu kwa Watanzania waweze kufuga nyuki kisasa na wayatumie mapori yetu vizuri ili wapate kipato. Wizara iwasaidie vijana, wafugaji kwa kuwapa elimu, mikopo na vifaa vya kufugia nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwindaji haramu; pamoja na Serikali kuendelea kupinga biashara hii haramu, ujangili na mauaji ndani ya mbuga zetu, nahitaji kufahamu mambo haya na nisipopata majibu nitashika shilingi.

(i) Kuna Mchina alikamatwa na lori la meno ya tembo katika mbuga ya wanyama Katavi. Mchina yule akaachiwa eti alikuwa hajui Kiswahili. Je, hamuoni kwamba kuwaachia maharamia hawa ni Serikali imeshindwa kusimamia uharamia huu? Naomba majibu Mchina alifanywa nini na kesi ikoje?

(ii) Kuna taarifa kuhusu majangili kutoka nchi jirani za Rwanda, Kongo na Burundi wanaingiza makundi ya ng'ombe mbugani wanajifanya wanachunga au wamepotea njia na kuingia hifadhini. Je, Usalama wa Taifa kuhakikisha upotevu na uharamia huu haufanyiki uko wapi kuyasemea haya? Je, hamuoni ujirani huu tusipokuwa makini tutapoteza rasilimali zetu? Mkakati wa Serikali kuhakikisha mnazuia hawa maharamia wafugaji kuingia na kuvuna pembe za ndovu ukoje?

(iii) Rushwa kwa wawekezaji katika mbuga zetu. Serikali imeweza kudhibiti rushwa hizi na kulinda uwindaji haramu, waliokamatwa na pembe za ndovu kuachiwa Wizara ya Maliasili imeshindwa kusimamia hili.

(iv) Wafanyabisahara (wa China) wa meno ya tembo kuendelea kuisaidia Serikali kutoa misaada ni kujificha nyuma ya pazia.

(v) Usimamizi wa ukataji miti hovyo Kibaoni, Nkasi leo hii ni jangwa kabisa. Serikali ione namna ya kuzuia uharibifu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha mbuga za Mikoa wa Kusini; Lindi/Mtwara (Selous), Katavi (Katavi), Rukwa (Rukwati), kuna kigugumizi gani kuzitangaza mbuga hizi? Mnaitangaza Serengeti kila leo wakati kuna mbuga kubwa hamzitangazi kuna nini hapo? Katavi kuna twiga mweupe na tembo wakubwa lakini Serikali haina mkakati kabisa wa kuzitangaza mbuga hizi kuna nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miundombinu, Serikali iboreshe viwanja vya ndege Katavi, Kigoma na Mwanza ili watalii wasipande ndege zaidi ya mbili kufika Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua ni namna gani Serikali itaitangaza Katavi angalau tupate watalii kutoka Zambia? Kwa nini Mikoa ya Kusini hamuitangazi mnaendelea kuzitangaza mbuga ambazo zimetosha kutangazwa kama Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa *operation* tokomeza ujangili, ni lini mtawafidia wananchi waliochomewa nyumba zao, biashara zao, wakabakwa, wakateswa nje ya utaratibu wa kutafuta majangili? Ni lini mtawalipa hawa wananchi fidia zao kwa mateso waliyopewa; na huku Askari Wanyamapori wapo wanaishi kwa furaha huku wananchi hawa wakiishi katika mazingira magumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvunaji wa misitu, magogo na mbao, kuna uharibifu wa misitu unafanyika katika mapori yafuatayo:-

(i) Ipole – Tabora;
(ii) Inyonga – Mpanda;
(iii) Lyamgoloka – Mpanda Vijijini; na
(iv) Jimbo la Nsimbo – Kata nyingi zinafanya biashara hizi na watendaji wa Kata kuuza magogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mkakati gani wa kuwawajibisha hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi wa viboko katika Mbuga ya Katavi unahatarisha uhai wa viboko kutokana na kukithiri kwa vizibo vya umwagiliaji na viboko kukosa maji.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa na nzito wanayokabiliana nayo. Niwatie moyo kuwa mnaweza na muendelee kuchapa kazi na kutatua kero zilizopo ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia hifadhi ambazo zipo karibu ya makazi ya wananchi na kwa miaka mingi hifadhi hizo haziendelezwi badala yake hifadhi hizo zimekuwa mapori. Mfano, Hifadhi ya Lukunda Pachambi, msitu huu unaingia kwenye kata tatu; Kata ya Mtego wa Noti, Kata ya Mganza na Kata ya Nguruka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi kama hizi za Lukunda Pachambi na Tandala Ilunde ziwekewe mikakati maalum ikiwezekana baadhi ya maeneo yatengwe kwa ajili ya wafugaji ili kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie migogoro ya baadhi ya vijiji na hifadhi zetu. Naona Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu hiki cha bajeti kazungumzia tatizo hili la migogoro ya hifadhi na vijiji (ukurasa wa 61) kuwa timu iliundwa ya kutatua migogoro ya wafugaji na wakulima na ilifanya kazi kwenye mikoa mitano. Kamati ilihusisha Wizara ya Maliasili na Utalii, TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hapa nizungumzie mgogoro wa Hifadhi ya Mahale na vijiji vya Sibwesa, Kalilani, Lubilisi na vijiji vingine vilivyopo karibu na hii Hifadhi ya Mahale. Mgogoro wa Hifadhi ya Mahale na vijiji viwili kati ya hivyo hapo juu, kijiji cha Kalilani na kijiji cha Sibwesa una miaka zaidi ya 30 na vijiji hivi vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria. Natambua zoezi la uwekaji wa *beacons* ni agizo la

Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini vijiji hivi vilitangazwa kwa mujibu wa sheria na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri kwa nini suala hili la vijiji viwili vya Sibwesa na Kalilani ambapo mgogoro wake umedumu kwa takribani miaka 30; kwa nini basi usuluhishi usifanywe na Wizara ya Maliasili, wananchi kwa maana ya Serikali za Vijiji vya Sibwesa na Serikali ya Kijiji cha Kalilani, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi na TAMISEMI?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hili ili mazungumzo yafanyike kwa utaratibu wa Serikali na siyo hivi sasa Hifadhi ya Mahale inavamia na kuweka *beacons* pasipo ushirikishi wa Serikali za Vijiji na TAMISEMI, kwa sababu *GN* za vijiji zinaingiliwa na *beacons* hizi. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri, natambua ni mtu sikivu sana na muelewa kwa miaka mingi sana. Hivyo, tuombe haki ya wananchi hawa wa vijiji hivi ilindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuishukuru *TANAPA* kwa kutoa shilingi bilioni 1.6 za kujengwa madaraja matatu. Daraja la Rukoma, Daraja la Lagosa na sasa wanaendelea kujenga daraja la mwisho. Kwa niaba ya wananchi wa huu Ukanda wa Ziwa Tanganyika tunaishukuru sana *TANAPA* kwa msaada huo na bado tunaomba msaada wa ujenzi wa barabara inayokwenda Mahale kilometa 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepongeza wakati wa kuchangia moja kwa moja Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sana kwa dhati bajeti ya kitengo cha utangazaji wa utalii wetu kupewa kipaumbele ndani ya utalii kwa kutangazwa mapema vivutio vyetu kwani kuchelewa kwetu kunapelekea nchi jirani na vivutio hivyo kuvitangaza ndani ya nchi zao kama Kenya - Mlima Kilimanjaro au Zambia - *Kalambo Falls*(Rukwa) ni hatari na kutupunguzia mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuweke timu maalum ya kufuatilia vivutio hapa nchini na kutimiza taratibu kwa uharaka na kuvitangaza kwa kwenda sambamba na utekelezaji wa kuweka mazingira rafiki ya kuwafikisha watalii kwenye maeneo hayo. Tunashukuru Mkoa wa Rukwa Serikali kulishughulikia eneo la *Kalambo Falls* kuweka miundombinu, kasi hiyo iongezeke kukamilisha zoezi tuanze kupokea mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ni muhimu sana kutekelezwa kikamilifu na Wizara ya Fedha kwa maana ya Hazina hutoa fedha kwa kufuata maidhinisho ya Bunge kwa hii Wizara kwani ina mchango mkubwa na unaweza kuongeza Pato la Taifa ikiwa itasimamiwa ipasavyo kwa maslahi ya nchi. Penye rupia penyeza rupia. Mfano, mwaka 2016/2017 kuliidhinishwa fedha za miradi ya maendeleo shilingi bilioni mbili na zikatolewa shilingi milioni 156.6 sawa na asilimia nane kwa fedha za ndani na nje wakatoa asilimia 82. Hali hii tunahitaji mabadiliko makubwa kwani sisi ndiyo wenye uchungu na haya maendeleo, kilio na mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio yetu sasa ni kwa Wizara hii pamoja na upana wake, lakini ina maslahi makubwa kwa nchi na maendeleo kwa watu wake, hivyo bajeti ya mwaka 2017/2018 ya shilingi bilioni 51.8 itatoka hata asilimia 75, kwani tunahitaji kwenda kwenye nchi ya viwanda na uchumi wa kiwango cha kati na mafanikio yake mengi ni ya muingiliano na Wizara kadhaa, hivyo ni mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tunaomba hizo changamoto zilizofuatiliwa na timu ya pamoja za Wizara husika, taarifa hiyo ikafanyiwe kazi kwa mujibu wa taratibu na hatua husika. Ikibidi hadi Bunge tuletewe ili tuweze kufanya marekebisho kwa lengo la kuondoa malalamiko ya wananchi wetu na haya matope tunayopakana viongozi wa kisiasa na Kiserikali.

Mheshimwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Nianze kwa kuipongeza Wizara kwa hotuba nzuri yenye ufafanuzi unaoeleweka kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori *(TAWIRI)* imekuwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa wataalamu wa kutosha, ninashukuru hotuba imelitambua pia suala hili ni imani yangu kuwa Serikali itaongeza wataalam ambao wengi wapo mitaani hawana kazi na wengi wao pia ni vijana ambao wamekuwa wakihangaika kutafuta kazi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hiyo ya ukosefu wa wataalam wa kutosha, bado taasisi hii ya *TAWIRI* inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa vitendea kazi, suala ambalo ni muhimu katika kukamilisha majukumu ya taasisi. Pamoja na hilo bado vitendea kazi vilivyopo ni vichakavu na hivyo basi nipende kuiomba Serikali kuipa kipaumbele taasisi hii kwa kuipatia fedha za kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hotuba hii na Mkoa wa Mwanza, kwanza kabisa nianze kwa kuelezea masikitiko yangu makubwa kwa namna Wizara ilivyoutenga Mkoa wa Mwanza. Ukipitia hotuba yote toka ukurasa wa kwanza hadi wa mwisho, hakuna sehemu yoyote utakayokuta mpango wa kuboresha, kutangaza au kuendeleza utalii Mkoani Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la aibu sana ukizingatia masuala yaliyopo Mwanza ambayo yangeweza kuvutia watalii wengi na kuliingizia Taifa fedha kupitia utalii. Ni muda mrefu sasa Serikali imekuwa haiuweki Mkoa wa Mwanza kwenye mpango wa kuendeleza utalii nchini, tunajiona kama vile tumetelekezwa na Serikali ukizingatia Awamu hii ya Tano Serikali imebakiza miaka mitatu tu na kwa miaka miwili hii ya mwanzo bado haijaona umuhimu wa utalii wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niikumbushe Serikali kuwa Mkoa wa Mwanza una Hifadhi ya *Saanane Island* ambapo wanyama wengi wapo na kuna kilele kirefu ambacho mtu huweza kuliona Jiji la Mwanza na uzuri wake kwa ujumla. Zipo pia sauti za makumbusho mbalimbali kama Bukumbi ambayo inajenga historia ya dini ya kikristo na muhimu kwa kumbukumbu ya uanzishwaji wa dini hiyo kwa Uganda na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo pia makumbusho ya Kageye ambapo kuna makaburi ya watafiti au *explorers* Frederick Barker ambaye alifariki mwaka 1875 kwa kuugua kipindupindu na Dkt. Junker ambaye alitumwa na nchi ya Urusi kuja Afrika kutafiti nchi za Sudan na Egypt.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kipo pia kituo cha makumbusho cha kabila kubwa kabisa la Wasukuma maarufu kama *Bujora Sukuma Museum* ambapo kuna historia ya *chiefdoms* zote za kabila hilo lililosambaa katika mikoa minne ambayo ni Simiyu, Mwanza Shinyanga na Tabora. Na kila mwaka kituo hiki huandaa tamasha la kitamaduni maarufu kwa jina la Bulabo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka enzi za utoto wangu kijiji changu cha Bujora kilikuwa kinasheheni watalii kutoka pembe mbalimbali za dunia kuja kujionea ngoma za Kisukuma katika tamasha hili la Bulabo na kwa mwaka makumbusho hayo yalikuwa yanatembelewa na watalii sana. Kama sijakosea na kwa ufahamu wangu duniani kuna jiwe moja tu linalocheza na lipo Wilayani Ukerewe. Pamoja na vyanzo hivyo vya utalii bado Mkoa wa Mwanza unapakana na nchi za Uganda na Kenya, ukivuka Ziwa Victoria na kwa kutangaza utalii wa Mkoa wa Mwanza tungeweza kuvutia wengi kutoka nchi hizo na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali ni kuhakikisha kuwa masuala haya ya utalii Mwanza yanatangazwa na ukweli itafika kipindi na sisi tutachoka kuona Serikali inatusahau kila mwaka na huku vijana wa

Mwanza wanahangaika kwa kukosa ajira wakati wangeweza kuajiriwa ama kujiajiri kupitia sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kulitazama ombi langu kwa ukaribu kwani tunapoteza mapato mengi mno kwa kutokujali kuendeleza utalii wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huu naunga mkono hoja.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kuendelea kunipa afya njema hadi leo na kuweza kuwatumikia wapiga kura wangu wa Jimbo la Mchinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuendelea kuorodhesha na kuweka kumbukumbu juu ya matatizo makubwa ambayo wakulima wanakutana nayo kutokana na adha kubwa wanayosababishiwa na tembo, ambao wanatoka mbali katika Mbuga au Hifadhi ya Selous. Mfano, mwaka jana pekee zaidi ya ekari 100 za mazao ya kilimo zililiwa, lakini hakuna hatua yoyote ambayo Wizara yako imeichukua hadi sasa.

Mheshimiwa Waziri, naomba sasa kile kiasi kidogo (kifuta jasho) kiwafikie wakulima wote, lakini mwaka huu ndio kuna tembo wamefunguliwa mlango, wamekuja tembo zaidi ya 20 hadi hivi sasa tembo bado wapo Jimboni wanaendelea kusababisha hasara kubwa kwa mazao ya wakulima. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri jambo hili ulifanyie kazi, ukimya wako katika jambo hili unanikatisha tamaa pia unawaumiza sana wapiga kura wangu.

Mheshimiwa Waziri jambo lingine ni kuhusu ahadi yako ya kuwapatia huduma ya maji wananchi wa Tendegura sehemu ambayo mjusi mkubwa *dinosaur* alipochukuliwa na kupelekwa Ujerumani. Ombi letu kubwa ni kuhakikisha kuwa eneo lile lipatiwe maji na barabara ili watalii wale wanaokwenda kule waweze kupata barabara nzuri na pia huduma za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba kufahamu ni kwa nini basi Wizara yako haitaki hata kulitangaza eneo lile kuwa ni miongoni mwa maeneo muhimu ya utalii ili wazungu na watalii wengine waweze kuja kufanya utalii hivyo Mkoa na Taifa kuweza kupata kipato kinachotokana na utalii huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu, pia kuniwezesha kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. Nichukue nafsi hii kipekee kumpongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mchango wangu kuiomba Wizara kufuatilia vivutio ambavyo vinaonekana vidogo vidogo, lakini vikiwekewa mazingira mazuri, miundombinu na kuvitangaza, vinaweza kuwavutia watalii kuja kuvitembelea na kuiingizia Serikali pesa nyingi na kuinua uchumi wa Taifa letu. Nasema hivi kwa sababu mfano kule kwetu Kyerwa, tuna vivutio vingi ambavyo vikitangazwa vitaingizia Wizara pesa za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maji ya moto ya Omokitagata, maji haya watu wanapoyaoga au wanapokanyaga kwenye maji hayo hupokea uponyaji wa magonjwa mbalimbali. Pia tuna Hifadhi ya Rumanyika Orugundu, tuna maporomoko ya Mto Kagera ambavyo ni vivutio, ninaomba Wizara kuvitembelea na vyenyewe viwe kwenye vivutio vya Taifa ili kuongeza wigo mpana wa utalii kuliko kila wakati wanapelekwa maneo yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa tatizo lilijitokeza kwenye Hifadhi ya Rumanyika Orugundu, kutokana na chanzo cha maji kilicho

kilometa moja ndani ya hifadhi ambacho kilikuwa kinatumiwa na wananchi wa kata ya Bugomora na sehemu ya Kata ya Kibale. Chanzo hiki kimekuwa mkombozi wa wananchi wa kata hizo kuwapatia maji safi na salama, lakini baadae Meneja alivunja kisima hicho kilichojengwa na wafadhili na kuwazuia wananchi kutumia chanzo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumweleza Mheshimiwa Waziri na kuona umuhimu wa kuwapatia wananchi maji safi na salama kwa sababu ndicho chanzo pekee cha kuwapatia maji, Mheshimiwa Waziri aliruhusu wananchi wangu kuendelea kutumia chanzo hicho cha maji, nakushukuru sana kwa kuwajali wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa muingiliano wa wananchi na hifadhi, naomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu wananchi hao hawana chanzo kingine cha kuwapatia maji safi na salama na ili kuendeleza ujirani mwema kati ya wahifadhi na wananchi walio jirani na hifadhi, Wizara ione namna ya kuwasogezea maji ya chanzo hicho karibu na wananchi kwa kutumia chanzo hicho, au kama inawezekana eneo hilo la kilometa moja lirudishwe kwa wananchi kama ilivyokuwa mwanzo, maana chanzo hicho mwanzo kilikuwa kwa wananchi na ndio maana wafadhili waliweza kukijengea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee juu ya hifadhi zetu; hifadhi zetu lazima zitunzwe bila kuingiliwa na kitu chochote. Nchi yetu tunakabiliwa na janga la ukame kwa sababu ya uharibifu wa mazingira, tusipokuwa makini nchi yetu inaelekea kuwa jangwa kwa sababu ya baadhi yetu kutosimama kwenye nafasi zetu tulizopewa kusimamia hifadhi zetu ambazo zilitengwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wafugaji wanakosa maeneo ya kufugia kwa sababu maeneo yaliyotengwa na Serikali yaliachwa bila usimamizi na yakaingiliwa bila kufuata sheria zilizowekwa, ndiyo maana leo hii tunasema Serikali iruhusu hifadhi zetu ziingizwe mifugo, hili siyo sahihi na halikubaliki. Mfano kwangu Kyerwa mwaka 1987 Serikali

ilitenga maeneo ya wafugaji na yakatangazwa kwenye Gazeti la Serikali na kupewa *GN* 620. Maeneo haya yamevamiwa na kubadilishwa matumizi wafugaji hawana maeneo ya kufugia, tunadai Serikali iruhusu mifugo kuingizwa kwenye mapori ya hifadhi zetu, naiomba Serikali kufuatilia maeneo yote yaliyotengwa ili yarudishwe kwenye matumizi ya mwanzo ndipo tutaondoa mgogoro wa ukosefu wa maeneo ya kufugia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kunipa uhai na kuweza kuchangia hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro kati ya hifadhi na wananchi imekuwa sugu na ya muda mrefu. Nilipokuwa Mjumbe wa Bodi ya *TANAPA* ulitayarishwa mpango mkakati wa kutatua migogoro hiyo, watendaji wa *TANAPA* waliainisha maeneo yote yenye migogoro na wananchi, yaliwasilishwa kwenye Bodi ya Wadhamini na maamuzi yalifikiwa kama ifuatavyo:-

(a) Maeneo yenye migogoro na ambayo hayana madhara yoyote kwa hifadhi au ekolojia ya eneo la hifadhi waachiwe wananchi na mipaka irekebishwe.

(b) Maeneo yale yenye migogoro na uwepo wa *human activities* kuhatarisha bionuai na ekolojia ya hifadhi, wananchi washawishiwe kuachia maeneo hayo na Serikali iwape ardhi nyingine na kuwalipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi haya hayakutekelezwa kwa sababu muda mfupi baadae aliyekuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Pinda aliunda Tume ya kuchunguza migogoro yote ya ardhi na kutoa mapendekezo, baadae tena Waziri wa Ardhi naye aliunda Tume kwa jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwa Serikali kushindwa kutoa uamuzi kwa jambo nyeti linalogusa hisia za jamii. Serikali ichukue maamuzi magumu ya kutatua kero hii badala ya kujificha nyuma ya Tume na Kamati zinazoundwa kila mara ili tu isifanye maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro hii sasa na zaidi ya miaka kumi tangu nimeanza kuisikia, ni matumaini yangu kwamba kabla Awamu ya Tano haijamaliza muda wake wa miaka mitano itaacha alama ya kudumu ya kutatua kero hii.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea kuhusu migogoro ya mipaka baina ya hifadhi za wanyamapori au misitu na wananchi; katika Jimbo la Manyoni Mashariki jumla ya vijiji 12 vimepakana na hifadhi za misitu za Kizigo na Muhesi. Vijiji hivi ni Chikola, Chikombo, Mpola, Heka, Azimio, Nkonko, Chidamsulu, Iseke, Mpapa, Simbanguru, Sasilo, Chisinjisa na Imalampaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi katika vijiji tajwa wanalalamikia uhaba wa ardhi kwa ajili ya kilimo, malisho ya mifugo, uchimbaji wa madini na ufugaji wa nyuki. Aidha, wanalalamikia pia kuzuiwa kutumia maji ya mto uliopo mpakani kati ya hifadhi na vijiji. Uhaba wa ardhi umejitokeza badala ya ardhi yao kuchukuliwa na Serikali ulipofanyika upanuzi wa mipaka ya hifadhi za misitu tajwa mwaka 1994.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Muhesi Game Reserve* imeanzishwa rasmi kupitia *GN. Na*. 531 ya tarehe 04/11/1991 na kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 09/03/1994. Muhesi ni hifadhi changa yenye kilometa za mraba 2,000, imesababisha machungu makubwa kwa wananchi katika maeneo haya. Tangazo la kuipandisha Muhesi kuwa *Game Reserve* mipaka yake mipya imeleta madhara makubwa kiuchumi, kwani imechukua maeneo muhimu kama eneo muhimu la kilimo cha mahindi liitwalo Chiumbo na eneo la Machimbo ya dhahabu aina ya *Alluvial* yaliyogunduliwa mwaka 1991. Hii ni dhahabu bora ambayo haijawahi kuonekana na kuchimbwa mahali

pengine katika nchi hii rejea Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania ya1992.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo au vitongoji vingine vilivyochukuliwa ni pamoja na Chosola, Msisi, Ilevelo, Machocholoni, Mkindilya, Chigugu, Ngongolelo na Chibwee. Aidha, maeneo haya yaliyochukuliwa yalitegemewa sana katika malisho ya mifugo, ufugaji wa nyuki na vyanzo vya maji safi ya kunywa binadamu na mifugo katika mito ya Muhesi na Kizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko mengine ni unyanyasaji, utesaji na udhalilishaji unaofanywa na Askari *Game Reserve* dhidi ya wananchi. Naambatanisha na taarifa ya malalamiko ya wananchi yenye kichwa cha habari; "Yah: Malalamiko ya wanananchi kuhusu migogoro ya mipaka baina ya vijiji 12 na Hifadhi za Muhesi na Kizigo na manyayaso ya Askari wa hifadhi dhidi ya wananchi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko haya yaliwasilishwa na wananchi 18 kutoka Jimbo la Manyoni Mashariki wakiongozwa na Mbunge wao Mheshimiwa Daniel Mtuka walipokutana kwa mazungumzo ya ana kwa ana ofisini kwao Dodoma. Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii *Engineer* Ramo Makani tarehe 27/05/2016 mchana na Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Tate Ole Nasha tarehe 27/05/2016 mchana. Tunasikitika hadi leo hatujajibiwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba wananchi wangu bado wanasubiri majibu.

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja iliyotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Wizara kwa kuainisha mambo mengi kwa ufasaha, lakini changamoto kubwa ambayo naiona ni migogoro kati ya mipaka ya hifadhi na wananchi (vijiji). Naomba Serikali ishughulikie kwa

umakini sana tatizo hili. Mfano, katika Wilaya ya Nanyumbu kuna mgogoro katika vijiji vya Marumba kwenye vitongoji vya Nambunda na Namaromba na kijiji cha Mbangara Mbuyuni, kitongoji cha Wanika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi hawa wamekuwepo hapo kabla ya uhuru wa nchi hii lakini wananchi wamekuja kujua kuwa vitongoji hivyo vipo ndani ya hifadhi baada ya muda mrefu sana, takribani kama mwaka 2014. Hali hii inafanya wananchi kuchukia Serikali wakiamini kuwa wanaonewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ikaone hali halisi ya vijiji hivyo na ikiwezekana tuwaache wananchi ili waendelee na kazi, kuwaondoa tutawapeleka wapi? Gharama za ujenzi wa nyumba na mali mbalimbali nani atalipa? Naomba sana Serikali itatue haraka tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu wa maandishi katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na migogoro ya mipaka kati ya wafugaji na wakulima (vijiji). Kumekuwa na migogoro ya mipaka ya muda mrefu kati ya hifadhi zetu na wafugaji na wakulima ambao wako jirani na hifadhi. Migogoro hii imekuwa kero kubwa sana hata kusababisha madhara makubwa sana kwa wananchi, kupigwa risasi na askari wa hifadhi na kusababisha vifo vingi vya wananchi, wanawake wengi kubakwa na askari wa hifadhi. Katika kata za Aya Mango, Gedamara na Gijedabung' walibakwa hadi kufa na mpaka sasa Wizara haikushughulikia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ifanye mpango wa haraka wa kumaliza migogoro hii katika vijiji vya Gijedabung', Aya Mango, Gedamara, Maweni, Mdori, Nkaiti, Mwada - Kisangaji na Sangaiwe ambao umedumu

kwa takribani miaka kumi sasa. Kwa sasa hali ya mahusiano ya wananchi na wafanyakazi wa hifadhi ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria ya kulipa fidia na kifuta jasho, ni jambo la kawaida sana na la hatari sana kwa Wizara hii kwani mpaka sasa pesa inayotolewa kama kifuta jasho ni ndogo kwa waathirika walioathiriwa na wanyama. Kwa mfano, tembo kuharibu mazao, kuua watu, simba kuua watu na kukamata wanyama wafugwao. Naomba Wizara iangalie namna ya kuongeza kifuta jasho hicho kwani madhara ni makubwa sana ambayo haiendani na hiyo shilingi milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Utunzaji wa Mazingira *(EMA)* na Sheria ya Ardhi kuhusu mita 60 kutoka katika kingo za mito na bahari.

(i) Sheria ya Ardhi *(Land Act 4/5 1999)* inaeleza juu ya mita 60,
(ii) *Land Survey (Act Cap 324 RE. 2002);* na
(iii) *Planning Act (No. 8 2007).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mazingira ya mwaka 2000 kifungu namba 57 imeelezea mambo haya ya utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tuliyonayo pamoja na sheria hizi ni nyingi sana, kumekuwa na uharibifu unaotokana na mmomonyoko wa ardhi katika maeneo mengi, hasa katika maeneo ya ukanda wa Bonde la Ufa. Kunapotokea hali hiyo ya tendo la asili la ardhi kumomonyoka, kingo zinasogea na zile mita 60 zinapungua, wakazi wa maeneo husika kusumbuliwa kuondolewa katika maeneo hayo, Wizara inajipangaje kuelimisha wananchi kuhusu madhara yatokanayo na mmomonyoko wa ardhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri; Wizara iandae utaratibu wa kujenga mahusiano mazuri katika kutangaza utalii na hifadhi zetu kwa kushiriki shughuli za kijamii katika maeneo yote yenye hifadhi. Kwa mfano,

kujenga vyumba vya madarasa (shule), kujenga zahanati, huduma za maji, kuanzisha timu za mpira, michezo ya riadha na mashindano ya mavazi ya asili ili jambo hili liwe chanzo na mwanzo mzuri kwa Wizara hii kuwa na mahusiano mazuri na jamii inayowazunguka. Hili ni jambo muhimu ambalo litajenga mahusiano makubwa mazuri na kuwajengea uwezo mpana na uelewa juu ya hifadhi zetu, faida za hifadhi zetu kupitia huduma wanayopata kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii. Ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelalamika sana hapa Bungeni juu ya mateso na maumivu yanayosababishwa na utendaji mbovu wa baadhi ya watendaji wako na hasa *Game Rangers.* Wilaya ya Kaliua na Jimbo la Kaliua imezungukwa na hifadhi, zaidi ya vijiji 30 vimesajiliwa kisheria, Serikali imepeleka huduma muhimu kama shule, zahanati na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali imeunda Tume kuangalia namna ya kutatua tatizo sugu la migogoro ya ardhi na hifadhi, Askari wa Wanyamapori na Misitu wamewachomea nyumba, vyakula, mazao wananchi wa Kagome, Lumbe, Usinga, Luhembe - Iga na kuwaacha hawana chochote. Watu wa misitu kuweka *beacon* za mipaka kati ya wananchi na hifadhi kwenye maeneo hayo hadi kwenye nyumba za wananchi bila kuwashirikisha kwa lolote. Wanaingia, wanawapiga, wanawatupia vitu nje, wanaweka alama *(beacon),* wanakamata mifugo ya wananchi na kupiga mnada, wanakuja na wanunuzi wanawaacha wananchi maskini hana hata ndama wala mbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapora vitu vya wananchi na kwenda kuuza ikiwepo simu, *solar panel,* pikipiki, baiskeli, kuku, majembe ya kulimia kwa ng'ombe.

Askari wa Wanyamapori wanakwenda kijiji cha Shela, kata ya Usenye, wanachukua mifugo katikati ya kijiji na kuwaswaga kupeleka hifadhini na kuwapiga faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha wanyamapori kilichopo eneo la Kagome, Lumbe, kata ya Zugimlolo, askari *(Games)* walioko pale wote ni wezi, wanawafilisi wananchi. Mheshimiwa Waziri aeleze Bunge hawa *Games* wanapewa kazi ya kulinda wanyamapori au kupora mali za wananchi na kupiga minada mifugo ya wananchi, kuuza majembe, *solar panel* za wananchi, simu na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vilivyosajiliwa ndani ya hifadhi vilipewa vyeti vya usajili wa vijiji vyao. Maafisa Wanyamapori walivichukua vyeti hivyo kutoka vijijini tangu mwaka 2014 na mpaka leo hawajavirudisha. Waziri aeleze vyeti hivyo viko wapi na lini vitarudishwa kwenye vijiji hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ieleze kwa nini inasuasua kurekebisha gharama za *concession fee* za hoteli zilizopo ndani ya hifadhi zetu ziendane na hali halisi ya sasa. Ni lini hasa *fee* hizo zitafanyiwa marekebisho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Uanzishwaji wa Hifadhi ya Ngorongoro imepitwa na wakati na inahitaji maboresho ili kuendana na hali ya sasa. Ni lini italetwa hapa Bungeni turekebishe? Hifadhi ya Ngorongoro imekuwa inawahudumia wananchi wanaoishi ndani ya hifadhi kwa chakula, elimu, afya na kadhalika, Serikali itaweza kufanya hilo jukumu kwa muda wote? Kwani watu wanaongezeka na huduma inaongezeka mwisho jukumu la hifadhi litapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu mingi ya asili imeteketea kwa sababu ya ukataji wa miti kwa kuchoma mkaa. Wanaokata mkaa hawapandi miti hata mmoja, pamoja na kuwa malundo ya magunia na mikaa imejaa barabarani na viongozi wanaona, hakuna juhudi za kuwaelimisha wapande miti na kuwaelimisha kuhusu mkaa

endelevu. Ni mikakati gani ya Serikali inafanya kupunguza matumizi ya mkaa na kuokoa misitu yetu?

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na Kiti chako, napenda kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu Mji wa Mikindani. Mji huu ni wa kale wenye majengo mengi na historia kubwa ya asili tangu wakati wa miaka *200 BC.* Mji huu umeachwa na historia hii ya pekee nchini inatoweka bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu *Trade Aid.* Kuna taasisi ya Kiingereza inaitwa *Trade Aid* ambayo ni *charity group* inayofanya kazi ya kuangalia baadhi ya majengo kwa maslahi yao binafsi na sio Taifa kama Taifa. Kampuni hii ya Kiingereza wanakarabati baadhi tu ya majengo na kutangaza nje ya nchi, kwa bahati mbaya kila kinachokusanywa ni chao kwa kigezo kuwa wanasaidia jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusaidia jamii ni jambo jema, lakini Serikali lazima ikarabati majengo ya kale ya Mikindani sambamba na kujenga kituo cha watalii Mtwara ili kuvutia watalii kufika Mtwara Mjini eneo la Mikindani. Ukikarabati majengo haya na kujenga vivutio vingi ni wazi kwamba vijana wetu watapata ajira kwa kuhudumia wageni mbalimbali na hivyo kuondoa umaskini Mtwara Mjini na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu ukarabati wa jengo la miaka 100. Kuna jengo ambalo linasemwa limekarabatiwa lakini jengo hili kubwa na muhimu halijakarabatiwa bali limezibwa milango tu. Wito wangu kwa Serikali, Waziri aje Mtwara – Mikindani kujionea hali; jengo hili muhimu likarabatiwe na Serikali siyo kuiachia *Trade Aid* na *Mikindani Tourist Center* ijengwe Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, utalii wa Kituo cha Mikutano Arusha *(AICC). AICC* Arusha ni nguzo muhimu ya watalii wanaokuja kwa ajili ya mikutano nchini. Kupitia kituo hiki cha *AICC,* Serikali inakusanya pesa nyingi sana bahati mbaya pesa hizi zinarudishwa kwa Mkurugenzi wa *AICC* na kufanya ukarabati ambao hauko sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *AICC* wamekarabati Ukumbi wa Simba kwa shilingi bilioni 3.5 lakini wamejenga majengo marefu yenye ghorofa sita kwa shilingi 1.8. Ukarabati wa Ukumbi wa Simba umetumia pesa vibaya kuliko kujenga jengo kubwa jipya. Wito wangu *CAG* aende akakague ukarabati huu wa *AICC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu sheria iliyoanzisha Shirika hili la *AICC* ni kuendeleza ujenzi wa kumbi nyingine za mikutano nchini. Kama ukarabati tu unazidi ujenzi, sidhani kama tunaweza kujitanua katika utalii wa mikutano. Naomba *CAG* akakague ukarabati wa *AICC* Ukumbi wa Simba. Ahsante.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kuhusu hali ya utalii nchini. Sekta ya utalii ni moja kati ya sekta ambazo huliingizia Taifa mapato makubwa na pia hutupatia fedha za kigeni. Pamoja na umuhimu wake bado bajeti yake ni ndogo, lakini pia Serikali haijakuwa na mipango mizuri kiasi kwamba ushindani kati yetu na nchi jirani unakua siku hadi siku. Kwa kukosa mipango mizuri, imefikia leo Tanzania pamoja na mbuga nyingi na kubwa, mapango, maporomoko, maziwa, wanyama wengi, ndege, wadudu na samaki, mapato yetu bado hatuifikii Kenya, Ethiopia, Botswana, Zambia, *South Africa,* Rwanda na kadhalika, bado mapato yetu ni madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikishe wadau mbalimbali katika kutoa mchango

wa mawazo katika sekta ya utalii ili yatapatikane mawazo mengi yenye manufaa na yataisaidia Serikali. Kwa mfano, *advertisements* (matangazo), bado Tanzania hatujatangaza utalii wetu katika mataifa ya nje kiasi cha kutosha ukilinganisha na washindani wetu Kenya, Uganda, Malawi, Namibia, Rwanda na kadhalika. Tuwatumie Watanzania wanaoishi nje *(diaspora)* washirikiane na Mabalozi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunadhani utalii ni wanyamapori na hoteli tu, sivyo. Katika ukurasa wa 12 – 59 wa hotuba ya Waziri anazungumzia wanyamapori tu. Je, Makumbusho, *Olduvai Gorge, Tongoni Ruins, Amboni Caves,* Michoro ya Kondoa Irangi, Magofu ya Pangani, *Amboni Sulphur Bath,* yote haya tunayaacha bila ya kuyatangaza. Nashauri sasa tufanye matangazo ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tanga na utalii; Tanga ni mji wa kihistoria, una majengo mengi ya kihistoria, una bandari, *railway* na hata makazi ya kale, kuna visiwa vilivyokuwa na magofu na makaburi yaliyodumu kwa zaidi ya miaka 200. Hivyo, naishauri Serikali itenge eneo la Posta na Uhindini kuwa eneo la kihistoria kama lilivyo eneo la *Stone Town,* Zanzibar. Tanga tunayo Mapango ya Amboni *(caves), Tongoni Ruins* na *Amboni Sulphur Bath.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *sports tourism* kama *football, basketball, netball, golf, cricket, etc* ni michezo ambayo nchi za wenzetu wanaitumia na kuingiza mapato kwa kufanya mashindano ya kimataifa, mfano *Dubai Open, golf* umekuwa ni mchezo mkubwa unaoingiza fedha nyingi katika sekta ya utalii na pia *surf (swimming and fishing)* ni michezo ambayo tukishirikiana na sekta binafsi tutaweza kufanya vizuri kwa kuwa wenzetu wa nchi za Kenya, *South Africa* na Mauritius wanafanya vizuri, tusibaki nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mali kale na makumbusho, hadi leo mjusi wa Tanzania *dinosaur* yupo Ujerumani na anaiingizia fedha za kigeni nchi ya Ujerumani. Kwa nini asirejeshwe kama fuvu la Mkwawa na awekwe

katika Makumbusho ya Taifa? Tunahitaji mjusi wetu arejeshwe Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna 1424km$^3$ za bahari kuanzia Jasini *(Mkinga District - Tanga)* hadi Msimbati (Mtwara), amegundulika samaki kisukuku *(coelecanthy)* ambae alikosekana zaidi ya miaka 80 iliyopita, Tanga – Kigombe (Muheza) amepatikana. Taasisi za kimataifa kupitia Mradi wa *Coast Zone* wameweka kambi na wanaendelea na kukusanya taarifa zake. Je, Wizara wana habari? Habari ndiyo hiyo.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii idhibiti mauaji ya tembo ambao wapo mbioni kupotea kabisa. Tembo wameendelea kuuawa mwaka hadi mwaka hivyo tutapoteza watalii wengi kutokana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ya Maliasili na Utalii iwazuie askari wake kuwapiga risasi na kuwaua wananchi wanaoingia maeneo ya hifadhi. Kuwaua wananchi ni kosa kubwa sana, ni bora hatua kali zichukuliwe kwa askari hawa watovu wa nidhamu. Naomba kuwasilisha.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika hotuba ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Utalii Tanzania bado inalo jukumu la kuutangaza utalii ndani na nje ya Tanzania. Katika ukurasa wa 100 - 107 katika hotuba ya Waziri imeeleza kwa kirefu namna ambavyo bodi imefanya kazi kuutangaza utalii wa Tanzania ndani na nje kupitia matamasha makubwa yaliyofanyika ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mwanza ni Jiji ambalo limepewa jina la *Rock City,* hii ni kutokana na mkoa huo kuwa na vivutio vingi vya mawe na majabali yanayoufanya mji huo kupendeza na kuvutia kijiografia. *Bismarck Rock* ni jiwe kubwa linalopatikana ndani ya maji

ya Ziwa Victoria, jiwe hili lilipewa jina la *Counselor* maarufu wa Ujerumani. Kivutio kingine ni mawe yenye maumbile tofauti tofauti yaliyobebana yanayopatikana katika Milima ya Miama, Wilayani Ilemela, Mkoani Mwanza. Huko pia kuna *beach* nzuri zilizotulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kivutio kingine ni mawe yanayocheza yanayopatikana katika Kisiwa cha Ukara, Wilaya ya Ukerewe. Mawe hayo yanavutia kwa kuwa hucheza mara yanapoimbiwa nyimbo za kimila na wazee wa kimila. Kivutio kingine ni Nyumba ya Makumbusho ya Bujora. Nyumba hii inaonesha maonesho ya mila na desturi za kabila kubwa Mkoani Mwanza ambalo ni Wasukuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivutio vingine ni *Saanane Island* na *Kirejeshi Game Reserve* ambapo wanyama mbalimbali kama vile swala, chui, twiga na simba huonekana kwa urahisi. *Serengeti National Park* pia inapatikana kwa umbali wa saa mbili tu kutoka Uwanja wa Ndege wa Mwanza, hivyo, kuwa rahisi kufika. Kivutio kingine ni Mnara wa *MV Bukoba* ambapo watu hutembelea na kutoa heshima zao kwa *victims* waliozama na kupoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mwanza katikati ya mji kuna mti uliotumiwa na Wakoloni wa Kijerumani kuwanyongea wahalifu. Hivyo basi, niishauri Serikali kupitia Bodi ya Utalii Tanzania kwa kushirikiana na *television* zote nchini pamoja na majarida ya mashirika ya ndege hapa nchini kutangaza Mji wa Mwanza kama mji wa kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote, naunga mkono hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za Mkoa wa Tabora ni kama zifuatazo:-

(i) Ukarabati wa jengo la utawala na maabara katika Chuo cha Nyuki Tabora ili kiwe cha kisasa;

(ii) *OC* kwenda kwa wakati, pia malipo ya wazabuni yaangaliwe;

(iii) Kutangaza Chuo cha Nyuki, nchini na nje ya nchi ili kupata wanafunzi wa kutosha; na

(iv) Kuanzisha mafunzo mbalimbali ya ufugaji nyuki kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania *(TAWIRI)* kituo cha Tabora kwa miaka mingi hakifanyi kazi na kilianzishwa kwa ajili ya tafiti za nyuki, mazao ya nyuki na mizinga yenye tija na kusababisha wataalam na watumishi kukaa bila kazi. Kwani gari liliondolewa katika kituo hicho, pia mpaka *computer* zimetolewa, nini hatima ya Kituo hicho cha Utafiti Tabora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Mheshimiwa Waziri afike Tabora kujionea haLi halisi na Mkurugenzi husika ili kutatua changamoto hizo. Nakushukuru.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara hii kwa masikitiko makubwa juu ya kero ya wananchi wa Jimbo langu juu ya migogoro ya mipaka kati ya Hifadhi ya Akiba ya Uwanda na vijiji vya Kilangawana, Mpande, Maleza, Legeza, Kapenta, Ngomeni na Nankanga kwa kuweka mipaka hadi katika makazi ya wananchi pamoja na mashamba yao, jambo ambalo limeleta mgogoro mkubwa hadi kuhatarisha amani katika eneo hilo.

Naomba Mheshimwa Waziri afike kutafuta muafaka wa pande zote mbili. Nimemuomba Mheshimiwa Waziri mara kadhaa afike katika maeneo hayo, naomba majibu. Mheshimiwa Waziri kama huwezi kwenda wananchi wamejiandaa kuja ofisini kwake kwa maandamano na tayari wamechangishana fedha za safari hiyo.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa utekelezaji wa majukumu yao kwa kiwango na cha kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali katika kukubali ombi la wakazi wa Wilaya ya Malinyi, Ulanga na Kilombero katika kufanya marekebisho ya mipaka ya Pori Tengefu la Kilombero kwa kushirikisha wananchi. Wakazi wa Wilaya hizo tatu tunafahamu umuhimu wa kuhifadhi Bonde la Kilombero na ardhi yake. Ushirikiano wanaopewa wananchi na wataalam wa wanyamapori katika kurekebisha mipaka sio rafiki kabisa kwani wanayokubaliana au kujadiliana na viongozi wa vijiji na kata au wananchi hayatekelezwi. Wananchi bado wana mahitaji ya kutengewa (kupewa) ardhi ya nyongeza kutokana na hali halisi ya kuongezeka kwa matumizi ya ardhi kwa kilimo, mifugo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kubwa ya wananchi hao ni kwamba ile ardhi ya *buffer zone* ni kubwa (pana sana) kwani kuna maeneo yana upana wa kilometa 8 -12. Ombi letu wakazi wa Malinyi, Ulanga na Kilombero upana wa eneo (ardhi) hiyo ya *buffer zone* ungepunguzwa iwe na upana wa angalau kilometa 1 au 2 tu kati ya ardhi za vijiji na kiini cha Pori Tengefu la Kilombero. Ardhi hiyo itakapoongezeka kwa wakazi itatupunguzia kwa kiasi kikubwa migogoro baina ya hifadhi, wafugaji na wakulima. Ahsante.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, sekta hii muhimu kwa uchumi wa Taifa. Kiwango cha kutangaza utalii kipo chini hali ya kuwa na tozo nyingi zinazotozwa zikidaiwa matumizi yake ni *promotion* kupitia Bodi ya Utalii mfano watalii wanalipa dola moja *per head* wanapolala kwenye hoteli *per night* na zinapelekwa Bodi ya Utalii. Matozo mengi yanafanya watalii wengi kukimbilia

Kenya na mpaka Kenya wana-*captalize* Mlima Kilimanjaro ni wao na watalii wanafikia kwao *due to number of charges* zisizo na sababu. Katika eneo la matangazo mfano ndege za Kenya zimeandikwa Kilimanjaro na zinakwenda nchi nyingi duniani, kwa hiyo, ni rahisi kuwaaminisha wageni kuwa Mlima Kilimanjaro upo Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwe na *strategies* nzuri za ku-*promote* utalii na kuondoa siasa kama za kusema tunanunua ndege kubwa ya *Dreamliner* itakayoruka Ulaya mpaka Kilimanjaro ikiwa na watalii *is this a strategy?* Hapo hapo mkoa wenye utalii umejaa siasa za chuki mpaka kukera wageni, kwa mfano *RC* kaweka mtu ndani muda mrefu kwa zaidi ya miezi minne bila dhamana kwa kesi ambayo ina dhamana, yote haya wageni wanayaona na wanatushushia *value.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA* wafanye kazi na kupunguza matumizi yasiyo na lazima. Kwa mfano kuna Mawaziri walikuwa wanatumia mali za *TANAPA* kama magari, ndege kama mali zao binafsi na zikatumika mpaka kwenye kampeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Faru John na Faru Fausta ambapo Faru Fausta gharama za matunzo yake ni kubwa wakati matukio ya ujangili ni makubwa na yanaendelea. Hata taarifa ya Faru John namna alivyopotea inajulikana ila imefunikwa funikwa na imepita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoteli nyingi za kigeni zina-*charge* gharama kubwa na masharti yake ni magumu. Hoteli hizi zinawalenga hata wazawa ambapo huendi bila *appointment* na ndiyo hao faru wanapotelea kwenye hizo hizo hoteli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maliasili na nishati, matumizi ya mkaa yanaendelea kuongezeka nchini na hii inatokana na kupanda kwa gharama za gesi. Serikali huwezi kuhimiza matumizi ya nishati mbadala wakati gesi na umeme gharama yake ipo juu. Makaa ya mawe,

wawekezaji kama Dangote amepewa achimbe kwa nini yasitumike pia kwa wazawa kama nishati ili waache kuchoma mkaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro maeneo ya hifadhi namna ambayo wawekezaji wanapewa vipaumbele kuliko wazawa na mwisho huwa ni migogoro isiyoisha. Wawekezaji wana viwanja vidogo vya ndege ndani ya hifadhi mfano Serengeti wanavifanyia nini kama siyo vinatumika kuhujumu uchumi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi ambayo ipo Mtwara tulihakikishiwa kuwa itakuwa muarobaini wa mambo mengi ikiwemo matumizi ya nyumbani ili kunusuru ukataji misitu, ikiwa ni pamoja na matumizi ya gesi ya majumbani na bei itakuwa chini. Kuna sehemu kama Dar es Salaam yalitandazwa mabomba ya gesi mitaani lakini hakuna lolote, mkaa tani na maelfu ya tani kila siku yanapelekwa Dar es Salaam.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *we must go out of the box,* si sawa kwa mifugo kukaa hifadhini lakini ni wajibu wa Serikali kuwapanga wakulima na wafugaji ili watumie vizuri maeneo walionayo na hivyo kutolazimika kuingia hifadhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichopo Wizara na Wakuu wa Mikoa wamejikita kwenye operesheni na kufilisi bila kuiona hii kama fursa ya kugeuza mitazamo ya wafugaji na kushirikiana na wawekezaji ili mifugo iwe fursa. Mfano, Wilaya ya Biharamulo 54% ya eneo ni hifadhi, 46% maeneo ya watu, hata hivyo 46% *is under-utilized* kwa kuwa haikupangwa. Tujipange na inawezekana tuachane na mambo ya operesheni haya kwani yanaishia kutengeneza mianya ya kuonea watu na rushwa. Fikeni Biharamulo muwasikilize wananchi itawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maliasili na Utalii ni Wizara moja lakini kuna idara au mashirika mbalimbali kama *TANAPA*, Misitu, Ngorongoro, *TAWA* na kadhalika. Watumishi

wanalalamika kuwa tofauti ya mishahara ni kubwa mno hata kwa watu wenye vigezo vinavyofanana. Wanaolalamika ni wa Serikali Kuu na Idara ya Wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Katavi ni muhimu sana, inatakiwa kuwekewa mkakati wa kuboresha miundombinu kwani barabara ni chache. Pia hakuna sehemu za huduma kwa watalii kama simu, hoteli za hadhi ya nyota tano, barabara za ndani na visima vya upepo kukabiliana na ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza ujirani mwema *(corporate social responsibility)*, hifadhi za Taifa husaidia kero mbalimbali. Hivyo basi, Hifadhi ya Katavi ina mpango wa kuchimba visima vitatu vya maji ambapo wananchi wanatakiwa kuchangia 30% ya gharama. Tunaomba Serikali ibebe mzigo/gharama zote za mradi ili kumsaidia mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tanzania Tourism Board* inahitaji fedha za kutosha ili kuweza kufanya kazi ya kutangaza utalii wa aina zote uliopo katika nchi yetu. Serikali lazima ihakikishe kuwa inatoa pesa kama sera ilivyo ambapo 3% ya mapato ya *TANAPA* na Mamlaka ya Ngorongoro yawe yanawasilishwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za utalii. Tanzania imekuwa na kiwango cha chini cha huduma katika utalii kutokana na kutokuwa na *package* nzuri kulingana na uwezo wa watu mbalimbali. Hivyo, *TANAPA* na Serikali ni muhimu kuhakikisha kuwa watoa huduma wanakuwa na elimu na uwezo wa kutosha pia kuwe na *standard* zinazofuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hifadhi za misitu; maeneo mengi ya Tanzania yamevamiwa na wafugaji hivyo tunahitaji Serikali kufanya mpango bora wa matumizi ya ardhi na kudhibiti uharibifu wa misitu. Hivyo, Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza maeneo kiasi ili kuondoa

migogoro. Mfano Halmashauri ya Nsimbo tunahitaji maeneo katika Kata za Ugala, Sitalike, Kange na Kapalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZUBEDA H. SAKURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mchango wangu katika mjadala wa Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tunduru ni mojawapo ya Wilaya kongwe nchini ambazo zimekuwa na matukio ya muingiliano wa shughuli za binadamu na wanyamapori hasa tembo. Baadhi ya matukio yamepelekea kuwepo na mauaji ya tembo hao na kisha wananchi kuwaondoa pembe na kugawana nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni zaidi ya tembo 20 walivamia vijiji vya Wenje vilivyo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji wakitokea Msumbiji (Aprili, 2017) na wananchi waliwaua na kisha kuondoa meno yao na kugawana nyama. Vilevile wengine walivamia kijiji cha Jakika wakitokea Pori la Akiba la Selous na kuharibu zaidi ya ekari 50 za mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tukio hilo, zaidi ya watu watano walikamatwa. Pamoja na kuwa kuna muingiliano wa vijiji zaidi ya vitano na Pori la Selous na tembo hao wamekuwa wakisumbua zaidi, ipo haja kuweka mikakati madhubuti itakayoweza kuwadhibiti tembo kuingia katika vijiji hivyo na pia kuwashirikisha kwa karibu wananchi ili kupunguza mauaji ya tembo pale wanapoingilia maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shehena ya meno ya tembo; Tanzania inaonekana mbele ya Jumuiya ya Kimataifa kama Taifa ambalo halitambui kwamba kushamiri kwa vitendo vya ujangili ni pamoja na kutaka kuuza shehena ya meno ya tembo. Ikumbukwe kuwa kadri siku zinavyoenda idadi ya tembo nchini inapungua huku ikichochewa pia na kutokuwa na mbinu na mikakati madhubuti ya kukomesha

vitendo vya ujangili. Mkoa wa Ruvuma ni moja ya mikoa inayoongoza kwa matukio ya kukamatwa kwa shehena za meno ya tembo na nyara za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Serikali ya Tanzania bado imeshikwa na kigugumizi licha ya kuwa na idadi kubwa ya matukio 11,000 ya mauaji ya tembo kila mwaka, kutekeleza ahadi yake ya kuteketeza tani zipatazo 90 za shehena ya meno yaliyohifadhiwa katika maghala yake baada ya kuzikamata. *CITES* iliweka msimamo wa nchi zenye shehena kuteketeza shehena pamoja na kulifunga soko la China ili ku-*discourage* ujangili. Kwa masikitiko makubwa, Tanzania bado inashikilia kuuzwa shehena hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Mstaafu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete aliwahi kusema katika kongamano nchini Uingereza kuwa imesitisha na kufuta msimamo wake wa kuuza shehena ya meno ya tembo. Muda mrefu sasa umepita tangu ahadi hiyo itolewe. Je, Serikali inatueleza ni lini itateketeza shehena hiyo kama walivyofanya majirani zetu Kenya? Pamoja na hayo, ipo haja ya Serikali pia kupinga kwa vitendo uuzaji wa meno na pembe za ndovu waliokufa *naturally* ili kuua kabisa soko la ndovu duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utangazaji wa vivutio vya utalii; Tanzania imebarikiwa kuwa na vivutio vya utalii lakini havijatangazwa vya kutosha ili kuwavutia watalii wa ndani na nje ya nchi. Nimeona msanii wa kike Vanessa Mdee ni mmoja wa wasanii ambao wametumiwa na Afrika Kusini kutangaza vivutio vya nchi hiyo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwatumia wasanii maarufu/mashuhuri na Watanzania kama mabalozi wa kutangaza vivutio vya utalii nchini? Pia ni lazima kuhakikisha Balozi zetu katika mataifa mbalimbali zinaandaa utaratibu wa *economic diplomacy* ili kuhuisha sekta ya utalii katika kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongeza ajira kupitia sekta ya maliasili na utalii; vijana wengi hawana ajira nchini na hii imetokana na mwenendo wa dunia katika ajira

lakini hii isisababishe Tanzania kupoteza lengo la kukuza ajira hasa kupitia sekta hii muhimu. Leo sekta ya utalii inakua lakini ajira zinazopatikana katika sekta hii ni chache sana. Hata vyuo vinavyotoa kozi za utalii nchini havikidhi hitaji kubwa la watu kwenye sekta ya utalii. Ipo haja ya kuwa na *integration of national plans* katika kutatua tatizo la ukosefu wa ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utunzaji wa mali kale katika kukuza utalii; ipo haja ya Serikali kuwekeza ipasavyo katika kutunza mali kale ili kukuza sekta ya utalii. Mji Mkongwe Zanzibar, Isimani, Bagamoyo na maeneo mengine ni mojawapo ya maeneo yenye malikale lakini havijatunzwa na ku-*maintain status* zake (hadhi zake) ili kuvutia watalii wengi zaidi kutokana na historia za maeneo hayo. Miji hiyo ni ya kihistoria, Wizara ishirikiane na Wizara ya Utamaduni ili kuhakikisha maeneo hayo yanatunzwa ili kuongeza Pato la Taifa kutokana na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu biashara ya vinyago na utalii; ipo haja ya Wizara kuhakikisha kuwa wachongaji na wasanii wa vinyago hasa katika maeneo ya utalii wananufaika na kazi zao. Ni namna gani Wizara hii inahakikisha kuwa vinyago vinavyochongwa nchini vinanufaisha wachongaji wake na pia Serikali inanufaikaje na uuzaji wa vinyago hivyo? Iwapo Serikali itawekeza vya kutosha kuwasaidia wachongaji hawa itaweza kukusanya kodi na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na wimbi kubwa la wanyama waharibifu katika kata za Ketaketa, Ilangu, Mwayasuga na Chilombora, hasa viboko wanaharibu mazao kwa kiasi kikubwa sana na kupelekea njaa. Afisa Wanyamapori yupo mmoja hawezi kutokana na ukubwa wa eneo.

Naomba mtuongezee maafisa ili kunusuru mazao na kupunguza hali ya wasiwasi kwa wananchi (usalama).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Selous Game Reserve*; kumekuwepo na mgogoro katika maeneo ya kata nyingi hasa Ketaketa, Ilonja, Mbuge na Lukande kwa sababu watu wanazaliana hivyo kuwa na ufinyu wa ardhi kwa ajili ya kilimo na makazi. Nashauri tuweke utaratibu wa watu kulima maeneo ya *Selous* ili watu hawa waweze kujipatia chakula ili kuweza kupambana na maisha kwa sababu tukiwaacha watakosa shughuli ya kufanya matokeo yake wanawinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo kubwa la Ulanga limetengwa kama eneo oevu *(buffer zone)* hivyo hakuna sehemu nyingine ambayo watu wanaweza kulima hivyo kupelekea watu kukosa chakula. Serikali iharakishe mchakato wa kumilikisha kipande cha eneo oevu ili watu wapate maeneo ya kulima ukizingatia watu wengi wameshavamia kiholela bila ya utaratibu kwa kuwa hakuna mwongozo.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Lwanfi Game Reserve* iko Nkasi Kusini, hatujawahi kupata mchango wowote katika shughuli zozote za kijamii licha ya ukweli kuwa vijiji kama nane vimepakana na mbuga hii. Vijiji hivi ni Kasapa, Kiing'ombe, Mlambo, Kilambo, Ngundwe, Mlalambo, Kizumbi, Nkata, Namansi na vinginevyo kote huko tuna shida za kujenga miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo ujenzi wa madarasa, zahanati, nyumba za walimu na shida ya maji tunaambulia vipigo vya mbwa mwizi pale ambapo mwananchi anapokamatwa na mbao moja tu. Tunaamini tuna mchango katika uhifadhi wa *Lwanfi Game Reserve*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ukatili uliopita kiasi, licha ya umuhimu wa maliasili zetu kulindwa na askari wanyamapori lakini sheria hazifuatwi. Askari hawa huchukua sheria mkononi kwa kufanya matendo mabaya ikiwepo kuua, kutesa, kupiga sana na kadhalika. Jambo hili si la kistaarabu, tujaribu mara zote kufuata sheria labda kama mazingira yanahatarisha usalama wa wahifadhi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa misitu ya *TFS;* mamlaka hii kama imezinduka toka kusikojulikana, wameweka mipaka kwenye vijiji vyetu hadi ndani ya vijiji na kufanya vijiji vingine ambavyo vipo miaka mingi kisheria kuonekana havina ardhi kabisa. Maeneo yaliyokuwa yanalimwa na wananchi yametwaliwa na kukosa mahali pa kulima, wananchi wanalima, mnafyeka mazao. Kijiji cha Kasapa, Msitu wa Kalambo ni mfano unaothibitisha hali hii ambayo ni ukatili. Wananchi hutengeneza Serikali, mnawaadhibu namna hii, haikubaliki hata kidogo. Kamati ya kutathmini migogoro ije Nkasi tafadhali.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo, nitoe ushauri kwa Serikali na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulinda na kuhifadhi eneo oevu la *River Malagarasi.* Eneo hili ni *Ramsar Site* chini ya udhamini wa *UNESCO*. Eneo hili limevamiwa na ng'ombe wengi ambao baadhi yao ni wale walioondoshwa huku Burigi Pori la Akiba na Kimisi. Ng'ombe hawa wanahatarisha uhai wa Mto Malagarasi. Chukueni hatua haraka bila kuchelewa ili kuokoa rasilimali hii muhimu kwa Taifa na kimataifa. Bila Mto Malagarasi hakuna Ziwa Tanganyika na bila Ziwa Tanganyika hakuna Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la Msitu wa Taifa wa Makere Kusini maarufu Kagera Nkanda lenye ukubwa wa hekta 97,000; Wilaya ya Kasulu tumeomba hekta 20,000 - 25,000 ili wananchi wapate eneo la kilimo na kufanya shughuli za kufuga nyuki na wanyama wengine. Tunahitaji sasa eneo hili lipimwe upya ili kuhuisha mipaka ya wakoloni (Waingereza) ambao walitangaza msitu huo mwaka 1954. Zaidi ya miaka 60 haiwezekani mambo yawe yale yale wakati idadi ya wakazi imeongezeka mara kumi. Baada ya *re-mapping* hiyo hali ya amani na utulivu itarejea baina ya wananchi na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mbuga ya Hifadhi ya Gombe na Mahale zilizopo Mkoani Kigoma; mbuga hizi ni

mpya, ardhi ni mpya na miundombinu yake ni mipya. Juhudi kubwa lazima ifanywe ili kutangaza vivutio vya pekee vya sokwe wanaopatikana katika mbuga hizo mbili katika nchi yetu. *TTB* wafanye kazi ya kutangaza vivutio hivi kwa juhudi kubwa. *TTB* wanaweza hata kutumia mbinu ya *PPP/TTB Joint initiative*. Taasisi ya Jane Godall watafiti wa sokwe Kigoma wanaweza kushirikishwa pia. Jengeni upya wa fikra katika tasnia hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivutio vipya vya utalii vilivyopo katika Mkoa wa Kigoma ambavyo vinahitaji kutangazwa na *TTB* pamoja na *TANAPA* ni pamoja na:-

(i) Njia ya watumwa ya Kigoma/Ujiji - Tabora - Dodoma - Morogoro hadi Bagamoyo. Hiki ni kivutio kikubwa sana kama kitakuwa *promoted* na *developed*. Njia hii ipo kihistoria, kazi ni kuwa na mkakati wa muda mrefu na dhamira ya dhati ya Wizara hii na *TTB*, tuanze sasa.

(ii) Makumbusho ya Dkt. Livingstone alipokutana na Dkt. Henry Morton Stanley 1871. Jengo la makumbusho lipo limejengwa, likamilike ili lianze kazi. Utendaji kazi wake lazima uende sambamba na *promotion* ya kivutio hiki. Nina hakika eneo hili linaweza kuingiza mapato mengi Serikalini.

(iii) *Cultural tourism* - Kigoma *is rich in cultural activities lets promote this area*. Tuanze sambamba na kutangaza mbuga zetu za Gombe na Mahale.

(iv) Ziwa Tanganyika na fukwe zake, hiki nacho ni kivutio kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TTB* amkeni sasa, njooni na mikakati endelevu.

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuwa na afya njema na kushiriki katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimpongeze Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, Wenyeviti wa Bunge na watendaji wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa pamoja na Baraza lote la Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuwaletea maendeleo wananchi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya Waziri, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Naibu Waziri, Mheshimiwa Injinia Ramo Makani na watendaji wote wa Wizara hii, mfano, katika kupambana na majangili katika hifadhi zetu, kuendelea kutatua migogoro kati ya hifadhi na vijiji vilivyo jirani na hifadhi na kutangaza utalii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha iliyoko umbali wa kilometa 130 kutoka Mjini Iringa ina sifa za kipekee kuliko mbuga zote nchini na katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sifa hii bado haijatoa tija inayostahili kwa Taifa. Miundombinu hasa barabara itokayo Iringa Mjini siyo rafiki kwa watalii wa ndani na nje ya nchi. Ujenzi wa barabara ya lami kutoka Iringa Mjini kuelekea mbugani hadi sasa uko katika kilometa zisizozidi 15 kutoka Iringa Mjini. Siyo rahisi kwa watalii wengi kuvutiwa na safari ya kilometa 115 katika barabara yenye vumbi hivyo tunakosa mapato mengi ambayo yangeweza kupatikana kwa kukosa wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, tunalo jengo la kumbukumbu ya Chifu Mkwawa (Mtwa) liko umbali usiozidi kilometa 3 kutoka Kijijini Kalenga, njia inayoelekea katika kumbukumbu hii haina lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, iboreshe uwanja wa ndege ili ndege kubwa na ndogo ziweze kutua na kuruka jambo ambalo litavutia watalii wengi. Aidha, ujenzi wa barabara ya lami kwenda *Ruaha National Park* uharakishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *TANAPA* iendelee kusaidia maendeleo hasa katika maeneo ambayo vivutio vya utalii vinakopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Maghembe na timu yake kwa kazi nzuri ya usimamizi wa maliasili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walio wengi hawajui umuhimu wa uhifadhi, faida za uhifadhi na kuwa hakuna somo la uhifadhi katika mitaala yetu na hata kwetu sisi Wabunge ni wachache sana waliowahi kutembelea mbunga za wanyama, malikale na kadhalika. Nashauri somo la uhifadhi liingizwe kwenye mitaala ili mtoto wa Kitanzania akue akijua umuhimu wa uhifadhi, kutunza misitu, malikale na kadhalika. Vijana wakiwa mashuleni wajifunze kupanda miti, kufuga nyuki na wawapende wanyama, kwa jinsi hiyo tunaweza kupunguza malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusu uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utalii wa ndani kwa vijana wetu litiliwe mkazo. Kwa kufanya utalii wa ndani vijana watajifunza mengi na kuacha uadui na wanyamapori na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna migogoro ya ardhi na hasa mipaka ya vijiji na Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na kadhalika. Migogoro mingi huchangiwa na Serikali kutokuwa makini, wananchi hawalimi kwa siku moja ndani ya mapori, wanalima kwa miaka kisha wanajenga nyumba bora za kuishi, zahanati na shule bila Serikali kuchukua hatua yoyote.

Ni vizuri Serikali ikachukua hatua mapema wananchi wanapovunja sheria za uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo wangu sioni sababu ya kuwepo kwa *TTB. TTB* haina vyanzo vya mapato, kazi zinazofanywa na *TTB* zinafanywa na *TANAPA* na *NCAA.* Ni halali mashirika hayo kuichangia *TTB? TTB* haiwezi kufanya kazi ipasavyo. Hata hivyo, tulielezwa kwenye semina kuwa vivutio vya Tanzania havitangazwi ipasavyo hii ina maana kwamba *TTB* wameshindwa kazi. *TTB* ni hasara kwa Taifa, ivunjwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Balozi zetu katika nchi mbalimbali kuwepo na kitengo cha utalii kitakachofanya kazi ya kutangaza vivutio vya Tanzania. Kwa kuwa *TTB* hawawezi kwenda kila mahali kutangaza vivutio vya Tanzania, Kitengo cha Utalii kwenye Balozi zetu kinaweza kufanya kazi nzuri yenye manufaa kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wanyamapori wanafanya kazi kubwa na yenye hatari kubwa ya kupambana na majangili, lakini wanalipwa mishahara midogo sana sawa na askari wanaofanya kazi kwenye maeneo yasiyo hatarishi. Pamoja na hayo wanafanya kazi kwa masaa mengi kwa sababu ni wachache. Serikali ieleze ni lini askari wanyamapori wataajiriwa wa kutosha na kupewa motisha ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu ya Tanzania haina mwenyewe, mtu yeyote na kwa wakati wowote anaweza kufyeka miti atakavyo na asichukuliwe hatua yoyote. Nchi zingine duniani mtu haruhusiwi kukata miti bila kibali cha Serikali. Serikali inafanya nini kulinda misitu ya nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna madini ya chokaa yaliyoko mbuga ya wanyama Moyowosi eneo la Kakonko. *TCCIA* na wadau wa maendeleo walileta ombi Wizarani kupitia *DCC* ili kuongeza eneo la

kilometa 15 kuingia mbugani kusababisha eneo lenye chokaa kuwa nje ya mbuga na kuwafanya wananchi wanufaike na chokaa hiyo lakini hadi sasa hakuna majibu yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ijikite katika kutangaza utalii nje na ndani ya nchi. Kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kutangaza utalii hasa nje ya nchi hakitoshi. Nchi ya Kenya wamefanya vizuri kwenye matangazo ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na wimbi la mauaji ya wananchi ndani ya hifadhi kana kwamba wanyama ni bora kuliko wananchi. Hali hii inatupunguzia heshima kimataifa na kitaifa. Uwekwe utaratibu mzuri wa kuhakikisha hakuna raia/mwananchi anayepoteza maisha kwa kukutwa kwenye hifadhi ya wanyama au misitu. Kuua watu marufuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mauaji ya wananchi/raia kuna mifugo inayoingia kwenye hifadhi na kuuawa/kuzuiliwa na hivyo ama kutozwa faini au kuuzwa kwa njia ya mnada ambapo fedha zinakuwa za Serikali. Huu ni wizi wa Serikali. Hata kama wamekosea kuingiza mifugo kwenye hifadhi bado mifugo ni mali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo nyingi kwenye sekta ya utalii; *VAT* iliyoongezwa mwaka jana kwenye utalii kwa mtalii kulipia kulichangia kupunguza idadi ya watalii waliokuja nchini kwani nchi jirani yetu hawana hiyo *VAT* na hivyo watalii wengi kukimbilia nchi hizo kwa sababu ya gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi zinachukua eneo kubwa sana na mengine hazifanani na idadi ya wanyama waliopo. Hali hii ikilinganishwa na ongezeko la watu husababisha wananchi kukosa ardhi ya kilimo na mifugo. Nashauri ifanyike tathmini kwenye hifadhi zote kuona hali ya hifadhi na mahitaji ya ardhi kwa wananchi wanaozunguka hifadhi ili hifadhi zisogezwe ndani zaidi kuwezesha wananchi kupata ardhi. Hii itapunguza ugomvi kati ya wafugaji na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijipange vizuri katika zoezi la kuzuia matumizi ya mkaa bila kuja na nishati mbadala. Bei ya gesi na umeme viko juu kiasi kwamba mwananchi hawezi kutumia gesi/umeme kwa kupikia, hataweza kumudu gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TFS* Kakonko, Jimbo la Buyungu. *TFS* wanatesa wananchi Wilayani Kakonko kwa kukamata wananchi wenye hata mbao moja au gunia la mkaa. Hali hii haikubaliki kwani bado wananchi wanahitaji kujenga, kutengeza samani na kadhalika. Mateso haya hayavumiliki.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ya kuongoza Wizara hii muhimu. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu na watumishi wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Idara ya Malikale ishirikiane na Halmshauri ya Karagwe na Ofisi ya Mbunge kuendeleza maeneo ya Malikale ikiwemo yaliyokuwa Makao ya Chifu Rumanyika. Mara nyingi nimekuja kuwaona Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri juu ya jambo hili, naomba msaada kwa niaba ya wananchi wa Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iweke utaratibu wa ujirani mwema na vijiji vinavyopakana na Pori la Akiba la Kimisi kwenye Kata za Rugu, Nyakasimbi, Nyakakika, Nyakabanga na Bweranyange kwa kusaidia kuboresha sekta ya elimu hasa kusaidia ujenzi wa madarasa ya shule za msingi, nyumba za walimu, matundu ya vyoo na kuchimba visima vya maji. Msaada huu ni wa muhimu sana na utasaidia kujenga *royalty and sense of community ownership* kwa maliasili za umma zilizo kwenye Pori la Akiba la Kimisi badala ya kulitazama *with contempt.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri arejee *memo* yangu niliyomwandikia tarehe 19/05/2017 humu Bungeni juu ya ombi la kuleta wataalam toka Idara ya Utalii

kuangalia *border belt* ya Wilaya za Ngara, Karagwe na Kyerwa ili kufanya ukanda huu ukuze utalii kwa kutumia vivutio vya Malikale, Maporomoko ya Rusumo, Mto Kagera, Ziwa Lwakajunju, *Game Hunting* kwenye Bonde la Kimisi, Ibanda na *Rumanyika Game Reserves* na vivutio vingine tulivyojaliwa na Mwenyezi Mungu kwenye *border belt* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti,majirani zetu Rwanda *on the other side of the border* wanajipatia fedha nyingi za kigeni, kwani wametumia fursa asili nilizozitaja kukuza utalii Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naomba nijibiwe maombi haya kwa maandishi. Ahsante.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya pamoja na timu yake kwa ujumla na hotuba yenye mtazamo chanya na iliyojaa matumaini mazima katika sekta ya utalii, pamoja na matumaini makubwa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali yangu Tukufu katika suala zima la upandaji miti katika maeneo yote yaliyozungukwa na misitu pamoja na watu binafsi. Sambamba na hayo, pia tuna misitu iliyoungua, kwa mfano, misitu ya Wilaya ya Lushoto, imeungua toka mwaka 1994, lakini mpaka sasa misitu ile haijaota tena. Kwa hiyo, naishauri Serikali ipande miti maeneo hayo ya misitu iliyoungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wakala wa Mbegu yaani *TTSA* na *TAFORI.* Wakala hawa ni muhimu sana, kwani hawa ndiyo watakuwa wakombozi katika kurudisha uoto wetu wa asili uliotoweka, lakini Mawakala hawa hawana mafungu ya kutosha, pamoja na vifaa vyao wanavyotumia ni vya zamani.

Kwa hiyo, naisisitizia Serikali yangu kama kweli ina nia ya dhati ya kupata miche kwa ajili ya kupanda miti katika nchi hii, basi wawape mafungu ya kutosha mawakala hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hawa *TFS* wanafanya kazi yao nzuri sana ya kuhakikisha misitu yetu haihujumiwi hovyo. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu iwawezeshe kwa vifaa vya kutosha, kama magari pamoja na ma-*grader* kwa ajili ya kuchimba barabara za msituni ili kurahisisha kupitika kwa haraka wakati wa majanga ya moto yanapotokea kuliko ilivyo sasa, tunategemea wananchi kuzima moto, pamoja na vifaa vya kuzimia moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wana mwamko wa kupanda miti, lakini wananchi wanapangiwa kuvuna miti yao waliyopanda wenyewe. Naiomba Serikali iitoe sheria hiyo, kwani inakandamiza wakulima wa miti. Hii imekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwawezeshe vijana waliojiunga kwenye vikundi hasa katika Wilaya ya Lushoto, kuna vijana wamejiunga kwenye vikundi vya upandaji wa miti, lakini hawana *support* yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la utalii katika Wilaya ya Lushoto; kama unavyojua, Wilaya ya Lushoto ina vivutio vingi kama malikale, milima yenye vivutio, maporomoko *(waterfalls).* Pamoja na hayo, Wajerumani waliishi sana Lushoto. Kwa hiyo, Serikali ifuatilie na itambue vivutio hivi ili tusikose mapato, kama inavyofanyika sasa kienyeji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, wapo vijana wengi pale Lushoto wanaotembeza watalii. Naiomba Serikali yangu iwajengee uwezo na kuwatambua ili wasifanye kazi kienyeji na kuhakikisha mapato yanapita katika Serikali yetu pamoja na kuwajengea uwezo wa kuwaendeleza kielimu na kama siyo kufungua Chuo cha Kitalii Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyojulikana, Lushoto ni eneo lililozungukwa na misitu ya asili na misitu ya kupandwa, lakini barabara ya kuingia Wilaya ya Lushoto ni moja tu. Kama ilivyo sasa hivi, mvua zinazoendelea kunyesha zimesababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara

pamoja na madaraja. Hii imepelekea uchumi wa Lushoto kurudi nyuma pamoja na Serikali kukosa mapato kwani magari yanayopitisha mbao hayapiti, watalii hawafiki Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna kilio kikubwa sana cha barabara katika Wilaya ya Lushoto. Kwa hiyo, Serikali lazima ichukue hatua za haraka kujenga barabara nyingine na mchepuo, ambayo inatakiwa ijengwe eneo la kuanzia Dochi kupitia Ngulwi hadi Mombo. Kwani ikijengwa barabara hii ya mchepuo itakuwa barabara mbadala na kumaliza tatizo la maliasili zetu kupita kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mgogoro wa Ngorongoro, naomba niishauri Serikali yangu kuwajengea wafugaji wale mabwawa, visima na malambo ili kunusuru uharibifu wa hifadhi zetu unaotaka kutokea. Pia naishauri Serikali yangu iunde *WMA* katika eneo la Loliondo na kuwa na sheria kali za kusimamia eneo lile, kwani kuna vyanzo vya maji vinaharibiwa siku hadi siku na mwisho wa siku wananchi na wanyama wetu wa porini watakosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tulinde, tutunze hifadhi zetu ili na sisi tuweze kurithisha kama waliopita walivyoturithisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu na watendaji wao wote wa Wizara kwa kazi nzuri sana wanayofanya. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa misitu kwanza huhifadhi maji, makazi ya viumbe hai, misitu, ni muhimu kwa

matumizi mbalimbali ya binadamu kama vile mbao, dawa, chakula, kuni, mkaa na matumizi mengine. Misitu pia hutumika kwa makazi ya binadamu kama Wahadzabe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa misitu ni muhimu sana, hata hivyo ni vyema wananchi wasifanye uharibifu wa misitu; wasifyeke misitu ovyo na kusababisha jangwa/ukame ambao huleta njaa nchini. Wananchi wasichunge mifugo yao kwenye vyanzo vya maji kwa kuwa maji ni uhai, maendeleo na uchumi wa nchi yetu; wananchi wasijenge kwenye vyanzo vya maji; wananchi wasichome misitu ovyo, kwa kuwa misitu huvuta mvua na bila mvua hakuna chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote haya, Serikali iruhusu wananchi waendelee kutumia/kupikia mkaa na kuni kwa kuwa hawana mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza watendaji wa sekta ya utalii kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Pamoja na pongezi, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sekta ya utalii inachangia Pato la Taifa wajitahidi kuhakikisha kwamba watalii wanaongezeka kila mwaka ili Pato la Taifa liongezeke kuliko hali ilivyo sasa; watalii wapate huduma bora kama vile barabara ziwe nzuri na zinazopitika wakati wote wa masika na kiangazi; kuongeza vivutio kwa watalii ili waweze kuongezeka; huduma ya usafiri iwe bora ili watalii wasisumbuke; waongoza watalii wawe na lugha nzuri na tabia nzuri/njema; na huduma ya chakula na malazi iwe bora kwa watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watalii siyo lazima wawe wa kutoka nje ya nchi tu, hata utalii wa ndani. Ushauri wangu kwa Serikali, zijengwe hoteli za bei nafuu kwenye mbuga zetu za wanyama ili watalii wa ndani waweze kumudu gharama za malazi na chakula kwenye mbuga zetu za wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii napende kuchangia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uhifadhi na utalii ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Sekta ya utalii inachangia takribani asilimia 17.5 ya uchumi wa Tanzania. Kuna umuhimu sasa Serikali itie mkazo katika kuhakikisha sekta hii ya utalii inafanya vizuri ili kuongeza mapato na kukuza uchumi wetu wa Tanzania. Serikali inatakiwa ifanye jitihada kuhakikisha ifikapo mwaka 2020 idadi ya watalii nchini iwe imeongezeka kufikia milioni mbili ambapo itaongezeka mpaka asilimia 20 - 25 katika uchumi wa Tanzania. Kuna umuhimu pia kuweka jitihada/mkazo kwenye utalii wa fukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara/Serikali iweke mikakati mizuri katika kuhamasisha utalii wa ndani kwa kuongeza matangazo katika sehemu muhimu ili wananchi watembelee maeneo ya utalii kama *Ruaha National Park* kule Iringa, wajulishwe uzuri wa kule, mfano kuna simba wanaotembea kwa makundi makubwa ambayo ni kivutio kikubwa. Mbuga ya Kitulo kule Mkoa wa Njombe, mbuga yenye maua mengi ya kila aina tuitangaze ili kuweza kupata watalii wengi, ni kivutio cha aina yake.

Mhesimiwa Mwenyekiti, Serikali pia iongeze mbinu za kupambana na ujangili ili tuweze kulinda wanyama wetu kama faru, tembo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashauri kwamba elimu ya uhifadhi itolewe kwa wananchi, waelewe faida ya uwepo wa mapori ya hifadhi. Kwa kufanya hivi tutaweza kuepusha migogoro ya wananchi na hifadhi kama kule Loliondo na maeneo mengine. Wahifadhi wa pori watoke kwa wananchi kutoa elimu ya uhifadhi, wasikae maofisini tu

na Serikali iboreshe mikakati ya kuvutia watalii wengi zaidi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Utalii, *TANAPA* pamoja na *NCAA* waendelee kutangaza vivutio vya utalii kwa kasi kubwa zaidi. Serikali/Wizara iweke mabango mengi na kuyasambaza kwenye maeneo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Serikali iwapatie *budget*/pesa za kutosha Wizara hii ili waweze kufanikisha shughuli zilizokusudiwa kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nishati ya mkaa holela ni hatari kwa ustawi wa nchi yetu. Tukisubiri gesi au umeme itatuchukua karne nyingi hadi kufikia wananchi wote kuachana na mkaa wa kuni.

Hivyo basi, kwa kuwa tangu mwaka 2012 kuna shirika linalojishughulisha na mafunzo kwa wanavijiji vipatavyo 30 vya Wilaya za Kilosa, Morogoro na Mvomero uchomaji wa mkaa endelevu kwa kutenga misitu ya kuchoma mkaa. Shirika hilo linafadhiliwa na watu kutoka nje ya nchi na tija ni kubwa na ndiyo mkombozi wa misitu yetu. Hivyo Serikali itenge bajeti ya kuwezesha Halmashauri kufundisha miradi ya mkaa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine napenda kupata majibu ya Serikali kuhusu madhara wanayopata wananchi wa Jimbo la Mlimba, kata ya Utengule na Msagati kwa kuchomewa nyumba, vyakula na kadhalika. Jambo hilo linafanywa na wamiliki na kitalu cha uwindaji *(Kilombero North Safari).* Tumefuatilia sana kwa Mkuu wa Wilaya ya

Kilombero ambapo ufumbuzi haujapatikana wa kuainisha mipaka ili wananchi waishi kwa amani katika vijiji vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kuna timu ya pamoja iko Wilaya ya Malinyi na Ulanga inarekebisha mipaka ya eneo oevu *(Ramsar Site)* ambao umeleta usumbufu kwa kuwa hawashirikishi wananchi na kuweka mipaka upya na hata wanapowashirikisha hawafikii muafaka, kwani wanalazimisha mipaka.

Hivyo basi, kazi hiyo inayoendelea huko haina tija bali ni kukuza migogoro. Ushauri wangu, naomba Mheshimiwa Waziri afanye ziara Mlimba na maeneo yote ya Bonde oevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata majibu ya Serikali, ni kwa nini ndani ya Bonde la Oevu mmeacha ng'ombe wengi tena inasemekana ni ng'ombe wa viongozi? Badala yake mnawanyanyasa wafugaji katika vijiji na kuwaacha wenye makundi makubwa ya ng'ombe wakiharibu Bonde la Kilombero huku mkipokea misaada ya fedha toka nje kwa madai mnahifadhi ardhi oevu?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Profesa Maghembe pamoja na Naibu wake Mheshimiwa *Engineer* Ramo Makani kwa kazi kubwa inayoendelea katika kukuza utalii nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana na kumshukuru Katibu Mkuu, Meja Jenerali Malinzi pamoja na timu yake ya wataalamu kwa kazi nzuri. Nawashukuru kwa tuzo ya uhifadhi wa mazingira ya *Jane Goodall* kupitia taasisi yake ya *Roots & Shoots* kwa kushirikiana na Makumbusho ya Taifa. Nawapongeza sana kwa kuendeleza Maporomoko ya Kalambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nikiwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, nilijitahidi kadri ilivyowezekana kuona jambo hilo siku moja linawezekana. Mara nyingi mhamasishaji

akiondoka na wazo linakufa, lakini kwa jambo hili imekuwa tofauti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa kuibua vivutio vingine kama jiwe la Mbuji na Mapango ya Makolo/ Matiri. Kama nilivyochangia wakati wa semina, ipo haja ya kuviibua vivutio vingine na kuvilinda kwani vivutio kama miamba ya hapa Dodoma, mkichelewa mtakuta watu wameshavivunja na kugeuza kokoto, jambo ambalo hamuwezi kurejesha tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuache utani, *Southern Circuit* inayoacha Ziwa Nyasa mmefikiria nini? Kwa hiyo, Nyasa itakuwa ni *Southern of Southern?* Lengo langu ni kuwaomba kuwa ikiwezekana basi, ijumuishwe humo na utalii na fukwe ni vema upewe uzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nyasa tumekubaliana kuanza kidogo kidogo, hivyo kila tarehe 30 Desemba ya kila mwaka ni kilele cha Tamasha la Utalii - Nyasa. Nawashukuru kwa *support* mliyotupatia mwaka huu. Sasa tuko kwenye maandalizi; na kila mwaka lazima tuseme angalau tumefanya nini. Hivyo tusaidiwe katika kuipanga fukwe hiyo, kuipamba *(beautification)* na kuboresha utoaji wa huduma hasa kwa akina Mama Lishe na waongoza watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutembelea Jimbo langu na kutoa ushauri muhimu kwetu. Miundombinu ya barabara ni tatizo, naomba Wizara yenu kuendelea kutusemea katika vikao vya Wizara mbalimbali ili Mbinga - Mbambabay iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiwe la Pomonda nalo lipewe uzito (lipo Liuli – mchezo wa kuruka majini) litangazwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nawashukuru sana *TFS* kwa kazi walioyoanza ya kupata miti Nyasa na naomba kuwasilisha.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ijitazame kuchachua utalii katika maeneo yafuatayo:-

(i) *Festival Tourism:* Nchi lazima ijipange vyema kuanzisha matamasha mapya na kuimarisha yaliyopo. Nionavyo kama Taifa tutimize na ku-*advertise Busara Festival* na *Zanzibar Film Festival,* kwa sababu ya *effect* yake, tunaweza kuwa *promoted* katika kiwango cha Taifa. Ni kosa kutotangaza *as part of National Tourism Campaign.*

(ii) *Songkran Festival* ya Thailand ambayo ni ya siku tatu huingiza *US Dollar 428.08 million.* Afrika Kusini *35 percent* ya utalii wake ni matamasha ya utamaduni. Tuwe na matamasha ya sanaa na mengine.

(iii) Nyingine ni *Conference Tourism* ambayo inatarajiwa kuipa Rwanda *US Dollar 76 million* mwaka huu na kupandisha utalii kutoka *US Dollar 1.2 million* kwa 2014 hadi *US Dollar 1.3 million* hapo mwaka 2015; na mapato kutoka *US Dollar 318 million to US Dollar 400 million* kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema sana kwa kuwa Dar es Salaam imepumua kuwa *Capital City,* sasa tukielekeza jiji hilo kuwa *hospitality and commercial city* na *conference tourism* ipigwe jeki kubwa kuifanyia matangazo. Tuhimize uwekezaji wa *Multipurpose Convention Centers* na hii itaendana vizuri na ujio wa uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *water sports* ni muhimu pia.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika majumuisho Wizara ya Maliasili na Utalii itoe maelezo ni kwa nini mpaka sasa haijawezesha Pori la Akiba la Pande kugeuzwa kuwa bustani ya wanyama na kivutio cha utalii? Suala hili Serikali imekuwa ikinipa ahadi toka mwaka 2011. Mwaka 2015 Serikali ilijibu Bungeni na kuomba ipewe mwaka mmoja tu, huu ni mwaka 2017, miaka miwili imepita.

Aidha, baada ya Mkutano huu wa Bunge Wizara iandae ziara ya kikazi pamoja na Mbunge kutembelea pori husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kati ya mwaka 2011 mpaka 2015, nilihoji kuhusu Kiwanda cha *Tembo Chipboard* kilichopo Mkumbara ambacho kiko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Wizara ilijibu kuwa kulikuwa na matatizo katika ubinafsishaji, hali iliyosababisha kiwanda kuacha kufanya kazi. Wizara iliahidi kwamba itaingilia kati kuwezesha kiwanda kuweza kufanya kazi ipasavyo. Hata hivyo, mpaka sasa kiwanda hakijarejea katika hali ya kawaida.

Hivyo, ni vema Wizara ikafanya utaratibu mkataba uliokuwepo uvunjwe na kiwanda kirejee katika hali yake ya awali ya kufanya kazi. Wizara izingatie kuwa Serikali ilishatoa ahadi Bungeni kwamba viwanda vyote ambavyo vilibinafsishwa lakini waliopatiwa wameshindwa kutimiza masharti ya kimkataba, vitarejeshwa Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka imepita toka Bunge lipitishe maazimio kuhusu Operesheni Tokomeza. Nilitarajia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri angeeleza hatua ambazo zimechukuliwa katika kutekeleza maazimio husika ya Bunge.

Hivyo basi, katika majumuisho Mheshimiwa Waziri aelezwe hatua ambazo Wizara imechukua kutekeleza maazimio ya Bunge kuhusu Operesheni Tokomeza.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kukuomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Mheshimiwa Naibu Waziri mtembelee wananchi wa pembezoni mwa Hifadhi ya Kigosi/Moyowosi yaani pembezoni mwa Halmashauri ya Ushetu - Kahama, Mkoani Shinyanga hususan Kata za Ulowa, Ubagwe, Ulewe, Nyankende na Idahuria, mjionee shida

zilizopo; mikakati ya uhifadhi shirikishi, uonevu, mawazo mazuri ya wananchi, eneo lililopoteza sifa na upungufu wa eneo la malisho. Ziara itahamasisha sana uhifadhi maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Serikali iweke mipaka inayoonekana kwenye hifadhi zetu kama inavyotajwa na *Section 28* ya Sheria Na. 14 ya Hifadhi ya Misitu ya mwaka 2002. Hii itasaidia kupunguza migogoro kwani wananchi wataona kirahisi na kuiheshimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Section 29* ya Sheria na 14 ya Hifadhi ya Misitu ya mwaka 2002 *(Forest Act, 2002)* inampa nafasi Mheshimiwa Waziri kupitia mara kwa mara hifadhi za misitu yetu na kuifuta ile ambayo imekosa sifa. Namuomba Mheshimiwa Waziri/Serikali ifanye mapitio ya eneo la Msitu wa Usumbwe *(Usumbwe Forest)* ililolitwaa mwaka 1966 na kuliunga na Hifadhi ya Kigosi/Moyowosi kwani msitu huu hauna sifa; urejeshwe ili wananchi watumie kuwa malisho, bwawa la kunyweshea na kilimo cha umwagiliaji. Hii itasaidia kutokuwa na uharibifu wa hifadhi yetu ya Kigosi/Moyowosi na kupandisha uchumi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kuwa sekta ya maliasili na utalii ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwamba nguzo za umeme ambazo zinazalishwa *Sao Hill* na mahali pengine ndani ya nchi yetu, zitumike ndani ya Tanzania na nchi nyingine, tuache kununua nguzo kutoka nje wakati tunazo nguzo zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya upasuaji mbao katika msitu wa Serikali uliopo Wilaya ya Mufindi *Sao Hill* kipaumbele ni vijiji vinavyozunguka misitu, vikundi vya vijana, wanawake wapewe vibali vya kupasua mbao; viwanda

vidogo vidogo vipewe vibali na viwanda vikubwa vipewe vibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa misitu inahifadhi udongo na vyanzo vya maji, nashauri Serikali kwenye vyanzo vya maji ipandwe miti ambayo inahifadhi maji kwa mfano, Miwengi ni miti ambayo inahifadhi maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo cha mabondeni, Serikali itoe mbadala kwa wananchi ili wananchi waweze kulima na kupata chakula; chakula ni muhimu kwa maisha ya binadamu. Kilimo cha mabondeni (vinyungu) hakuna madhara yoyote ya kukausha maji katika mabonde yetu. Kinachotakiwa ni kupanda miti ya kuhifadhi maji, kilimo cha mabondeni, viazi, miwa, nyanya, mpunga, mboga mboga na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wanapanda miti ili kusaidia kuinua uchumi wao. Mtu akiwa na tatizo anauza miti ili kutatua tatizo ambalo analo. Watu wengi wamejenga nyumba bora kutokana na biashara ya miti; wanasomesha watoto ndani ya nchi na nje ya nchi kutokana na biashara ya miti. Naiomba Serikali iache kuweka vikwazo kwa watu ambao wanapanda na kuvuna misitu yao. Mtu anatunza misitu kwa gharama kubwa ili kupata faida baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Maghembe, Naibu Waziri, *Engineer* Ramo Makani, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kutuletea bajeti yao ili tuweze kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Wanyama ya *Ruaha National Park* ni hifadhi ya pili kwa ukubwa katika Afrika na hifadhi yenye wanyama wengi sana. Cha kushangaza hifadhi hii barabara inayoenda katika mbuga

hii haina lami na kiwanja cha ndege cha Iringa hakuna ndege kubwa inayotua katika kiwanja hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijajua Wizara hii inafanya juhudi gani kuhakikisha miundombinu ya kuwezesha watalii wanaofika na kufanya matangazo ya kutosha ili tupate watalii wa kutosha? Ni kwa nini Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Serikali haiwekezi kama ilivyo Kaskazini? Kwani kuna vivutio vingi sana. Ni vizuri Serikali ingetupatia mkakati wa kuendeleza mbunga hiyo na utalii wa Nyanda za Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kitabu kilichotolewa na *TFS* kilichotoa mwongozo wa kutoa vibali, tunashukuru kwa kutangulia kutoa kipaumbele kwa wenye viwanda na wananchi watakaozunguka msitu; lakini nitoe ushauri wangu kwa Serikali kuwa katika mwongozo wake ungeongeza na yale makundi maalum; makundi ya akina mama wajane, akina mama wenye vyama vinashughulikia makundi ya kijamii. Kwa sababu tumeshuhudia mara nyingi wananchi wanaozunguka msitu hawafaidiki na rasilimali hiyo, wakati wao ndio walinzi wakuu wa mazingira hayo, hata wakati mwingine moto ukitokea wanakuwa wakitoa msaada mkubwa. Naiomba Serikali jambo hilo liangaliwe tena na tupatiwe majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie upya suala la fidia kwa wananchi wanaopatwa na maafa. Kwa mfano, Mkoa wa Iringa kuna wananchi walipata matatizo ya kuuawa na mamba wengine kupata ulemavu.

Pia tembo walileta uharibifu wa mali na vifo katika Kata ya Nyanzwa, lakini tunashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Ramo alishawahi kufanya ziara katika eneo hilo na kilio kikubwa kilikuwa ni fidia kidogo sana ukilinganisha na uharibifu unaojitokeza. Ni vigezo gani huwa vinatumika au ni lini sheria itarekebishwa ili ianze kukidhi vigezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Iringa una vivutio vingi sana ambavyo bado hatuoni kama Serikali inavitendea haki ya kuvitangaza ili viweze kuchangia pato

na kukuza utalii katika eneo la Nyanda za Juu Kusini. Tunaona kama upo ubaguzi. Nini mkakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyenzi Mungu aliyeniwezesha kuchangia leo japo kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Maghembe, Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer* Makani, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu uharibifu wa mazingira/maliasili. Serikali inajitahidi sana kutoa agizo na usimamizi wa upandaji miti, lakini baada ya kupanda, nani anafuatilia kuona kati ya miti milioni 1.5 iliyopandwa kwa mwaka ni mingapi imekufa na mingapi inaendelea kustawi kwa kila Halmashauri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Maafisa Misitu Mikoani na Wilayani wapo. Kwa hiyo, naomba kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri kupitia kwa Wakuu wa Mikoa watoe agizo la ufuatiliaji wa miti iliyopandwa kwa mwaka husika na ni mingapi imekufa na mingapi imeendelea kustawi? Namna hii tutaweza kuimarisha ufuatiliaji na kutoa *report* kwa Waziri. Pia itasaidia uwajibikaji wa upandaji miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kama miti yote au asilimia kubwa ya miti inayopandwa itashika na kuendelea kustawi, tutaweza kurudisha uoto na ukijani wa sura ya nchi mahali pengi Mikoani na Wilayani mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu ninaousema ni wa vitendo vya binadamu kwa kukata miti ovyo ovyo bila ya kibali maalum cha kuruhusiwa, ni wapi ukate? Pia kukata tu bila ya kupanda (bila ya kujali sera ya bwana misitu ya kata mti, panda mti) ni kweli wote mnajua kuwa miti nchi nzima

inakatwa bila ya mpangilio, hasa katika misitu ya asili. Misitu inakwisha! Naishauri Wizara kuhimiza jambo hili hasa la kutunza miti ya kupanda miti ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shaka na Mheshimiwa Waziri, naamini ni mtalaam wa misitu, pamoja na watalaam wake. Tafadhali naomba Mheshimiwa Waziri aokoe nchi kwa kuhimiza utunzaji wa misitu ya Tanzania. Sitaki kurudia faida moja moja ya misitu kwani najua mnajua faida zote za misitu, tatizo ni kuisimamia ili iendelee kustawi na kupunguzwa au kukatwa kwa kibali maalum kutoka Wilayani ambapo Mkuu wa Wilaya ndiye Mwenyekiti wa Kamati husika. Naamini mambo mengine yanaingiliwa na Wizara kwa Wizara tofauti. Shirikianeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miti hiyo inakatwa kwa madhumuni mawili makubwa; kuni na mkaa. Namba ya tatu ya ukataji wa milunda ni kwa sababu ya ujenzi na miti mingine inakatwa bila vibali kwa madhumini ya kutengeneza mbao. Tafadhali tafuta mbadala ya kila kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu asilimia 90 ya wananchi (Watanzania) wanatumia kuni na mkaa. Mheshimiwa Waziri, wewe ni mzoefu wa miaka mingi katika tasnia hii; je, tufanyeje kuokoa nchi na kupunguza au kuokoa kilio cha miti? Nashauri chekecheni vichwa watalaam, saidianeni na Katibu Mkuu, Naibu Waziri na Waziri mwenyewe kutafuta nishati mbadala ya kuni na mkaa ambayo itakuwa rafiki na wananchi wengi kama siyo wote kufuatana na aina ya nishati na mahali walipo. Kwa mfano, huu ushauri, ukiambatana na agizo na Sheria Ndogo ya Halmashauri tunaweza kushinda tatizo hili lililo mbele yetu kwa miaka yote. Kwa upande wa familia za wafugaji nashauri waelimishwe kutumia *biogas* kwani wanayo *source.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na wafugaji, pia wananchi wengine wanaofuga ng'ombe wachache au mifugo mingine nao wapewe elimu ya *biogas*. Wananchi wengine kwa kushirikiana na watalaam husika waelekezwe jinsi ya kutumia joto la jua *(solar).* Naamini ni kujipanga na

kuamua, wananchi wakielekezwa ni nini cha kufanya na kubanwa na utaratibu, sera, sheria ndogo watafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia ya wananchi wanaotumia gas asilia ya nyumbani imeongezeka kidogo na hasa ukichanganya na asilimia ndogo sana inayotumia umeme. Tatizo kubwa ni bei. Mtungi wa gesi wa kati sasa ni kati ya shilingi 68,000; shilingi 54,000 mpaka shilingi 52,000 kufuatana na mkoa kwa mkoa. Mtungi huu ukibahatika utachukua wiki mbili au mwezi kwisha (inafuatana na wapishi na matumizi). Hivi kweli kufuatana na mishahara yetu, wangapi Watanzania wataweza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iingilie kati kushauriana na wafanyabiashara wa gesi ya nyumbani ili bei ipangue watu wengi waweze kumudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa umeme, sisemi kwani ni ghali zaidi. Shaurianeni na Waziri wa Nishati. Namna hii tutaokoa maliasili yetu hasa misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi wakati wa Maonesho ya Nane Nane wavumbuzi wajasiriamali wanaonesha aina mbalimbli za nishati, lakini hakuna anayezitilia maanani, mbali ya kuziona na kuwasifia. Nashauri tujaribu kuziendeleza zinaweza zikawa mkombozi kwa mfano, makaa ya magazeti/karatasi, joto la majiko (banifu), pumba *(husks)* ya mpunga na kadhalika. Okoa maliasili yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie utunzaji wa misitu. Huu ndiyo ushauri na ombi la Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo niongelee utalii. Nashauri utalii na hasa vivutio vya kila mkoa vitangazwe kikamilifu kwa pamoja na kuwavutia watalii wengi. Tamaduni za makabila yetu, pia ni utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu wa kuzungumza, ninayo yafuatayo; *TDL* - Sekta ya Utalii kutoza 1.5 *USD Bed Night Levy* siyo nzuri kimapato. Utaratibu ungewekwa tozo hii iwe kwa asilimia kwa sababu *it is unfair* kwa anayelaza kwa shilingi 30,000/= anatozwa *1.5 USD* sawa naye anayelaza kwa dola 50 na kuendelea, hata kiuchumi siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa takwimu za watalii ni *1.2 million* na kwa kuwa utalii wetu ni ule tunaitwa *Low Volume High Yield.* Hivi hata kwa hesabu za *common citizen*, kwa mfano, kwa mujibu wa takwimu katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 136 jedwali Na. 9 wastani wa siku za kukaa watalii hotelini ni siku 10. Sasa kwa mahesabu ya haraka tuchukulie wageni *1.2 million* wamelala siku tano, maana yake hizo ni *a total of 6,000,000 nights* ambazo ukifanya ile *Bed Night Levy* ya *USD 1.5 per bed* ambayo ni kama shilingi 3,000/=; maana yake ni 6,000,000 x 3000 = *18 billion* ambayo ingeweza kabisa kutusaidia katika kuutangaza utalii, kuimarisha mafunzo hasa kupitia Chuo cha Utalii na hata kutoa ruzuku kwa wajasiriamali wa miradi ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba tuanzishe chombo maalum cha kuratibu *TDL,* chombo hiki kitabainisha njia mbalimbali za namna ya kuimarisha makusanyo kupitia *TDL.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushirikishwaji wa sekta binafsi sambamba na kuanzisha *One Stop Centre,* ni wazi kuwa Serikali haiwezi kujenga mahoteli zaidi ya kujishirikisha na ujenzi wa miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege. Kwa sababu hiyo, ushirikishwaji wa sekta binafsi haukwepeki. Tufike wakati sekta binafsi tuione kama mdau na siyo adui/mwizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 23 wa kitabu, umeelezea kuhusu *VAT,* kuna *confusion.* Wadau wanasema imeathiri Sekta ya Utalii, lakini Serikali inaonesha kuwa hakuna athari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kama ilivyoshauriwa na Kamati, Wizara ikae na wadau kupitia na kujiridhisha kuhusu suala hili. Nasisitiza pia pawepo na *One Stop Centre* kwa ajili ya masuala ya ku-*facilitate* masuala ya utafiti kama ambavyo *TIC;* ukifika unakutana na Idara zote kuanzia *BRELA, TRA* na kadhalika. Tufanye hivyo katika utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani nikiwa Afisa Mambo ya Nje, Mama Blandina Nyoni akiwa Katibu Mkuu Maliasili alitoa *USD 10,000* (dola 10,000) kwa baadhi ya Balozi zetu kutumia kutangaza utalii, na ilisaidia sana. Kila Balozi ilitumia kadri ya mazingira. Wapo walionunua *TV* na kila mgeni akija kufuatilia visa, wakati anasubiri anaangalia filamu mbalimbali kuhusu utalii wa Tanzania. Nashauri tupanue wigo wa kutangaza utalii kwa kuendelea kuhusisha taasisi nje ya Wizara kulingana na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli kama tunasema katika sera kuwa jamii zinazozunguka mbuga na hifadhi zitakuwa sehemu ya kunufaika, mbona hii *single entry* inaenda kuua kuliko kunufaika? Hoja kwamba kuna ukwepaji wa mapato bado inaweza kutazamwa hasa katika baadhi ya maeneo. Hili suala ni kama vile kuwalinda wawekezaji wakubwa na kuwamaliza wawekezaji wadogo na hasa wanavijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Ryoba ni ya msingi na muitazame. Leo hii ufugaji unaongezeka badala ya ng'ombe 500 kama ilivyokuwa awali. Kuna ng'ombe 8,000 matokeo yake ni nini? Wataanza kuingia kwenye hifadhi, dhana ya *conservation* kama matokeo ya *WMA*. Hii itazamwe upya, tuwe *open minded*, tufikirie zaidi namna bora ya kudhibiti upotevu wa mapato lakini kwa kuzingatia ustawi wa jamii zinazozunguka hifadhi.

Kuhusu misitu *vs* vibali; kwanza nashukuru ushirikiano ambao Mafinga tunapata kutoka *Sao Hill* na *TFS*. Tumepokea madawati na Halmashauri yetu iko tayari kutoa eneo kwa ajili ya Ofisi ndogo na *parking* kama sehemu ya ushirikiano. Nimesoma kijitabu na niliitwa na Kamati kuhusu utaratibu

wa upatikanaji malighafi *Sao Hill,* hata hivyo nashauri kuwa pamoja na utaratibu huo, usawa na uwazi *(fairness na transparency)* ni muhimu sana. Siyo sawa mtu mmoja (sitamtaja) alijidai kuwa eti ana mkataba na Serikali *(TFS)* apewe ujazo mkubwa kisha awauzie wengine tena kwa majigambo makubwa kwamba wataendelea kumtegemea yeye. Hili halikubaliki! Ni vizuri mgao wa malighafi uzingatie uwezo wa kiwanda na sio umaarufu wa mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutotoa mgao kwa vikundi, pamoja na kuwa ni sheria/kanuni, nashauri suala hili litizamwe upya. Ni muhimu sana kutenga kiasi kidogo kwa ajili ya makundi ya mahitaji maalum kama wenye ualbino na vikundi vya wajane *as CSR (Corporate Social Responsibility).*

Suala la wanachi kupata vibali ndipo wavune miti yao sio sawa na litatuletea mgogoro na wananchi bila sababu yoyote. Nimechangia kwa kuzungumza, lakini nasisitiza maamuzi kama haya yawe shirikishi kuliko ku-*impose* tu. Mtu ana shida, anataka kuuza msitu wake atatue shida yake, *why* tumwekee mlolongo? *Je, capacity* hiyo mnayo? Tutafakari upya na nakuletea tangazo hilo, barua Na. *TFS/SH2/MUF/MSC/VOL.1/113* ya tarehe 9 Mei, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa hatuwezi kumrejesha mjusi aliyeko Ujerumani. Ushauri wangu ni kwamba shirikianeni na Wizara ya Mambo ya Nje, Wajerumani walishaonesha nia kwamba pale kwenye shimo alipotoka yule mjusi pajengwe *reception* na hoteli ambayo itatumika na wageni watakaopenda kuona lile shimo alipotoka mjusi. Jambo hili linataka utashi tu na linawezekana na litaongeza idadi ya watalii na hivyo kuongeza mapato.

Pili, Wajerumani pia wako tayari kutoa *funds* lakini *specifically* kwa ajili ya kuimarisha masuala ya *archeology* na *conservation.* Yote hayo ni *in connection* na huyu mjusi. Aidha, Mheshimiwa Dkt. Mwekyembe anaweza kuwa msaada katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, iwe ni kwenye misitu, uwindaji au utalii kwa ujumla ni vizuri viongozi wa kuchaguliwa kuanzia Wenyeviti wa Vijiji/Mitaa, Madiwani na Wabunge washirikishwe ipasavyo hasa katika maamuzi yanayokusudiwa kufanywa, yanaathiri maisha ya wananchi kwa asilimia 50. Mfano, suala la mkaa, vinyungu, *single entry* na kadhalika. Naomba kuwasilisha.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na umuhimu wa Wizara hii ya Maliasili na Utalii ambayo inachangia pato kubwa kwa Taifa letu, kuna kila sababu ya kubadilisha utaratibu wa kuendesha Wizara hii ili kuongeza idadi ya watalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubadilisha aina ya matangazo kutokana na hali ya ushindani ni mkubwa sana, ni vyema Serikali ikabadilisha utaratibu wa matangazo kwa vivutio vilivyopo nchini kwa kutumia njia kama shuleni, ngazi ya msingi, sekondari na vyuo vikuu na vyuo vya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu ili kupata watalii wengi nchini kwa kutengeneza miundombinu ambayo itakuwa rafiki kwa watalii wanaokuja nchini ili kuongeza idadi ya watalii na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wananchi kulingana na migogoro ambayo inaendelea nchini katika maeneo mbalimbali ikiwemo Simanjiro ambao umechukua muda mrefu sana kupeleka mifugo na wananchi kuuawa, ni vyema migogoro hii ikamalizwa kwa wakati na bila kuathiri haki ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya hifadhi ichunguzwe upya kwani idadi ya watu imeongezeka lakini maeneo ya hifadhi pamoja na mapori tengefu wakati ardhi ni ile ile. Hivyo, nashauri Serikali kupitia upya mipaka hiyo ya maeneo ya hifadhi ili kuwatendea haki wananchi wanaoishi karibu na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na uzoefu na matatizo mengi yanayotokea katika maeneo ya hifadhaji ili utekelezaji wa yale waliyokubaliana yafikie malengo, suala la bajeti kufika kwa wakati kulingana na umuhimu wa Wizara hii ambayo ni miongoni mwa sekta muhimu za kiuchumi katika nchi yetu, ni vyema bajeti ikatolewa kama ilivyotengwa na kupitishwa na Bunge na iende kwa wakati.

Suala la kushirikiana na Wizara nyingine ambayo ni Wizara ya Ardhi, Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Kilimo ili kuweza kuwa na mkakati wa kudumu wa kumaliza changamoto zinazowakabili wananchi na watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manyanyaso kwa wananchi wanaopita katika hifadhi kulingana na hali iliyopo katika maeneo mbalimbali wanatakiwa kupewa elimu na siyo maamuzi na hatua kali zinazochukuliwa kwa mifugo na wananchi wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kalemani dakika tano. Mheshimiwa Wambura dakika tano.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue nafasi fupi sana kuchangia katika Wizara hii, lakini awali ya yote niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu yake ya wataalam. Nawapongeza kwa kazi kubwa waliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo nitachangia kwa kiasi kikubwa sana ni matumizi mbadala ya mkaa pamoja na kuni. Kama ambavyo wameeleza wenzetu katika taarifa hii, mkakati waliouweka ni pamoja na kuonyesha kwamba matumizi ya mkaa pamoja na kuni yanapungua kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo mkakati mkubwa na wenye dhamana kubwa ya kuhakikisha kwamba mkakati wa kuni na mkaa unaisha na kwamba sasa tunatumia nishati mbadala ni Wizara yetu ya Nishati na Madini, kwa hiyo nitajielekeza kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tuna mpango wa kimataifa wa matumizi endelevu unaotaka kuhakikisha kuwa matumizi ya mkaa pamoja na kuni yatakomea ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba matumizi ya mkaa katika nchi zinazoendelea hadi sasa yanafikia asilimia 90 ya nishati ya umeme duniani. Hiyo ni takwimu ya Benki ya Dunia. Lakini pamoja na hayo bado kwa nchi zetu zinazoendelea hasa zilizoko chini ya Kusini mwa Afrika, pamoja na maendeleo ya nchi za Afrika tani milioni 2.3 kwa nishati tunayotumia inatokana na kuni pamoja na mkaa. Kwa hiyo, ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama Serikali, mpango madhubuti uliopo ni kwamba, moja, sisi ni wanachama wa kimataifa wa matumizi mbadala ya nishati ya kuni pamoja na mkaa. Mkakati madhubuti ambao Serikali tumechukua, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba sasa Shirika letu la *TPDC* kuanzia mwaka 2013/2014 lilianza rasmi kujenga miundombinu ya matumizi ya gesi kuanzia mijini mpaka vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa hatua ya kwanza, tumeanza na Dar es Salaam. Mwaka 2014/2015 tumeshaunganisha wateja 70 ambao tumewaunganishia miundombinu ya gesi katika maeneo ya Mikocheni. Kwa hiyo, ni hatua kubwa, lakini hatua ya pili tumepeleka matumizi hayo hayo ya gesi kwenye magari yetu. Hadi sasa tunapozungumza magari takriban 60 yanatumia gesi, hiyo ni hatua ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatua ya pili ni kupeleka miundombinu ya matumizi ya gesi, na hii gesi ninayoizungumzia ni ya aina hii ya *mathane*, si ile gesi ambayo tumeizoea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna taarifa yetu itakuja hapo baadaye tutaeleza kwa upana zaidi; lakini kwa ufupi tu niseme kwamba kuanzia mwaka 2017/2018 tutaunganisha matumizi ya gesi katika Mikoa ya Mtwara na Lindi pamoja maeneo yote ya Dar es Salaam yakiwemo maeneo ya Mbagala, Kurasini, Buguruni na maeneo mengine ya jiji ya Dar es Salaam. Tunatarajia wananchi 30,000 tunawaunganishia gesi ili matumizi makubwa ya mkaa na kuni yapungue. Asilimia 70 ya mkaa unaotumika hapa nchini unaingia Dar es Salaam, kwa hiyo tukishaunganisha gesi kwa wananchi wa Dar es Salaam tutapunguza kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira, hiyo ni hatua ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili, kwa sababu muda ni mfupi sana, inahusu usambazaji wa umeme mijini na vijijini. Kama ambavyo mnajua tunapeleka umeme katika mikoa yote katika miji yote na vitongoji vyetu. Tuna mpango wa kendeleza umeme mijini, na mpango huu unaanza mwaka 2017/2018 kwa maeneo ya mjini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante, Mheshimiwa Wambura.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Maghembe na Naibu wake *Engineer* Ramo pamoja na timu nzima ya Wizara kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika Wizara ya Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti mchango wangu uko katika maeneo mawili, kwanza ni kuhusu utalii wa utamaduni, lakini pili nimalizie kuhusu suala la Vazi la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukiri kabisa kwamba tuna vivutio vingi vya utalii wa utamaduni katika nchi yetu kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu, lakini Wizara yetu ina kazi kubwa, iko katika

mchakato wa kutekeleza Mkataba wa *UNESCO* wa mwaka 2003 ambao unahusu Urithi wa Utamaduni Usioshikika na ule mkataba wa mwaka 2005 wa Kulindwa na Kukuzwa kwa Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni.

Sasa tunachofanya sisi Wizara ni kukusanya taarifa na tafiti kutoka kwa wadau mbalimbali zikiwemo Halmashauri, na taarifa hizi zinahusu maeneo ya kihistoria, kimila, kidesturi na vivutio vya utalii wa kiutamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika zoezi hili tunashirikiana kwa karibu kabisa na Wizara ya Maliasili, Kitengo cha Malikale pamoja na TAMISEMI na zoezi hili ni endelevu na uendelevu wake utaona kwamba kuanzia mwezi Agosti, 2016 hadi sasa tumeshapata vivutio vipya kutoka Halmashauri 35 na Mikoa 19. Lengo kumbwa ni kuzitumia taarifa hizi katika kuwasaidia wananchi kuweza kutumia utalii wa kiutamaduni kuongeza kipato. Kwa hiyo, nitoe wito kwamba Halmashauri zote ziendelee na zoezi hili na tuna dhamira kubwa ya kutumia baadhi ya mila na desturi zetu katika kuzipeleka kwenye orodha wa Urithi wa Utamaduni wa Dunia. Kwa mfano, mila na desturi ya jando na unyago ambayo iko katika Mikoa ya Kusini na Mikoa ya Ukanda wa Pwani kama vile Wamakonde; na ile mila ya Wamasai ya kurithisha ngazi ya rika ya kipengele cha Engpaata Yunoto na Olng'esher. Kwa hiyo, vivutio hivi vikiingia katika Orodha ya Urithi wa Dunia vitasaidia sana kuwa vivutio vya utalii wa utamaduni katika yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi binafsi nikiri kwamba nimeshawahi kutembelea baadhi ya vivutio na niseme tu kwamba bado Halmashauri zetu zina kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba zinaboresha mazingira katika maeneo yale ya vivutio. Kwa mfano, Halmshauri hizi zihakikishe kwamba kunakuwepo na vyoo, barabara nzuri, maeneo ya kulia chakula kwa sababu vivutio vingine vingi viko katika maeno ya maporini, lakini ni vizuri sana. Kwa mfano nilishawahi kufika katika kichuguu ambacho kinacheza kule Babati, kunahitajika maboresho ili kusudi watalii wengi waweze kufika. Nishauri tu Halmashauri zione

umuhimu wa kutenga bajeti ili kusudi kuweza kuboresha maeneo hayo

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande mwingine nizishauri halmashauri pia ziwatumie wacheza filamu pamoja na waigizaji katika maeneo yao kwa kuwapa mikopo ili kusudi waweze kucheza filamu za...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumrudishia sifa na utukufu Mwenyenzi Mungu kwa kila jambo. Ninamshukuru Mungu kwa wema na fadhili zake kwa kutujaalia afya njema na uhai sisi Wabunge, viongozi na watumishi wote wa Bunge wa Bunge lako Tukufu na kwa kutuwezesha kumudu majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi tukiongozwa na viongozi wetu wa wakuu wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu ili niweze kuchangia mjadala ulioko mbele ya Bunge lako tukufu kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala wa hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kufafanua baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa kadri muda utakavyoniruhusu ninapenda kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii wakiongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye na Makamu wake Mheshimiwa Kemirembe

Julius Lwota kwa kuendelea kuishauri na kuisimamia Wizara yetu katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa katiba, sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wananchi wa jimbo langu la Tunduru Kaskazini kwa kuendelea kuniamini lakini pia nashukuru familia yangu. Pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia kwa maandishi na kwa kuzungumza na sasa nianze kufafanua baadhi ya hoja zilizotolewa kupitia Taarifa ya Kamati ya Kudumu, Taarifa ya Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Taarifa ya Kamati kutokana na muda niseme tu kwa ujumla kwamba maoni yaliyotolea kwenye Taarifa ya Kamati mengi ni maoni ambayo hakuna jambo tunaloweza kufanya isipokuwa ni kuyachukua na kwenda kuyafanyia kazi. Tunapokea maoni hayo na ushauri wote ulitolewa toka kwa Kamati kama yalivyoainishwa katika sehemu ya tatu sura ya sita ukurasa wa 22 mpaka 34 wa taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kuzungumzia tu mambo mawili kwa muda huu ulionipa. Kwanza nitazungumzia suala la *WMAs* ambazo kwenye Taarifa ya Upinzani limezungumzwa kwa kirefu hasa ukurasa wa 13 kuna hoja zimetajwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hoja ya mgawanyo wa mapato katika *WMAs* kuwa haufuatwi ipasavyo kwa mujibu wa sheria au kanuni, iko hoja ya kwamba Serikali inachukua kiasi kikubwa cha fedha kinachotokana na mapato ya utalii kwenye hizo *WMAs*, iko hoja inasema Serikali inachukua asilimia 55 na kuacha kiasi cha asilimia 45 peke yake kwa *WMAs.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipengele hiki napenda kusema kwamba Kambi ya Upinzani iende ikaangalie upya kule ambako wameweza kuchukua taarifa hizo na hasa takwimu ili waweze kuja na takwimu ambazo

ni sahihi, kwa sababu kwa mujibu wa kanuni zilizosainiwa mwaka 2012 mgawanyo wa mapato yanayotokana na utalii kwenye *WMAs* hauoneshi kwamba *WMAs* zinapata mapato kama ilivyoainishwa kwenye taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato kwenye utalii wa uwindaji yapo ya aina nyingi kama sita hivi, mimi nitaje haraka haraka tu, ipo *block fees* ambayo *WMAs* inapata asilimia 75, *game fees WMAs* inapata hiyo asilimia 45 na nyinginezo. Kutokana na muda kiufupi niseme tu kwamba mapato yanayotokana na shughuli za uwindaji wa kitalii *WMAs* zinapata mgao ambao si mdogo kulinganisha na ule ambao unakwenda kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia yapo mapato yanayotokana na utalii wa picha. Kwenye upande wa utalii wa picha kanuni zinasema kwamba *WMAs* zinapata asilimia 70 na wala si asilimia 45 kama ilivyoainishwa. Ninazo hizo takwimu hapa kwa mujibu wa hizo kanuni, Waziri Kivuli akizihitaji nitaweza kumpatia kwa rejea yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lipo suala la *WMA* ya Burunge kwamba kwa mujibu wa taarifa hiyo ni kwamba *WMA* ya Burunge imepata mapato yafikiayo takribani shilingi bilioni sita na kwamba *WMA* hiyo inaambulia shilingi milioni 800 pekee. Ukweli ni kwamba kwa sababu mgawanyo wa mapato unakwenda kwa mujibu wa sheria, ni vema tukazingatia kwamba takwimu ambazo zipo sahihi ndizo peke yake zinazoweza kutoa mwelekeo juu ya mgawanyo wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama nilivyosema pale awali kwamba takwimu zilizotolewa na Kambi ya Upinzani zinatakiwa zifanyiwe marejeo kwa maana ya kwamba tunawaalika waje wazitizame kwa sababu kosa kama hili haionekani kama lingeweza kutokea kwa sababu ni kosa kubwa sana. Hii ni kwa sababu jumuiya ya hifadhi ya wanyama pori moja haiwezi kupata pato la shilingi bilioni sita ingawa hakutaja ni kipindi gani. Kwa sababu kwa mujibu wa kumbukumbu tulizonazo kama Serikali pato la shilingi

bilioni sita ni pato la *WMAs* zote nchini, tena si kwa mwaka mmoja, ni kwa miaka mitatu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa mapato yote ya *WMAs* kwa muda wa miaka mitatu, 2014/2015, 2015/2016 na 2016/2017 ni shilingi bilioni 5.515. Kwa hiyo, kwa upande huo wa takwimu niseme tu kwamba tunamkaribisha aje aweze kuchukua takwimu sahihi ili aweze kujenga hoja zake sawasawa kwa mujibu wa kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini iko hoja moja iliyozungumzia kuhusu ucheleweshaji wa fedha kwenda kwenye zile *WMAs.* Kwenye hoja hii tunauona ukweli, kwamba ni kweli kutokana na utaratibu uliopo kwa mujibu wa kanuni muda unaotumika unaweza kufanyiwa kazi na tukaweza kuupunguza ili *WMAs* zikaweza kupata ule mgao wao kwa wakati ambao ni pungufu ya ule wanaoupata hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninaloweza kulizungumzia kwa sasa ni suala hili la mahusiano au mwingiliano baina ya wanyamapori na shughuli za kibinadamu, hasa mashamba lakini pia makazi ya wananchi, mahali ambapo wakati mwingine hutokea wanyama huharibu mazao mashambani lakini wakati mwingine hudhuru hata wananchi; na baadhi yao hujeruhiwa na pengine wengine hupoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa ninachoweza kusema ni kwamba kwanza napokea pongezi kutoka kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Nsanzugwanko akiwa mmojawapo ambaye ameipongeza Serikali kupitia Wizara kwa kudhibiti ujangili ambao matokeo yake ni kuongezeka kwa idadi ya wanyamapori hasa tembo. Tuna idadi kubwa ya tembo sasa hivi ambao wanavinjari kwenye maeneo mbalimbali, wengine walikuja mpaka *UDOM* juzi. Hiyo ni mafanikio kwa upande mmoja, lakini kwa upande mwingine wa pili kuna changamoto zinazotokana na ongezeko hilo la wanyamapori hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kumekuwa kukizungumzwa jambo linalohusiana na vifuta jasho na vifuta machozi. Hapa napo pia kama Serikali kupitia Wizara tumefanya kazi kubwa kwa kulipa sehemu kubwa ya madeni yaliyodumu kwa muda mrefu ambayo kwa muda wa miaka mingi yalikuwa hayajalipwa bado. Hata hivyo, mpaka ninavyozungumza hivi sasa jumla ya fedha takribani shilingi bilioni 2.08 ambazo ni mkusanyiko wa madeni ya mpaka Disemba, 2016 yamelipwa kwa maana ya vifuta jasho na vifuta machozi. Hadi kufikia sasa deni la jumla tulilobaki nalo la vifuta jasho na vifuta machozi ni shilingi milioni 500 peke yake fedha ambazo kwa mujibu wa mpango tuliojiwekea na malengo tuliyojiwekea ndani ya mwaka wa fedha huu tulionao tunatarajia kumaliza kuzilipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema changamoto niliyonayo ni ya muda, lakini kwa ufupi nilitaka nizungumze hoja hizo mbili. Hata hivyo niseme ya mwisho inayohusiana na *WMAs* kwamba Taarifa ya Kambi ya Upinzani imezungumza kwa kina juu ya changamoto zilizopo kwenye *WMAs.* Kwa kweli baadhi ya hoja zilizotolewa lazima niseme ukweli kwamba ni hoja ambazo ni za msingi na zinapaswa kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini imekuwa bahati nzuri kwamba na sisi Serikali kwa upande wetu tarehe 9 Mei, 2017 tumekabidhi taarifa iliyofanya uchambuzi baada ya kufanya uchunguzi wa *WMAs* zote nchini kuangalia changamoto zao na changamoto kwa ujumla kwa mujibu wa sheria tuliyonayo na kanuni zake zinazoendesha *WMAs* na kwa hiyo tumeorodhesha baadhi ya hatua ambazo Serikali ni lazima ichukue ili kuweza kuboresha utendaji wa *WMAs* zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *WMAs* zote nchini ambazo kwa ujumla wake zipo 38, kwa sababu ya madhumuni ya msingi ya kuanzisha *WMAs* ambayo kimsingi ni kuboresha usimamizi, ushirikishaji wa wananchi katika kusimamia uhifadhi nchini, Serikali itahakikisha kwamba tunaongeza mikakati zaidi, mbinu zaidi lakini pia kuwekeza zaidi ili kuweza kuhakikisha kwamba madhumuni hayo

ambayo tumeyaainisha kwa mujibu wa sheria yanaweza kutekelezwa kwa manufaa ya uhifadhi nchini lakini kwa lengo la juu kabisa ni pamoja na kupata yale manufaa yanayotokana na shughuli za utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu yale ambayo niliona nikikadiria kwa muda niliopewa yanaweza yakatosha kwa muda huu nimekwisha yakamilisha napenda kuishia hapa na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua fursa hii kukushukuru sana wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kupokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri pamoja na maelekezo katika maeneo pengine kufuatia hotuba ya makadirio ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2017/2018. Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Atashasta Nditiye, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa uchambuzi na maoni kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu wa fedha unaokuja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati umegusa maeneo ya ufinyu wa bajeti, ushirikishaji wa mamlaka nyingine za Serikali na wananchi, utangazaji wa utalii, migogoro ya ardhi kati ya maeneo yaliyohifadhiwa na wananchi, mgongano wa sheria, uwekaji wa mipaka, utatuzi wa mgogoro wa Loliondo...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge, mmetoa hoja za msingi sana na sasa Serikali inajibu, inaelekea kama vile hamtaki kusikiliza. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**...udhibiti wa ujangili na masuala kuhusu maendeleo ya sekta ya utalii nchini.

Ushauri na maoni haya ya Kamati utazingatiwa na wizara na tutaufanyia kazi kwa jinsi ambavyo tutaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nafasi hiyo hiyo namshukuru Mheshimiwa Esther Nicolas Matiko, Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kutoa maoni ya kambi yake na maoni hayo na yenyewe tumeyapokea na tutayaangalia kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yetu imejadiliwa na Waheshimiwa Wabunge kwa undani sana; jumla ya Waheshimiwa Wabunge 142 walijadili bajeti yetu. Waliochangia kwa mdomo walikuwa Waheshimiwa Wabunge 76 na walioleta maandishi kama mchango wao ni Waheshimiwa Wabunge 66.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda ambao umenipa na michango ambayo imeletwa ukubwa wake, ubora na umuhimu wake hatutaweza kuyatendea haki mawazo yote haya yaliyotolewa katika hotuba hii ya dakika 30. Ninachowaomba na kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge ni kwamba tumepokea michango hii na tumeifurahia kwakuwa *critical review* ya *performance* ya Wizara ya Maliasili na Utalii na tutaichukua kwa hali hiyo na kushughulika nayo mpaka tupate majawabu. Tunategemea kabisa kwa ushirikiano ambao umeonyeshwa hapa, *willingness* ya Waheshimiwa Wabunge kushiriki na kutusaidia hakuna litakaloshindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kujibu masuala ambayo yamejitokeza na yamejitokeza kwa nguvu, si kwa umuhimu kwamba yale ambayo hatutayafikia siyo muhimu, ni kwa sababu tu ya muda.

Kwanza nitaongelea juu ya Kamati ya Wizara tano ambayo imeundwa kwa ajili ya kutatua migogoro ambayo inaisibu Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Kilimo, Wizara ya TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu na pengine inasibu Wizara ya Mazingira lakini ikiwa chini ya Uenyekiti wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii imeundwa na Kamati ilipoundwa imepitia taarifa zote za migogoro ya ardhi na migogoro mingine ambayo ni kati ya wananchi na Serikali katika maeneo mbalimbali ya nchi hii. Jumla ya ripoti 19 zimepitiwa na ni zote ambazo zimetokana na Bunge, Serikali yenyewe na kadhalika. Ripoti hizo zikaifanya Kamati ikatembelea mikoa kumi kama sampuli ya maeneo ambayo yameguswa na ripoti na ikaja na migogoro 1,246 ambayo inahitaji kutatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ikawasilisha migogoro hiyo kwa makatibu wakuu ambao nao tarehe 8 Mei, 2017 wakaiwasilisha kwa timu ya Mawaziri wanne. Tukaipokea ripoti ile na tukaona kwamba Kamati ile iendelee na kazi ili iweke mkakati wa utekelezaji wa ripoti ambayo wameileta. Tumewakea *timeframe* na kwamba kabla ya tarehe 10 Juni, 2017 wataiwasilisha ripoti yao kwa Makatibu Wakuu wa Wizara sita na tarehe 10 Mawaziri wa Kilimo, Maliasili, TAMISEMI, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais tutakutana chini ya uenyekiti wa Waziri wa Ardhi kuiangalia ripoti hiyo na mkakati wake wa utekelezaji kabla hatujapeleka ripoti hiyo kwa viongozi wetu kwa kupata kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo,nataka niwaombe sana wale wote ambao wameongea hapa kwa hisia kubwa juu ya migogoro iliyopo kati ya hifadhi zetu na mifugo, kati ya hifadhi zetu na wakulima, kati ya hifadhi zetu na watu waliojenga katika maeneo mbalimbali kwamba wavute subira kwa sababu hili jambo linafanyiwa kazi na kazi hii inafanywa kwa nguvu sana na kwa usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutapata majawabu na hatutateteleka katika kuyatekeleza. Nimemsikiliza sana Mheshimiwa Joseph Musukuma, *classmate* wangu Profesa Anna Tibaijuka jana na nimewasikiliza sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu wakina Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Joseph Kakunda na Mheshimiwa Cosato Chumi, nimewasikiliza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza na wengine na jambo hili tunakwenda kulitekeleza, lakini wakati tulipokuwa tunasikiliza mambo haya pia tumejifunza vitu hapa maana yametolewa madarasa aina mbalimbali. Kutokana na madarasa hayo tumejifunza kwamba kuma muingiliano mkubwa sana wa shughuli za kibinadamu na uhifadhi. Hili ni jambo ambalo lazima tuanze nalo. Pili ni kwamba tunahitaji kilimo kwa ajili ya kushiba kwetu vile vile kwa ajili ya kujenga uchumi wa nchi yetu, lakini kilimo kinahitaji maji kwa ajili ya umwagiliaji. Kwa sababu hiyo kama tunataka kumwagilia maji na tunaongea na kusema kwamba hatuwezi kuwa na tija katika kilimo lazima tuhifadhi misitu kule ambako maji yanatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji sana mifugo, na mimi ninaamini kabisa kwamba hili ni *giant* kubwa ambalo limelala. Mchango wa mifugo bado hatujauona. Mchango wa mifugo ule unaouona kule Uholanzi, kwenye ile *cattle belt* ya Marekani, hujauona hapa. *Potential* ya hilo *giant* ipo na *giant* hilo linahitaji maji, *giant* hilo linahitaji mvua, *giant* hilo linahitaji kutunzwa na linahitaji liepushwe na magonjwa na maambukizi mengine ya mifumo ya ikolojia ambayo inaweza kuzingatiwa na hifadhi zetu. Kwa hiyo, tunahitaji misitu itupe mvua, itupe maji, itupe hewa na itupe bidhaa nyingine zile za kiikolojia ili maisha yetu yaweze kuwa bora na vilevile ili tuweze kufanya shughuli zetu hizi za uchumi, kilimo, mifugo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji sana wanyamapori na Mwenyezi Mungu ametupa wanyamapori hawa sisi Watanzania kwa ajili ya utalii. Kama mmejumlisha tarakimu vizuri hapa sekta hii ya utalii inachangia asilimia 21.4 ya Pato la Taifa ukijumlisha aslimia 3.9 ya misitu na asilimia 17.5 ya utalii na wanyamapori. Lakini wanyama hawa wanatusaidia pia katika kutafuta dawa kwa maisha yetu ya baadaye, ni viumbe ambavyo lazima tuwe nao ili kuhakikisha maisha yetu na *longevity* ya maisha yetu. Kwa hiyo, wakati umefika, kwa kweli, na amesema hapa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati. Sisi katika kujifunza mambo yaliyopita hapa ndani tumejifunza kwamba wakati umefika sasa tusiwe

na makampuni zaidi ya manne ndani ya sekta hii ya wanyamapori, tuwe na kampuni hii moja tu ambayo itapunguza gharama katika uendeshaji. Tutafundisha Jeshi la Wahifadhi na jeshi hilo tutakalolitengeneza ni jeshi moja tu ambalo litakuwa na malezi chini ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ili kujenga nidhamu, kuheshimu haki za binadamu na kufanya kazi kama ambavyo maslahi ya Taifa yanahitaji. Kwa hiyo, jeshi hilo ambalo tunaliandaa hivi sasa (Jeshi Usu) litakuwa na *chain* ya *command* moja na litawajibika kijeshi kwa makosa ya haki za binadamu na usaliti wa Taifa au usaliti wa uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, hilo ni moja ya masomo ambayo tumejifunza hapa.

Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea kwa uchungu juu ya utalii. Kwanza niseme kwamba tumefurahi sana kupata michango hii ya utalii, lakini nimeona katika maono yetu na *definition* ya utalii naona kama kuna tofauti hivi ya mawazo. Sisi tumetumia maana ya utalii kama inavyotumiwa na *United Nations Tourism Organisation,* hiyo ndiyo *definition;* ya mtu anayeondoka pale alipo kusafiri kwenda nchi za nje au kutoka pale alipo kwenda mahali pengine kwa shughuli inayozidi saa 24 lakini haifikii mwaka mzima akiondoka nyumbani kwake; hata kama anakwenda kwa biashara, anakwenda kwa vitu vingine, lakini wakati akiwa kule atakuwa anatoa huduma ambazo mtalii akifika mahali anazipata kama kukaa kwenye hoteli na kutumia huduma za aina hiyo kule anakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo takwimu ambazo tumezitoa ni takwimu ambazo zimekusanywa vizuri sana na timu ambayo inaundwa na Wizara yangu ya Maliasili na Utalii, Jeshi la Uhamiaji, Benki Kuu ya Tanzania, Kamishna wa Utalii kule Zanzibar na huduma zetu za kiuchumi wa ndani ya nchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani wakati ukiwa na nafasi nitakupa hizi takwimu ili uweze kuona ni jinsi gani tumezikokotoa na ni jinsi gani ambavyo ile *thought process* imekwenda na kwamba zile takwimu ambazo umetupa hapa si za kweli. Tumepata mawazo, na ni kweli kwamba utangazaji wetu wa vivutio vya utalii bado ni mdogo kwa sababu ya fedha ambazo tunazo. Hata hivyo

Serikali imeondoa hatua ya kwanza na inakwenda mbele na mwelekeo ambao tunao na mipango ambayo tunayo inatuwezesha sasa tupige hatua kubwa katika kuujulisha ulimwengu kwamba yule *giant* wa utalii anayeitwa Tanzania sasa ameanza kutembea. Kama mnavyokumbuka, sisi kwa tathmini ya *World Economic Forum* ya mwaka 2014, sisi ni wa pili baada ya Brazil kwa kuwa na vivutio vizuri, hasa vile vya *nature,* tukifuatia Brazil huku duniani, hakuna nchi nyingine tena. Lakini kuanzia mwaka 2014, tukafika mwishoni mwa 2015, tumeanza kushuka kwa sababu tumekuwa na maono tofauti kwa jinsi ambavyo tunaviona hivi vivutio vya utalii. Wengine kati yetu wanayaona ni maeneo mazuri ya kuchunga ng'ombe, wengine wanaona ni maeneo mazuri ya kupeleka utalii, wengine wanaona ni maeneo mazuri ya kulima, na kwa sababu ya vitendo hivi mbalimbali tumefika mahali sasa tumefika Taifa la nane katika mataifa ya duniani katika ubora wa vivutio vyetu vile ambavyo ni *natural.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niwaombe ndugu zangu, tuvilinde hivi vivutio vyetu vya utalii kama tunavyoweza kuweka mboni na kulinda macho yetu, na hatujachelewa. Hatujachelewa kwa sababu nina imani kabisa hii Kamati yetu itaweka matumizi mengine hapa, matumizi mengine hapa na utalii na uhifadhi hapa na tutarudi kule ambapo tulikuwa. Katika Bara la Afrika kuna vivutio vya kimataifa, vya kidunia 50, kati ya hivyo 50, vivutio vya kwanza nane vinatoka Tanzania. Tusiharibu jambo hili zuri namna hii kwa kuwa tu tunataka tuoneshe kwamba sisi *we are on top of the world and we can use it for anything,* tusifanye hivyo. Tulinde na tuangalie ni kitu gani kinaleta ugali ndani ya midomo yetu, na kule kwingine tuangalie ni namna gani ambavyo sasa tutaboresha kilimo. Hatuwezi kulima sasa mashamba kwa kukimbilia kulima hekta 200 ili tupate magunia 200 ya mahindi, lazima tulime hekta 10 tupate magunia 200. Lazima tufuge vizuri tupate maziwa, tupate nyama na mazao ya kufuga mazuri ili tufurahie nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto katika utalii. Moja ya changamoto iliyotajwa hapa ni leseni. Ndugu

zangu nawaomba mnielewe, leseni za biashara zinatolewa kwenye *categories* mbalimbali. Leseni ni kibali cha kufanya biashara, sio kodi. Mtu mwenye kaduka kwenye mtaa tunapoishi anakata kodi lakini kodi ya mtu mwenye duka la mtaani ni tofauti na kodi ya Kampuni ya Mabasi ya Shabiby, ni tofauti na kampuni ya ndege na ni tofauti na kampuni za aina nyingine. Katika utalii, tangu mwaka 1992 leseni ya kufanya utalii ni dola 2000. Nimewawekea kwenye *bag* sheria zote ambazo zinaongoza maliasili na Sheria ya Utalii nimewawekea mule ndani na zile kanuni za leseni na namna ya kufanya hiyo biashara nimewawekea kwenye lile *bag;* naomba mzisome na mzielewe vizuri. Mtu anayepandisha watu Mlima Kilimanjaro akapandisha kundi la watu kumi, kila mtu mmoja kwa bei ya sasa analipa dola 4,000. Kama wako kumi watalipa 4,000 mara kumi na mtu yule anaweza kupandisha makundi matano mpaka sita ya watu hao kwa mwaka. Mimi nina rekodi kule kwenye Wizara kwa hiyo najua. Kwa hiyo huwezi kusema kwamba ni mdogo asilipe leseni ya dola 2,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani *interpretation* hapa na udogo na ukubwa una tofauti. Udogo na ukubwa unaangaliwa kwenye kulipa *corperate tax,* wakati wa kulipa kodi ile asilimia 30 ndiyo unaangalia mdogo kwa sababu ya biashara yake ilivyo ndogo na mkubwa kwa sababu biashara yake ni kubwa. Lakini katika kukata leseni, ni lazima tuangalie biashara kama biashara ya kawaida na tumeanza kupanua utalii katika *zones* mbalimbali, katika kanda mbalimbali. Upande wa Kusini, tunaboresha miundombinu katika mbuga za wanyama za Ruaha, Selous, Mikumi na Ruangwa pamoja na Kitulo. Serikali pia kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imekwenda ikakagua barabara kutoka Iringa mpaka kwenye lango la Hifadhi ya Ruaha. Kwa hiyo, tuko njiani kuboresha maeneo yale, lakini kikubwa ni kwamba kuboreshwa kwa *ATCL* kumesaidia sana na kutasaidia sana kupunguza gharama za ndege za kwenda kutembelea Hifadhi za Ruaha, Ruangwa na Kitulo na kwa hiyo, kufungua lango la Kusini mwa Tanzania. Hivyo hivyo, tumefanya kazi kubwa sana ya kupeleka zile Kampuni za Utalii za Kimataifa katika mbuga yetu ya Katavi, kwenye ufukwe wa Ziwa

Tanganyika na katika Hifadhi yetu ya Gombe kule Kigoma, na kuanzia mwezi Aprili, 2017 tumeanza kupata watalii kutoka Uyahudi kwenye sekta hiyo ya Magharibi, na *Air Tanzania* imetusaidia sana kupokea wageni wanapofika Dar es Salaam na kuwarusha kwenda Kigoma na kutoka Kigoma kwenda Mpanda. Kwa hiyo, kazi inaendelea, naomba mtuunge mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nimesikia sana malalamiko makubwa kuhusu mkaa. Ndugu zangu, mkaa unasababisha ukataji wa asilimia 80 ya miti yote inayokatwa hapa Tanzania. Sisi tunaelewa kabisa kwamba bado tunahitaji wananchi wetu watumie mkaa katika vijiji, watumie kuni na katika miji midogo hii watumie mkaa kwa ajili ya maisha yao. Lakini huu mkaa unaokatwa unatengeneza tani milioni 2.3 za mkaa kila mwaka na zaidi ya nusu ya mkaa huu unaingia Dar es Salaam. Kiini macho tu. Maana kutoka Dar es Salaam mwingine unakwenda Zanzibar na kutoka Zanzibar unakwenda Oman na unakwenda Mombasa. Mkaa unakatwa kwenye hifadhi zetu za Magharibi za Burigi, kule Moyowosi, Kigosi, unakatwa unachomwa kule unakwenda nchi jirani za DRC, Burundi na mataifa ya kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho ninataka niwaambie ndugu zangu ni kwamba hatuwezi kukubali miti yetu ikatwe kwa ajili ya kupeleka mkaa Kenya na majirani wengine. Tunataka mkaa ukikatwa utumike hapa Tanzania. Kwa hiyo, hatujakataza kuchoma na kuuza mkaa ndani ya Tanzania na mtu ambaye anafanya hivyo anavunja sheria na ninataka niseme, kuzungusha mkaa ndani ya mji au ndani ya vijiji au maeneo ambayo watu wanaishi kwa baiskeli au kwa pikipiki, hakuna mtu aliyekataza. Kinachokatazwa ni wale ambao wana-*smuggle* mkaa kutoka misituni kwa ajili ya kupeleka nchi za nje na kupeleka kuuza kwenye maeneo ambayo haina kibali cha kuuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kwanza tuanze vizuri, cha kwanza, nimeambiwa wapo watu wengi sana wamekamata baiskeli za watu, zipo baiskeli malundo na malundo. Nimeambiwa kuhusu malundo yaliyopo Kasulu,

nimeambiwa kuhusu malundo yaliyopo Geita, nimeambiwa kuhusu malundo yaliyopo Ushirombo na maeneo mengine. Kuanzia leo, Maafisa wa Misitu wote wa maliasili wanaagizwa warudishe baiskeli za watu wetu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hebu rudia.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pikipiki...

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaagiza kwamba Maafisa Maliasili, Maafisa Misitu, Maafisa Wanyamapori walioshika pikipiki za watu, baiskeli za watu na vifaa vya wananchi ambavyo havina kesi mahakamani, waviachie mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu ambao wanasaidia sana nchi hii kwa kupanda miti katika maeneo yao na mashamba yao, na mimi nataka niwape pongezi kubwa kwa kufanya kazi hii kwa niaba ya Taifa. Watu hawa wengi wapo katika Wilaya za Njombe, Wanging'ombe, Mufindi, Mafinga, Kilombero na Morogoro. Nataka niseme hivi, Wizara na Serikali hatuna tatizo na watu hawa kuchagua matumizi ya miti yao.

Aidha, hatuna tatizo na watu hawa kukata miti yao wakati wanapotaka. Lakini tungependa kuwashauri, kwamba kama ni miti ambayo inatakiwa kutumika kwa ujenzi au kutengeneza vifaa kama hiki ambacho ninaongelea hapa, ni vizuri miti ili iachwe ikomae ili vifaa vile viweze kuwa vya kudumu na miti yao iweze kuwa na faida kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu wapo watu wengi sana wanaofanya biashara ya magogo na mazao mengine ya miti, ni muhimu Maafisa Misitu waweze kuhakikisha kwamba hii inatoka kwenye mashamba yao na kwa sababu hiyo wasiwabugudhi, lakini wote ambao wanatoa kwenye mashamba ya Serikali, katika Misitu ya Serikali, Misitu ya Vijiji na Misitu ya Halmashauri ni lazima wapate vibali na leseni za kuvuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti viko vitu vingine hapa ambavyo vilisemwa kwa hisia kubwa sana nami najisikia kwamba labda nipate muda niviseme tu hata kwa sentensi mbili. Hapa kimesemwa Chuo cha Nyuki cha kule Tabora kwamba chuo kimefungwa, kama Kituo cha Utafiti kimehamishiwa Arusha. Sasa nataka kusema, hii siyo kweli. Chuo cha Tabora kipo na Chuo cha Utafiti wa Nyuki Tabora kipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kile ni muhimu sana kwa sababu kulikuwa na uvumi wakati fulani kwamba asali inayotokana na miombo kule Tabora ina *nicotine,* kwa hiyo, haifai kuuza nchi za nje. Kituo kile ndiyo kimechukua sampuli za aina mbalimbali za asali kutoka maeneo yote ya Tabora; maeneo yanayolimwa tumbaku na yale ambayo hayalimwi tumbaku na hakuna tofauti ya kihesabu yaani *statistical* kati ya uwepo wa *nicotine* kwenye asali inayotoka ndani ya misitu ambapo hakuna kabisa tumbaku na ile ambayo inayotoka katika maeneo ambayo yako karibu na tumbaku. Nyuki wenyewe wana uwezo wa kuchagua na kutengeneza zao zuri. Kwa hiyo, nataka kile chuo kiendelee kukaa pale na tutashirikiana na Waheshimiwa Wabunge wa Tabora kuhakikisha kwamba tunakijenga na kukiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliambiwa *computer* ziliondolewa, *computer* hazijaondolewa. Kama wameondoa watazirudisha, kesho ukifika pale utazikuta. Gari halijaondolewa limepelekwa kutengenezwa. Gari ni la mwaka 1989 na ni *Land Rover* ile ya zamami. Kwa hiyo, nimewaagiza kwamba wawaletee gari nyingine ili waweze kufanya utafiti vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limesemwa hapa likanigusa sana ni akina mama kuliwa na mamba wakati wanachota maji kwenye Mto Ruvuma. Hili limeletwa hapa na Mheshimiwa Bwanausi ambaye amelieleza kwa uchungu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwahakikishia tu akina mama wa Lulindi kwamba tuko pamoja, tumetuma

wataalam wa kupima maeneo ambayo yana maji ya chini ya visima ili kuhakikisha kwamba hakuna mwana mama anakwenda kuchota maji kule kwenye mto. Nasi tutatoa fedha ili visima hivyo viweze kujengwa na kuhakikisha kwamba akina mama hawaliwi na mamba wakienda kuchota maji. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo hapa ambayo bado nilikuwa nataka niyaseme, lakini kwa kweli muda tu ndiyo unanishika mkono na mimi nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutawapa majibu mazuri kwa maswali yenu yote ambayo mmeuliza na tutaomba msaada wenu katika kuendeleza sekta hii ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo naomba ushirikiano wenu katika kupitisha bajeti ya Wizara ili tuweze kwenda kufanya kazi. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo. Naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshmiwa Spikaameridhia yafanyike mabadiliko madogo kwenye ratiba ya Mkutano huu wa Bajeti unaondelea kufuatia ombi la Serikali la kusogeza mbele tarehe ya kusomwa bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Mabadiliko yaliyofanyika ni kama ifuatavyo:-

(i) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki itawasilisha bajeti yake tarehe 29 Mei, 2017 badala ya tarehe 31 Mei, 2017.

(ii) Wizara ya Fedha na Mipango itawasilisha bajeti yake tarehe 30 - 31 Mei, 2017 badala ya tarehe 01- 02 Juni, 2017.

(iii) Wizara ya Nishati na Madini itawasilisha bajeti yake tarehe 01- 02 Juni, 2017 badala ya tarehe 29 - 30 Mei, 2017

Ratiba mpya inayoonesha mabadiliko hayo itasambazwa hivi sasa humu ndani.

Sasa Mheshimiwa Waziri umetoa kauli ya kuhusu baiskeli na pikipiki, mara nyingi kauli zenu hapa huko mikoani hawazizingatii na wananchi wanaendelea kuteseka na wewe umetoa kauli ndani ya Bunge. Nakuomba sasa utoe waraka kuwaandikia Maafisa wako wote wanaohusika kwa kauli uliyoitoa hapa na watu warudishiwe vyombo vyao vya usafiri.

Kwa maneno hayo jamani si niwahoji tu sasa hivi?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MWENYEKITI:** Mnasemaje? Katibu! *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungunza bila mpangilio)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kif.1001 - *Admin. and HR Mgt.* ................Shs. 5,557,992,404/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimeshapewa majina ya mshahara wa Waziri na ninalo jina la Mheshimiwa Joseph Musukuma, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Nape Nnauye, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Hamidu Bobali, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Paresso na Mheshimiwa Ryoba.

Mheshimiwa Joseph Musukuma!

**MHE JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kueleza niliyonayo. Nilisema nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kama hatatoa majibu ya yale niliyoyauliza hususan sana suala la uonevu wa watu wa Maliasili unaondelea kwenye maeneo yetu hususan Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nilieleza vizuri na katika majibu ya Mheshimiwa Waziri sijaona mahali ambapo hata ametoa kauli ya kutusikiliza wakati tukitoa yale malalamiko, amezidi tu kueleza yale yale wakati kesho kuna mnada mwingine ng'ombe 1,200 zinauzwa kwa *style* ile ile na wateja wao ni wale wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kama Mheshimiwa Waziri ameeleza hayo na mimi sijaridhika, naomba kutoa hoja tu Wabunge wenzangu wa...

**MWENYEKITI:** Acha Mheshimiwa Waziri akujibu kwanza.

**MHE JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo ya kina kwa Mheshimiwa Waziri aweze kuniridhisha, pengine anaweza kutoa kauli ya kufuta hizo kesi zinazoendelea na huo uonevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na hapo, nitashika shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa nafasi. Nimeeleza kwa ujumla kazi ambayo imefanywa na Serikali katika kujiandaa kutatua migogoro kama ile ambayo ameieleza Mheshimiwa Joseph Musukuma leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo ambayo katika utekelezaji wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori tunaweza kuyafanya katika Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini yako mambo ambayo katika utekelezaji wake yako kwenye mhimili wa Mahakama. Yanapoingia kule, yakitoka kule, hatuyawezi. Isipokuwa leo mchana nimeanza kutekeleza zile ahadi ambazo tumezitoa wakati wote kwamba nimewaagiza na nina uhakika kabisa Katibu Mkuu wangu ametoa maagizo kwa wafanyakazi wa Wizara kule kwenye maeneo anayoyasema Mheshimiwa Musukuma kwamba kama kuna ng'ombe ambazo wanataka kuzipiga mnada, basi mnada huo usimame mpaka timu yangu itakapokuja katika maeneo yale na timu ya Serikali katika kipindi cha wiki ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo *commitment* ambayo naweza kuitoa na ndiyo hatua ambayo tumeweza kuichukua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa maelezo haya mepesi mepesi ya Mheshimiwa Waziri, kiukweli sijaridhika na wewe mwenyewe umeweza kusema hapo mwanzoni alivyoachia pikipiki kwamba yanakuwa ni maneno tu mepesi, yanatufurahisha humu lakini kule mnada unaendelea na wanasema haya ni maneno ya wanasiasa. Kiukweli sijaridhika na hatua ambayo Mheshimiwa Waziri anasema wameanza. Sisi kama Bunge tuna uhakika gani kama itakuwa hivyo? Ingepigwa simu ama waraka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Toa hoja yako Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Naomba kutoa hoja ili Wabunge wenzangu mniunge mkono ili tuweze kujadili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ulega, Mheshimiwa Ryoba.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mchengerwa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kalanga, Mheshimiwa Mchengerwa, Mheshimiwa Ishengoma, Mheshimiwa Mukasa...

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Kanyasu!

**MWENYEKITI:** Subirini basi! Mheshimiwa Keissy, Mheshimiwa Khatib, Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Waziri wa Mifugo utakuwa mwisho. Mheshimiwa Flatei, wewe Mheshimiwa Lijualikali eeh?

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Ndiyo!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka nimeshakutaja. Mheshimiwa Lulida...

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Bilago!

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Kanyasu!

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Bilago!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago, Mheshimiwa Mlata tayari, Mheshimiwa Ole-Nasha.

**MBUNGE FULANI:** Asha Abdallah!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MBUNGE FULANI:** Tisekwa.

**MWENYEKITI:** Haya kaeni chini.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge hili gumu, wengine wanalalamika watu wengi, wengine wanalalamika watu wachache. Kwa hiyo, kiti ndiyo kinaamua. Tunaanza na Mheshimiwa Ulega.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niseme tu kwamba tatizo la mifugo kwenye nchi yetu ni kubwa sana na sisi ambao tunatoka katika jamii ya wakulima tatizo hili la kuhama kwa mifugo kutoka katika jamii za wafugaji kuja kwetu limeleta athari kubwa sana kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwangu Mkuranga wananchi wa kata kama vile za Panzuo, Mkamba, Kisegese wanalia kila kukicha na mambo haya yameleta chuki, mahangaiko, mafadhaiko ya hali ya juu kwa wakulima wale. Mheshimiwa Waziri hapa ameeleza kwamba tunahitaji chakula kwa ajili yetu wenyewe kuwa na uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, pamoja na yote haya mazuri sana aliyoyaeleza Mheshimiwa Waziri ya namna ambavyo tunaweza kuenenda, tukubaliane, ni lazima tulinde mazingira yetu, ni lazima tulinde wakulima wetu, ni lazima tulinde wafugaji wetu pia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, namwomba sana mtani wangu, babu yangu hapa, Mheshimiwa Joseph Musukuma akubaliane na Mheshimiwa Waziri, tuungane kwa pamoja sasa kwenda mbele kuhakikisha kwamba tunaishi kwa amani na utulivu. Kwa kuwa ameshatoa *commitment* ya kutaka kwamba hili jambo likomeshwe kule, basi akubali amrudishie shilingi yake na baadae...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Robya, ajiandae Mheshimiwa Kalanga.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ryoba na Mheshimiwa Kalenga ajiandae.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya Wabunge unaowaona humu wengi ni watoto wa wafugaji. Niseme... *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mwacheni Mjumbe azungumze na Kiti.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoendelea kwa sasa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ryoba. Kwa hatua hii ya Kamati ya Matumizi, mimi ni Mwenyekiti na ninyi ni Wajumbe. Ndiyo Kanuni inavyosema. Mjumbe endelea.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoendelea kwa sasa kati ya wafugaji na askari wa *National Park* ni rushwa. Ukija kama pale kwangu kwenye vijiji vinavyozunguka pale imekuwa ni biashara kati ya askari na wafugaji. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri ni vizuri yeye kama Wizara yake waangalie utaratibu wa kudhibiti ng'ombe siyo kama ilivyo sasa. Kwa sasa ni biashara inafanyika pale wala hakuna hela yoyote inayoingia kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri ni vizuri wafugaji katika nchi hii, yatengwe maeneo, wapewe ili waweze kufanya ufugaji wa kisasa. Lakini ilivyo sasa kwa kweli mnawaumiza wafugaji wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Musukuma kwamba wafugaji wasinyanyaswe katika nchi hii, ni nchi yao, wapewe maeneo ya kufugia ng'ombe wao.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kalenga na Mheshimiwa Mchengerwa ajiandae.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu naitwa Kalanga Laizer siyo…

**Mwenyekiti:** Kwa hiyo, utakaa chini basi! *(Kicheko)*

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nirekebishe jina.

**MWENYEKITI:** Haya, endelea.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uuzaji wa mifugo kiholela katika nchi hii katika maeneo ya Maliasili inawasababishia wafugaji umasikini mkubwa katika nchi yetu. Kama Bunge hili tutaendelea kulitazama jambo hili katika suala la wakulima na wafugaji tutaligawa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikatai maelezo ya Waziri, lakini hatuwezi kuwasaidia wafugaji wa nchi hii kwa hisani ya Waziri. Tunataka kauli ya Serikali katika jambo hili kwamba suala la kutaifisha mifugo na kuuza kienyeji ni suala ambalo halikubaliki mahali popote. Kwa sababu Waziri anaweza akazuia leo, kesho Bunge likaisha, halafu baada ya hapo suala la ukamataji na uuzaji wa mifugo ya wafugaji kienyeji likaendelea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, je, hii ni kauli tu ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu anataka kupitisha bajeti au ni kauli ya Serikali kwamba ni marufuku sasa kutaifisha na kuuza mifugo ya wananchi hovyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Musukuma kwamba tunataka kauli ya Serikali katika jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mchengerwa na Mheshimiwa Ishengoma ajiandae.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa linaloikabili nchi hii ni Watanzania kutofuata sheria. Waziri Profesa Maghembe anachokifanya

ni kusimamia Ibara ya 26 ya Katiba ambayo inamtaka kila Mtanzania kufuata sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo sheria zetu. Pia siyo kila wananchi tu kutokufuata sheria, yapo maamuzi mengine ambayo hutolewa na baadhi ya watendaji wa Serikali ambayo yanakwenda kinyume na sheria. Kwa mfano, mwaka 2006 Serikali iliruhusu mifugo kutoka Bonde la Ihefu kwenda Bonde la Mto Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero hii ndiyo inaleta matatizo makubwa, manung'uniko ya wananchi kwa sababu leo hii Warufiji hawawezi kulima tena. Kuanzia Kibiti, Mkuranga mpaka Rufiji wakulima wetu wale hawawezi tena kushiriki kwenye kilimo kwa sababu mifugo inatafuna mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba ndugu yangu Mheshimiwa Musukuma atambue kwamba Mheshimiwa Profesa Maghembe anasimamia sheria, anasimamia Ibara ya 26 ya Katiba na ni jukumu la Bunge hili sasa iwapo tunaona yale maelekezo ya sheria zilizopo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mchengerwa, ahsante.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ishengoma na Mheshimiwa Khatib ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hapa nchini ni kweli wakulima wameteseka sana, ila wakulima na wafugaji tunawapenda. Ila ni lazima tufuge ufugaji wa kisasa na tuweze kutunza mazingira yetu. Nikisema mazingira tuweze kutunza misitu

yetu kwa sababu misitu ndiyo chanzo cha maji. Bila ya maji hatuwezi kufanya kilimo. Kwa hiyo, tufuate sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Waziri kwa mambo aliyoyasema. Kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Musukuma amrudishie shilingi yake kusudi tuweze kutunza mazingira yetu na kupitisha bajeti yetu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib na Mheshimiwa Sakaya jiandae.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kwa dhati kwamba analolitetea Mheshimiwa Musukuma ni jambo jema, lakini wema wa jambo lake hakusababishi maumivu kwa watu wengine. Anapotetea wafugaji, lazima aangalie na haki ya wakulima, hili ni lazima tukubaliane. Huwezi kuona wafugaji wanaingiza mifugo wanapotaka, iwe mbuga za Serikali, iwe kwenye mazao ya wakulima, lakini kwa sababu wanaofanya amejiita jamii ya Wasukuma, mimi nasema wafugaji wapo Tanzania nzima, siyo Wasukuma peke yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, lazima haki iwe kwa watu wote. Wafugaji wasidhulumiwe lakini na wakulima wasionewe na kunyanyaswa katika nchi hii. Mheshimiwa Waziri unachokifanya unasimamia sheria na ninataka niseme wazi, katika Mawaziri wanaosimamia sheria kikamilifu wewe ni nambari moja kama ilivyo CCM unavyoitaja.

Ahsante, endelea kusimamia sheria, tupo pamoja na wewe na tunakulinda kwa nguvu zote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Lulida na Mheshimiwa Tibaijuka ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Musukuma. Kama Taifa tunatakiwa tutafute *solution* ya kudumu ya migogoro ya ardhi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda uhifadhi, tunataka uhifadhi uendelee kuwepo, lakini wakati huo Serikali imeunda Tume kuangalia migogoro hii, watu wanaumizwa, mifugo inauzwa, watu wanabakwa, watu wanaibiwa. Askari wa Wanyamapori wamegeuka kuwa ndio wanaoleta maumivu na mateso kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka Mheshimiwa Waziri aseme, wakati Tume inafanya kazi, Serikali haijapata ushauri nini kifanyike. Lazima...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka na Mheshimiwa Lijualikali.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami nakushukuru. Jana nilizungumza kuwa baadhi ya wafugaji wanatumika na majangili. Wafugaji wanaingia ndani ya mbuga wakiwa na silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wafugaji Wanyarwanda wanaingia Burigi kwa biashara moja ya pembe na pembe zinauzwa Rwanda barabarani na sokoni na Burundi. Leo wafugaji wametolewa Ihefu wamepelekwa Lindi, Lindi ni jangwa. Tupeleke Tanzania nzima iwe jangwa kwa ajili ya kuwafurahisha wafugaji? Haikubaliki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda leo Kilwa, Kilwa ni jangwa, Liwale jangwa, Selous jangwa, ukienda Kisongo, jangwa, Monduli jangwa, Singida jangwa, tutafika katika mazingira kama hayo? Haiwezekani kuwaacha wafugaji kwa vile wako wengi watufanyie fujo wanavyotaka. Wafuate sheria, taratibu na kanuni. Kuwa Mbunge kwa maslahi yako,

haiwezekani, usiangalie maslahi ya nchi. Tuko katika nchi moja, tunataka tufanikiwe kwa pamoja tushikamane. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tibaijuka, ajiandae Mheshimiwa Lijualikali.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza sana Mheshimiwa Waziri, maelezo yake ni mazuri na jana mimi ndio niliweka hii hoja mezani juu ya suala la kumalizana na migogoro. Sasa katika suala hili hata katika vita yoyote inafika mahali unaweka *stand still position* kwamba ngoja kwanza tutulie kama Serikali tulivyosikia Kamati zinafanya kazi, haziwezi kufanya kazi wakati huku porini minada inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri tunachokitaka hapa, minada ile wajue kwamba Serikali mpaka tarehe 10 Juni tumeambiwa watu waweze kuendelea na maisha yao kule. Hili ni jambo la msingi. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri amejieleza vizuri, lakini sasa hawezi kuacha Maafisa wake kule wanaendelea kukamata mifugo maporini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo nalisisitiza, kauli ya Mheshimiwa Waziri itoke vizuri na Mheshimiwa Musukuma tupo pamoja katika hili. Kauli itoke.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lijualikali, ajiandae Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ambao hawana wananchi ambao wanafuga, wanaweza wakadhani hili suala ni dogo. Nataka niwaambie kwamba lazima Serikali iwaambie Askari wa Wanyamapori namna wanavyowa-*treat* wafugaji sio kibinadamu. Hatukatai kwamba wafugaji wana matatizo, lakini hoja yangu ni kwenye *treatment.* Haiwezekani mtu anafanya kosa, unampiga risasi, yaani mtu afe kwa sababu ya ng'ombe? Haiwezekani! Lazima Mheshimiwa Waziri

atuambie kama anaruhusu wafugaji kwa sababu wanafuga, basi wafe, atuambie leo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mfugaji amekosea, *treatment* iwe ya kisheria, lakini siyo ya kihuni. Huweze kuua mtu kwa sababu ana ng'ombe, haiwezekani! Simba hawezi kuwa na haki kuliko mtu bwana!

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kanyasu na Mheshimiwa Keissy ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba watu wengi wanawachukua wafugaji wanafikiri ndio wanaokata miti. Mfugaji hakati miti, wala ng'ombe hakati miti. Wanaokata miti ni wachoma mikaa na wakulima. Niambie mfugaji ambaye anakata miti. Mkulima anakata miti kwa sababu ya kufukuza ndege. Sasa unakimbia, unaanza kupambana na mtu ambaye hana kosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la pili, lazima tukubaliane kwamba tunachopambana nacho ni tatizo la Serikali kushindwa kuweka mpango wa namna ya kuwahudumia wafugaji, siyo tatizo la wafugaji. Lazima tulione hili. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Keissy, atafuatiwa na Mheshimiwa Tisekwa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hili Bunge kazi yake ni kutunga sheria. Sheria ya mwaka 2009 imesema kwamba mifugo yoyote ikiwa ndege, meli, kitu chochote kinachoingia kwenye Hifadhi ya Taifa, kinataifishwa. Sheria imetungwa na Bunge. Hapa hatuko Manzese hapa! Sheria ni msumeno, tunafuata sheria. Hatuwezi kuruhusu mifugo iingie popote pale, tunafuata sheria. Sheria lazima ifuatwe! Hakuna kuvunja sheria...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa!

**MWENYEKITI:** Hamna taarifa hapa.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa, taarifa!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Kama mmekuja hamjui sheria, kajifunzeni sheria. Someni sheria inavyosema. Hatuko Manzese hapa! Hatuko kwenye vijiwe! Tunafuata sheria. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tisekwa.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli siungani na ndugu yangu Mheshimiwa Musukuma kwa sababu hii mifugo inapotolewa kwenye hifadhi hizi za wanyamapori na kadhalika, wanakimbilia kwenye mashamba ya wakulima. Tatizo ni kubwa sana Mkoa wetu wa Morogoro, watu wanauawa, Madiwani wanapandikiziwa kesi, hawa wanavunja sheria. Kwa hiyo, sheria ifuate mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba, kama binadamu anafanyiwa *family planning* kwa ajili ya ku-*control population pressure,* kwa nini hawa wenye mifugo wasifanyiwe *zero grazing* ili kupunguza haya matatizo? Msipofanya hivi nchi hii, ujue kutatokea vurugu na njaa. Morogoro sasa hivi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa naomba nafasi, na mimi ulinitaja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei halafu Mheshimiwa Nasha.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Musukuma kwa asilimia mia kwa mia. Ukweli ni kwamba kila kitu kina mahali pake. Hakuna wakati ambako maisha ya binadamu yanaweza kupotezwa tu kwa sababu ya ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kuna sababu ya kufuata sheria. Kama kuna shida katika mifugo, mifugo ipelekwe Mahakamani, siyo askari wa *game* wanaamua kuua mtu. Jambo la mauaji ni kitu kibaya sana. Kwa hiyo, mimi nafikiri hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Serikali ije na mpango pia wa kuhakikisha kwamba eneo la wakulima linajulikana na eneo la wafugaji pia linajulikana. Binadamu anaweza kuwa mfugaji na wakati huo huo binadamu naweza kuwa mkulima. Kwa hiyo, ukulima na ufugaji hapa visitutenge, kwa sababu wakati mwingine mkulima anaweza kuwa mfugaji na mfugaji anaweza kuwa mkulima. Kwa hiyo, Serikali ije na mpango wa kusaidia watu hawa wasigombane. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nasha na Mheshimiwa Tizeba ajiandae.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinitaja halafu umeniacha na ni muathirika mkubwa Biharamulo, naomba nafasi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Musukuma amrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi.

Kimsingi Mheshimiwa Waziri alichofanya, ametoa ahadi na maagizo kwamba ile mifugo ambayo ilikuwa inapigwa minada isimamishwe mpaka wiki ijayo ili Serikali ione cha kufanya. Hiyo ndiyo ilikuwa hoja ya msingi. Namwomba tu Mheshimiwa Musukuma kwamba katika hali ya kawaida ni vigumu kuingilia suala ambalo tayari linafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ametoa ahadi, naye ndio Kiongozi wa hiyo Wizara, lazima kila mtu ataheshimu anachosema. Kwa hiyo, tumpe muda. Sasa tukimshikia shilingi, hata hiyo kwenda kushughulikia hilo tatizo atashindwa. Kwa hiyo, namwomba sana aachie shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mukasa kwa upendeleo maalum, halafu Mheshimiwa Tizeba.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hatuko kupambana kati ya wakulima na wafugaji, kwa sababu Biharamulo kwa mfano hakukuwa na mgogoro kati ya wafugaji na wakulima. Baada ya kuwaondoa wafugaji hifadhini bila mpango, ndiyo mgogoro umeanza wa wafugaji na wakulima. Halafu wanaoongelea sheria, huwezi kutunga sheria nyumbani kwako kwamba hakuna kutumia kibatari wala mshumaa, lakini hulipi bili ya umeme. Watu watatumia tu. Ni akili ya kawaida tu! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupange kwa asilimia 80, tutumie nguvu asilimia 20. Sasa hivi tunafanya nguvu asilimia 80 kupanga asilimia 20, hatuwezi kumaliza hii migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sheria, nisamehe nimalizie. Sheria hiyo hiyo Mahakama ilisema juzi hapa Biharamulo, uza ng'ombe wa huyu, akakata rufaa, akashinda; lakini ikauzwa. Kwa nini huku mfuate sheria upande mwingine hamfuati sheria? Kwa hiyo, tukae tuwapange wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tizeba.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siku tatu zilizopita hapa, nilitoa maelezo ya kuhusu migogoro inavyoendelea na namna Serikali inavyoishughulikia. Tumetoa kalenda ambayo wenyewe katika Serikali tuna dhamira ya kuifuata kuhakikisha kwamba majawabu ya kudumu yanapatikana kwenye hili jambo la

mifugo, migogoro sijui ya wakulima na wagugaji na mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la muhimu, hili jambo lisiposughulikiwa kwa umakini litaligawa Taifa letu. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, tupunguze jazba. Hili ni jambo linalomgusa kila mtu nchini hapa. Kwa hiyo, tunahitaji kuwa makini, Wabunge wenyewe kwanza kama viongozi na watu wengine ambao tutawafanyia maamuzi yatakayogusa maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ng'ombe wamekuwa wanakamatwa wanapigwa minada kwa amri za Mahakama au kwa namna ambayo Sheria ya Wanyamapori inasema, lakini utekelezaji wake kwa baadhi ya Maafisa wa Serikali umekuwa siyo sahihi. Hili jambo sio kwamba Serikali hailijui. Ndiyo maana sasa hivi tumeweka agizo la kuzuia kuendelea kufanya hiyo minada mpaka hapo tutakapokuwa tumejiridhisha kwamba kinachofanyika ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Musukuma, hili jambo limekwishafahamika kwamba kinachofanyika yawezekana siyo sahihi ndiyo maana Mheshimiwa Waziri ameelekeza, na mimi natumia nafasi hii kuwaagiza Maafisa Mifugo katika Wilaya zote nchini, wahakikishe kwamba minada hii hata kama ulikwishatolewa maelekezo na Mahakama isimame kwa sababu mtekelezaji ni Serikali. Kwa hiyo, Mheshimiwa Musukuma rudisha shilingi ya Mheshimiwa Waziri utupe nafasi ya kufanya kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri mhusika.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona Bilago hujamsema?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Ethiopia wana ng'ombe zaidi ya Tanzania na hawana migogoro ya wafugaji wala wakulima. Naomba hebu limalizeni hili. Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema pale awali kwamba Wizara yangu imetoa amri kwa wafanyakazi wake walioko kwenye eneo lile kwamba wasimamishe minada ambayo imepangwa huko mpaka tutakapokuwa tumelitatua jambo hili. Wiki ijayo tunakwenda huko kulikagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, *this is the best we can do as government,* hiki ndicho tunaweza kufanya. Na mimi nawaomba sana muiamini Serikali na mturuhusu bajeti ipite ili tuweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho hatukiwezi kama Serikali, Serikali inafanya kama mhimili wa dola, lakini kuna mhimili huo ambao ninyi ndiyo nguzo zake, halafu kuna mhimili wa Mahakama. Mahakama kama ina nguvu yake ndani ya kitu hatuwezi kuzuia, lakini kile ambacho tunaweza ndiyo tumekiwekea *stop* ili kingoje utekelezaji wa Kamati ya Mawaziri watano ambao nimewataja hapa, na mimi nina uhakika kwamba jambo hili litakwisha, naomba sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Kwanza naomba niwaambie Wabunge, mimi sina tatizo na shilingi ya Mheshimiwa Waziri, lakini nimewashangaa sana Wabunge, kwanza mmejichanganya, mimi sikuwa na mgogoro wa wakulima na wafugaji. Nawashangaa, nawashangaa! Nimelalamika kuhusu wafugaji wanaotolewa kwenye pori ambako hakuna mashamba. Hata wanyama sisi hatuna. Nashangaa pia, anasimama Mbunge anasema tutekeleze sheria. Hizi sheria za wasomi si ndiyo yamemfyatua Mheshimiwa Muhongo hapa! Eeh! Si alikuwa anatuibia hapa! Unatekeleza… *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuache ushabiki, wala hakuna mtu mwenye chuki na Serikali. Tunapofika mahali tuzungumze matatizo ya wananchi. Kuna watu hamna ng'ombe humu. Kuna watu tumeshindwa kusoma kwa ajili ya kuchunga. Kwa nini tusitetee ng'ombe? Kuna tatizo gani?

**MBUNGE FULANI:** Taarifa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma! Kaa chini Mheshimiwa Keissy!

*(Hapa baadhi Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, kaa chini!

**MBUNGE FULANI:** Taarifa Mwenyekiti!

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilinde dakika zangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma kaa chini.

Waheshimiwa Wabunge, katika hatua hii hatuna taarifa. Naomba utulivu, muacheni mtoa hoja afunge hoja yake kwa utaratibu wa Kanuni. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Narudisha shilingi ya Mheshimiwa Waziri, lakini natoa ushauri mdogo tu kwamba ni kweli utafiti wa Wizara ya Mheshimiwa Maghembe umeona kwamba ng'ombe wetu zinapoingia kwenye mapori kula majani, hazili miti wala hazili wanyama waliomo, ndiyo unasababisha kupotea kwa mvua, hilo la kwanza.

**MWENYEKITI:** Kwa mujibu wa Kanuni naongeza muda wa nusu saa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Maghembe aje na utafiti wa sasa hivi,

siyo wa zamani ya kwamba miti ndiyo inaleta mvua. Napata kigugumizi kwa sababu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma nimekuelewa, nakushukuru. Sasa baadae kaa na Mheshimiwa Waziri mweleze hayo unayoona ni muhimu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mafuriko, wewe vipi?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa hii nafasi. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kurudisha pikipiki na baskeli. Sasa sijui kama ameruhusu mkaa uendelee kuchomwa na miti kukatwa, sijui, sina uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka kuzungumzia ni kwamba leo tumesikia kwamba kuna fursa ya kupeleka mkaa hata nje ya nchi. Sisi kwa Mikoa ya Iringa, Njombe na Morogoro tumekuwa tukilima miti kwa ajili ya kuchoma mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri kwa kuwa sisi tayari tumekuwa tukilima miti kwa ajili ya kuchoma mkaa ambayo inaruhusiwa kisheria, ambapo hatupati ruzuku kama wanavyopata wakulima wa pembejeo wala wachimbaji wadogo wadogo. Sasa unasemaje wakati tunakwenda kwenye nchi ya viwanda kwamba tupewe ruzuku ya kutosha ili tuweze kulima miti ya mkaa, ili tupeleke nje ya nchi na kuwa-*encourage* watu wengine ambao walikuwa wanakata mkaa miti ya pori wasiendelee kukata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri asipokuja na hoja nzuri ya kutoa ruzuku kwenye kilimo chetu hiki nitatoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii ina mradi mahusisi kabisa, tena tumepata msaada kutoka Finland wa kusaidia wananchi wa Nyanda za Juu Kusini kupanda miti kibiashara. Kwa hiyo, sio kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mwamoto kwamba Serikali haiwasaidii watu wanaopanda miti katika maeneo hayo, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili nimesema kwamba wale watu ambao wanalima na wanapanda miti yao ukipanda miti yako ni kama umekuza zao lako, kwa hiyo wewe mwenye ndio mwenye mamlaka ya kusema kwamba unautumia namna gani.

Kwa hiyo Wizara hainashida kabisa na wale wajasiliamali wanaopanda miti kuitumia kwa namna wanavyotaka na hata wakati mwingine kuuza wanapotaka. Kwa sababu tukifanya hivyo tutazuia nguvu za soko na hatuna sababu yoyote za kuzuia nguvu za soko za wale wananchi ambao wanapanda miti yao wao wenyewe. Na sisi katika Serikali tunawapongeza sana wananchi wa Nyanda za Juu Kusini kwa kuwa wao wameonyesha mfano kwamba kupanda miti, kuhifadhi na kutunza ni jambo ambalo linazalisha pesa, linalipa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwamoto

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siwezi kusema sio kweli lakini nasema huu mradi ulizinduliwa Njombe na Wa-Finaland miaka mitatu iliyopita. Lakini haujawafikia walengwa zimekuwa zikifika kwa watu ambao hawahusiki kwa hiyo fedha haziwafikii walengwa. Sasa unasemaje kwamba wananufaika Mheshimiwa Waziri na mimi nataka kwa kweli uniambie vizuri *otherwise* bado shilingi.

**MWENYEKITI:** Hapana!

**MBUNGE FULANI:** Toa hoja

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mgimwa, Mheshimiwa Cosato Chumi, Mheshimiwa Joram Hongoli, Mheshimiwa Makamba January na Mheshimiwa Kigola.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na huku.

**MWENYEKITI:** Kuna Mheshimiwa Yussuf, Mheshimiwa Mpina na wewe unataka, bosi wako si yupo?

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapunda.

**MWENYEKITI:** Haya Mapunda, haya tunaaanza Mheshimiwa...

**MHE. DANIEL E. MTUKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtuka.

**MWENYEKITI:** Haya tunaanza Mheshimiwa Kigola.

**MHE. DANIEL E. MTUKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtuka, Mtuka.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaotoka porini.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namuunga mkono mtoa hoja ukiangalia kwamba Mheshimiwa Waziri anasema kwamba kuna fedha zilitoka kwa wafadhili na wakulima wadogo wadogo wa Mufindi ambao wanapanda miti sehemu nyingi sana, mimi nikiwa kama Mbunge sijawahi kuona mpandaji miti mdogo mdogo amepewa hizo fedha. Tunaomba Waziri atuthibitishie vizuri na watu wangapi ambao walisaidiwa wakapewa huo msaada? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naungana na hoja Mheshimiwa Mwamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Mwamoto mradi huu aliozungumza Mheshimiwa Waziri ulifunguliwa miaka mitatu iliyopita, lakini Mheshimiwa Waziri anatakiwa atusadie kuna taasisi ya kwake pale inaitwa *Tanzania Forest Fund* inasaidia kupeleka hela kwa wakulima wadogo wadogo wa miti. Lakini kama *Tanzania Forest Fund* ingefanya kazi yake ipasavyo hela zingewafikia walengwa.

Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atusaidie kwenye maeneo haya na ziende kwenye maeneo husika kuliko hizi hela ziwezinaenda kwa watu wajanja wajanja. Kwa hiyo, wakulima wengi wa miti tuliokuwanao katika Wilaya ya Mufindi wanashindwa kufanya kazi yao ipasavyo kwa sababu *waste* nyingi inapotea, tungewasaidia wakapata hela za kutosha wangeweza kutengeneza viwanda vidogo vidogo ambayo vingeweza kuzalisha mkaa kuliko.....

**MWENYEKITI:** Ahsante umeshaeleweka, Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaki kukubaliana na Mheshimiwa anayesema hii hoja ya kwamba fedha hizi ziwafikie wale walengwa au haziwafikii. Sheria ya *Village Afforestation* inasema kwamba miradi yote au fedha ya miradi wapelekewe wale wahusika kwa maana ya kupelekewa *seedlings* yaani miche, utaalamu pamoja na elimu ile ya kupanda ile miti sio fedha ziwafikie watu kwa ajili ya matumizi yao. Kwa hiyo, *Village Afforestation* inakataa hivo wanavyotaka wao kwamba mtu agawiwe pesa la kwanza. Lakini la pili ni ile *extension,* wale waenezi wanaopeleka zile taarifa au ile elimu ya ule mradi hawawezi kuwafikia wakulima wote kwa mtu mmoja mmoja kwa hiyo Wabunge wanapokuja na hizi hoja wanatakiwa wafahamu ile Sheria ya *Village Afforestation* inasema nini na ule mradi unaenda kufannya nini sio waje wapinge tuu hapa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mpina, halafu Mheshimiwa Makamba.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Baada ya kuona kwamba tunahitaji kasi kubwa ya kuwawezesha wananchi kupanda miti tukaja na ule mpango wa kupanda miti wa mwaka 2015/2016 mpaka mwaka 2020/2021. Mpaka sasa hivi tunavyozungumza maelekezo yaliyoko ni kwamba taasisi yetu ya *TFS* ya Serikali ambapo kila Wilaya kwa sasa hivi kule mwanzo hatukuwa na *facility* hii tumeweza, wanamaelekezo ya kuhakikisha kwamba kila Wilaya wanaandaa miche kati ya 150,000 mapaka 500,000 kwa ajili ya kugawia wananchi katika Wilaya hiyo; na sasa hivi tunahakikisha kwamba katika kila Wilaya kuna Ofisi ya *TFS* na kwamba bado wanaendelea kusaidia jamii za uzalishaji miti katika eneo hilo. Kwa hiyo hoja ya Mheshimiwa ....

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa majibu yako mazuri Mheshimiwa Chumi, halafu Mheshimiwa Makamba.

**MHE.COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona Mheshimiwa Waziri amesema kwamba tani za mkaa milioni 2.3 na amekiri kwamba zinaenda mpaka Oman kwa hiyo maana yake ni kwamba kiuchumi kuna fursa. Sasa ikiwa watu wanaopanda katika maeneo hayo watapewa ruzuku maana yake ni kwamba tutajitosheleza kwa mkaa sisi wenyewe lakini pia na Pato la Taifa tutaliongeza ndio kilio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheikh Yussuf anachosema hatoki kwenye miti Yussuf Zanzibar hakuna miti kama sisi, kwa hiyo, tunaposema hoja hii sisi tunaijua ndio maana tunasema patolewe ruzuku kama wanavyotoa ruzuku kwa wachimba wa dogo maana yake tutaongeza Pato la Taifa, ndio *point* yetu tuliyoisimamia. Kwa inayotoka sasa hivi hiyo ya kupanda miti kibiashara *mostly* ni ya mbao, sasa miti kama hii ya miwati kwa ajili ya mkaa hakuna utaratibu huo ndio *point* yetu watu tunaotoka kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Makamba.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunafurahi kwamba Waheshimiwa Wabunge wote tunakubaliana kuhusu haja ya kulinda misitu yetu ya asili ili isikatwe hovyo kwa kutengeneza mkaa. Lakini pia tunakubaliana kwamba ili kuokoa miti ya asili ambayo inatunza vyanzo vya maji basi biashara sasa ya miti ya kupanda kwa ajili ya kutengeneza mkaa liwe ni jambo rasmi na liwe sehemu ya sera na mipango ya Serikali, hilo kwetu kama Serikali hatuna kipingamizi.

Sasa utaratibu wa fedha kwa ajili ya ruzuku kwa ajili ya kutoa mbegu na miche kwa ajili ya mashamba ni jambo linalozungumzika na linazungumzika pale tutakapofanya mambo mawili; kwanza kupitisha bajeti hii tunayoijadili sasa, lakini pili kutusaidia sasa Mfuko wa Mazingira ambao tumekuwa tunauzungumza kwa muda mrefu...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Makamba baadae utatoa.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** ...Na wenyewe upate fedha ili na wenyewe uweze kutoa ruzuku kwa ajili hiyo ili mifuko hii iwezekusaidia na kushirikiana kwa hiyo ni jambo linalozungumzika, naomba umrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uliniambia nitaongea halafu umeniruka, Mapunda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mapunda muda wenyewe unauona huu tushapata ile *theme* na *spirit.*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba nimefurahishwa na mjadala, lakini niseme tuu kwanza kwamba mradi huu unatekelezwa kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge Yussuf ameeleza hapa kwamba ruzuku inatolewa kwa wale wakulima wadogo waliotayari kupanda miti wanapewa

miche, halafu wanapewa utaalam wa namna ya kupanda na namna ya kutunza na wanashiriki katika kupata elimu juu ya jambo hili. Baadae Serikali inaendelea kuongea na lile shirika linaitwa *GEF* ili waweze kulipwa kiasi cha *cabon* ambacho wanakiondoa kwenye hewa wakati miti yao inakuwa. Jambo hili bado liko kwenye mazungumzobado halijapata ufumbuzi lakini linakuja, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hili wakulima 3,000 wanashiriki katika jambo hili na sisi tuko tayari kama Wizara kuwapeleka Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo kuwaonyesha kazi ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili *Tanzania Forest Fund* ina miradi 395 ya kusaidia wajasiriamali wadogo kupanda miti. Kati ya miradi hiyo miradi 65 ipo katika Mkoa wa Njombe peke yake na zaidi ya nusu ya miradi hii na Mheshimiwa Mgimwa anaelewa maana yake alikuwa Naibu Waziri kwenye Wizara zaidi ya nusu ya hii miradi 393 iko kwenye Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Iringa na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana wanirudishie shilingi maana yake niko kazini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri tatizo lilokuwepo Wabunge wanasema huo ushirikishwaji hata wao hawaujii? *(Makofi)*

Sasa ili uendenao vizuri kutana na Wabunge wote wadau wa maeneo hayo ili uwaelimishe na wao wajue mipango mizuri ambayo Serikali mnafanya. Sasa mnaweza kuwa mna mipango mizuri, lakini haiwafikii watu, mmeelewa jamani kaa sijakwambia usimame kaa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kujieleza vizuri sana Mheshimiwa Waziri kwanza nikupongeze lakini kwenye hii *Tanzania Forest Fund* fedha ambayo umepeleka ni kidogo sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto hiyo hoja nyingine sasa wewe baadae kutana naye.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO**: Kwa hiyo, pamoja na kuwa mimi nikuombe tu Mheshimiwa shilingi yako mimi nakurudishia lakini naomba ufanye ziara Kilolo.

**MWENYEKITI:** Ahsante kaachini yamekwisha, Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 19 Mei 2016 Wizara ilisitisha biashara ya kupeleka nje viumbe hai na kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri hapa ni kwamba wamesitisha kwa miaka mitatu. Sasa baada ya mwaka mmoja wamefanya tathimini na kwa ripoti iliyopo hapa wanakiri wao kwamba wako tayali kutoa kifuta jasho.

Sasa hoja yangu ya msingi ambayo niliizungumza hapa na kwa kweli sikupata majibu itabidi nikamate shilingi ni kwamba kwa kuwa wameshafanya tathimini na ripoti wanayo ya tathimini hakuna sababu ya kusubiri miaka mitatu wakati watu wanaendelea kupata hasara, wamechukua mikopo, wamelipwa tayali pesa kwa ajili ya kupeleka hao wanyama na wanao wanyama kwenye baadhi ya mazizi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ripoti hii tayari ipo mimi nadhani nilishauri hapa na ndio ombi langu kwa Serikali sasa tuwaruhusu hawa wanyama wapelekwe nje hasa wale ambao tayari wameshakatwa na wapo na hawa watu walifuata utaratibu katika *process* ya kuwakamata, wamelipa kodi, wamelipa leseni na wamechukua mikopo sasa watafilisiwa tukiendelea kusubili kwa miaka mitatu, ndio lilikuwa ombi langu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni jambo kubwa na Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba ilitokea hapa nchini mtu mmoja aliiba wanyama 123 akiwepo na Twiga na wanyama wengine wakubwa wakawekwa kwenye ndege na kusafirishwa kwenda Qatar. Sasa wakati ule hatua zilizochukuliwa zilikuwa kali, lakini bado watu walikuwa wanaiba wanyama wa Tanzania wanakamatwa kwenye bandari za ughaibuni mara kwa mara na tunapata aibu kama Taifa ambalo linasafirisha wanyama hai bila utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanyama wanaweza kufikiriwa kama ni vitu vidogo vidogo kwa mfano kama hawa *beetles,* mijusi, ndege au popo lakini wanyama hawa wanavinasaba maalum ambavyo ni vya Tanzania na baadae vinasaba hivi tutavitumia kwa ajili ya utafiti wa dawa, kutibu magonjwa na vitu vingine ambavyo ni muhimu. Hivi sasa dunia inafaidika na *edge* au zana za mawasiliano; kesho, keshokutwa zinakuwa ni zana za vinasaba na *molecules* ambazo nchi inazo kwenye viumbe ambavyo nchi inavyo. Na viumbe vyetu wanachukuliwa bure bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusimamisha wakati ule imekuja *Soviet Institute of Mammalogy* sasa inatuomba kwamba tuwapelekee nyani wale aina ya kipunji na nyani hao wengine wadogo wadogo, wanakwenda kufanyia utafiti ambao matokeo yake ni *billions of shillings.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nawaomba ndugu zangu kitu tunachofanya sio kusimamisha kabisa, tunachofanya ni kuhakikisha kwamba hatuibiwi, hatuendelei kuibiwa kila siku, tunaweka utaratibu wa ili.... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante umeelewaka vizuri tuu, Mheshimiwa Nape Waziri amejieleza vizuri.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima kaa, kaa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti kuhusu utaratibu ni Kanuni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima kaa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa si unisikilize.

**MWENYEKITI:** Mimi na *override* Kanuni zote saa hizi hapa soma 68(10) kila kitu kikohapa kwangu na kama hupendi maamuzi yangu unaandika barua kwa Katibu. Kaa chini sijakwambia usimame. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Nape kama unaendelea au unafunga hoja yako au kama umeridhika.

**MHE.NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona ni Waziri anapiga chenga kwenda *straight* kulitatua tatizo hili na kwa sababu tatizo ni kubwa naomba kutoa hoja jambo hili lijadiliwe.

**MWENYEKITI:** Ahsante tuna humu ndani mkikaa muwe mnasikiliza Wabunge wenzenu wanasema nini na usirukie huyu hakusema, huyu kasema, huyu hakusema mimi ndio nilisema nani kasema nani hakusema.

Mheshimiwa Millya, Ikupa, Bilago jamani muda wetu umekwisha siwezi kuwachukua wote maana wakati mwingine nikiandika haimaanishi kuwa nawapeni wote. Tunaanza na Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha sana pale ambapo Serikali inakuwa imechukua fedha kwa wafanyabiashara kupitia kodi wanazolipa. Halafu wafanyabiashara hao inashindwa kuwaruhusu waendelee na biashara zao, wanakaa na bidhaa hiyo inazuiliwa kwa *reference* ya watu walioiba twiga miaka iliyopita, yaani wezi walioiba wanawaathiri hao wafanyabiashara ambao ni wafanyabiashara wasio na

dhambi, *innocent people* wanaadhibiwa na wizi wa twiga aliyeibiwa na wezi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni waajabu sana tunashindwa kuzuia wezi tunakuja kukomaa na waliofuata taratibu vizuri katika nchi yetu, kwa hiyo, mimi namuunga mkono sana Mheshimiwa Nape. *(Makofi).*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Nape na hata jana kwenye mchango wangu wa maandishi niliuliza yafuatayo; nikasema hawa waathirika wa hili katazo maana yake Mheshimiwa Waziri alisema tuu kwamba watapewa kifuta machozi nikauliza hicho kifutamachozi kitatolewa lini? Kwa sababu hawa watu wanadaiwa wamekopa kwenye mabenki. Lakini la pili nikahoji kwamba je, hiki kifuta machozi kitaendana na uhalisia wa gharama walizotumia?

Kwa hiyo, mimi naomba Serikali iwe tuu *specific* na itoe muda kwamba hizi fedha zitalipwa lini? Hawa watu wanadaiwa na wanabughudhiwa na miongoni mwao Mheshimiwa Waziri ni zaidi wamo watu wenye ulemavu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ikupa umeeeleweka Mheshimiwa Waziri majibu. Hamjajipanga?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umenitaja mimi wa kwanza halafu haujanipa nafasi niongee.

**MWENYEKITI:** Nimesema unaweza ukatajwa usipate, ndio utaratibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya tathimini ya gharama ambazo wale wafanyabiashara ambao wamekubwa na jambo hili, watarudishiwa zile fedha ambazo

wametumia katika kuwapata wanyama wale kutoka Serikalini na tumetoa takwimu kabisa wakati ninatoa hotuba yangu hapa, kwa hivi hatutawaacha wale wananchi, na sasa umebaki mwaka mmoja tu, mimi nawaomba wale wananchi wavute subira, walipwe hela zao na wajiandae kufanya biashara mwaka huu utakapomalizika.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kauli ya Mheshimiwa Waziri sio kifuta jasho ispokuwa ni kurudishiwa gharama zote walizozitumia, sina matatizo nalo, akibaki na kifuta jasho, kifuta jasho unaweza ukapewa shilingi moja, kifuta jasho unaweza ukapewa hela yoyote, kwa hiyo kama inabaki kauli kwamba ni pesa zote walizotumia kama gharama zao wanarudishiwa mimi namrudishia shilingi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ryoba.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye mchango wangu niliongelea *issue* ya *single entry* jinsi ambavyo inavyoathiri *Ikona WMA,* ili uingie *Ikona WMA* lazima u–*cross Serengeti National Park* na kutokana na hili, wawekezaji nane waliokuwa wamewekeza kwenye hii *WMA* wameanza kuondoka, vijana wa kijiji cha Robanda na maeneo mengine wamekosa ajira, nilitaka nipate majibu ya Waziri kama hayataniridhisha nitatoa shilingi.

**MWENYEKITI:**Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *single entry* Serikali ilikwisha lipokea wakati wa michango na tumelijadili kwa kina wakati tukiwa tunapitia hoja zote hizi, ieleweke kwamba madhumuni ya kuweka masharti yale ya *single entry* na kwa wale wasiofahamu ni sharti la kuingia ndani ya hifadhi, eneo la utalii ndani ya saa 24 na huyo anayeingia haruhusiwi kutumia kibali kile kile kama atatoka nje na atakapotaka kurudi tena ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sharti hilo liliwekwa kwa ajili ya kudhibiti udanganyifu ambao kwa kiwango kikubwa ulikuwa unasababisha hasara kwa Serikali. Lakini baada ya kupitia maendeleo ya teknolojia tuliyonayo na mambo mengine mengi ambayo tumeyaangalia tumeona ziko njia ambazo tunaweza tukazifikiria kuweza kudhibiti udanganyifu, lakini bado tukatoa fursa kwa kumwezesha mtu ndani ya saa 24 kama ana sababu ya msingi aweze kutoka na kurudi tena.

Lakini katika hatua hii, hatuwezi kusema kwamba tayari tumekamilisha uchunguzi na kwamba tunaweza tukaliachia wazi, lakini nimuombe Mheshimiwa Mbunge aliachie Serikali kukamilisha kazi ambayo imekwisha kuianza na tukifanikiwa kukamilisha suala hili, basi tutaweza kutoa maelekezo ambayo yatakuwa ni maelekezo kwa faida ya pande zote mbili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ryoba umeridhika?

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwa kweli nishukuru, Mheshimiwa Waziri, kikubwa tu niombe hebu shirikisha wadau na nikuombe ikiwezekana njoo pale *Ikona WMA,* ongea nao uone uhalisia, *otherwise* sina sababu ya kushikilia shilingi yako. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante tunataka uungwana huo, Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru...

**MWENYEKITI:** Hebu Bobali ngoja mna nini hapo,ana hoja gani Waziri Kivuli.

**WABUNGE FULANI:** Si umeshasikilizwa wewe.

**MWENYEKITI:** Unasemaje wewe? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Bobali endelea.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwenye Sera ya Mambo ya Malikale ya Tanzania ya mwaka 2008 inaainisha namna gani Nchi yetu inapaswa kunufaika na rasilimali za kale zilizopo ndani ya nchi yetu, na zile ambazo zimechukuliwa kupelekwa kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilisimama nikashika shilingi mshahara wa Waziri, na wewe ulikuwandio unaongoza kiti hicho ukatoa muongozo kwamba Mheshimiwa Waziri tuonane tuweze kujadili suala hali, lakini ule muongozo wako ulioutoa haukufanyiwa kazi.

Kwa hiyo, Waziri asiponijibu vizuri, nitashika shilingi na nitatoa hoja watu tujadili ni kwa nini mpaka leo Serikali haitaki kutoa maelezo ya kina kwamba tunanufaikaje na rasilimali yetu iliyoko Ujerumani ile *dinosaur* kwa nini mpaka leo hamtaki kutoa majibu hayo na sisi tukajua? Hoja yangu ni hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimwia Mbunge ni kweli ni hoja iliyodumu muda mrefu sana humu ndani, wale tuliokuwepo Bunge lililopita na pengine hata waliotangulia hapo kabla, wanakumbuka kwamba hoja hii imekuwa mezani kwa muda mrefu, lakini yapo masuala ambayo tunapaswa tufahamu wote kwa pamoja, tukiwa na uelewa wa pamoja itatusaidia kuweza kufanya maamuzi sahihi kama Bunge, mjusi anayezungumziwa *size* yake kwanza, urefu ni mita 50 nusu ya uwanja wa mpira wa miguu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kaa chini, kaa chini.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umefika tunaingia kwenye *guillotine*. *(Makofi/Kicheko)*

**Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Mgt.* ....................Shs. 5,557,992,404/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts*............Shs. 1,473,747,653/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ..............Shs. 1,379,893,515/=
Kif. 1004 – *Gvt. Comm. Unit*...........................Shs. 304,731,861/=
Kif. 1005 – *Internal Audit Unit* ....................Shs. 451,673,837/=
Kif. 1006 – *Procurement and Mgt. Unit*........Shs. 512,135,361/=
Kif. 1007 – *Legal Unit* ..................................... Shs. 394,344,000/=
Kif. 1008 – *Mgt. Information Systems*.........Shs. 549,484,273/=
Kif. 2001 – *Wildlife*..................................Shs. 21,634,289,088/=
Kif. 3001 – *Forestry and Beekeeping*........Shs. 52,047,863,642/=
Kif. 4001 – *Tourism* .............................. Shs. 8,307,474,417/=
Kif. 4002 – *Antiquities Unit* ....................Shs. 4,181,031,949/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*.....................................Shs. 0/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ..............Shs. 1,000,000,000/=
Kif. 2001 – *Wildlife*..................................Shs. 42,711,844,000/=
Kif. 3001 – *Forestry and Beekeeping*........ Shs. 7,591,440,000/=
Kif. 4001 – *Tourism* ................................. Shs. 500,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae! Mtoa hoja! *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu lililokaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake, naomba sasa Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Bajeti imepita nakupongeza Mheshimiwa Waziri na timu yako nawapongeza Wabunge wote kwa kazi nzuri mliyofanya hapa nina tangazo dogo kwa kesho timu ya Yanga italeta Kombe hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, subirini kwanza.

**MBUNGE FULANI:** Rudia, rudia.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Umetamka vizuri Yanga, umeitamka vizuri.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, subirini mimi natoa tangazo na natoa na *ruling* vilevile muongozo, asubuhi kulikuwa na tangazo la Katibu, aina ya wageni na muda wa kuingia humu ndani, sasa kwa tangazo hili na tangazo la asubuhi sidhani kama hii kitu ina-*qualify. (Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Aaah ina sifa.

**MWENYEKITI:** Huo ndio utaratibu, kama mtapata huruma ya Katibu sawa, lakini kwa mujibu wa tangazo la asubuhi mko....

**MBUNGE FULANI:** Siku moja kabla.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lirudie tangazo la asubuhi, lirudie.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Matumizi mabaya ya madaraka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko unasemaje, haya leta Mwongozo wako, sema.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) nadhani sina haja ya kuisoma, nadhani Wabunge tunatakiwa tuutumie muda wetu vizuri na tuwajibike wakati wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni kawaida kwamba wakati wa kushika shilingi muda unapofika,wanakuta umepata majina lakini unachukua muda mwingi sana na siku zote mnaanza upande wa CCM unachukua muda mwingi sana ku–*cover* wale wanaoshika shilingi upande wa CCM, na unachukua majina mengi, ikibaki dakika tano, ndio unakuja upande wa Upinzani, unampa mtu na wakati mwingine inafikia hata hapati *support* kama ameamua kushika shilingi, unasema unaingia kwenye *guillotine. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako hii ni kitu ambayo mmepanga katika kuhakikisha Bunge halifanyi kazi yake kama inavyostahiki, au kuna mkakati gani ambao kwa kweli ni wa kusikitisha, nakumbuka Bunge la Kumi nilikuwepo, tulikuwa tunaenda wakati mwingine mpaka saa nne za usiku. Tunamaliza kushika shilingi na tunaingia kupitia vifungu. Lakini sasa hivi Bunge la Kumi na Moja Wabunge

tumeamua kutumika na ndiyo maana hata kaka yangu Msukuma amesema zile sheria tunazozipitisha huku bila kuzisoma kwa kina zinakuja kui-*cost* nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako ni Kanuni ipi ambayo inapelekea kila ambao mnakaa kwenye Kiti hapo mkija kwenye kushika shilingi lazima muanzie CCM muda mwingi mnachukua mkiwa mmeanzia CCM na baadae huku, mnashindwa kutupa nafasi. Na zaidi....

**MWENYEKITI:** Ahsante, umeshaeleweka Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:**Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie.

**MWENYEKITI:** Haya maliza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tume-*raise* hapa kwamba pamoja na kwamba imebaki dakika tano basi hata hiyo nafasi ungeweza kuitoa kwa Waziri Kivuli. Ulichotuandikia, umeandika ki-*memo* ukisema mambo yenu ya kibwege bwege unatuandikia sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muongozo wako, tumekuja huku ndani kama mabwege, yaani wananchi wa Tarime Mjini mimi bwege wamenileta niwawakilishe wao mabwege wa Tarime Mjini. Naomba Mwongozo wako.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nataka muelewe kitu kimoja, Bunge hili linaendeshwa na Kanuni, Kanuni ya 104 ambayo inatoa fursa kwa Kiti kuingia katika *guillotine* na Kanuni hizi hizi zinatoa fursa kwa vyama kuleta majina ya wachangiaji, CHADEMA mmeleta majina matatu, Mheshimwa Esther Matiko, Mheshimiwa Ryoba...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** Sasa mimi si ndio nasema, wewe umesema mimi nimekaa kimya, mimi nasema unasema sijui kuna karatasi ya kibwege bwege, hiyo karatasi ya kibwege bwege mimi siijui imetoka wapi, kwa hiyo, umesikia.

Sasa wewe unaweza ukaichukua hiyo karatasi ukaipeleka kwa Katibu ili ifanyiwe *forensic* sawa, baada ya maneno hayo, muongozo hapa hakuna, sababu Kanuni zimetumika ipasavyo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 2.13 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 25 Mei, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*